

25 MEI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 25 Mei, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2013/2014.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014
Wizara ya Nishati na Madini

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea pale tulipoachia siku ile. Sasa nitamwita Mheshimiwa Devotha Likokola, atafautiwa na Mheshimiwa Josephine Chagula, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Abdul Mteketa, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa

25 MEI, 2013

James Lembeli, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis na Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi. Kwanza niishie hapo halafu tutaendelea baadaye. Mheshimiwa Likokola!

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii. Kwanza kabisa, niungane na Wabunge wenzangu, kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Ninashukuru sana na ninaipongeza Wizara hasa Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini pia wameweza kutengeneza timu nzuri sasa Wizarani kwa ajili ya kuendeleza masuala ya Nishati na Madini katika nchi yetu. Ili maendeleo ya nchi yoyote yaweze kufikiwa, yanahitaji rasilimali watu, lakini pia yanahitaji rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, suala la rasilimali watu, tunashukuru Wizara imejipanga vizuri, imetengeneza taasisi nzuri, ambazo zinaweza kuleta mafanikio makubwa ya mageuzi katika masuala ya nishati katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo ninataka tuliongelee leo kwa kina ni la rasilimali fedha. Wabunge na Wananchi wote wa nchi hii, kwa mwaka huu tuna ajenda moja kubwa ya umeme vijiji. Hakuna Mbunge ambaye hataki vijiji vyake vipate umeme na hakuna Diwani ambaye hataki vijiji vyake vipate umeme. Serikali yetu imefanya jambo zuri, imetengeneza Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*).

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo kwako ili tuweze kuhakikisha kuwa, *REA* inapata fedha za kutosha na umeme vijiji uende wa kutosha; tutoe hoja gani? Ni suala la kusikitisha sana, leo Watanzania wengi wako vijiji, asilimia 80 wako vijiji na watu hawa hawana umeme, Kamati ilioomba *REA* ifanye makadirio ili umeme vijiji uweze kwenda wangehitaji kiasi gani. Wametoa takwimu zao kwamba wanahitaji shilingi bilioni 800 na sisi ndiyo tuna wajibu wa kugawa bajeti ya nchi hii, leo tunawapa bilioni 150, bilioni 650 atazitoa nani?

Leo ninaomba sisi Wabunge kama kweli tuna wajibu

wa kupidisha bajeti ya nchi hii vizuri ili Wananchi wanufaika, tutoe hoja gani ili umeme vijijini uweze kwenda. Hatutakubaliana na hoja yoyote ambayo itaendana na Wizara hii bila kuongeza pesa za *REA*. *REA* waongezewe pesa, umeme vijijini uweze kwenda. Mheshimiwa Waziri, ametamka hapa, bajeti yake ina takwimu na *figure*; hizo takwimu na *figure* kama hazina pesa zina maana gani? Lazima tuwe wakweli na hapa tuliusiza Wabunge tunataka pesa za *REA* zitoke wapi? Tuliishauri Serikali; kuna hela za mawasiliano, kuna hela za mafuta, kwa nini hela hizi haziendi *REA*?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapojoibu, atueleze kinagaubaga kwamba kwa nini *REA* inaendelea kupata fungu dogo na inaendelea kuwachanganya Wataalamu wa *REA*, hawawezi kufanya kazi nzuri bila kupata fedha za kutosha? Wana nia nzuri, wana moyo safi, lakini kulingana na ufinyu wa bajeti wanayopata, wanashindwa kuendeleza umeme vijijini.

Ninaomba nizungumzie umeme wa kutoka Makambako kwenda Songea. Ajenda hii ya umeme wa kutoka Makambako kwenda Songea ni ya miaka mingi tangu wengine hatujawa Wabunge, tangu wengine hatujazaliwa umeme wa Makambako – Songea, *Mtwara Corridor* tunasikia habari hizi. Lakini kila siku kwenye Bajeti ya Serikali tunasikia ooh kuna *Mtwara Corridor* kuna umeme wa Makambako – Songea; mbona hautekelezeki?

Bajeti hii pia umeme wa Mkambako – Songea imewekwa lakini sisi tunataka utekelezaji. Safari hii ninakuomba Mheshimiwa Spika, kwa sababu na wewe umeme huu utakugusa katika Jimbo lako la Njombe, tuungane mkono Wabunge wa Ruvuma na Wabunge wa Njombe, kuhakikisha kuwa kipaumbele ni Mradi huu wa Umeme wa Makambako – Songea. Wananchi wa Songea wanapata shida sana, suala la umeme limekuwa ni kero kubwa.

Mheshimiwa Spika, Umeme Vijijini; Wilaya ya Nyasa ambako kuna Bandari kubwa ya Mbamba Bay, hakuna

umeme. Ninaomba *REA* mfanye kila linalowezekana, ile Bandari haiwezi kufanya kazi vizuri kama hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni tunasikia kinagaubaga Mikoa mingine vijiji vyao vina umeme na ni vijiji vingi watu tumefanya mahesabu kuna Mikoa mingine vijiji 30, vijiji 20, vijiji 60, lakini Mkoa wa Ruvuma ni vijiji viwili tu. Mkoa mzima wa Ruvuma ni Peramiho umeme umeenda na masuala ya Chipole. Nawapongeza sana wale Masista, bila ule Mradi wa Masista Chipole tungkuwa Mkoa wa Ruvuma katika vijiji vyetu ni Kijiji cha Peramiho tu ndicho kingepata umeme; kweli hii ni haki?

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikuulize hii ni haki; Mkoa wa Ruvuma ambao ndio wazalishaji wakubwa wa chakula kwa nchi hii, wanalisha nchi hii; umeme hakuna katika vijiji vyao vyote; kweli jamani siyo vizuri! Mheshimiwa Waziri, ninakuomba ajenda ya Mkoa wa Ruvuma ni lazima uipe kipaumbele, kwa sababu haiwezekani, Mkoa wa Ruvuma ni watu ambao wamejikita katika uzalishaji na imekuwa bahati mimi kuwepo katika Kamati hii, tumekwenda kutembelea vijiji vingine umeme umeenda Wananchi hawawezi kuunganisha, hawana uwezo. Mkoa wa Ruvuma, Wananchi wake wana uwezo, pelekeni umeme Wananchi wataweka, wataunganisha katika nyumba zao kwa sababu wale Wananchi ni wazalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie masuala mazima ya Vijiji vya Mkoa wa Ruvuma, ambavyo wakipelekewa umeme kwa haraka wangeweza kusaidika sana. Wilaya ya Tunduru, umeme uko pale katikati kidogo tu, lakini tunahitaji uende maeneo mbalimbali. Tuna suala zima la makaa ya mawe ya Ngaka; pale pana matatizo, Serikali iliahidi kuwalipa fidia watu, lakini wengine walilipwa kidogo na wengine hawakulipwa, imesababisha mpaka tarehe 30 mwezi wa nne mradi ule ulifungwa kwa muda. Serikali imeahidi mpaka tarehe 15 mwezi wa sita wale watu watakuwa wameshalipwa. Ninaomba Serikali msifanye mchezo katika hilo, hatutaki machafuko yatokee katika nchi yetu.

Ninashukuru sana kwa umeme wa Namtumbo; umeme umewaka lakini umewaka pale Namtumbo tu Kindakindaki na tunafurahi sana Wananchi wa Namtumbo kuwasha umeme pale, lakini tunataka umeme uende Namabengo, uende Suluti, uende vijiji vingine vya Litola, vijiji mbalimbali mpaka Lumecha, mpaka Songea. Pale Namtumbo sasa hivi ni rasilimali ya Taifa, ninyi wenyewe mnajua Namatumbo kuna nini; kwa hiyo, kama umeme hauingii, itakuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna Miradi ya *Solar*, ninaombwa Wizara ieleze kinagaubaga ili mashule yetu yaweze kupata watoto. Kuna mwaka hapa watoto wa Mkoa wa Iringa walungua kwa ajili ya umeme wa kusomea. Kwa nini mashule yetu yasiwekwe *solar* mpaka tupoteze watoto? Umeme wa *solar* ungeweza kuwasaidia watoto waweze kusoma katika mabweni yao.

Mheshimiwa Spika, ninaombwa Miradi mingine tuipe kipaumbele ili tuweze kuendeleza gurudumu letu la masuala ya Nishati mbele. Kama kweli tunataka maendeleo ya nchi hii, bila kuwekeza katika umeme hakuna uchumi. Wananchi wanazalisha wanashindwa *ku-process*, wanauza malighafi, wanashindwa kuweka viwanda vidogovidogo; kwa nini hatuelewi? Mbona ni mahesabu ya kawaida kabisa kwamba, huo uchumi hata tukiwaambia walime vipi kama *hawa-process* hawawezi kunufaika; mbona ni mahesabu madogo madogo haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, ninaombwa nikimaliza kuongea hapa, unipe Mwongozo nitoe hoja gani *REA* waongezewe pesa ili umeme vijiji uweze kupatikana na Wabunge wenzangu ni nani hataki umeme kwenye vijiji vyake? Na kama tunataka si tunapitisha bajeti hapa, basi tuazimie *REA* ipate pesa, hakuna Mbunge ambaye hataki umeme kwake. Haina maana, tunapitisha bajeti halafu tunaacha umeme kwenye vijiji vyetu hatupati, haiwezekani, Wabunge wenzangu tuungane, leo ni leo, *REA* wapate pesa, umeme vijiji uende. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la wachimbaji wadogowadogo. Wizara imefanya kazi nzuri kuwaunganisha wachimbaji wadogowadogo na tunaomba kazi hiyo isiishie hapo, wale wachimbaji wadogowadogo pamoja na matatizo yote, wana matatizo ya mitaji. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Umekataa halafu unaunga mkono hoja! (*Kicheko*)

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Josephine Chagulla!

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Nishati na Madini. Ninaanza na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili Waziri akaendelee na kazi nzuri aliyoianza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo siri, wote tumeshuhudia ni muda mfupi sana tumeona mabadiliko makubwa katika Wizara hii; kwa hiyo, tunawapongeza sana na tunawaomba waendelee na kazi hiyo na Mwenyezi Mungu, atawaongoza. Tunawaomba kasi waliyoanza nayo waendelee kuwa nayo.

Niende kwenye hoja yangu; Mkoa wa Geita ni mionganoni mwa Mikoa mipya, ambayo imeanzishwa hivi karibuni. Wananchi wa Mkoa wa Geita wanahitaji umeme katika majumba yao, wanahitaji umeme katika shule zao za sekondari na za msingi, wanahitaji umeme makanisani na katika vijiji vyao. Ni haki ya kila Mtanzania kupata umeme. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kujibu hoja za Wabunge, awajibu Wananchi wa Mkoa wa Geita kuwa

ni lini Serikali itawapa umeme Wananchi wa Mkoa wa Geita pamoja na Wilaya zake za Bukombe, Mbogwe, Chato na Nyang'hwale?

Mheshimiwa Spika, umeme ni maendeleo, bila umeme hatuwezi kuendelea, ninawaomba sana tena sana, Serikali iwaone Wananchi hawa, kwa sababu ni Mkoa mpya waweze kupata umeme ili Mkoa wao uweze kuendelea mapema. (*Makofi*)

Ninakuja kwenye madini, Mkoa wa Geita ni Mkoa ambao una madini mengi sana na tuna wachimbaji wengi sana. Kinachotushangaza na kutusikitisha sisi Wananchi wa Mkoa wa Geita, ni pale wachimbaji wetu wadogowadogo wanapoanzisha sehemu zao za kuchimba madini, Serikali inawaondoa na kuwapa wawekezaji; hii siyo sahihi. (*Makofi*)

Unapowaondoa wachimbaji wadogo hawa maeneo yale ni mashamba yao, ni sehemu zao za kuweza kujikimu, tunaiomba Serikali iwasaidie wachimbaji wadogo hawa wapate ruzuku, wapate mitaji, wapate leseni ili na wao waweze kuendesha maisha yao katika maeneo yale. Nikisema hivi sina maana kuwa hatutaki wawekezaji Geita, wawekezaji tunawapenda sana, lakini na wenyeji nao waangaliwe kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba niwaombe Wananchi wa Mtwara, wakwe zangu, watulie, Serikali imesikia kilio chao waache kuuana hovyo, wasubiri matunda mazuri, Serikali ina mpango mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba nianze kwa kuzungumzia misamaha ya kodi na upotevu wa mapato ya Taifa yanayotokana na Wizara hii. Kuna ripoti moja inaitwa *The African Department of IFM Report* ya mwaka 2006 na kuna sehemu hapa ninaomba ninukuu kidogo inasema: "All the

evidence suggest that the disadvantages of tax incentives vastly outweigh the advantages." Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, hasara na athari zinazotokana na misamaha ya kodi ni mikubwa sana kuliko faida zinazopatikana na misamaha ya kodi na kuna sehemu kidogo pia inasema: " *Tax incentives are not an important factor in attracting foreign investment.*"

Mheshimiwa Spika, baada ya nukuu hizo, hata jana tulikuwa tunazungumza hapa kuhusu *tax incentives*, lakini Serikali haichukulii hili jambo *serious*. Katika Ripoti ya *IFM* ya mwaka 2006 kuna takwimu inasema, katika kipindi cha miaka miatano iliyopita *exportinayotokana* na madini; kwa mfano, dhahabu, imeongezeka kutoka *five thousand million US Dollars* mpaka *1.5 billion US Dollars*, lakini mapato ya Serikali ya Tanzania yamebaki kwenye wastani wa *one hundred million US Dollars*, kwa sababu ya misamaha ya kodi, yaani *hundred million* ndiyo imebaki *average pale pale*. Pamoja na kwamba, mapato yameongezeka kwa sababu ya ongezeko la thamani ya dhahabu katika soko, lakini *average imebaki pale pale* kwa sababu ya misamaha mgingi ya kodi. Ripoti ndiyo inasema.

Mheshimiwa Spika, wametoa mfano na ninaomba nimpe Mheshimiwa Waziri; kwa mfano, kwenye *fuel/levy* peke yake, *exemption* inayotokana na *fuel levy* uki-refer kwenye Ripoti ya Bomani inasema kwamba, mwaka 2006/2007 hasara zilizopatikana kwa upotevu wa mapato ilikuwa ni Shilingi za Kitanzania 39.8 bilioni, mwaka 2007/2008 imeongezeka kwenda Shilingi za Kitanzania 59 bilioni, mpaka mwaka 2011 mwishoni makampuni yanayochimba dhahabu nchi hii yalikuwa yanaidai Serikali kwenye *275 million US Dollars* kama fidia ya ile *exemption* wanayopewa.

Meshimiwa Spika, hii ni hasara kubwa sana. Hoja ya msingi ninayotaka kujenga hapa ni kwamba, kuna Ripoti ninayo hapa inaitwa *Enhancing Revenue Collection in Tanzania*, hawa watu wamefanya *study* inasema moja ya swali kubwa walilouliza ni kwamba; kuna *mechanisms* zipi ambazo Serikali inatumia kufanya *control*. Kwa mfano,

wanaauliza na hili swali ninakuuliza Meshimiwa Waziri; tunapotoa kwa mfano misahama ile *fuel levy*; ni *control mechanism* ipi tullyonayo *in place* inayohakikisha kwamba mafuta ambayo wanatumia wanaochimba, inaenda kwa ajili ya hiyo kazi tu ya uchimbaji?

Zipo ripoti za siri zinasema kwamba, hata mafuta tunayotoa misamaha, kuna wengine wanaenda kuuza tena haiendi kwenye *intended use*. Wanasema hata mashine ambayo tunatoa misamaha inayokuja kwenye migodi, kuna zingine zinakuja tunauza tena.

Kwa hiyo, ninachotaka kujua kutoka Serikalini ni *control mechanism* ipi ipo *in place* inayohakikisha kwamba, kama misamaha tunatoa inaenda kwenye ile *intended use* peke yake ili kupunguza hasara inayopatikana kwa misamaha hii tunayotoa?

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kinachonishangaza sana na Mheshimiwa Waziri utueleze; je, kama Serikali tunao uwezo wa kujua kwamba *Geita Gold Mine* kwa mfano kwa mwaka wamechimba dhahabu kiasi gani na wamesafirisha kiasi gani. Kama wanavyo viwanja vya ndege kwenye migodi na ndege inaweza ikaja pale ikaruka *direct* ikaenda hadi Nairobi. Je, tuna Ofisi ya *TRA* pale? Kama Sheria ya Madini ya 2008, *contract* inasema huwezi ukafanya *snap check* kwenye migodi, lazima umwambie *investor*, yaani umpe ripoti ya awali kabla hujaenda hata kufanya *snap check*; *what is the control mechanism?*

Mheshimiwa Spika, ninachohoji ni kwamba, viwanja vya ndege vinavyokuwepo kwenye maeneo ya *mining* ni vya kufanya nini? Je, tuna Ofisi ya *TRA* pale? Tuna ofisi ya *Immigration* kwenye viwanja vya ndege? Kuna taarifa sahihi kwamba, ndege inaweza ikaruka kutoka *Gold Mine* ikaenda *direct* Nairobi; *what is the control mechanism?*

Je, Mheshimiwa Waziri unaweza ukaliambia Taifa kwamba kwa siku moja; kwa mfano, *Nyamongo Gold Mine* kule Tarime wanapata dhahabu kiasi gani? *What is is the*

control mechanism humu, yaani ni kwamba, taarifa unayopata Mheshimiwa Waziri unategemea taarifa wanayotoa wao kwa hisani yao, sisi hatuna control mechanismya kujuwa kwamba what is realy happening in daily basis?

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza sana, hata *audit* iliyofanyika kwa mara ya kwanza ya *Tanzania Mining (TMA)* mwaka 2010, yenewe pia imegundua kuwa kuna matatizo. Kwa mfano, kuna matatizo kwenye haya makampuni makubwa duniani kote, kuna *study na research* imesema kwamba, maeneo mengi wanadanganya. Sasa kama maeneo mengi wanadanganya na sisi hatuna *control system* ya kutosha na ndio maana hata hii *Audit* ya kwanza ya mwaka 2010, ilibaini kwamba, kuna maeneo mengi *wana-over estimate* mpaka *cost of operation* ili ije i-affect kama kuna kodi yoyote wanatakiwa walipe.

Sheria yenu mbovu ya *Mining Act* kuna sehemu inasema *they can actually carry unlimited loss forward*. Kwamba, mwaka huu wanaweza wakafanya kazi wakasema wamepata hasara, mwaka kesho wakipata faida ile hasara waliyoipata mwaka huu inakuwa *carried foward*. Kwa hiyo, *definetely Serikali bado haiwezi ikapata chochote*. Hiyo sheria mbovu ya *Mining Act*, 2008, pamoja na marekebisho yake yaliyofanyika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza zaidi ni kwamba, kama *Kabanga Nickel*, naambiya utafiti ulianza toka tunapata Uhuru mpaka leo; hivi sisi hatushtuki! Mtu anafanya utafiti kutoka Uhuru mpaka leo; anafanya utafiti gani kutoka Uhuru mpaka leo hatushtuki?

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie habari ya umeme. Juzi hapa nilimwuliza Mheshimiwa Waziri ndani ya Bunge, nikamwambia ni kweli kwamba, *TANESCO* wanachukua pesa za watu, fedha nyingi kweli, mtu anaenda ana-*apply* umeme analipa, anakaa mpaka miezi sita. Mwanza kuna kesi nyingi sana, Kata ya Mkolani, Bugarika, Ilemela, Maina, watu wamelipia umeme toka mwezi wa nane

mwaka jana, wengine wamelipia umeme toka mwaka jana mwezi wa kumi na mbili, hawajaunganishiwa mpaka leo. Siku ile niliwahoji hapa huu utaratibu wa *TANESCO*ukupa fedha kwa Wananchi na kufanya biashara utakoma lini?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mtu anaenda benki anakopa fedha au anaenda kwa mtu anachukua pesa ili aweke umeme aunganishe afanye biashara, labda aweke mashine asage arudishe pesa. Sasa kama mtu anakopa pesa anaenda ku-*apply* umeme *TANESCO*inachukua mpaka miezi sita hajafungiwa umeme; huu utaratibu ni upi?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri ilitueleza hapa wakati tunashughulikia tatizo la *TANESCO*, alituambia na katika Hotuba yake, ukurasa wa 29, nafikiri kuna sehemu ametoa takwimu ya bei ya nguzo ya umeme.

Mheshimiwa Waziri alituambia kwamba, watu wa *TANESCO* walikuwa wanachukua nguzo Iringa wanapeleka sijui Mombasa wanagonga muhuri wanarudisha inaonekana kama imetoka South Africa. Wakati kipindi hicho takwimu zako zinaonesha nguzo za Tanzania ni za gharama ya juu kuliko nguzo zinazotoka nje; je, ulilidanganya Bunge? Kwa sababu *logically* hajji akilini kama bei ya nguzo Tanzania ipo juu. Sasa mtu atachukuaje tena halafu hizo hizo ndiyo zisafirishwe zirudishwe tena kwamba zimetoka South Africa wakati *logically* takwimu zako na wewe unakiri kwamba nguzo za Tanzania zipo bei ya juu!

Mheshimiwa Spika, ningependa tupate tamko la Serikali kwamba, tabia ya *TANESCO* kuchukua fedha za Wananchi wanakaa nazo itakoma lini na wale Wananchi wa Mwanza walioomba umeme toka mwezi wa sita mwaka jana mpaka leo hawajapewa umeme wataunganishiwa lini? Siku hiyo, Naibu Waziri aliniambia kwamba, amepiga simu *TANESCO* Mwanza lakini mpaka leo hawajaunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, napenda nimweleze Waziri, akienda kama Marekani, ukinuya hata soda ukahudumiwa

25 MEI, 2013

kwenye baa, unalipa *tip ya ten percent* iko kwenye sheria. Sasa sisi tunashindwaje kuweka *serious policy* iwe sheria *in terms of percentage?* Hata siku ile tukiwa Pius Msekwa kuna Mbunge aliwashauri, kwa sababu ukiangalia hata hii Ripoti hawa jamaa wanasema, ukilinganisha mabilioni ya fedha ambazo haya makampuni yanapata kutoka kwenye machimbo yetu na ukilinganisha na vyoo wanavyokuja kujenga kwenye shule na mabwawa wanayotuchimbia ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante, muda umeisha. Sasa ninamwita Mheshimiwa Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga na wengine nitawataja baadaye.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo tunajadili Wizara ya Nishati na Madini, lakini kimsingi sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ambazo tulizitoa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Kwa hiyo, kwa dhati kabisa na kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea kama nchi, ni wajibu wetu sisi kuipitisha mipango ambayo tuliwaahidi Watanzania ili hatimaye kufikia malengo ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Bajeti umeeleza mambo mengi sana na ni jambo dhahiri kwamba, kwa mwendo huu tunaokwenda nao, mambo yanayosemwa katika Sekta ya Nishati na Madini ni dhahiri kwamba, mpango wa kuifanya nchi yetu iwe na uchumi wa katika ifikapo mwaka 2025 upo wazi kabisa. Ndiyo maana bila mashaka yoyote, naunga mkono hoja hii na bajeti hii na pia napenda niwatangazie Wanaseremba kwamba, katika mambo mazuri ambayo Wizara imeyasema hasa masuala ya umeme ambayo yamekuwa yakiipasua nchi kwa muda mrefu sana.

Wanasengerema wanafaidika na mambo mengi, vijiji vingi vitapata huduma ya umeme, wakiwemo Wananchi wa Kijiji cha Ibondo ambapo hivi karibuni tutakuwa tunafanya uchaguzi wa marudio kumpata Mheshimiwa Diwani.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati Wizara ya Nishati na Madini inawasilisha bajeti yake, lakini kabla ya hapo ilitanguliwa na Wizara ya Fedha, tulihabarishwa kwamba, hali ya Uchumi wa Tanzania na kwa kupindi kile kwa kuangalia kigezo cha mfumuko kwa bei, tulikuwa karibia asilimia 20, tulikuwa kwenye asilimia kumi na nane na pointi kadhaa kama siyo kumi na tisa ya asilimia ya mfumko wa bei. Tuliambiwa kwamba, mambo ambayo yalikuwa yamesababisha mfumko kwa kiwango kile ilikuwa kwanza bei ya chakula, lakini pia bei ama gharama za uzalishaji wa umeme. Sasa hivi tunavyoongea, kiwango cha mfumko wa bei kimeshuka hadi chini ya asilimia kumi, maana yake ni kwamba, Serikali ya CCM kama ilivyotuhidi mwaka jana, imetimiza wajibu wake kwa Watanzania kuualetea nafuu ya kimaisha kwa kuwapunguzia mfumko wa bei, kwa kuhakikisha kwamba mgawo wa umeme unadhibitiwa na hatimaye tunajonesha katika hali halisi ilivyo leo. (*Makofii*)

Kwa hili naipongeza sana Serikali na tunaona ukisoma Hotuba ya Waizri katika ukurasa wa 12, Serikali kwa dhati imeamua kutoa bilioni 402, ukijumlisha na mkopo ambao wameupata kutoka taasisi za kifedha wa zaidi ya bilioni ya mia moja ili kudhibiti mgawo wa umeme. Hili ni jambo jema, ni jambo ambalo tunatakiwa tuipongeze Serikali kwa maamuzi haya. Tumpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuliona hilo, kwa sababu mgawo wa umeme kama tungeendelea na juhudu zetu za kutolisaidia Shirika la Umeme *TANESCO*, kutoisaidia Wizara hii, leo maisha ya Watanzania yangetuwa katika hali mbaya sana. Ndiyo maana tunasimama hapa kifua mbele kwa dhati, kuipongeza Serikali kwa mipango hii ambayo imeiletta, kwa juhudu ambazo Serikali imechukua, masuala mengine tutayajadili baadaye. Bila juhudu hizo, leo Watanzania tungekuwa tunaumia sana na pengine hali isingekuwa hivi

25 MEI, 2013

kama tunavyoongea. Kwa hiyo, tunaipa mkono wa pongezi Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukihabarishwa na Serikali kuititia Wizara hii na hata Wizara zingine kwamba, mpango wa Serikali ifikapo mwaka 2015, wa kigezo cha uzalishaji wa umeme ni lazima tuwe na megawati zisizopungua 3000. Tunaona miradi iliyotajwa katika Hotuba ya Waziri inakidhi na kujibu utashi na matarajio ya Watanzania. Tuna sababu gani ya kutoiunga hoja hii mkono? Kwa sababu miradi ambayo inatekelezwa sasa ambayo utekelezaji wake umeanza miaka kadhaa, kwa hakika inatupeleka zaidi ya kuzalisha megawati 3000. Miradi ya usafirishaji imesemwa pamoja na usambazaji.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi ambayo yamefanyika katika Wizara hii, ambayo tunahitaji kuipongeza Serikali; mojawapo ya mambo ambayo yamefanywa vizuri sana na Wizara hii ni pamoja na kudhibiti biashara ya mafuta Tanzania. Kuititia Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati, (*EWURA*), tumeona utekelezaji wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja na hata lile zoezi la kuweka vinasaba, imeisaidia sana nchi yetu kupunguza kiwango cha uchakachuaji wa mafuta. Pia imewezesha Serikali kupata mapato na kupata takwimu sahihi kwa mapato ambayo vinginevyo ilikuwa ngumu sana na kulikuwa na mianya mingi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kuikosesa Serikali mapato. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukisoma Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuna mahali wanamtaja Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kinana, wakisema kwamba, kwa sababu wakati fulani alihuishwa kuwa mmojawapo wa Wakurugenzi wa kampuni iliyokuwa inaitwa *Artumas*, ambayo baadaye ilinunuliwa na Kampuni ya *Wentworth*, wanatumia kigezo hicho kuanza kujaribu kumpaka matope Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Mazoea haya ni jambo baya sana, tunahitaji kulikemea kwa dhati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo zipo taasisi ambazo

zinaongoza kuchangia mapato ya kodi kwa uchumi wa Taifa, ikiwemo Kampuni ya Bia Tanzania (*TBL*) na *Serengeti Breweries*. Makampuni haya mlongoni mwa Viongozi wake katika usimamizi wa taasisi hizi ni Watanzania. Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Cleopa David Msuya ni Mwenyekiti wa *TBL*, hapo inapokuwa imefikia hatua hiyo ujue kwamba Watanzania tumefikia hatua ya kujivunia, tunaaminika, makampuni yamesajiliwa katika masoko ya hisa za Dunia. Mpaka kufikia nafasi ya kuaminiwa katika kiwango hiki, siyo rahisi sana; kwa hiyo, najaribu kuwashauri wenzangu kwamba, tunapokuwa tunawataja hawa watu, tunawataje tu kwa sababu ya siasa zetu. Yapo maeneo ambayo tunaweza kwenda kuchakachua na kwenye maeneo ya majukwaa, lakini tunapokuwa katika jumba hili takatifu ambalo tunachangia baada ya kusoma dua na kumwomba Mungu kwamba atuongoze katika mjadala huu, ninatarajia kwamba, wenzangu pia wawe na umakini wa hali ya juu, kutojaribu kutumia jumba lako Tukufu kuwapaka matope Watendaji wa Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kinana kuwa mmojawapo wa Wajumbe wa Kampuni iliyokuwa inaitwa *Artumas* haikuwa dhambi, ndiyo maana leo tunajivunia ushiriki na imani ambayo makampuni ya nje yamewapa wazee wetu kama Mheshimiwa David Msuya na akina Mzee Bomani, Mzee Ufuluki kwenye Kampuni ya *Geita Gold Mine*, wapo wengi, akina Mzee Mengi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la hatari sana, kwa sababu siasa bila uchumi haiwezi kwenda. Mimi nina uzoefu wa kutosha, kauli zetu za kisasa zimekuwa zikichoma na zinaogopesha wawekezaji katika nchi hii hata wale wa ndani. Mwaka 2009, baada ya mitambo ya Dowans, Serikali kushindikana kuinunua tena kwa bei ya kutupa ya dola milioni 59.7, niliitisha kikao na Shirikisho la Wafanyakishara Tanzania (*CTI*), akina Mzee Mengi na akina Mzee Chande na Mzee Mosha, nikawashauri kwa sababu Serikali na *TANESCO* tumeshindwa kununua mtambo huu, ninaomba ninyi muunganishe nguvu zenu mwanzishe kampuni kubwa, mnunue mtambo huu kwa bei ya kutupa ambayo

ingetusaidia kuzalisha umeme. Walichoniambia Waziri wakati huo, hoja yako tunaiona lakini siasa zenu zinatutisha.

Mheshimiwa Spika, siasa kama hizi za kuwashambulia Watanzania ambao wanaaminawa, wanasimama na sisi inakuwa kigezo cha kujivunia, ni hatari kwa Taifa hili, ni lazima tuzikemee. Mtambo ule ule tuliookataa kununua Watanzania umenunuliwa na Wamarekani kwa zaidi ya dola milioni mia moja. Tumeutumia mtambo ule, umetusaidia kupunguza mgawo wa umeme, tunautumia kwa muda mrefu na tunalipa *capacity charge*. Ingekuwa ni Watanzania wamenunua bila kutishwa na kauli kama hizi, leo Watanzania tungekuwa tunanufaika sana. Haya ni mambo ya hatari. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tunapita katika hali ngumu, tupo kwenye *trial moment*, ninawaomba Watanzania, Wadau wote na hasa Viongozi wa makundi yenye ushawishi mkubwa wakiwemo Viongozi wa Dini tushirikiane. Mambo haya makubwa ambayo Taifa tunayafanya sasa ndiyo msingi wa kutuondoa katika umaskini ambao Taifa letu limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu. Naomba Viongozi wote wa Dini na Viongozi wa Kisasia, tushirikiane kusaidiana na juhudzi za Serikali kutekeleza mipango ambayo itatutoa hapa na kutusogeza hatua mbele zaidi. Sisi kama Taifa, tuache tofauti zetu za kidini na za kisiasa na hata tofauti za kimitazamo, kwa sababu mambo yaliyotajwa katika Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ni kielelezo tosha cha dhamira ya kweli ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi; kututoa hapa tulipo na kutusogeza hatua nyiningine.

Ninaomba sana Watanzania watuelewe, tunapokuwa hapa sisi kama Chama Tawala, tunatekeleza wajibu wetu, lakini nao kwa sababu baada ya Uchaguzi Mkuu uliopita na ndivyo inavyokuwa katika nchi inayoongozwa na demokrasia, wenzetu wana dhamira ya dhati ya kutung'oa madarakani, siyo kwa risasi lakini kwa sababu ya mabishano na kujaribu kutudhoofisha kwa kadiri watakavyoweza. Kwa hiyo, Watanzania wafahamu kwamba, zipo kauli zinatolewa hapa lengo ni sisi kung'olewa madarakani.

Ndiyo maana tunaposimama hapa tunaunga mkono mipango ya Serikali yetu kwa sababu ndiyo iliyotuaminisha kwa Watanzania wakatuchagua kwenye uchaguzi uliopita. Tutaendelea kuwaambia Watanzania kwamba sisi tunasimamia uchumi na maendeleo ya Taifa hili. (*Makof!*)

Hatutaogopa kusema ukweli kwa sababu Taifa hili ni la kwetu sote. Lakini na nyinyi mtaendelea na kazi yenu kwa kadri mtakavyoona fursa ambazo zinawezekana, mtasema, lakini nasi tutajibu mapigo kwa nia ya kujenga Taifa letu kwa sababu hili ndilo Taifa ambalo Watanzania tunajivunia. Usione Mataifa makubwa yanakuja hapa kushirikiana na sisi, ni kwa sababu tuna rasilimali, tunaaminika na tuna uwezo wa kuwa na *impact* katika dunia ya leo. Lakini kwa siasa ambazo zinasemwa, hatuwezi kufika huko. Chama cha Mapinduzi tutasimama imara. Twendeni tukashindane kwenye siasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukawaambie, barabara zinajengwa, mgao unadhibitiwa, miradi ya umeme inasambazwa na inaongezewa fedha. Mtakayokuanayo, myaseme pembedi... (*Makof! Kicheko*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Muda umekwisha. Namwita Lucy T. Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Mteketa.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa, nianze kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyozungumza hapo awali, nianze kwa kuipongeza Wizara hii. Nampongeza sana Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Prof. Mhongo pamoja na Katibu Mkuu - Bwana Aliakim Maswi pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara

hii. Kazi mnayoifanya ni kubwa sana, endeleeni na kazi hii, mmeisafisha Wizara kwa kiwango cha juu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda tu mimi ni-*declare interest* kwamba mimi ni mmoja kati ya waumini ambao ninaamini katika *principal* ya Kimarekani ya *fire and hire*. Mtu kama hatekelezaji wajibu wake lazima aondoke! Watendaji, kama ni Wahasibu wa Wizara hii, kama ni watu ambao wanafanya kazi katika Wizara hii ambao wanaonekana kwamba wahafai, ambao wanaonekana kwamba wanaihujumu nchi yetu wanatakiwa waondoke, waingie wengine wapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umeme ni uchumi. Nchi yetu tuko katika matatizo ya aina mbalimbali. Lakini kitu pekee ambacho kitatusaidia kuweza kukabiliana na hali hii ya matatizo mbalimbali ya kiuchumi ambayo tunakabiliana nayo ni suala moja kubwa sana nalo ni upatikanaji wa umeme katika maeneo ya vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kuhusu upatikanaji wa umeme vijijini. Niungane tu pamoja na wenzangu tangu majadiliano haya yameanza kuhusu kutoa pesa *REA*. Lakini labda tu nimsaidie Mheshimiwa Waziri; sisi tunalalamika *REA* ipewe pesa, naye hana budi kutafuta *support* ya kwetu sisi ili tumuunge mkono. Serikali kwa ujumla wake iweze kuangalia uwezekano wa kupata pesa. Lakini ye ye lengo analo. Cha msingi tu, tuangalie pesa hii tutaipata kutoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu, imeonekana umeme uki-*stabilize*, *inflation* inashuka. Mwaka 2012 kuanzia Septemba mpaka Desemba na mpaka Februari mwaka huu *inflation* ilifika kiwango cha asilimia 19.3, *almost* asilimia 20. Lakini baadaye kuanzia Aprili mwaka huu mpaka hivi sasa imeshuka imefikia asilimia tisa. Ni kiwango ambacho inaonesha kwamba umeme ukifika vijijini, hali za maisha yetu na hali ya Tanzania na uchumi wetu itaboreka kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili, *REA* wamepewa Shilingi bilioni 150, wanahitaji Shilingi bilioni 881 kutekeleza miradi katika kipindi cha miaka miwilli kukamilisha miradi yao. Lakini kwa kipindi cha mwaka huu mmoja wanahitaji Shilingi bilioni 450.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge, ni lazima tuangalie njia za kuweza kuhakikisha Serikali inapata pesa ili *REA* iweze kuongezewa pesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mahitaji katika maeneo ya vijijini yanaongezeka. Kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu kwa mwaka 2012/2013 mahitaji yalikuwa ni *Megawatts 851.35*. Lakini mwaka 2011 ilikuwa ni *Megawatts 820*, hii ni kutokana na maendeleo ya miradi mingi vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niko hapa na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Hamoud - Mbunge wa Kibaha Vijijini. Yeye alikuwa ananiambia hapa kwamba miradi kule kwake Chalinze, Magindu na Lukenge, mradi umeanza kuanzia mwaka 2009 lakini mpaka sasa hivi haujakamilika. Hii miradi ambayo imeshaanza huko vijijini ikamilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini *solution*, mimi ambalo nalionia katika hili, ni lazima tuwe na utaratibu wa kuangalia Serikali inasimamiaje mapato yake, lazima sasa ufile wakati wa kutokuoneana aibu, lazima sasa ufile wakati wa kuwajibishana kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Obama anakuja Tanzania. Hii kwanza inaonesha kwamba Taifa letu linathaminiwa, linaheshimiwa na bado Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali ambayo bado hata haya Mataifa makubwa, bado yana imani na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata kwa wale ambao wanaanza kujipa labda matumaini na zile ndoto za mchana kwamba labda tunaondoka mwaka 2015 wasahau. Kwa sababu haya Mataifa makubwa, kiongozi mkubwa kama

Obama hawesi kuja kwenye Taifa ambalo anajua kwamba Rais wa hii nchi anaondoka baada ya miaka miwili au Serikali ya hii nchi inaondoka baada ya miaka miwili ijayo. Kwa hiyo, nawaombeni tu msahau, kwa kifupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara hii kwa *launch* ile ya *round four* ya utafutaji wa gesi. Hii ni hatua ya msingi sana kwa sababu kwa kipindi kirefu sana *launching* hizi zimekuwa zikifanywa Houston na London. Kwa hiyo, kwa kufanyika hapa Tanzania, tunatangaza Taifa letu. Lakini napenda kuwaambia wenzangu kwamba haya maneno mengine ambayo yanasemwa na baadhi yetu sisi Wabunge na hasa hawa wenzetu wa upande wa pili, haya mambo ya kusema hii *launching* ikifanyika, utafutaji huu ukifanyika, basi na vibali vinatoka hapo hapo, siyo kweli. Utafiti huu unafanyika mpaka kukamilika ni miaka 10 au 11. Sasa kama inachukua miaka 11 mpaka kuja kukamillka, yasipoanza sasa hivi, itakuwa ni muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, sisi kama Wabunge, tusione haya majukwa na hizi *microphone*, basi tunakaa tunafurahia tu, ukiona hivi na haya makofi yanazidi kuwa mengi na nini, tujue kabisa kwamba baadhi ya maneno ambayo tunayasema tunapotosha Watanzania wenzetu. *Launching* hii ikishafanyika, baada ya miaka 11 ndiyo masuala ya vibali yaanza kufanyika. Hii *Serikali* siyo kwamba ni Serikali ambayo imelala tu, kwamba mambo yatakuwa yanafanyika kiholela holela tu, siyo namna hiyo. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuipongiza Serikali, kwamba kwa kufanya hivi tumetangaza Taifa letu kwa kiwango cha juu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine, nayo ni taarifa iliyopo katika nchi yetu kuhusu upotevu mkubwa sana wa madini katika nchi yetu. Upotevu wa rasilimali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sana ambalo mimi nalionia katika nchi yetu. Nalo ni kutokuwepo na

Ministerial Inter-connection katika nchi yetu. Kwa nini nasema namna hiyo? Tunapokaa tunasema kwamba Wizara fulani, kwa mfano, Wizara ya Nishati na Madini, inasimamia nishati, inasimamia madini. Lazima Serikali yote kwa ujumla wake, tujipange na tuangaliane: Je, tuko pamoja? Kwa sababu tusipoangalia, tunaweza kujikuta tunakaa; Wizara moja inakuwa iko *strict* inasimamia *principals* kwamba sisi tumesema hatutaki madini yasafirishwe nje kwa wizi. Lakini kuna watu wengine ambao wanawajibika na masuala hayo ya usimamizi, *let us say* Polisi, au watu wengine wa *TRA*. Wale watu wasipotekeleza wajibu wao hatuwezi kufika pale ambapo tunapataka.

Nitolee mfano, tarehe 8 Desemba, 2012 Bwana Fung Jung, huyu ni Mchina; alikuwa anapita katika kiwanja cha ndege cha *KIA* akiwa na madini ya *Tanzanite*, madini ya vito yenye thamani kubwa sana. Wizara ya Nishati na Madini *TMAA* wakamkamata yule mtu. Baada ya kumkamata yule mtu, wakamkabidhi Polisi pamoja na watu wa *TRA*, watu wa Forodha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumfikisha kule, hiyo nilikuwa ni tarehe 8 Desemba, 2012. Baada ya siku hiyo kumkabidhi kule; akaa, aka-*lobby*, akaongea na Polisi na alikamatwa na mtu mmoja anaitwa Tumaini Makwesa pale *KIA*. Baada ya kumaliza pale, siku iliyofuata yule mtu ambaye alikuwa na Hati namba G24938191 alitoroka kupitia kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam. Ina maana kwamba aliachiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara hii, ninaomba Wizara ya Mambo ya Ndani na kama siyo leo nitawenza kusikika kwa leo, nitakuja kurudia siku nyingine. Naomba watu wote waliohusika na kumwachia Mchina huyu ambaye alikuwa anasafirisha madini, ambayo yalikuwa yana thamani kubwa sana ya *billions of money* kuachiwa na badala yake, yule Bwana Tumaini Makwesa anaendelea kusumbuliwa.

Naomba huyu mtu asiondoke pale! Kwa sababu anaonekana kwamba huyu mtu ni mzalendo, tuko naye,

anaumia na tatizo hili la utoroshwaji wa madini katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizopo katika nchi yetu, tani 20 za dhahabu katika nchi yetu ambazo zinazalishwa, ni tani mbili tu ndiyo zinapita katika mkondo rasmi ambaou unafaa. Tani 18 zinapotea tu kiholela, Tunaibiwa pesa nydingi sana! Pesa nydingi sana zinapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Abdul Mteketa, atafuatiliwa na Mheshimiwa Lolencia Bukwimba, halafu nitaendelea tena. (*Makofi*)

MHE. ABDUL R. MTEKETA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusema "Shika Neno, Tenda Neno." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Pili, napenda kuipongeza sana Wizara, Waziri na hasa Naibu Waziri Mheshimiwa Simbachawene ambaye anakuwa msikifu na mchapakazi na mwadilifupi. Kitu ambacho nataka kusema ni kwamba Tanzania yetu ina utulivu mkubwa sana, na Tanzania yetu inasifikasi kote. Lakini leo hii Tanzania inataka kuharibika.

Mheshimiwa Spika, toka zamani Tanzania, watu wote ni waungwana. Chakula chetu tukipata, tuna-share, tunakula pamoja. Leo hii tunaonekana Watanzania tunaanza kuwa wachoyo kwa kusema hiki change, hiki chako. Hicho kitu tunaomba tukifute kabisa! Kuna watu wanakaa wanankuu kauli ya Baba wa Taifa, wakisema Baba wa Taifa amesema hivi, amesema hivi. Lakini ni hao hao wanakwenda kinyume, wanawachonganisha watu, wanaanza kuleta fujo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kabisa watu wa namna hiyo wasitumie jina la Baba wa Taifa kuharibu jina

lake bure. Kwa sababu Baba wa Taifa hajasema hata siku moja tugombane au tutengane. Wote tuwe kitu kimoja. Naomba kabisa hicho kitu kiachwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili mimi nataka kujikita hasa katika Jimbo langu. Kwanza, napenda sana kuipongeza Wizara katika miradi ya umeme ambayo miradi itakayotekelawa kwa ruzuku kutoka Mfuko wa Nishati Vijijini mwaka huu na mwaka kesho 2014 ambapo katika Wilaya ya Kilombero nimepata Chita, Ikule, Mkangawago, Mchombe, Njage, Idete, Mofu, Namawala, Mbingu, Mgeta, Gereza la Idete na Kisawasawa. Nawapongeza sana kwa kunisaidia kwa sababu sisi kwanza katika Jimbo la Kilombero tuna gridi mbili za umeme na sisi miaka yote tunalinda tu nguzo kutoka Kihansi mpaka kuja Kidatu. Tunalinda tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba kwamba mlivyotuangalia, tunawashukuruni sana na tunawapa hongera nyingi kwamba Kilombero mmeikumbuka na mtekeleze, siyo kwamba imeandikwa tu isitekelezwe. (*Makofi*)

Vile vile tuna tatizo kubwa sana Ifakara. Niliongea na Mheshimiwa Waziri, kwamba Ifakara kila wakati umeme unazimika. Ukizimika, ikija mvua kidogo, umeme umezimika. Ukija upepo, umeme unazimika na ukizimika unachukua wiki moja au wiki mbili au siku tano. Sasa hatuelewi sababu ni nini hasa. Tunaomba sana, Meneja wa kule tunaongea naye lakini majibu yake hayaturidhishi. Tunaomba Wizara iangalie kwa nini Mji wa Kilombero umeme kila saa unazimika. Umeme ni kitu cha maana sana katika jamii, na sisi kwetu kule kuna malori mengi ambayo inabeba mizigo kutoka Mbingu kuleta Ifakara. Zinakatatika *spring*; zikikatika *spring* wakitaka kwenda kuunga umeme hakuna kwa siku tatu au siku nne. Hiyo ni dhahama kubwa sana ambayo tunaipata. Tunaomba kabisa Wizara iangalie suala hilo kwamba sisi tunapata taabu Kilombero hasa Ifakara umeme hakuna, hakuna hakuna!

Mheshimiwa Spika, wawekezaji pale ni wengi, kuna watu wana mashine za kusaga, watu wana maduka ya *stationery* na vitu vingine vingi. Vile vile kama mlivyopanga

kuweka umeme Mbingu, Mbingu tunashukuru sana, umeme uje haraka kwa sababu kuna matunda mengi sana. Watu wanaweza kuweka mashine ya *processing* wakatengeneza kila aina ya matunda katika makopo na katika vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema, ila nataka kutoa shukrani sana kwa Wizara kwa kunikumbuka na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante kwa kuniazima muda. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Rweikiza.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Wizara hii ni muhimu sana kwangu hasa kwa wananchi wa Jimbo la Busanda na Geita kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusikiliza kilio cha wananchi wa Geita kwa upande wa fidia ambao wamechukuliwa maeneo yao na GGMna vile vile kwa hatua ambayo Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aliyofikia. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, ahadi yake ya kwamba baada ya Bunge atatembelea Geita ili kuweza kusuluhiha migogoro hii na kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wa Geita wanalipwa fidia zao. Namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba anatimiza ahadi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nianze na mambo ya madini. Kama jinsi ambavyo nimesema, mimi ni mdau mkubwa sana katika shughuli za madini. Katika Mkoa wetu wa Geita kwa kweli Mungu ametubariki kama ambavyo huwa nasema kwamba tunayo madini ya kutosha ya dhahabu, na tuna wachimbaji wadogo wadogo ambao wanajishughulisha na shughuli za uchimbaji. Uchumi wa Mkoa ule unainuliwa zaidi na shughuli za uchimbaji wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wa madini wanazo changamoto nyingi sana. Cha kwanza, hawana mitaji, lakini

vile vile hawana elimu ya kutosha kuhusiana na namna nzuri ya kuchimba madini haya. Kwa hiyo, naomba tu kwamba kwa vile katika Sera ya Taifa ya mwaka 2009 ya Madini imesema wazi kabisa kwamba Serikali ni wajibu wake kuhakikisha kwamba inawezesha wananchi wake kuchimba madini haya na kuweza kunufaika vizuri zaidi, kwa hiyo, naomba Serikali kwamba Sera hii itafasiriwe sasa ili wananchi waweze kunufaika na sera hii ya Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu katika suala la madini, wananchi wetu wanahitaji mitaji kama jinsi ambavyo wakulima kwa mfano katika upande wa Kusini kuna hii *SAGCOT* ambayo inawawezesha wakulima, wanapewa ruzuku. Kwa hiyo, hata katika madini vile vile naomba Serikali iwekeze kwa wachimbaji wadogo. Maana wachimbaji wadogo wakiwezesha, nina hakika kwamba kipato chao kitaweza kuongezeka na hivyo kuweza kuchangia katika pato la Taifa letu, na hapo tutaweza kufikia malengo ya milenia. Kwa sababu hatuwezi kufikia malengo ya millennia pale ambapo tunawaacha wananchi wetu wakishindwa kunufaika kutokana na raslimali zao ambazo Mungu amewajalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwamba, Serikali kwa hatua ya kutoa maeneo kwa ajili ya kuwawezesha, tayari imekwishatoa maeneo katika baadhi ya maeneo kule kama Rwanagasa. Lakini vile vile nimeona katika ramani ambayo ametupa Mheshimiwa Waziri, ramani ile imeonesha pia hata Nyarugusu ni eneo limetengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Naomba sasa Serikali ihakikishe wananchi hawa wanapewa hilo eneo, maana kimekuwa ni kilio chao cha muda mrefu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kule Kaseme, Sobora, ni eneo ambalo ni muhimu, wananchi wanahitaji wapewe maeneo hayo waweze kunufaika kwa ajili ya uchimbaji madini. Vikundi vingi sana vya uchimbaji wa madini vimejunga katika eneo la Jimbo la Busanda na ni vikundi kama 100 hivi vyenye watu zaidi ya 1,000. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kweli iwekeze kwa wananchi hawa, ili kuweza

kupata ajira. Watu wengi wataweza kujajiri kutokana na shughuli hizi za uchimbaji wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika suala hilo hilo la madini, ni vyema sasa Serikali ikaanzisha kuweza kuwawezesha wachimbaji wadogo kuweza kuongeza thamani ya madini kwa sababu, bila ya kuongeza thamani ya madini, haiwezekani kabisa kupata faida kutokana na shughuli za uchimbaji.

Kwa hiyo, Serikali, iwawezeshe wananchi hawa, ianzishe Vituo kwa ajili ya uongezaji wa thamani, iweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji hawa, ili madini wanayoyapata waweze kuyaongeza thamani. Kama ni hereni za dhahabu, watu wavutiwe basi hata kuja Geita; kuwepo na kituo maalum kwa ajili ya kuuzia madini haya, ili wananchi waweze kufaidika; na mikufu mizuri mizuri kwa ajili ya akina mama. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie namna ya kuwawezesha wananchi hawa kuongeza thamani ya madini, hasa katika Mkoa wa Geita, ambako ndiko ni Mji wa dhahabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie pia masuala ya huduma katika maeneo haya. Wote tunatambua kwamba maeneo ya uchimbaji wa madini kuna *population* kubwa sana. Watu wengi wanavutiwa na shughuli za uchimbaji wa madini. Kwa hiyo, unakuta kwamba, huduma za kijamii ambazo Serikali inatoa, zinakuwa hazitoshi. Kwa mfano, pale Nyarugusu, kuna watu wengi sana, kwa hiyo basi, wanahitaji huduma za jamii. Haiwezekani mkapeleka dawa sawasawa na Kijiji kingine.

Kwa hiyo, naomba tu kwamba Serikali iangalie sehemu hizi za madini kwamba, iweze kuongeza huduma kulingana na idadi ya watu. Kwa mfano, huduma za afya, vilevile barabara, kwa sababu magari yanapita kwa wingi sana na uzito mkubwa. Serikali, ikijenga barabara baada ya muda mfupi inaharibika. Kwa hiyo, naomba tu kweli Serikali ituangalie zaidi katika maeneo kama haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halafu sambamba na hilo, miaka miwili iliyopita *GGM* walikuwa wameanza kufanya utafiti kuhusiana na barabara ya kutoka Geita kwenda Kakora kwa ajili ya kuiwekeea lami.

Kwa hiyo, ningependa kujua kwamba wamefikia hatua gani kuweza kujenga lami barabara hii, barabara ya Geita kupitia Bukoli kwenda Kahama. Naomba kwa kweli watu wa mgodini waweze kujitahidi kuiwekeea lami barabara hii maana magari yanapita kwa wingi, yanaleta vumbi kubwa na kuleta athari kwa wananchi walioko kandokando ya barabara hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna baadhi ya sehemu ambazo zimepitiwa na bomba la maji la *GGM*. Kwa mfano, Kijiji kile cha Chigunga kule Salagurwa, kwa kweli, bomba linapita pale, lakini wananchi wale hawana maji. Kwa hiyo, naionomba Serikali pia iangalie uwezekano mzuri wa kuwasaidia wananchi ambao wanaishi karibu na rasilimali hizi ambazo watu wa *GGM* wanatumia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umeme, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali, kama jinsi ambavyo tunasema kwamba, unapofanyiwa mambo mazuri ni vizuri ukashukuru. Kwa hiyo, mimi nashukuru sana kwa umeme wa *MCC*, japokuwa bado haujawaka, lakini wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri, alinaihidi kwamba kufikia Septemba, wananchi wataanza kufaidika na umeme huu kwa sababu, utakuwa umewaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu umeme huu ni muhimu sana kwa ajili ya uchumi wetu, hasa katika Wilaya ya Geita na Mkoa Mpya wa Geita, naionomba Serikali kwamba umeme huu unapopita katika maeneo ya Kijiji fulani penye Shule za Sekondari zote, Serikali ihakikishe inaweka umeme huu katika Vituo vyote vya Afya. Kwa mfano, pale Bukoli, Kituo cha Afya Bukoli kiwekewe umeme, Shule ya Sekondari Bukoli iwekewe umeme, vilevile Shule ya Sekondari ya Rwamgasa iwekewe umeme, Kituo cha Afya cha Genge Kumi pia kiwekewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna baadhi ya sehemu muhimu kabisa ambapo kuna huduma ambazo zinatolewa kwa ajili ya wananchi wengi, kwa mfano, Gereza ille la Butundwe. Ninashukuru kwamba Serikali katika bajeti ya mwaka huu kupitia umeme wa REA, tayari imeweka bajeti. Nilikuwa naomba utekelezaji ili wananchi waweze kunufaika na huduma hii ya umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema tu kwamba pale Katoro, kwa mfano shule ya Sekondari ya Katoro, haina nguzo za kwa ajili ya kuwekewa umeme. Naiomba tu Serikali ihakikishe shule hii ya Sekondari wapate huduma ya umeme.

Vilevile kuna biashara pale, kuna shughuli ndogo ndogo, viwanda vidogo vidogo vya kukoboa mpunga pale Katoro, pamoja na pale kona ya kuelekea Nyamigota, naiomba Serikali ihakikishe kwamba wananchi hawa wote wanapata umeme wa kutosha ili tuanze kunufaika sasa na umeme huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwaombe watu mbalimbali, wawekezaji, waje Geita sasa kuwekeza maana tunapata umeme wa uhakika. Ni umeme wa Gridi ya Taifa na tunajivunia kwamba, kuanzia mwezi wa Tisa, nina uhakika kwamba, sasa wawekezaji tunawakaribisha waje kuwekeza katika Mkoa Mpya wa Geita, maana tutakuwa na umeme wa uhakika kabisa wa Gridi ya Taifa.

Halafu, vilevile kule tuna matunda. Kwa hiyo, niwaombe tu kwa kweli, mje mwekeze katika viwanda mbalimbali vya matunda ili kuwawezesha wananchi wa Geita kupata ajira ndogo ndogo kwa maana hakika Serikali imetuona katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, napenda kusema kwamba, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja, nikiamini kwamba Serikali, sasa inakwenda kuyafanya kazi haya yote ambayo nimeyazungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mbassa.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami niseme kwamba, naunga mkono Hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapa pole wananchi wa Bukoba ambao hivi karibuni walikumbwa na maafa ya mvua kali na upepo mkali na kupoteza mazao mengisana na nyumba zaidi ya 200 zimeporomoka na mvua, na mtoto mmoja kule Kasule Kata ya Kisogo amefariki kutokana na mafuriko hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye umeme na hasa Umeme Vijijiini. Nitumie nafasi hii kuishukuru sana Wizara na hasa Wakala wa Umeme Vijijiini, (*REA*). Namshukuru Dkt. Mwakalesa na timu yake kwa kazi nzuri anayoifanya. Anafanya kazi nzuri sana kupeleka umeme vijijiini, sehemu nyingi za vijijiini zimepata umeme, na hii ni kazi nzuri ya Serikali ya *CCM*, hasa kuititia *REA*. Lakini hawa watu wanafanya kazi kwa mafanikio makubwa, lakini kwa mazingira magumu; Hawana pesa za kutosha. Wanapeleka umeme wakiwa hawana hela ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwamba siku anawasilisha Bajeti yake alisema kuna watu ambao hawakutoa hata senti tano, lakini wanajitapa kwamba wao ndio wamepeleka umeme Vijijiini. Hali hii iko Bukoba. Kule Bukoba tuna mradi mmoja mkubwa uliokamilika wa *Ikimba Area*, unakuta umeme unawaka vijiji zaidi ya 50. Kuna mtu kule anasema ye ye ndio amepeleka umeme, kwamba ye ye kwa fedha zake ndio amepeleka umeme kule. Anasema kwamba ye ye amepeleka umeme kwa fedha zake, na siyo Serikali.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba, kuna watu wa namna hiyo, na kwamba ule mpango aliousema wa kupeleka Mawaziri, Naibu Waziri, kwenda kufungua miradi hii, aanzie Bukoba, ili wawaeleze wananchi kwamba ni kazi ya Serikali ya CCM, siyo kazi ya mtu binafsi yule anayejitapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye mradi huo kuna sehemu chache zimerukwa, kama pale Ilanga, pale Kaibanja, kuna sehemu pale Katoma; juu kuna waya za umeme, chini watu hawana umeme. Sasa naomba jitihada ziongezeke kusudi wapate umeme. Pale Bujugo, Kata nzima imezungukwa; baada ya mradi huu kukamilika, kote kuna umeme. Mashariki kuna umeme, Kaskazini kuna umeme, Kusini, kila mahali kuna umeme isipokuwa Kata hii imerukwa, imekuwa kama kisiwa na yenye we iangaliwe ipewe umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye orodha tuliyopewa hapa, kuna vijiji vingi ambavyo vimeorodheshwa hapa vya Bukoba Vijiji ambavyo vitapata umeme, naomba nivisome. Vijiji vya Bugabo, Kagabiro, Buhendagabo, Kagya, Kishanje, Rubifu, Ibosa, Mwizi, Izimbya, Kyaitoke, Kasikizi, Ibwero, Mugajwale, Makongola, Kanyabuguru, Kanyabuhoro, Kitoro, Kalego, Nyakaka, Kyampisi na Kangabusaro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni jitihada nzuri lakini nina wasiwaso, kwa sababu najua kwamba, *REA* hawana pesa za kutosha. Miradi ambayo iko *REA* inasubiri kutekelezwa inahitaji Shilingi bilioni 881, hela walijonayo mwaka huu kwenye Bajeti kwenye Book hili kubwa, ni Shilingi bilioni 150, haifiki hata robo; ni hela ndogo sana. Kwa hiyo, nina wasiwaso kwamba hata miradi hii huenda isitekelezwe kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nina pendekezo ambalo nataka nilitoe. Nawashukuru Wizara walishafanya ubunifu mwaka 2011 na mwaka 2012 na *REA*. Wakaja na pendekezo kwamba kwenye simu za mkononi kuwe na tozo ya Sh. 4/= kwa dakika. Hela hii iende *REA*, ipeleke umeme vijiji. Wakati huo ilikuwa Sh. 4/= kwa dakika, wakati kupiga simu kwa dakika

moja ilikuwa ni Sh. 150/= mpaka Sh. 200/. Gharama ilikuwa kubwa, wakapendekeza Sh. 4/= tu kwa dakika. Leo simu zimeshuka bei baada ya kuingia kwenye Mkongo wa Taifa, ni Sh. 30/= mpaka Sh. 40/= kwa dakika. Kwa hiyo, naomba hii Sh. 4/= ianze mara moja, iingie kwenye simu za mkononi, tozo hii ianze ili pesa hii ipatikane iende *REA* isaidie kupeleka umeme vijiji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012 kama mradi huu ungeanza, *REA* ingepata Shilingi bilioni 123. Zingesaidia sana kupunguza pengo la pesa na kupeleka umeme vijiji. Lakini nasikia kwamba Wizara ya Mawasiliano inazuia mpango huu usitekelezeke. Sasa sijui kama ni kweli! Naomba Mheshimiwa Waziri aeleze, kwa nini mpango huu hauanz? Leo gharama ya simu imeshuka kutoka Sh. 150/= mpaka Sh. 200/= kwa dakika hadi Sh. 30/. Kwa hiyo, hata wananchi hawatasikia uchungu kama itaongezwa kwenye simu hii Sh. 4/= au Sh. 5/=, hata ikiwa Sh. 10/=, itakuwa nafuu sana kupata umeme vijiji. Huu ni mpango mzuri ambao utasaidia vijiji kupata umeme. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, bila umeme huwezi kufanya kazi na simu, na minara ile inatumia umeme. Simu hizi huwezi kutumia bila kuzi-charge na umeme. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linategemeana. Napendekeza kwamba, mpango huu uanze, Sh. 4/= zitozwe au Sh. 5/= au hata Sh. 10/= kwenye kila dakika ili *REA* ipate pesa ya kutengeneza miradi yake iliyonayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hivi leo *TANROAD* inatoza Sh. 250/= kwa lita ya mafuta, dizeli na petroli, Sh. 250/= tu! Si unaona kazi wanayofanya! Nchi nzima wanajenga barabara za lami, Mikoa inaunganika kwa Sh. 250/= tu kwa lita moja. Wameomba waongezewe Sh. 150/= ziwe Sh. 400/=, mimi nasema hapana. Isiende Sh. 150/= kule, iende *REA* angalau Sh. 100/=, iongezwe *REA*, ndani ya mwaka mmoja mpaka miwili, itapatikana Shilingi bilioni 800 na miradi hii itakamilika. Tutapata umeme vijiji na miradi mingi itaweza kukamilishwa na vijiji vitapata umeme. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni huo. Nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mbassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Maige na Mheshimiwa Lembeli ajiandae.

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia hoja iilyoko mbele yetu. Labda kabla sijaanza mchango wangu naomba nieleze machache. Ni kweli kabisa kazi yetu kama Wabunge ni kuisimamia Serikali na kuishauri pale inapowezekana na kuweza kueleza yale mabovu ambayo yanajitokeza, ili kusudi tuondokane na hali ambayo ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, tunapoeleza mambo ya ujisadi Kambi ya Upinzani, siyo kwamba tunakuwa tunayafurahia, hapana. Tunataka yakomeshwe na yasirudiwe. Lakini imekuwa wazo kwamba kila tukiongea kitu, inaonekana tunarudia kitu kile kile. Tunaeleza ukweli uliopo na namshukuru Mheshimiwa Lucy kwa yale aliyoysesema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kumekuwa na kauli kwamba, sisi tuna-*quote* kauli za Baba wa Taifa; ni kweli kabisa kama tungezifuata kauli za Baba huyu, Taifa hili lisingekuwa mahali hapa hata siku moja. Sasa kwa anayetenda mazuri lazima tumsifie na kwa aliyetenda mabaya, lazima tueleze ili kusudi tuondokane na uchafu huu unaoendelea katika nchi yetu. Ni kweli, Baba wa Taifa, alikuwa mwadilifu na ndio maana katika shughuli zake zote hakuwahi kuvaa sare ya Chama chochote, lakini watu wanaovaa sare, ndio hao wanaoturudisha nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nirudi nichangie sasa yaliyoko Jimboni kwangu. Jimbo langu la Biharamulo Magharibi, ni kati ya sehemu ambako tatizo la umeme ni kubwa sana. Kilio chetu kimekuwa cha muda mrefu na tumekuwa tukilieleza hili mara kwa mara, lakini ni kutokana na sababu kwamba, tuna *generator* mbili ambazo zimechoka, tunazitumia *generator* hizi pamoja na wenzetu wa Chato, kwa ndugu

yangu Mheshimiwa Dkt. Pombe John Magufuli, ambapo sasa umeme wa mgawo umekuwa ni jambo la kuzoeleka.

Mheshimiwa Spika, lakini inasikitisha kwamba juzi kati hapa, Naibu Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Simbachawene akijibu maswali, alisema kuna *generatos zinateremshwa* Biharamulo na Ngara. Kwa kweli nilisikitika sana, jambo ambalo siyo kweli; lakini nilifikiri labda ulikuwa ni mpango huu ambao umeelezwa katika kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 10 kwamba kuna mashine tatu ambazo zinakuja kwa ajili ya Biharamulo, Mpanda na Ngara.

Mheshimiwa Spika, umeme ni kila kitu. Leo hii uzalishaji wetu ungekuwa juu sana, vijana wengi wangejajiri, lakini kama hawana nishati ya umeme hawawezi kufanya lolote lile. Ni wazi kabisa kwamba watu walioko pembezoni wanaweza kusema wameachwa kwa sababu, gridi ya Taifa haipiti kule. Sasa juhudhi hizi zinapofanyika, zifanyike ikijulikana kwamba watu wanahitaji umeme na wanahitaji umeme wa kweli na siyo mambo mengine. Naomba mradi huu ambao wanasema upembusi yakinifu umeshafanyika, utekelezaji wake ndiyo bado haujafanyika; utekelezaji wake unaotajwa katika mwaka huu 2013/2014 tunaomba tupate japo maeneo ya jumla, lakini tupate *time frame*, unaanza lini na unakamilika lini? Watu wa Biharamulo wanahitaji umeme na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na miradi mingi ambayo imekuwa ikitajwa ya umeme. Kwa mfano, kuna mradi nilishawahi kuusikia wa Masaka kupitia Karagwe kwenda mpaka Rusumo, uunganishwe na umeme wa maji ambao ulikuwa unapaswa uanzie pale Rusumo kuja mpaka pale Nyakanazi. Lakini katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake nimejaribu kupitia, wala sioni sehemu yoyote hata ambako suala hili linatajwa kwa urefu na upana wake. Sasa linapoongeleta suala zima la kubadilisha umeme wa gridi kutoka KV 220 kwenda mpaka KV 400, sijui kama ndiyo mradi huu unaoongeleta. Naomba Mheshimiwa Waziri, anapokuja kutoa maelezo, basi atueleze kama ndiyo mradi

huu, tuweze kujua Wana-Biharamulo tutakuwa katika hali gani?

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine linalosikitisha ni suala zima la gharama za ufungaji wa umeme majumbani mwa watu. Gharama hizi zimeendelea kuwa juu sana na zinatakiwa zilipwe kwa mkupuo mmoja, kiasi kwamba, watu wengine hawawezi. Kwa nini kusiwepo na utaratibu kwamba watu wafungiwe umeme na wawe wanalipa taratibu wanapokwenda kununua umeme?

Mheshimiwa Spika, hili lingesaidia sana na lingefanya watu wengi sana waweze kupata nishati hii adimu, iweze kuwasaidia katika shughuli zao. Leo hii kuna baadhi ya wanavijiji inafika mahali mpaka wanachanga pesa zao; wanakwenda kwa Meneja wa *TANESCO*kuomba wafungiwe, lakini inakuwa ni vigumu. Wanarudishwa kwamba, wakaandae miutasari, wakaandae sijui vitu gani, vitu ambavyo wakati vimeshafanyika lakini inashindikana kutoa maamuzi. Wizara hii ina mpango gani? Mameneja hawa wanawasaidiaje wananchi hawa ambao wanahitaji kupata nishati hii, angalau hata kile kidogo kilichopo kiweze kuwasaidia? Naomba Waziri anapokuja, atusaidie katika hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, ukurasa wa 23 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameongelea suala zima la usambazaji wa mradi wa umeme vijijiini, *REA*. Ninashukuru kwa vijiji alivyovitaja. Vijiji vile viko karibia 12, lakini vijiji vile ukiangalia viko kwenye mwelekeo ambao pamoja na hayo, kuna vijiji ambavyo vingeweza kupata.

Ukiangalia mradi unaotoka pale kabindi kuja *Runazi Centre* kuja Katahoka, Nyamahanga, Ntungamo, Kibale, Nyambale mpaka Lusahunga. Vilevile wangeweza kuchukua vijiji vinavyopitia katika Kata ya jirani kiasi kwamba watu hawa wangeweza kupata umeme. Mfano, kuna Kata ya Nyantakala, Nyantakala pale ni barabarani kabisa. Wako vijana wamejajiri wenyewe, wajasiriamali, viko vikundi mbalimbali vya ujasiriamali ambavyo laiti kama wangeweza kupata umeme huu, vingeweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, jirani hapo kuna Kata ya Nemba, kuna shule za Sekondari ziko pale, kuna Vituo vya Afya viko pale, Zahanati wanahitaji umeme huu, lakini vijiji hivi vimeachwa. Kwa kweli, naomba katika mradi huu uweze kuangalia maeneo hayo kwa ukaribu sana ili kusudi watu hawa nao waweze kujikwambua katika maisha yao ya kila leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine kinachonishangaza, leo hii watu wote tunahitaji huu mradi wa *REA* na mradi wa umeme vijiji ambako ndiyo 80% ya wananchi wetu wanaishi hawana umeme. Ukiangalia bajeti ya mwaka 2012, iliyotengwa, fedha zilizokuwa zimepangwa kwenda *REA* ni 13% tu imekwenda. Fedha hizi nyingine zimekwenda wapi? Kama zimepelekwa *TANESCO*, ni juhudini gani zinafanyika kusaidia hawa *REA* nao wapate fedha ya kutosheleza waweze kupeleka umeme vijiji? Tunapaswa tupate jibu la makini hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niongee suala lingine kuhusu Sekta ya Madini. Katika ukurasa wa 56 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ametaja migodi ambayo itafungwa mwishoni mwa mwaka huu ikiwa ni pamoja na mgodi wa Tulawaka na Mgodi wa *Golden Pride Nzega* ambayo inategemea kuchukuliwa na mwekezaji wa kati ambaye ni *STAMICO*.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeshapangwa na jambo hili linapaswa liangaliwe. Mgodi huu unapofungwa, kuna huduma za jamii ambazo zilikuwa zinapaswa kufanywa na migodi hii, zimeteklezwa kwa kiasi gani? Au hawa wawekezaji basi wanafunga wanaondoka wanaacha kukamilisha miradi hii ambayo walikuwa wameahidi kwenye jamii, na hapa ndiyo tunapozua migogoro na jamii iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kuna wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi katika migodi hii. Je, wakati hawa wanaelekea kufunga, stahili zao zimeshaanza kuangaliwa? Au ndiyo hawa wanaondoka tena tunaanza kushikana uchawi, kwamba Kampuni imeondoka, imekuja Kampuni nyingine? Naomba

tafadhalii kabla hawajakamilisha miradi yao, wahakikishe wafanyakazi wao maslahi yao yameandaliiwa vizuri na mikataba yao ieleweweke.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni ajira kwa hawa watu wanaokuja kuanza uwekezaji. Tunaomba ajira zitengwe na ziwekwe kwa wazawa wa maeneo hayo. Siyo watu wanakuja kuanzisha migodi pale lakini wanakuja na watu wao tayari wamekwishaajiri. Hili suala linafanya vijana wetu wanakuwa *demoralized* na kwa kweli wanajenga hisia na chuki kubwa sana. Watoe ajira kwa vijana walioko maeneo yale, sawa najua kuna stadi na ujuzi mbalimbali unaohitajika, lakini kwa kazi ndogo ndogo, wachukuliwe watu wa maeneo ya pale wafanye kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ni jinsi gani *STAMICO* imejjipanga kuendeleza wachimbaji wadogo wadogo na kuwapatia maeneo ya kufanya kazi? Jambo hili limekuwa ni tatizo kubwa sana, tumeliongelea hapa mara nyingi, lakini kila siku tunapata jibu la kwamba Serikali inajipanga, tunajaribu, tupo katika mchakato. Huo mchakato utakwisha lini?

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante, nashukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa James Lembeli na Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi ajiandae.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kumshauri Mheshimiwa Waziri. Mwaka 2012 nilimshauri Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani sasa ni vizuri nikamshauri Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Naomba Mheshimiwa Waziri nimrejeshe kwenye maandiko matakatifu kwenye kile kitabu cha Mithali aya ya 20, mstari ule wa tisa, unasema kwamba: "Mashauri ya moyoni ni kama kilindi, lakini mtu mwenye ufahamu atayateka." (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ushauri huu ninaompa, ninampa sio mimi tu, lakini pia aelege ninaongozwa na Roho Mtakatifu aliyenipeleka kuyasema hayo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie jambo la kwanza kabisa kwamba muda wa kutoa ahadi umekwishapita. Tulitoa ahadi mwaka 2010 tukataja vijiji vitakavyopata nini. Tulitaja vijiji vitakavyopata umeme, tulitaja vijiji vitakavyopata maji tukapigwa kura. Mwaka 2012 tulipewa orodha na ramani na mwaka huu tumepewa orodha na ramani.

Mwaka 2012 tulipewa orodha na ramani ikionyesha vijiji vya Wilaya ya Kahama kwa Jimbo la Msalala vitakavyopata umeme kupitia *REA* vilikuwa vijiji sita na vijiji vitakavyopata umeme kupitia *Electricity Five* vilikuwa ni vijiji vinne, jumla ni vijiji kumi. Mpaka hivi sasa vijiji vyote kumi havijapata umeme. Tulichotegemea leo, tungekuja kuambiwa katika vijiji kumi, vijiji vitatu tumefika hapa, vijiji vinne tunakwenda hivi. Kwa hiyo, wale wananchi walinipigia jana nikawaambia nimepewa tena ramani. Wakaniambia kwamba, mshauri Mheshimiwa Waziri asiendelee kutoa ramani, atoe umeme. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nilitaka nimwambie kwamba kumekuwa na matatizo makubwa ya umeme kwenye Mji wa Kahama kwa muda mrefu pamoja na Miji midogo ya Kagongwa na Isaka. Matatizo haya yanatokana na uchakavu wa njia ya umeme inayotokea Ibadakuli kuja kahama. Tumekwishaomba sana na ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa Lembeli, imekuwa ni kilio chake cha siku nyingi sana kwamba Mji wa Kahama uunganishiwe umeme kutoka Buzwagi. Kilio hiki kiliishawasilishwa na mpaka sasa hivi hakuna kilichofanyika wala hakuna *indication* yoyote kwenye bajeti. Naomba Mheshimiwa Waziri alizingatie sana hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili, ujumbe kutoka Mtwara; mimi nilivyopokea na kuelewa ni kwamba wananchi

wa Tanzania hivi sasa wanachokisema ni kwamba rasilimali hizi tuzigawane kwa kutambua maeneo ambayo zinapatikana. Niseme tu kwamba sidhani kama wananchi wa Mtwara au sehemu nyingine wanasema rasilimali yote ibaki kule. Nilikuwa kwenye Tume ya Bomanı, tulizunguka nchi nzima zenye madini, wananchi wanasema tugawane mrabaha. Hii siyo mara ya kwanza au siyo kitu kinachofanyika katika sisi kuanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Idara ya wanyamapori, tunafanya hivyo. Tunasema 25% ya mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii yabaki kwenye vijiji, inafanyika hivyo. Kwenye madini mbona inakuwa kwamba Taifa litagawanyika? Kenya wanafanya hivyo, *percentage* fulani ya rasilimali wamepitisha juzi kwenye Katiba yao, inabaki pale. Ghana wanafanya hivyo, India wanafanya hivyo, Afrika Kusini wanafanya hivyo na bado Mataifa yale yapo na yameendelea kuwa *strong*. Tunasema, tunaomba rasilimali hizi tubakishe kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Tume ya Bomanı tulipendekeza 40% ibaki kwenye maeneo madini yanapopatikana, 60% iende kwa Watanzania wote. Kwa hiyo, naomba sana, hatumaanishi kwamba madini haya yabaki pale yalipo, hapana. Kiasi fulani kibaki pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimweleze tu Mheshimiwa Waziri kwamba, Wasukuma kwa mfano, sio wapole kama inavyodhaniwa, na sio wajinga kama inavyodhaniwa wakati mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wasukuma ni wavumilivu. Lakini hawapendi kabisa kuiona Shinyanga iko hivyo, Mwadui iko pale ikijenga *South Africa* Johannesburg; hawapendi kuona Tulawaka iko pale inafungwa inaiacha Biharamulo ile, ikajenga Toronto; hawapendi kuona *Golden Pride* inafungwa ikiiacha Nzega iko vile ikajenga Australia; kadhalika hawapendi kuiona Kahama ikibaki vile, Bulyanhulu ikijenga *South Africa*, ikijenga Toronto, ikijenga *London*. Tunaomba tueleweshwe na ninaomba Mheshimiwa Waziri aelewé

kwamba vitu vyana namna hii vinawa-*provoke* wananchi na vinatuletea matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na hii *message* ya Mtwara, nimshauri Mheshimiwa Waziri, mkubali kupokea na kukubali kuwa na mjadala mpana kuhusu namna ya *ku-share rasilimali* za nchi. Tulisema mwaka 2012 na mwaka 2011 kwamba tusiwafanye wananchi wa maeneo ambayo rasilimali zinapatikana wakaona ni balaa kuwa na rasilimali zile. Rasilimali hizi ni Baraka, ni kweli rasilimali ni zetu wote, lakini *population* ya Kahama sasa hivi ni kubwa mara kumi ya vile ilivyokuwa kabla ya madini kugunduliwa. Maisha yamepanda, bei ya mkate ambayo tulikuwa tunanunua labda kwa Sh. 200/= sasa hivi imeongezeka *several times* kwa sababu ya kuongezeka kwa *population* iliyotokana na madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii athari inabebwa na wananchi wa Kahama, haibebwi na Watanzania wote. Ndiyo maana tunasema tunahitaji tutazamwe kwa jicho la kipekee na hatumaanishi kabisa kwamba madini yote yabaki Kahama, gesi yote ibaki Mtwara. Tunaomba, kama ilivyopendekezwa kwenye Tume ya Bomani. Kama hamuiamini, mliipa fedha, tukazunguka dunia nzima, tukaja na ushauri huo. Kama bado hamwamini, zungukeni tena mwaaulize Watanzania, mnasemaje kuhusu usimamizi na matumizi ya rasilimali hizi? Tusi-*command* kwamba wanataka hivi, tunataka hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Kahama, *Service Levy*; Kahama tuna sheria ya Serikali za Mitaasura namba 290 ya mwaka 1982 inaruhusu Halmashauri kukusanya ushuru wa huduma. Katika Mkataba *MDA* uliosainiwa ulivunja Sheria ile kwa kusema kwamba itakuwa inalipa kitu kinachoitwa *Consolidated Local Fees* kwa Dola 200,000. Tatizo lilloloko ni kwamba 0.3% ambayo ndiyo ushuru halali wa huduma, ni mkubwa kuliko Dola 200, 000 na Waziri aliyesaini Mkataba ule hakuwa na mamlaka ya kuvunja Sheria iliopitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, tunawasilisha na tulikwishakusema tarehe 8 mwezi wa Tano Mheshimiwa Leticia Nyerere aliuliza

swali na mimi nikasema naomba mwongozo; hatujalipwa *Service Levy* Kahama. Tulicholipwa ni *local fees* kwa mujibu wa MDA ya Bulyanhulu na Buzwagi iliyosainiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya *Service Levy* iliyopitishwa na Serikali za Mitaa au iliyopitishwa na Bunge hili, hakuna kilicholipwa na tunadai Dola za Kimarekani milioni 12.15. Tukilipwa fedha hizi ninaamini kabisa Kahama haitakuwa na vumbi kama ilivyo sasa, Kahama haitakuwa na mashimo na hatutachangisha wananchi kujenga zahanati wakati dhahabu yao ipo, *service levy* yao ipo, Sheria ilishapitishwa, mtu mmoja anakwenda anasaini mkataba. Kwa hiyo nilikuwa naomba suala hilo tuweze kuliona. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nizungumzie matatizo ya wafanyakazi wa mgodi wa Bulyanhulu, wana matatizo makubwa sana. Kwanza, kuna ubaguzi katika mishahara. Watanzania wanaofanya kazi sawa sawa na Wazungu wanalipwa wastani wa Sh. 800,000/= wakati Wazungu wanalipwa zaidi ya Shilingi milioni 12 kwa kazi zinazofanana. Nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri wa Kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pili wanaumia sana katika mazingira yao ya kazi, wanaendesa malori yasiyo na *spring*, wanavunjika *disk* za migongo, wapo Dar es Salaam, kuna *Hotel* inaitwa *Durban* wako wafanyakazi 42 as we speak wana matatizo ya afya. Tunaomba sana wafanyakazi wale watazamwe na hasa Wizara ya Kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la wachimbaji wadogo. Nimesikia orodha, Kahama haimo wakati ndiyo yenye madini sawasawa na Geita, sawasawa na maeneo mengine. Nashindwa kujiuliza, hivi kweli *pressure* ya Wachimbaji wadogo Kibaha inalingana na Kahama? Mnatenga eneo la wachimbaji wadogo Kibaha mnaacha Kahama? Sheria tulipitisha mwaka 2010 tukasema maeneo yatakuwa chini ya Waziri baada ya leseni ku-expire ili Waziri aweze kutoa kwa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana hii lugha ya kwamba mnaendelea kujadiliana na wawekezaji ili waangalie maeneo yanayobaki;

yaani wenyewe waangalie wachague wanachukua firigisi, wanachukua mapaja halafu sisi wanatuachia vipapatio? Hapana! (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba nitapenda sana kuunga mkono baada ya kusikia majibu hapa. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Hiyo juu yako. Sasa namwita Mheshimiwa Lembeli atafuatiwa na Mheshimiwa Brigedia Generali Hassan Ngwilizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na Mheshimiwa Gosbert Blandes ajiandae.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naomba kwa moyo wa dhati kabisa kuunga mkono yale yote ambayo Mheshimiwa Maige - Mbunge wa jimbo la Msalala, ameyazungumza kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kahama. Nami sitarudia mengi aliyoyazungumza, badala yake nitazungumza yale ambayo hakupata fursa ya kuyazungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2006 nilipoingia ndani ya Bunge hili, kila mwaka na bila kuchoka, nimekuwa nikichangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi na ustawi wa Taifa na wananchi wetu. Kwa nini nimefanya hivyo? Kwa sababu Jimbo la Kahama na Wilaya ya Kahama ina kero nyingi zinazohusiana na aidha Sekta ya Nishati au Sekta ya Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na madini, nilishawahi kusema ndani ya Bunge hili Tukufu na ndugu yangu, Mheshimiwa Maige amerudia hii leo. Kama Mbunge usiombe hata siku moja eneo lako lipatikane na madini. Ni balaa, ni kero kubwa, sio tu kwa Mbunge lakini pia kwa wananchi

wanaoishi katika eneo hilo. Kero ya kwanza, wananchi kutokusaminwa kabisa na wawekezaji, wakati mwingine hata Serikali inawatelekeza pale wanapodai fidia zao. Wananchi wengi waliokuwa wakiishi katika maeneo ya migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi waliondolewa katika maeneo hayo bila kusaminiwa kama wao sio wananchi wa Taifa hili na sasa wanahangaika kama mbuzi ambao hawana mwenyewe na Serikali ipo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, pale ambapo wachimbaji wadogo wakijitafutia maslahi yao, wanapogundua na kuanza kuchimba katika maeneo ambayo Wilaya ya Kahama kwa mfano, yote imeshagawiwa kwa wawekezaji kufanya utafiti wa madini na wanapokutwa wakichimba katika maeneo hayo, basi ni balaa lingine; wanafukuzwa, wanateswa, wanakamatwa na Polisi kana kwamba wao sio Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mambo haya hayastahili kabisa, hayafai, hata mbele ya Mungu ni dhambi. Sasa swalii, kwa nini Serikali inafumbia macho matatizo kama haya? Nitapenda kumsikia Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha, anajibu maswali haya ambayo nimeyazungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini tofauti na miaka mingine yote katika sekta ya madini, safari hii na leo kwa namna ya kipekee kabisa napenda niipongeze Serikali, nipongeze uongozi wa *African Barrick* na uongozi wa mgodi wa Buzwagi pale Kahama mjini. Baada ya miaka mingi ya kilio kwamba wananchi wa Mji wa Kahama na Vitongoji vinavyozunguka, hawaoni manufaa kabisa ya mgodi wa Buzwagi, sasa angalau wameanza kuona mwanga. Nami ninaamini pengine Roho Mtakatifu amewashukia na sasa kwa mara ya kwanza mwaka huu mgodi wa Buzwagi utajenga barabara ya lami ya kilomita tano katika Mji wa Kahama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni ndoto ya wananchi wa Mji wa Kahama kwa miaka yote, nami naomba uongozi wa *African Barrick* na mgodi wa Buzwagi na Serikali, hizi kilomita tano zisiwe danganya toto. Mwaka ujao wajenge

barabara nyingine za kilomita tano na mwaka unaofuata 2015 barabara nyingine kilomita tano za lami ili Mji wa Kahama kweli uwe *Gold town* kama ilivyo Johannesburg. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, hapa *African Barrick*, Buzwagi, ninawapongeza kwa niaba ya wananchi wa Wilaya na Jimbo la Kahama. Lakini isiishie tu hapo, waendeleze kasi ya kuchangia huduma kwa wananchi. Ninatambua mchango wao hivi sasa, wamejenga Kituo cha Afya pale Mwendakulima, wamejenga Ofisi ya Kata Mwendakulima, wamejenga Shule ya Sekondari Kidato cha Tano na Sita Mwendakulima wanaendelea kulipa Shilingi milioni 60 kwa Kijiji cha Mwime. Naomba Shilingi milioni 60 ni makubaliano ya miaka kumi iliyopita wakati bei ya dhahabu ilikuwa chini. Leo bei ya dhahabu imepanda, nauomba sana uongozi na Serikali iwasaidle wana-Mwime, kiwango hicho cha Shilingi milioni 60 kiongezwe kulingana na bei ya dhahabu katika Soko la Dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo mengine ambayo wanastahili kuyafanya. Maji katika vijiji vinavyozunguka mgodi huu wa Buzwagi; haiwezekani wao waendelee kumwagilia maji barabara kule ndani, lakini kijiji kilichoko mita 100 hakina maji. Maji yapelekwe kijiji cha Mwendakulima, Kijiji cha Mwime na Kijiji cha Chapulwa.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu nishati. Umeme katika Wilaya ya Kahama na Mji wa Kahama ni kero na ni dhihaka. Pamoja na kwamba Wilaya hii inajulikana kwamba imeunganishwa na *grid*'ya Taifa, ukweli ni kwamba ni uongo. Ni kiini macho. Mji wa Kahama umeme wake ni nguzo tu, hauwaki kama inavyotakiwa! Mgao wa umeme ni kila siku, tofauti na maeneo mengine yote hapa nchini. Tunachoambiwa ni nguzo za umeme, uchakavu wa miundombinu kutoka kule Shinyanga kuja Kahama.

Mheshimiwa Spika, tangu nimeingia Bunge hili, kila Waziri anapojobu, anasema uchakavu wa miundombinu. Sasa kilomita 150, urekebishaji wa mtandao ule uchukue miaka

sita! Mimi sikubali! Leo nataka nisikie kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, anasema nini? Mgao wa umeme Mji wa Kahama utakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mhongo alipochukua Wizara hii ndani ya Bunge hili alizungumza, tena kwa kauli nzito na kwa kujiamini akisema kwamba mgao sasa mwisho. Sasa wananchi wa Mji wa Kahama kila siku mgao, ana neno la kuwaambia wananchi wa Kahama?

Mheshimiwa Spika, watu wa Kahama wanataka umeme. Pale Buzwagi ni jambo la kusikitisha sana, kana kwamba nchi hii ina Mji wa London na wengine Kahama. Pale Buzwagi tangu wamewasha umeme kwenye mgodi ule haujawahi kuzimika hata siku moja. Lakini Kijiji na Mji wa Kahama ulioko kilometra tatu, nne kila siku kuna mgao wa umeme. Tumesema ule umeme unaowaka kila siku pale Buzwagi kwa nini hauwashi Kahama? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama aliviyosema ndugu yangu Mheshimiwa Maige, kweli leo nilikuwa na hamu sana ya kuunga mkono hoja hii. Lakini kwa suala hili, nitaunga mkono hoja hii, pale tu ambapo Mheshimiwa Waziri atasema na kwa uhakika, kwa nini umeme unaowaka Buzwagi hauwaki Mji wa Kahama? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namaliza. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Kwa mara ya kwanza, nasema Serikali inapeleka umeme katika vijiji vilivyopo kwenye Jimbo la Kahama.

Ndugu yangu Mheshimiwa Maige amezungumzia Jimbo la Msalala, nami sitaki kusikia hii ndoto tunayoambowiwa kwenye makaratsi haya ambayo yameletwa hapa kwa mbwebwe kwamba umeme vijiji utakwenda, lakini bajeti haioani na maneno yaliyopo hapa! Lakini kwa sababu kwa mara ya kwanza wananchi katika vijiji vya Jimbo la Kahama na wao wamekumbukwa, wameingizwa kwenye mradi huu wa upelekaji wa umeme vijiji, napenda niishukuru Serikali na nipongeze. Vijiji ambavyo vimezungumzwa hapa katika

Jimbo la Kahama, ni pamoja na Nyandekwa, Seke, Bukondamoyo, Wigehe, Mbulu, Kisuke na kule Bulungwa ninakotoka mimi anakoishi mama yangu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya, naomba nisipoteze muda wako mwingi, lakini pamoja na pongezi hizi, nasita kuunga mkono hoja hii. Kama alivyo sema ndugu yangu Mheshimiwa Maige na mimi nitasubiri mpaka pale Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha na kama atatoa maelezo nitakayoridhika nayo na kwa hakika wananchi wa Kahama, nitaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Wala hujanipa muda wa akiba! Sasa namwita Mheshimiwa *Brig. Gen.* Hassan Ngwilizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na Mheshimiwa Gosbert Blandes ajiandae.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze na kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais kuhusu rasilimali za Taifa, kwamba rasilimali za Taifa ni mali ya Watanzania wote. Hiyo ni kauli ambayo haihitaji mjadala, ni kauli ambayo inahitaji kuungwa mkono na Bunge hili. (*Makofi*)

Vilevile naunga mkono hatua za Serikali za kuhakikisha kwamba ulinzi, usalama na utulivu katika maeneo yale yote ambayo yametokea rapsha unadumishwa. Hilo ni jukumu la msingi la Serikali yoyote ile. Kwa wale wote ambao wanafikiria kuleta chokochoko, wajue kwamba nchi hii inavyo vyombo vya dola. Yakitokea yatakayowatoka, wasilaumu vyombo vya dola, wala wasije wakailaumu Serikali, wajilaumu wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo hapa, kwamba matukio haya, sasa hivi Watanzania tumeanza kuzoea kwamba tunapenda kuhadithiana; lilitokea hili na fulani kavunjwa mguu na sijui fulani kafanywa nini! Hili lilikuwa ni jukumu la Serikali kuzuia, siyo kungojea mpaka yatokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuripoti matukio ni kazi ya Waandishi wa Habari, na kazi ya Serikali ni kuzuia mambo haya yasitokee. Ndiyo maana viro vyombo vya dola na kazi yao ni hiyo ya kuhakikisha inawadhibiti wale wote ambao ni wakorofu ambao wanavunja sheria na kanuni za nchi hii. Hilo linatakiwa lifanywe na vyombo vya dola bila kujali mtu ana cheo gani, anatokea wapi na ana imani gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hilo nilidhani ni jambo la msingi la kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais kwani yeye ndio Rais wa nchi hii na yeye ndio Amiri Jeshi Mkuu. Anavyo vyombo vya kuhakikisha kwamba matarajio ya wananchi yanatimizwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nikubaliane na Mheshimiwa Waziri kwamba, umeme ni uchumi, umeme ni maendeleo, lakini naomba kuongezea zaidi, kwamba sasa hivi umeme ni haki ya Binadamu. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Sawa! (*Makof*)

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, tuondokane na dhana ya umeme kama suala la biashara tu. Sasa hivi umeme unahitajika na kila Mtanzania kama ambavyo anahitaji dawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuiuliza Serikali, simwulizi Mheshimiwa Waziri kwa sababu naamini kwamba Mheshimiwa Waziri nia yake ni nzuri. Naiuliza Serikali na katika hili naomba niipongeze sana Kamati ya Nishati na Madini. Azimio la Bunge lile la mwaka 2012, tuliloazimia hapa, kwamba tozo ya Sh. 5/= kwa kila dakika ya maongezi ya simu kwenda REA, kutenga Shilingi bilioni 300 kwa ajili ya matumizi ya umeme vijijini, kutoka katika Shilingi bilioni 600 ambazo ni kiasi kilichoolewa kutokana na uamuzi wa Serikali kulinganisha kodi za mafuta ya taa na dizeli: Kwa nini Serikali imeshindwa kutekeleza hili Azimio la Bunge? Kwa sababu inaelekeea Bunge tunatoa maelekezo hapa, tunaazimia hapa, lakini Serikali haitaki kutekeleza hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe changamoto hapa, kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja kutoa bajeti yake ya Serikali, atupe jibu kuhusiana na Azimio la Bunge hili. Kwa sababu kama Bunge linaazimia na Serikali inaamua kupuuza, maana yake ni kwamba Serikali imeamua kutosikiliza Bunge. Kama Serikali imeamua kutosikiliza Bunge, maana yake ni kwamba hata hii bajeti hapa tunayokaa kuzungumza haina maana. Tunapitisha bajeti hapa ambayo haitakwenda kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la nguzo za umeme. Nguzo za umeme bado ni kero. Mwananchi akitakaka kuunganishiwa umeme anaambiwa ni lazima alipie nguzo, lakini akishalipia nguzo ile, ni mali ya TANESCO. Hilo namwomba Mheshimiwa Waziri akija kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge atoe maelezo hapa; hivi kuna *justification* gani ya mwananchi kutakiwa kulpia nguzo ya umeme ambayo hawezi kuuita ni ya kwake, inaitwa ni ya Shirika la TANESCO? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile wote tunataka umeme uwake nyumbani kwake. Kila Mtanzania anataka hilo, ndiyo maana nikasema umeme ni haki ya binadamu. Lakini vile nchi zote zinazotuzunguka, iwe ni Msumbiji, Malawi, Zambia, Kongo sina hakika, Rwanda, Burundi, Kenya, Uganda barabara zao zina taa. Sisi Tanzania tunahitaji *formula* ya aina gani kuhakikisha taa za barabarani zinakuwepo katika miji yetu?

Mheshimiwa Spika, ni aibu, unaruka na ndege kutoka katika nchi hizo, ukishaingia eneo la Tanzania, ukishakuta huoni Miji, hiki ni kielelezo kwamba sisi tumeshindwa kuwasha taa katika nchi yetu.

Hata hivyo, Mkoloni alikuwa na utaratibu mzuri tu kwamba kila ambaye anatumia umeme anatozwa senti; wakati ule nadhani ilikuwa senti mbili kwa ajili ya kuchangia kuwasha taa za barabarani. Hali ile iliendelea mpaka miaka ya 1970. Hii ni kwa nini tumeiacha? Kazi yetu sasa hivi ni

kusema, Halmashauri zinazohusika, sijui ziwashe taa. Halmashauri hizo fedha zinatoa wapi? Kwa nini tusichangie fedha kila mteja anapochangia? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwamba kulingana na ramani zile, sasa umeme katika Jimbo la Mlalo utaendelezwa kutoka Viti kuelekea Manolo, Kibaoni, Pelei, Rangwi, Makose, na hatimaye utakwenda Sunga, Mamboleo, mpaka Mtae. Hiyo ni katika awamu ya kwanza, kwa sababu kila kitu lazima kiwe na mahali pa kuanzia. Katika Jimbo la Mlalo siyo Vijiji hivyo tu, tunayo Tarafa nzima ya Uwumba haina umeme hata kidogo. Tuna Kata kama Shume na Mbalamo hazina umeme. Kwa hiyo, nategemea kwamba katika awamu ya pili ya *REA* umeme utafika kule.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunazungumza kwamba tunawapelekea Watanzania umeme. Taa, sawa. Hata hivyo, tunazungumzia suala la uhifadhi wa mazingira. Kama hatujazungumzia Watanzania watapika vipi kwa kutumia kwa umeme, tujue kwamba mazingira yetu, misi...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza, naomba tushauriane. Yaani vurugu iliyopo hapa haijapata kutokea. Kila mtu hapa anasema nataka kuchangia, nataka kuchangia, lakini *limit* ya *time* tuliyokubaliana jana ipo. Hivi sasa nikimaliza na Mheshimiwa Blandes, nadhani ndiyo mwisho.

Sasa mna uamuzi, Jumamosi mnaweza kukaa mpaka saa 12.00, lakini lazima itolewe hoja. Kama haitolewi hoja ya kuongeza muda, mimi nitaendelea kwa muda tulipanga.

WABUNGE FULANI: Ndiyo! (*Makof!*)

SPIKA: Sana sana huwezi kuongeza zaidi ya saa moja, kama mnataka mtoe hoja. Mheshimiwa Waziri wa Nchi unaweza kutoa hoja kwamba tuongeze saa moja zaidi? Atoe hoja kama mnataka kuongeza na kama hamtaki basi. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, jana tulitoa hoja kwamba leo tutakuwa na Bunge mpaka saa 8.00. Kwa hiyo, kwa ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge, naomba Bunge lako likubali angalau tuongeze muda mpaka saa 9.00 alasiri leo. Naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante kwa kuunga mkono. Hoja imeungwa mkono. Alichosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba, kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa jana, kikao hiki kingekwisha saa nane. Lakini sasa kwa kweli hapa nina vurugu siyo kidogo. Hata hivyo, saa moja maana yake tutaongeza watu sita, haidhuru, siyo mbaya.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge lilitidhia hoja ya kuongeza muda wa
Bunge likae mpaka saa 9.00 jioni)*

SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Hamad Ali Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nashukuru kwa kupata nafasi hii. Mkutano wa Wachumi Duniani uliofanyika Marekani walikubaliana kwamba, nchi zote zenye rasilimali kama madini, gesi na nyngine, zinaingia kwenye migogoro ya wenyewe kwa wenyewe kwa sababu ya mgawano mbaya wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini ya dhahabu Tanzania. Tanzania kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukichimba madini haya ya dhahabu na kwa kweli ni tatizo la uelewa. Serikali lazima ibebe dhamana hii ya kwamba imekuwa ikitoa taarifa zisizokuwa pana kwa Watanzania kiasi kwamba wananchi walio wengi hawaelewi.

Mheshimiwa Spika, Mtanzania yejote, awe Mbunge au mwananchi wa kawaida akizungumza suala la dhahabu anajua ni rasilimali yenye thamani kubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wote huo ambao tumekuwa tukichimba dhahabu Tanzania, nina wasiwasi kwamba hata Waheshimiwa Wabunge humu ndani pamoja na wananchi wenyewe hawaelewi dhahabu hii inachangia kiasi gani katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge pia ni mashahidi, kila Mbunge anayetoka katika Wilaya na Vijiji ambavyo vinachimba dhahabu anaonesha kwamba dhahabu hii haifaidishi katika maeneo wanayotoka wao na wananchi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie mahusiano kati ya wachimbaji na wananchi wetu. Katika maeneo yanayotoka dhahabu, wananchi ambao wamezunguka maeneo ya machimbo ya dhahabu, wamekuwa wao na wachimbaji ambao ndio tunawaita wawekezaji wakiangalia kwa jicho la uadui, na wamekuwa wakipeana majina ya kiuadui kama vile wananchi kuwaita wachimbaji makaburu, wanyonyaji, wezi na kadhalika. Lakini hata Wawekezaji nao wamekuwa wakiwaita wazalendo kwa majina ya wachimbaji haramu, wavamizi, majambazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kusikia kwa kipindi kirefu sasa ama wananchi wanauawa katika maeneo hayo, au wana ugomvi na walinzi katika maeneo ya machimbo, Polisi na hata wawekezaji wenyewe katika migodi. Kwa mfano, maeneo ya Mererani, Mwadui, Buzwagi, North Mara, Isanga, na maeneo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wanaelewa kwamba madini haya yanayotoka kwenye maeneo yao yana thamani kubwa ambayo haiwafaidishi wao. Kwa kuzingatia hilo ndiyo maana wameamua kwa namna yoyote sasa na wao waone kwamba kuna haja ya kufaidika na rasilimali zao. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa ina wajibu wa kuzingatia kwamba angalau yale maeneo yanayochimbwa dhahabu, basi kuwe na angalau kiasi fulani kibaki katika maeneo yale kama mrahaba wao. Jambo hili lingeweza kuwapunguzia manung'uniko. Lakini katika maeneo hayo, wananchi wamebaki na matatizo; magonjwa mbalimbali, barabara zao ni chafu, hawana maji, hawana Zahanati na hawana majengo ya madarasa.

Mheshimiwa Spika, hivi ndiyo vipimo na vigezo vyta wananchi kuona kwamba wanafaidikaje na rasilimali zinazotoka kwao. Serikali inasema kwamba rasilimali inapopatikana popote ni mali ya Watanzania wote, ni kweli. Lakini Watanzania hawaelewi hiyo, wanachoelewa ni kwamba eneo lao linatoka rasilimali yenye thamani, kwa hiyo, na wao wanaangalia kufaidika. Ndiyo maana tunasema kwamba maeneo yale, basi yapewe, yaangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, hata wale vijana wetu wa Kitanzania wanaofanya kazi kwenye machimbo, wanaambulia maradhi mbalimbali yanayotokana na kemikali zinazotumika kwenye maeneo yale ya machimbo, wanapata magonjwa yasiyotibika, lakini bado hawaangaliwi kwa jicho la huruma hata kwa wale wawekezaji wanapoona kwamba hawa watu wameathirika wakachukua namna ya kuweza kuwafikiria.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumegundua gesi, inatia shaka kwamba tunaweza tukawa na petroli vilevile, lakini naomba ni sema kwamba jambo hili na tumwombe Mwenyezi Mungu sote kwa pamoja ainusuru nchi yetu isije ikaelekea huko kwenye nchi nyingine walikoelekea. Ajalie iwe ni neema

kwa Watanzania na isije ikageuka kuwa dhahama kwetu.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, watu wa Mtwara na Lindi ni Watanzania ambao wanaishi Tanzania, wanajifunza kwa kuona na kusikia katika maeneo mengie ambayo rasilimali hizi zinapatikana. Wamejifunza kwamba, kwenye maeneo mengi ya machimbo nchini kwetu wananchi wamebaki dhoofulhali, hawana matumaini, hawaangaliwi kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba niishauri Serikali kwamba bado tuna nafasi ya kwenda kuzungumza na watu wa Mtwara jambo la busara, na hili naomba Serikali tusione kwamba tutakuwa tumefanya jambo baya. Hakuna ambalo halizungumziki. Watu wanafika kuuana nchi nyingine na wanakaa kwenye meza wanaelewana, wanaishi. *(Makofi)*

Suala linaloendelea sasa hivi Mtwara, niwapongeze Wanajeshi wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamekuwa wakiwasaidia wananchi kuwaelekeza na kuwapa matumaini ya usalama wao, kiasi kwamba wameamua kutoka mafichoni na wamekuja katika makazi yao. Lakini kuna taarifa zisizokuwa nzuri kwamba Jeshi la Polisi, badala ya kulinda raia na mali zao, wanafanya udokoz. Jambo hili siyo zuri kwa Jeshi la Polisi, na ni sura mbaya. Naomba niwashauri kwamba wawe walinzi wa raia na mali zao na waachane na mtindo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niiombe Serikali kwamba, kwa kuwa sasa tunaelekea kwenye Sheria, Sera...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ah, nasikitika ni kengele ya pili.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Gosbet Blandes, Mheshimiwa Shah, halafu atakuja Mheshimiwa Arfi. Hawa ndio walikuwa bado.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri na timu yako tuna imani kubwa sana na ninyi, naomba mwendelee kuchapa kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza na Mgodi wa *NICKEL* wa Kabanga, ambao uko Wilayani Ngara Mkoa wa Kagera, kwenye Jimbo la Mheshimiwa Ntukamazina. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, huu ni mgodi wa siku nydingi ambao utaifaidisha nchi hii kwa kiasi kikubwa sana. Nililitaka nifahamu mikakati ya Serikali, Mheshimiwa Waziri atuambie, ni lini mgodi huu wa Kabanga wa *NICKEL* utaanza ili Taifa liweze kufaidika kama ambavyo ni matarajio ya watu wengi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, zimekuwepo ahadi nyiningine hapa Bungeni za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, mojawapo ya ahadi hizo, ni ahadi ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine - Mbunge wa Tarime, kuhusiana na mradi wa kupeleka umeme vijijini, kwenye Kata zake mbalimbali ikiwemo Kata ya Bumera, Susuni, Nyandoto, Gorong'a, Nyarukoba, Bungurere, Kangariani, Geta Gasembe, Komaswa, Ibaso, Kigongo, na kadhalika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Nyambari amekuwa ananyong'onyea sana, anataka kujua umeme utakwenda lini katika maeneo hayo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini tuna mgodi wetu wa *North Mara* ambao uko Mkoa wa Mara. Wamiliki wa mgodi huu waliahidi tena mbele ya Mkuu wa Mkoa na viongozi wetu wa kiserikali kujenga barabara inayotoka Nyamwaga kwenda Nyamongo, hadi Mto Mara kwa kiwango cha lami.

Wananchi wa Tarime walitaka kujua, hawa watu wa mgodi
huu ni lini watajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?
(*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua juhudini nydingi
sana na za makusudi ambazo Waziri na timu yake wanafanya
katika kupeleka umeme vijiji. Kwanza nawapongeza sana,
na mimi nawahurumia, pamoja na kwamba mmetoa orodha
hii ya vijiji, lakini nawahurumia, nia mnayo, lakini hamna fedha.
REA hawana fedha.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, wakati wa bajeti
2012/2013, tulipanga tozo ya Sh. 5/=, kutoka kila simu ya
mkononi kwa kuchangia Mfuko wa Umeme Bijiji. Bunge hili
tulipanga kwamba fedha hizo ziende *REA*, na *REA* waweze
kupeleka umeme. Orodha ya vijiji vyote ambavyo tunavyo
hapa, hakuna hata kijiji kimoja ambacho Serikali imeanza.
Sasa mwaka wa fedha umekwisha, tulitegemea kwamba,
mimi ninayo barua ambayo ilikuwa inasema mradi huu
utatekelezwa katika mwaka wa fedha ule uliokwisha. Sasa
leo Wizara haijaanza ni kwa sababu gani? Fedha hizi
hazijapelekwa kwenye Wizara baadaye zikaenda kwenye
mfuko wa umeme vijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lazima ifike mahali tuwe *serious!*
Bunge linapoamua mambo fulani, mambo yake, huyo mtu
asiyetaka kutekeleza tuleteewe hapa, na Mheshimiwa Waziri
usiwe mnyonge, sisi Bunge kama tumeamua, mtu hajaleta
fedha hizo, ulete taarifa hizo hapa, na sisi tufanye maamuzi
ya busara na magumu kwa haraka sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tulisema kwamba zitengwe
fedha kiasi cha Shilingi bilioni 300, zipelekwe katika Mfuko wa
Umeme Vijiji, fedha hizo ilikuwa zikusanywe kutoka kwenye
mafuta ya Taa. Tulifanya maamuzi magumu hapa kwa ajili
ya Taifa letu. Mpaka hivi ninavyozungumza, taarifa ambazo
ninazo hakuna hata Shilingi moja ambayo imepelekwa katika
Mfuko huo wa Umeme Vijiji. Mimi nilitaka njue, huyo ni nani
ambaye anapinga maamuzi ya Bunge hili? Kama mtu
anapinga, kwa nini tunasimama hapa kufanya maamuzi?

Nataka Mheshimiwa Waziri, najua pengine hatakuwa na jibu katika hili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tutakapofika katika Wizara ya Fedha, mimi nataka katika hili tulisimamie kwa nguvu zote, tuhakikishe tunajua fedha hizi, Shilingi bilioni 300 ziko wapi na kwa nini hazijaenda *REA* kwa ajili ya kupeleka umeme vijiji ni kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Wilaya ya Karagwe Mkoa wa Kagera, inapakanana na Wilaya ya Kyerwa. Mwaka 2012 tulizungumzia kupeleka fedha katika mradi wa umeme wa *Hydro* huko Mrongo, na tulitegemea kwamba shughuli hii iwe imeanza, na mradi wa Mrongo wa umeme (*Mrongo Water Falls*), tulitegemea ulete changamoto katika kujenga viwanda, migodi ya *Tin*, lakini pia tulitegemea fedha hizi zisambaze umeme katika Wilaya za Ngara, Biharamuro, Muleba, Bukoba Vijiji, Ngara na sehemu nyingine. Tulitegemea mradi huu wa Mrongo uweze kuchangia kuleta changamoto katika kukua kwa uchumi katika Mkoa wa Kagera. siyo hapo tu, pia hata Pangani, tunao mradi wa *Water Falls Pangani*, *Water Falls Rusumo* na sehemu nyingine. Pengine nilitaka nifahamu, Serikali imejipangaje katika miradi hii ya *Hydro* katika nchi yetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake na *REA* kwa ujumla, wameendelea kutuhabarisha habari ya mkakati wa kupeleka umeme vijiji ni. Mimi nashukuru vijiji vya Jimbo la Karagwe naviona humu, na wengine msishangae vijiji vya Karagwe vinaonekana vingi, lakini kwa sababu ya utitiri wa ukaribu karibu, utakuta ni 0.5 Kilomita, 0.4 Kilomita, lakini napenda kusema kwamba, nimewapelekea wananchi wa Jimbo la Karagwe orodha hii, nimetoa *photocopy* kwa kila kijiji, kwa kila Mwenyekiti wa Kitongoji, na kila Mwenyekiti wa Kijiji. Kwa kweli wote wamefurahi na wanashukuru na wanaipongeza Serikali kwa mkakati huo. Nimewaambia Serikali imeniahidi kwamba mradi huu utatekelezwa kabla ya mwisho wa mwaka 2014, utakuwa umekwisha na mkandarasi atakuwa ameondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naangalia Bajeti iliyopangwa kwa ajili ya miradi hii, nimeona zimepangwa Shilingi bilioni 153, wakati zinatakiwa Shilingi bilioni 881. Ninaanza kuwa na wasiwasi, inawezekana nikawa nimejichongea kwa wananchi wangu kuwapa habari njema hizi, ambazo pengine hazitatekelezeka. Nikiangalia kwa haraka haraka, hizi Shilingi bilioni 153, ambako kuna upungufu wa mabilioni kadhaa, kama hizi Shilingi bilioni 881 hazitapatikana, *REA* wakabaki na Shilingi bilioni 153, mradi huu wa kupeleka umeme vijiji kwa vijiji hivi tu vichache utachukua siyo chini ya miaka sita mpaka saba, na inawezekana humu ndani akawa hakuna Mbunge hata mmoja wa kukumbushia Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa napendekeza, nia njema sana ya Serikali, nia njema ya Kamati ya Nishati ya kupendekeza tozo la Sh. 100/= kwenye mafuta. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tukubaliane tozo ya Sh. 100/= kwenye lita moja ya mafuta, fedha hizo ziende kwenye Mfuko wa Umeme Vijiji, tukubaliane kwa pamoja. Kama mtu huyu hapeleki fedha, mumlete hapa sisi tumuwajibishe haraka iwezekanavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini tukubaliane tozo nyingine ya Shilingi tano mpaka kumi katika kila dakika ya simu ya mkononi. Tukubaliane fedha hizi ziende kwenye Mfuko wa Umeme Vijiji. Katika hili Mheshimiwa Waziri tunaomba uwe unatuletea taarifa angalau ya kila *quarter kwamba mfuko* huu umepokea Shilingi ngapi kutoka Serikani? Kama hawaleti, sisi tuchukue hatua za haraka sana, kwa sababu tukikaa mpaka mwaka uishe ni matatizo kwetu. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, tupe taarifa na sisi tujue cha kufanya kwa yule ambaye anakaidi agizo la Bunge.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupeleka mradi wa umeme katika Jimbo la Karagwe, katika vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi hadi Ihembe. Najua kwamba kuna *addendum two* inakuja, wananchi wananiuliza inakuja lini, pengine Mheshimiwa Waziri ni vizuri ukanijulisha hilo. Lakini

sambamba na hilo, tuliambiwa kwamba kuna fidia ya wananchi ambao waliharibiwa mazao yao kwa kuruhusu mradi huu kupita. Tuliambiwa kuna Shilingi milioni 200 ziko mahali fulani. Siyo kwamba tunadai, sisi tunapenda sana maendeleo. Lakini kwa kuwa tuliambiwa, tulipewa taarifa hizo, tungetaka kujua kwamba fedha hizo ziko wapi, na zitalipwa lini?

Mheshimiwa Spika, kwa leo kwa kweli niwashukuru, niwapongeze, Mheshimiwa *Professor* tuna imani na wewe, Katibu Mkuu - Maswi, watu wa *REA, TPDC*, wote tunawaamini, lakini tatizo ni fedha. Waheshimiwa Wabunge tujifunge katika *Bajeti* tuhakikishe kwamba suala la umeme vijijini linapatiwa ufumbuzi, fedha zinapatikana, na yule aliyekatalia Shilingi bilioni 300, tulizopitisha hapa, kabla hatujamaliza Bunge hili tunataka tufahamu ni nani na ziko wapi na tunataka ziende zianze kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Arifi, atafuatiwa na Mheshimwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Beartrice Shellukindo atafikiwa, Bwana Ussi atafikiwa, Mheshimiwa Ole- Sendika atafikiwa na Mheshimiwa "Buyogera atafikiwa.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia mimi kuitia Wizara hii ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa na mimi sina budi kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumpongeza Mheshimwa Waziri, Manaibu, Katibu Mkuu na timu yako yote ya wataalam, Iakini bila ya kumsahau Mkugenzi Mkuu wa *REA* kwa jithada zake zote anavyojitahidi kuhakikisha kwamba umeme unafika vijijini. Pia nisimsahau kwa Mafia, nimshukuru kwa pekee Ndugu Mramba - Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO*. Kwetu sisi Mafia ni muhimu na tunamshukuru na kumpongeza na kumtakia kila la heri na ninafikiri Serikali itakuona ikuthibitishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alivyoanza tu hotuba yake, alianza kusema neno kwamba umeme ni uchumi, umeme ni maendeleo. Nakubaliana naye kabisa na nasema na sisi wana-Mafia tumepokea, na tutapokea endapo hiyo kauli yako ikiwa ni thabiti. Naamini kwa umri uliokuwa nao, huwezi ukakaa hapa, ukasimama ukalihutubia Bunge hili, ukawahutubia Watanzania na dunia nzima ikakuona kwamba hapa unatulaghai. Siyo rahisi! Naamini kauli yako itakuwa thabiti, kwa maana ya kupitia umri na yale ambayo wewe unayategemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono maelezo ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kama Mheshimiwa Blandes alivyosema, kwamba lile tozo tulilosema la asilimia tano la muda wa maongezi wa simu, limekwenda wapi? Tunataka tupate maelezo kamili na ili tuweze kuchukua hatua. Isiwe hatua anachukuliwa mtu mwingine, lakini kuna mtu anayezuia maendeleo katika nchi yetu kwa ubinafsi wake tu akaamua kulizua na kuweza kuleta matatizo na kero kwa wananchi ambao wanaadhibika kule vijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze. Baada ya kuishukuru Serikali, naomba nitumie fursa hii kuishukuru Taasisi ya *Mafia Island Development Foundation (MIDF)*. Naomba ni-declare interest kwamba mimi pia ni member wa hiyo pamoja na wenzangu katika kuona kwamba jambo la kupeleka umeme vijiji, nafahamu Wizara inafahamu, na kama haifahamu imwulize Mkurugenzi Mkuu wa REA - Ndugu Mwakahesy, sisi *MIDF* tumechangia Shilingi milioni 500 kuweza kuharakisha mradi huu kuja katika vijiji vya Wilaya yetu ya Mafia. (*Makof*)

Tumehangaika, tumejitahidi, tumeweza kupata ufadhili wa Shilingi milioni 500. Sasa naomba mradi huu kwa Mafia usije ukawa tena unatubabaisha. Tumechangia nguvu zetu, Wamafia tumechangia. Hatukusubiri mpaka nyinyi Serikali peke yake, asilimia 100 kwa 100 mlete. Sisi tumechangia Shilingi milioni 500, ikiwa asilimia mbili, asilimia tano, ikiwa asilimia 10, lakini uchungu tulionao tumeuonyesha kwa kuweka nguvu yetu. Lakini pia nitumie fursa hii

kuwashukuru viongozi wangu wa *MIDF* kwa jitihada zao zote za kuhakikisha kwamba wameweza kutafuta fedha na kuweza kuchangia mambo haya, na mambo ni mengi sana ya kimaendeleo ambayo yanaletwa kuititia *MIDF*.

Mheshimiwa Spika, Mafia leo tunatumia mitambo ya kuzalisha umeme ya mafuta ya diseli. Nilikuwa naomba, nimeleta ushauri wa kimaandishi, lakini nataka niseme tu kidogo kwamba mafuta yale, mashine zile mbili zinazozalisha *Kilowatts* 800, 900, sasa hivi mmeweza kutuongezea, kutuletea mashine nyingine mbili zilizotoka Njombe na sasa zimeshafungwa, tunategemea zianze kufanya kazi. Zikifanya kazi kwa maana Mafia tutapata umeme wa *Megawatts* mbili. Lakini tupime kwenye gharama.

Mheshimiwa Spika, mashine mbili zile za mwanzo, kabla ya mbili zilizoletwa, gharama yake kwa mwaka zinatumia mafuta lita 1,286,000. Kwa gharama ya bei ya leo ya mafuta au kwa hesabu tuliyopiga, kila lita moja inafika thamani ya Sh. 2,500/=.

Kwa jumla kwa mwaka kwa mashine zile mbili, Serikali inatumia biliioni 3.235 kwa mwaka kwa kuendesha mitambo miwili inayozalisha *Kilowatts* 900. Mashine hizi hazitoshelezi, ndio maana mkaona umuhimu baada ya kumwambia Mheshimiwa Rais na Rais akalichukua, na ninafikiri utekelezaji wake mmeuonesha. Mmeleta mashine mbili nyingine zenye uwezo wa kuzalisha *kilowatts* 600, 600, kwa maana ukichanganya 600, 600, inakuwa 1,200 na zile 900 itakuwa kama 2,100.

Mheshimiwa Waziri, sasa hebu liangalieni, ukichukua hizi ukijumuisha kwa mashine nne, gharama za matumizi kwa mwaka ni zaidi ya Shilingi biliioni 3.29. Matumizi haya ya mafuta kwa mitambo hii miwili, ukija ukichanganya kwa kipindi cha miaka 25 na natoa mfano wa miaka 25 kwa sababu nimepata taarifa, nimesoma vijarida kuititia jarida moja linalotoka Wizara ya Nishati ya Zanzibar kwamba imetumia Shilingi biliioni 111, sawa na *Norwegian Krone* milioni 400 kulaza umeme *cable* ile ya Baharini kutoka Pemba hadi Tanga.

Sasa ukichukua gharama hiyo na kule urefu wake ni kilomita 72. Wakati Naibu Waziri alipokuwa Mheshimiwa Adam Malima, alitoa mawazo kwamba kwa nini tusivushe umeme kutoka Rufiji, Nyamisati kuja mpaka Mafia kwa kulaza *cable*. Pale umbali wake ni kilomita 35, 36 mpaka 37, haiwezi kuzidi hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia gharama hizi, tunaweza tukatumia shilingi bilioni 50 au 55 kwa kulaza *cable* kuja Mafia pamoja na mitambo yake yote na kulipa fidia lakini kama tukisema tutumie mashine hizi nne za mafuta ya dizeli, tutatumia zaidi ya shilingi bilioni 164.67. Kwa hiyo, tutaokoa mabilioni ya fedha na zitawezza kusaidia wananchi wengine au shughuli nyingine za kimaendeleo katika nchi yetu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri alipokee hili, alichunguze na waangalie uwezekano wa kuweza kudhamiria kulaza *cable* hii ni gharama ndogo tena ya miaka 30 *gurantee* kulala baharini. Kwa hesabu niliyokupa mafuta yasipande bei kwa miaka 25, kitu ambacho hakiwezekani. Kwa hiyo, tutaharibu mazingira yetu kwa mafuta yale na sasa hivi kuna mitambo mingine inayotumia *biomass* ya kukata miti, sijui wataalam tulifikiria nini lakini nachosema hii ndiyo *solution* peke ya kuweza kupata umeme wa uhakika kwa Mafia. Tukipata umeme huu, basi Mafia inaweza ikawa *Mini-Singapore* katika *East and Central Afrika*. Ni kisiwa ambacho kinaweza kikaleta tija katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana, nitumie fursa hii, kumwomba Mheshimiwa Waziri, vijiji vyangu 23 tuliookuchangia nguvu zetu, usitutupe mkono. Katika maombi yetu ya kwanza wakati wanaanda *study* ile walitaja vijiji 13 lakini tumeongezea hivi vijiji, naomba sana, vijiji ambavyo havikuorodheshwa na nilianidika barua maalum, nikamkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa *REA* kumwambia kwamba vile vijiji vilivyosahauliwa viweze kuingizwa katika hii *program* na waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema upande wa umeme, nikutakie kheri lakini tunataka tumjue nani yule aliyezula hii pesa wewe usipewe tullyokuwa tumeipitisha hapa Bungeni na kuitolea maamuzi mazito, kwamba shilingi tano ya muda wa maongezi ya simu zije kuchangia REA zimekwenda wapi? Hilo nataka kulijua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nizungumzie kuhusu ndugu zetu wa Mtwara. Niwaombe sana, mengi yamezungumzwa, busara nyingi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Haya ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Said Arfi, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimwia Agripina Buyogera.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini ninapaswa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kwa kunipa afya na kuweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Spika, tupo katika kipindi cha majoribu. Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi, alipomteua mja wake Nabii Suleiman, akampa ufalme na mali lakini Nabii Suleiman akamwomba Mwenyezi Mungu amjalie hekima. Pamoja na kuwa na ufalme na mali, Nabii Suleiman aliona amepungukiwa kama atakuwa hana hekima. Hekima imendikwa hulijenga Taifa. Ni matumaini yangu katika haya ambayo yanajiri katika Taifa letu sasa, hekima itatamatalki ili kuweze kuwepo amani na upendo mionganoni mwa Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote ile, kwa unyenyekevu napenda kuiomba Serikali na kuishauri sababu ndiyo wajibu wa Mbunge kuishauri Serikali, wawashirikishe wananchi katika masuala yanayohusu maisha na

mustakabali na maendeleo yao ili waweze kuepuka misuguano isiyokuwa na lazima. Rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu ametupa, ni kwa ajili ya manufaa na maslahi ya Watanzania wote. Ni elimu ya kutosha kama ingekuwepo na ushirikishwaji uliokuwa mpana, tusingefika hapa tulipofika lakini bado nina matumaini makubwa sana kwamba hekima na busara itatamalaki ili tuweze kufikia mahali pazuri. Kadri tunavyochelewa katika kulifika na kulitanzua tatizo hili, ndivyo tunavyorudi nyuma katika kupiga hatua za maendeleo. Kwa sababu majirani zetu Msumbiji sasa hivi wanakwenda kwa kasi. Hatua zozote za kuturudisha nyuma tusiende katika malengo tunayokusudia, tunaweza pia tukachelewa kufika katika hilo soko tunalotarajia kwenda. Kwa unyenyekevu niwaombe Watanzania wenzangu waweze kuona na kutanguliza maslahi ya Taifa letu na kudumisha amani na upendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, nizungumzie sasa wachimbaji wadogowadogo. Wasemaji waliotangulia wamezungumzia maeneo yao, nami sina budi nizungumzie Mpanda kama eneo moja ambalo limekuwa na wachimbaji wadogowadogo kwa takriban zaidi ya miaka 40. Cha ajabu, katika maeneo na mahekta zilizokuwa zimetengwa, maeneo ambayo yana migogoro ya wachimbaji wadogowadogo hayakuguswa kabisa, yametizamwa maeneo mapya kama yale ya Kibaha na Ilagala, mkaacha Kahama na Mpanda ambako kuna matatizo makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wachimbaji hawa wadogowadogo wamekuwa pale na familia zao wakiendesha maisha yao, wakitegemea kufanya kazi hizo lakini cha ajabu maeneo yao wamepewa wale wanaojiita kwamba ni wachimbaji wakubwa. Matapeli wachache na baadhi ya waliokuwa viongozi, wamehodhi maeneo hayo na muda ulipokwisha, wamebadilisha jina la Kampuni na wanaendelea kuhodhi. Hali hii haiwezi kuvumilika na wakati mwingine inasababisha wananchi kufikia kuchukua hatua kama hizo wanazozichukua sasa huko Buhemba. Ni lazima Wizara ikae na wachimbaji hawa wadogowadogo walioko

Mpanda, Kahama, Buhemba, waweze kwanza kutanzua migogoro iliyoko sasa kabla ya kufikiria kuanza kuchukua hatua zingine. Wanavyoendelea kuwapuuza hawa wachimbaji wadogowadogo, ndivyo wanavyozidisha chuki dhidi ya Serikali, chuki dhidi ya viongozi, kwa sababu hawajali na kuwaondolea kero zao.

Mheshimiwa Spika, badala ya kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo kilichotokea ni kwamba Wizara imeamua kupandisha ada na tozo mbalimbali za leseni ili hawa Watanzania maskini wasiokuwa na uwezo wasiweze kumiliki maeneo hayo ya kuchimba madini. Jambo hili si jema sana. Njiombe Wizara ijaribu kuangalia kama ina nia njema na kuwasaidia Watanzania maskini, viwango vinavyotozwa viangaliwe view ni vile ambavyo Watanzania wanaweza kuvimudu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua ya kupunguza gharama za kuingiza umeme huko Kusini kutoka gharama ya shilingi laki moja na kidogo mpaka shilingi elfu tisini na tisa, kwa kuwa na vigezo fulanifulani ambavyo walivitazama kutokana na hali za maisha za wakazi wa maeneo hayo lakini hali ya Watanzania inafanana. Kama mmeamua kupunguza gharama za kuingiza umeme kutoka Sh.160,000/= mpaka Sh.99,000/=, ziwe kwa nchi nzima. Kwa kufanya usawa huo mtakuwa mmelisaidia sana Taifa hili ili liweze kuflikia malengo yanayokusudiwa. Vinginevyo kuweka tabaka, eneo moja linapunguziwa, eneo lingine linapandishiwa, bado mtaleta manung'uniko na kelele kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, wametengeneza mpango wa kuwasaidia mikopo hawa wachimbaji wadogowadogo. Katika bajeti iliyopita ya mwaka 2012/2013 zilitengwa shilingi bilioni 8.9 lakini mpaka sasa hivi hakuna mchimbaji mdogomdogo hata mmoja ambaye amepata mkopo huo kutoka na urasimu, mchakato na mambo kadha wa kadha. Mikopo hii inategemewa itaanza kutolewa mwezi Julai, 2013, tena kuititia Benki ya *TIB* ambayo iko Dar es Salaam. Unamsaidiaje mchimbaji mdogomdogo wa Mpanda ili

aweze kupata mkopo kuitia *TBI* Dar es Salaam. Hili ni tatizo lingine ambalo kwa kweli bado linatusumbua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme, nimesoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mpanda ilikuwa mionganoni mwa ile awamu ya kwanza ya Kibondo, Kasulu na Mpanda kupata *generator* mbili mbili za umeme tena ikiwa ni ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado hazijafika. Sasa imeingizwa katika mpango wa Ngara, Biharamulo na Mpanda wa kupata *generator* moja. Nataka kuelewa ni kwa nini tumetoka kwenye mbili na kuja kwenye moja na kwa nini mpaka sasa haijafika? Pamoja na kwamba pengine Mheshimiwa Waziri, ulimi tu uliteleza akasema kwamba hivi sasa ninapozungumza na nyinyi, hizo *generator* zinateremshwa huko Ngara, Baharamulo na Mpanda ambapo si kweli, *generator* hizo hazijafika. Naomba sana kupata maelezo juu ya eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni mradi wa Malagarasi. Kanda ya Magharibi haijaunganishwa katika *grid* ya Taifa kwa maana ya Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa na sehemu kubwa ya Mkoa wa Kagera. Hakuna mkakati wa nguvu na wa makusudi na tegemeo kubwa ilikuwa ni mradi wa Malagarasi ambao umesuasua kwa sababu mbalimbali lakini kwa sababu sasa kuna *compact three*, tulikuwa tunataka tujue ni lini sasa mradi huu wa Malagarasi utaanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini *NDC* ilipoingia katika mikataba na makampuni haya ya Kichana ya kuchimba makaa ya mawe, upande mmoja wana hisa asilimia 30 na upande mwingle wana hisa asilimia 20? Je, Wizara haina mpango mahsus kwamba mikataba tunayoingia basi tutakuwa na hisa ya kiwango Fulani? Ni matakwa tu, ni makubaliano tu, hata tukiwa na hisa 10 zinatosha? Ni kigezo gani kinachotumika hapa iwe 30 na hapa iwe 20? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kujua mipango ya rasilimali zilizopo Liganga na Mchuchuma. Imeelezwa

habari za kufua umeme lakini chuma hakuna maelezo yoyote. Kuna mkakati gani sasa wa kuona kwamba rasilimali ya chuma inalisaidia Taifa hili?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ajiandae.

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na nianze *ku-declare interest* kwamba mimi ni mdau wa sekta hii sana. Ninafanya kazi za ushauri na Mungu akinijalia katika miaka mwili au mitatu ijayo nitakuwa *operator*. Napenda nikiri kuwa mimi ni Mwenyekiti wa Chama anayesimamia sekta hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe utangulizi au niwasaidia watu wa Serikali, shilingi bilioni 300 zinazongumzwa zilifikiwa vipi? Tulipofanya maamuzi yale, unaweza kuyaita vyovyyote, Serikali ilikuwa imeshindwa kudhibiti uchakachuaji wa mafuta, vitendo viovu ambavyo vilivyoingiza hasara nchi hii. Makadirio ya kitaalam, mimi ni mtaalam wa sekta hii, Taifa lilikuwa linapoteza Sh.50,000,000,000/= kwa mwezi na mwaka mmoja una miezi 12, ukizidisha miezi 12 na Sh.50,000,000,000/= unapata Sh.600,000,000,000/. Baada ya mafanikio ya kudhibiti tatizo hili, busara ikalituma Bunge kusema basi, mafanikio ya kudhibiti uchakachuaji Sh.300,000,000,000/= wapewe wananchi amba waliumizwa. Kwa hiyo, mtalaam wa Serikali atakayekuja kubisha, abishe kwa kuanzia Sh.50,000,000,000/= kwa mwezi na abishe kwamba mwaka wa Kitanzania hauna miezi 12. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpungeza Waziri, kwa namna alivyokuja na mpango wa umeme lakini mimi niende kwa Mtemi Chenge, Mjumbe wa Kamati kuweza kuchangia pamoja na Wabunge wenzangu namna gani tuweze kupata pesa za kumpa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi Serikali imehangaika

kutafuta rasilimali. Rais wa nchi hii amezunguka dunia nzima akitafuta rasilimali za kujenga barabara na umeme, waliobeza wamebeza lakini sisi busara za kwetu zinasema, "entukuru egarukoa nyamgarura." Unapomtembelea mtu na ye ye akikutembelea, ukimpelekea zawadi anakuletea zawadi. Kwa hiyo, waliombeza Rais wangu wanaokuja kumtembelea wanamletea zawadi. Rais wa China alilet a zawadi, kama hamkuona, angalia bomba litajengwa. Mheshimiwa Barack Obama, Rais wa Marekani, atakuja na zawadi, *Power for Africa* na *Power for Africa*, inazinduliwa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nashabikia kupewa lakini busara inanituma kwamba sisi kama Watanzania tukibebwa lazima tujikaze. Wakati umefika Watanzania tujitahidi kwa pamoja na sisi tuwe tayari kutoa, tupunguze matumizi yetu tuweze kutoa. Naungana na Wajumbe na Kamati yangu iliyosema kwamba tutoe Sh.100/= kwa kila lita ya mafuta tutumiayo kusudi kuchangia mfuko wa *REA*, tutaweza kupata Sh.250,000,000,000/= Kumbe makampuni ya simu yalikuwa yakitu-*charge* Sh.130/= mpaka Sh.150/=, sasa wamekuwa na busara, wamerudi mpaka Sh.30/. Tufanye maamuzi, tutenge Sh.20/= tuweze kukusanya Sh.250,000,000,000/= kwa mwaka tuiweke kwenye umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, natambua uwezo wako wa Kimataifa wa kuzunguuka dunia nzima kuomba lakini unapokwenda kuomba chakula basi na sisi tukusanye kuni nyumbani. Huwezi kwenda kuomba chakula, ukarudi ukaomba na kuni. Lazima na sisi kama Taifa tusimame tuchangie chochote kusudi uwe na uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, manufaa ya tozo. Mamlaka ya *REA*, itakapokuwa na tozo ya uhakika katika mafuta na simu, itakuwa na uhakika wa Sh.500,000,000,000/= kwa kila mwaka. Inaweza kumweka mkandarasi *site* bila kujua kama pesa itakuja kwenye bajeti au haitakuja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimewaona Wabugne wenzangu kila mtu ana haraka. Mimi nina haraka sana, hakuna kijiji katika Jimbo langu kitakubali kwamba kisipate umeme. Ninamshukuru Mheshimiwa Rwekiza, amewatangazia ndugu zangu wa Makongora kwamba umeme unakuja. Namshukuru sana ndugu yangu huyu. Napenda umeme uende Bulembo, Luanda, Kyanshenge, Lwigembe, katika sehemu hizi zote kwenye ramani ile hazipo. Mimi ile ramani ninaipenda sana tena ina rangi nzuri lakini nikiipelekea Jimboni watu wa Lwigembe, Bulembo, Kyanshenge, Ruanda wasipoiona hawatanielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimejenga hoja kwamba tuweke tozo na Wabunge wote wameshakubali, walikuwa wananiita nje wakaniambia, Waziri mnaelewana mwambie sisi tumekubali tozo. Sasa Wizara ya Fedha, sisi tumekubali wenyewe, mtu akikukinga kichwa mnyoe, kwa nini usimnyoe, tumekubali sisi kwa niaba ya wananchi wetu. Wananchi wa Kafunjo wanataka kuchangia umeme, msichange, tutachanga Taifa zima, twende kama Taifa, Taifa ni moja tuchange. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kuhusu wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wengi wana mapungufu. Ninajenga hoja kwamba Chuo cha Madini cha Dodoma kiimarishwe, kijitegemee, kiwe kama vyuo vingine imara. Kisiwe Idara ya Wizara, wapange mipango yao lakini mipango ninayoitaka ni mipango ile ambayo mwanafunzi anapoingia katika chuo ajue kwamba hatapewa kazi ila anapotoka pale anakwenda kujajiri. Kwa sababu tumejenga utamaduni wa kutoa mikopo, wale watakuwa wamepata mafunzo ya chuo, ndani ya chuo au kwenye *site*, wawe watu wa kwanza wa kupewa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, huwezi kumpa mtu mkopo wa *compressor* wakati hajawahi kuitumia, ataogopa kuvala *mask*, Mheshimiwa Profesa unayajua haya. Kwa hiyo, tunajenga hoja, kwamba Chuo cha Madini ukubali kiondoke. *Ukichkure*. Mtoto hata kama ukimpenda vipi, ukifika wakati

wa kuacha kunyonya, muachishe ziwa. Chuo cha Madini, kiache kitembee ukiangalie kwa mbali. Ni kwa kuwezesha Chuo cha Madini, wananchi watashiriki kwenye kuchimba na wakichimba watapata pato na wakipata pato wakalipe ushuru na wakili pa ushuru baki wanapeleka nyumbani, ndipo mtakapoweza kuona tangamano la faida ya madini. Huwezi kuona faida ya madini kwa kuyaangalia. Hata yangelichimbwa jikoni mwako lazima ushiriki. Unashiriki vipi? Kwa kuchimba au kwa kuwa mgavi wa kupeleka chakula. Tusibaki kuwa watazamaji katika shughuli ambayo Mwenyezi Mungu aliiweka mlangoni mwetu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa ninadanganya nisipozungumzia Kampuni ya Mafuta ya Taifa. Hofu na mashaka ya Watanzania walio wengi kuhusu sekta ya mafuta ni kwa sababu hawashiriki na wataalamu wa masoko wa *Unilever* walisema uktaka uhondo wa ngoma uingie ucheze. Sasa kama mafuta yana faida kubwa, napenda kuuliza, kigugumizi cha Serikali kwa muda wote kuanzisha Kampuni ya Mafuta ni nini? Nimuulize Waziri ambaye ni msomi aliyebolea katika nishati, kuna hasara kuanzisha Kampuni ya Kitaifa au hatuna Mameneja? Azaliwe nani aje awe Mkurugenzi ya Kitaifa?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliwahi kusema kwamba Tanzania tunayo *location advantage* na mimi niwaambie ni mtaalamu katika sekta hii, nchi zilizotuzunguka zinakuwa na busara ya moyo yaani *peace of mind* kama zitafanya biashara na kampuni ambayo ina dhamana ya kitaifa. Kampuni za Kongo, Rwanda na Burundi zikiagiza mafuta kupitia *National Oil Company*, zinakuwa na *peace of mind*, tunasubiri nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, haihitajiki mtaji kwani mteja wako wa kwanza ni Halmashauri, mteja wa pili ni mashirika ya umma. Imefika wakati kwamba wale watakaojitokeza zaidi kujenga nchi hii tuwawezeshe, upendeleo wa kuwaambia kampuni ya kitaifa i-supply mafuta katika mambo ambayo tuna *interest*, siyo kificho wala siyo uonevu, inafanyika hivyo Marekani na huko China na nilikuwepo juzi nimeona kwa mboni zangu mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la wawekezaji na nitawapa mfano mdogo. Mwezi Desemba rafiki yangu alikwenda nyumbani na gari aina ya *Toyota Noah*, mdogo wake mdogo kabisa akamwambia Kaka umekuwa fisadi, akamuuliza kwa nini, akamwambia umenunua gari la *Noah*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwashauri Watanzania wenzangu kwamba huwezi kupambana na umaskini ukiogopa utajiri. Kama kuna mtu ni fisadi mumpeleke Mahakamani ili wimbo wa fisadi uishe. Ninyi mnaowaita wenzenu mafisadi kwa sababu wanatembelea *Noah*, mnataka watembelee tumbo? Kama mtu ni fisadi, anahujumu, mtafute Wanasheria ili mumpeleke Mahakamani mambo ya ishe, *Noah* ni ujisadi? Kwa hiyo, ndugu zangu mambo ya kusema mafisadi yafike mwisho.

Mheshimiwa Spika, nirudie kwa niaba ya Kamati kuizungumzia *TANESCO*. *TANESCO* wanafanya kazi kubwa lakini wamebanwa mbele na nyuma, wana hali ngumu, wananaunua umeme ghali na wanauza rahisi. Waziri tumekushauri katika Kamati uwaangalie watu hawa, huenda upungufu wao unatokea hapo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Meneja wa *TANESCO* Muleba kwa kazi nzuri anayofanya ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Muleba. Wananchi wangu wamefikia hatua ya kutaka kuchanga ili kufikisha umeme.

*(Hapa kengele illilia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Jerome Bwanausa, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Buyogera wajiandae.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kweli ningesikitika sana kwa sababu nilikuwa na salamu za kutoka Kilindi.

Mheshimiwa Spika, inasemekana kwamba usiposhukuru kwa machache na makubwa huwezi kuyapata. Kwa niaba ya wananchi wa Kilindi ambao ndiyo nawawakilisha hapa, nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nimshukuru sana pia Naibu Waziri wa Madini, Kamishna wa Madini, Katibu Mkuu na wengine wote, kwa jinsi walivyoweza kushughulikia mgogoro ambao ulikuwa sasa unaingia kwenye sura tofauti ambayo kwa kweli ilikuwa inatuzuia kufanya maendeleo zaidi ya kuzungumzia mgogoro mmoja. Mgogoro huu ulikuwa katika eneo ambalo lilikuwa limetengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo yaani eneo tengefu. Katika eneo hilli wallikuwa wamepewa watu wa Ashanti ubia lakini leseni yao ilikuwa inapita kwenye maeneo ya vijiji vinne. Vijiji hivi vinne havikupewa haki yao mpaka hawa wakubwa niliowataja walipoweza kusimama kidete na kutoa maamuzi na hakika sasa tunashukuru. Vilevile nimeombwa sana kumshukuru Mheshimiwa Ngeleja kwa wakati wake, Mheshimiwa Malima na Mheshimiwa Kafumu wakiwa pale wao ndiyo walianza mchakato ambao sasa tumehitimisha, tumekuwa huru sasa na nafurahi kusema pale juu kwenye *gallery* kuna wananchi wametoka katika vijiji hivyo vya Msamu, Kikunde na Ludewa ambao wamekuja kushiriki siku ya leo na kuleta salamu za shukrani kubwa sana. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wangu nasema ahsanteni sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tumeahidiwa jana na Mheshimiwa Waziri kwamba tarehe 3/6 wanakwenda watafiti kutoka Wizara ya Madini *Geological Survey* watafika kule katika eneo husika ili kutathmini ukubwa wa eneo na mali iliyopo na kutoa maelekezo nini kifanyike. Kwa hiyo, tunaendelea kumshukuru sana Profesa Mduma. Vilevile tumeahidiwa na Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Maselle kwamba mafunzo yatakwendwa mara moja kwa watu wale ambao ni zaidi ya vijiji 12 na kwa sababu Kilindi

kila sehemu ni madini kwa hiyo kote kule wameahidi kwamba watatupa mafunzo kwa hiyo tunaendelea kushukuru. Tumeambiwa tukishajlunga kwa taratibu ambazo tutaelekezwa na wataalamu basi watu wetu wataweza pia kupata mikopo pamoja na maelekezo ya jinsi ya kutumia maeneo hayo kwa njia ya usahihi. Kipekee kwa niaba ya wananchi wangu, naomba niseme ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, niseme namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Simbachawene. Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Mr. Mwakahesya wa REA. Hawa nao wametusaidia sana, ni kweli tulipata umeme kipindi cha mwaka 2010 lakini wameendelea kuwa bega kwa bega na sisi na kusikia kilio chetu kila tulipokuwa tunakipeleka kwao, kwa hiyo, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, niendelee tu kusema kwamba pamoja na shukrani, kuna mambo machache ambayo ni lazima niyaseemee. La kwanza kabisa, tunashukuru kwamba tumepewa umeme katika awamu hii ya mwaka 2013/2014 katika vijiji vinne, Gairo ambayo tunapakana nao ambapo ndipo umeme utapita imepewa vijiji sita. Tumekaa na mwenzangu Mheshimiwa Shabiby tukaangalia vijiji vingine, wengine wana vijiji mpaka 50, 60 au 69 lakini sisi tumepewa kidogo ambapo kwa kweli umeme ndiyo kwanza umeanza kungia katika Wilaya zetu. Kwa hiyo, naomba tu nilisemee hilo.

Mheshimiwa Spika, lakin zaidi ya hapo, katika Wilaya ya Kilindi, vile vijiji vitatu ambavyo vimetajwa, Kijiji cha Mswaki, Mgera na Kwamaligwa, tayari umeme umepita pale. Mwaka 2011 niliuliza kwa nini umeme umepita lakini *transformer* haziwekwi watu wakanufaika na umeme? Nikaambiwa *transformer* hazikuwepo lakini zikifika tutawekewa. Mwaka 2012 nikaauliza swali hilohilo nikaambiwa sasa zimefika lakini zile nguzo fupi za *distribution* hakuna. Sasa niulize, hii ni miradi mipya au tunakwenda kukamilisha kazi ya awali? Kama ni kukamilisha kazi ya awali basi naomba vijiji vitatu katika Wilaya ya Kilindi, kati ya vijiji 102, vijiji 86 havina umeme wala hawajawahi kusikia,

naomba basi vile vijiji vitatu ambavyo tayari umeme ulipita ni kukamilisha tu kuweka *transformers*, basi vijiji hivi viongezwe lakini niseme tu nashukuru.

Mheshimiwa Spika, vilevile umeme Kilindi muda mwinci sana umekatika, sisi tupo kwenye *constant* mgawo, mgawo hauishi, mara *transformer* imeungua, mara nguzo zimeanguka yaani hatumalizi wiki tukiwa na umeme wa kudumu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, suala hili nimelifikisha mara kadhaa kwenye ofisi yetu ambayo iko Handeni vilevile nimelifikisha hata Tanga, lakini inaelekea tatizo ni kubwa zaidi. Naomba sana tuweze kusaidiwa kwa upande huu.

Mheshimiwa Spika, ofisi ya Madini Wilaya ya Kilindi ni mwaka wa nne huu tunaomba tuwe na Ofisi ya Madini. Robo tatu kama siyo yote ya Wilaya ya Kilindi ni Madini matupu ambayo tumeyatambua na ambayo hayajatambuliwa yaani yanayoendelea kutambuliwa. Tunaomba Ofisi ya Madini kwani kwenda Handeni kilomita 132 ni mbali na hata usimamizi unakuwa ni mgumu na ndio maana hata watu wetu hawawezi kupata elimu ya madini. Naomba sana Ofisi ya Madini, sasa jamani mlisema tuwape chumba, chumba kipo, njooni mfunge vifaa, tupeni wataalamu Mheshimiwa Waziri ili na sisi tuweze kufanya kazi na kuona tunanufaika vipi kwa kushirikiana nao ili tuweze kuona Wilaya yetu inanufaika vipi na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, toka tarehe 27/7/2012, Serikali ilipandisha gharama kwa kiwango cha juu na gharama hizi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa hizi leseni za utafutaji madini kutoka dola 100 mpaka 300, kodi ya mwaka dola 40 mpaka 100 kwa kila kilomita ya mraba ambayo hii kwa kweli ni fedha kubwa mno. Sasa kodi hizi zimekuwa ni kubwa, tumeendelea kupokea malalamiko mengi sana ambapo wananchi wa kawaida ambao wamethubutu kuingia kwenye shughuli hii, kwa kweli wanashindwa kuzimudu. Sasa mimi naomba kwa sababu kuna taarifa kwamba wengi sasa wanasema bwana

tumeshindwa inabidi tuachie, mimi naomba kweli suala hili sasa liangaliwe kwa upya ili kuhakikisha kwamba hatuathiri uchumi wetu na hawa Watanzania ambao wamekuwa wakifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wachimbaji wadogowadogo kama wa Kilindi ambao kwanza hawana elimu lakini pili wanachimba na nyundo na sululu, wana mazingira duni na hata hayo madini yenyewe mpaka wayapata madeni ni makubwa. Kulikuwa hakuna kulipia ada ya maombi ya leseni ndogo lakini sasa hivi wanatozwa Sh.50,000/=. Ada ya kutayarisha leseni kutoka Sh.20,000/= imekwenda kuwa Sh.50,000/=. ada ya mwaka ya leseni kwenye vito, almasi na dhahabu ni Sh.20,000/= hadi Sh.80,000/=, madini mengine kutoka Sh.10,000/= mpaka Sh.50,000/=, jamani hawa wananchi wanashindwa. Kuna dhana inayosema kwamba watu hawapendi kulipa kodi lakini tumefanya tathmini ya kuona kwa nini hawataki kulipa kodi? Kwa sababu mwananchi wa Kilindi anachukua muda mrefu kuchimba anakuja kupata gramu mbili lakini akiziuza anakuwa na madeni kuzidi ile gharama na hao wengine hali kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi naomba pamoja na kwamba sheria ya mwaka 2010, kifungu 112 inamruhusu Waziri na Ofisi yake kuweza kubadilisha hivi viwango vya tozo lakini palepale nimeona kuna kipengele cha tatu mbali na kusema kwamba ni lazima washauriana na Waziri wa Fedha na Kamishna na kadhalika labda hayo aliyafanya, anasema atashauriana na wadau wa sekta ya madini pamoja na wachimbaji wadogo, sasa hawa hawakuhusishwa. Mimi naomba ili tusiwaathiri, nia ni njema, Serikali inahitaji kupata mapato, tunakubali kabisa nia ya Waziri najua ilikuwa ni njema lakini basi tufanye utafiti tuone kweli tunachokifanya ni sahihi kwamba kitawasaidia hawa watu au ndiyo tunawaondoa kwenye sekta hii?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nisichukue muda mrefu, lengo langu kubwa lilikuwa kusemea hayo mambo mawili ya msingi sana ambayo nimeona kwa leo,

nikirudia tena kuwashukuru kwa niaba ya wananchi wa Kilindi. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Nimwite Mheshimiwa Jerome Bwanausi atafuatiwa na Mheshimiwa Mnyaa halafu Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia kwenye Wizara hii kwa kuungana na Wabunge wenzangu wote wanaosema *REA* kupatiwa fedha za kutosha kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini ni jambo muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe masikitiko yangu kuhusiana na Jimbo langu la Lulindi. Kwa kweli huyu mgeni *REA* wananchi wa Lulindi wanamsikia tu, naomba sana Wizara ihakikishe katika awamu hii vijiji vilivypopo katika Jimbo la Lulindi ambavyo havikupata awamu ya kwanza kabisa, viweze kupewa nafasi ili wale wananchi wa Kata za Chiwata, Mpindimbi, Nanjota, Mbuyuni, Namalenga, Navila pamoja na Chikolopola waweze kupata umeme katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na Mchaulu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ningeweza pia kumsemea Mheshimiwa Dkt. Kikwembe ambaye Wilaya yake ya Mlele, Inyonge inafanana na Jimbo la Lulindi, Kata zake zote hazijapata umeme nadhani ni vizuri nazo zikaweza kupata nafasi ya kupata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la ofa iliyotolewa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ya Sh.99,000/= . Mimi naishauri Serikali kupitia Wizara kwamba ofa hii isiwe ya vipindi vyatia miezi sitasita, ni vizuri sasa ikatangazwa kwamba ofa hii ipo ya kudumu kwa sababu tangu tutoe ofa hii wananchi wengi hawajanufaika kwa sababu upatikanaji wa vifaa kupitia *TANESCO* umekuwa ni wa kusuasua sana, kwa hiyo, ni vizuri hii ofa iwe ni ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka kulielezea ni juu ya kukatikakatika kwa umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Suala hili sasa ilmekuwa ni tatizo sugu. Bbahati nzuri sana Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa sasa haitumii gridi ya Taifa na tunao umeme wa kutumia gesi Mtwara lakini upo upungufu ikiwa ni pamoja na nguzo lakini kuna vifaa ambavyo *TANESCO* wanadai kwamba vinasambabisha umeme huu kukatikakatika. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri atakapokuwa anahitimisha hotuba yake, ajaribu kuwaeleza wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi hili tatizo la kukatikakatika kwa umeme litamalizika lini?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la upatikanaji wa vifaa kwa mfano mita za Luku, kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Maeneo mengi nchini ikiwa ni pamoja na Mikoa ya Kusini tumeanza kuwekewa Luku lakini unakuta kwamba kila wananchi wanapotaka kwenda kuomba, kwa kweli upatikanaji wake umekuwa ni wa kusuasua sana. Ni vizuri niishauri Serikali kupitia Wizara kuhakikisha jambo hili linafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la uwekaji wa viwanda katika maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Mimi naishauri Wizara kwamba ni vizuri ikatoa maeleo thabitii juu ya namna gani itakavyoweza kuweka vivutio vitakavyofanya wawekezaji wa viwanda wavutike kwenda kuwekeza katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Moja ya pendeleko ambalo napendelekeza kwa Wizara ni kwamba ni vizuri bei ya Gesi Mtwara na Lindi iwe tofauti na maeneo mengine ili kuvutia wawekezaji waone ni nafuu zaidi kwenda kuweka viwanda katika Mikoa hili badala ya kuweka katika maeneo mengine ambayo gesi itapelekwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine muhimu sana ni upatikanaji wa ardhii Mtwara kwa ajili ya wawekezaji, napo kusiwe na urasimu ili wawekezaji waweze kuona kwamba ni vizuri wawekeze viwanda vyao pale.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nashauri kuhusiana na maeneo haya ni suala la mafunzo. Suala la

mafunzo katika maeneo haya kuanzia kwenye ngazi ya Vitongoji, Vijiji, Mitaa pamoja na Wilaya na Mkoa kwa ujumla ni jambo muhimu sana. Naiomba sana Wizara wala wakati mwengine isione kwamba inapoteza fedha kwa ajili ya kufanya jambo hili bali jambo hili ni muhimu hasa ukizingatia kwamba sekta ya gesi katika nchi yetu ni jambo geni sana. Kwa hiyo, elimu inabidi itolewe vya kutosha ili wananchi waweze kunufaika kuielewa vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la kupewa kipaumbele kwa wananchi wa Mikoa hii hasa vijana kuingia kwenye mafunzo ya sekta ya gesi, madini na petroli. Bado utaratibu uliopo sasa nadhani unapaswa uboreshwe kwa sababu hata matangazo yanayotolewa sidhani kama yanafika mpaka kwenye ngazi ya Vijiji na Kata kwamba kunahitajika vijana. Kwa hiyo, kama kweli tumedhamiria kuwasaidia vijana hawa, ni lazima matangazo haya yawe wazi na yatangaziwe Mtwara na Lindi siyo Dar es Salaam ili wananchi waweze kupata unafuu wa kupata taarifa na kuweza kushiriki kikamilifu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mambo haya mengi ambayo yanazungumzwa na niwathibitishie wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwamba Kamati ya Nishati na Madini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mwenyekiti Victor Mwambalaswa inafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba inayatembelea maeneo hayo yote na kuweza kupata fursa ya kuzungumza na wananchi ili waweze kutoa dukuduku zao na kupata ufanuzi wa mambo mbalimbali ambayo yanatokana na hali iliyopo kule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana na napenda kuishauri Serikali ni juu ya makampuni ambayo yanapata nafasi ya kwenda kutoa huduma katika maeneo haya ya Mtwara na Lindi. Hivi sasa hata wafagizi na mamesenja wanatoka Dar es Salaam na maeneo mengine. Pamoja na kwamba *tender* zinatangazwa lakini ni vizuri wakati mwengine Serikali ikatoa maelekezo kwa hawa wanaoandaa hizi *tenderkwamba* wale wanaoshinda wahakikishe baadhi ya kada ambazo si za kitaalamu zaidi

ziweze kutoa fursa kwa wananchi wa maeneo haya ili waweze kupata ajira ili waondokane na matatizo yanayowakabili.

Mheshimiwa Spika, nilitaka pia nizungumzie suala la kutoa vipaumbele vyta walau mikopo midogomidogo kwa wananchi wa Mikoa hii. Kwa sasa ni kweli kabisa nyanya, nyama na kadhalika havitoki kwenye Mikoa labda kwa sababu upatikanaji wa bidhaa hii si wa kutosheleza kwa mahitaji ambayo yanatolewa. Sasa kama wananchi hawakupewa fursa ya kupewa mikopo kwa ajili ya ufugaji na kilimo, hata tukiwahamasisha kwamba walime ili wapate soko bado watakuwa katika mazingira magumu sana. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa vipambele vyta mikopo wananchi hawa ili wapate fursa ya kuweza kuchangia na kushiriki katika kunufaika na masoko yanayotokana na maeneo haya kutokana na upatikanaji huu wa gesi katika maeneo haya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana na sasa nimwite Mheshimiwa Engineer Mnyaa na Mheshimiwa Ole-Sendeka na wa mwisho ni Mheshimiwa Buyogera.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:
Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, mimi sitazungumzia gesi Mtwara baada ya Profesa Lipumba kuongea jana na Waandishi wa Habari na nafikiri maelezo yake yake kwenye mtandao. Vilevile tunategemea busara ya Bunge lako ambapo wananchi wa Mtwara bado wanaamini Wabunge wao.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita katika hotuba ya Waziri juu ya kitu ambacho kipo ukurasa wa 58, kwa ufupi kinaitwa *TEITI - Tanzania Extractive Industry Transparency Initiatives* au kwa Kiswahili Mpango wa Uhamasishaji wa Uwazi katika Mapato ya Madini, Gesiasilia na Mafuta.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, ni lazima nilishukuru Bunge lako Tukufu kwa vipindi au utaratibu tunaoita wa kuwajengea uwezo Wabunge au *capacity building* ambapo mimi pia nilibahatika wakati wa Bunge la Tisa kuhudhuria semina mbalimbali zinazohusiana na *Tanzania Resource Watch, FNF*na hii *TEIT/I*liyokuwa based Oslo. Nishukuru kwamba mambo haya sasa yameleta matunda kwa Jamhuri na mbio zetu za kutaka kiundwe chombo kama hiki katika Tanzania na kijiunge na jumuiya ya Kimataifa zimefanikiwa na mwaka 2007 Tanzania ilifanikiwa kujunga na sasa hivi tuna *Tanzania Extractive Industry*.

Mheshimiwa Spika, hatua hii imeleta manufaa kwani baada ya kuundwa tu kwa chombo hiki, Wizara hii ya Nishati na Madini ilikitumia na waliweza kupata *Hart Nurse Limited, ni Chartered Accountants* (UK) pamoja na *BDO* ya *East Africa*. Katika ripoti yao ya kwanza ya *reconciliation* wakagundua madudu makubwa kwamba Tanzania tunaibiwa kupitia makampuni yanayowekeza katika rasilimali za madini. Ripoti ile iliweza kugundua kiasi cha shilingi bilioni 254.9 ambazo Serikali ilikuwa haijalipwa kutoka kampuni ya *TPCC*. Bahati nzuri baada ya kugundulika, tarehe 16 Julai, 2012, fedha hizi zimeweza kulipwa Serikalini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika ripoti hiyo waligundua kwamba kuna dola milioni 18 pamoja na shilingi za Kitanzania milioni 657, pia kuna Sh.24,115,000,000/- ambazo zinatokana na *royalties* na kodi mbalimbali kama vile *Pay As You Earn (PAYE)* ambapo ilionekana *discrepancies* kwamba Serikali imekosa mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutokea matatizo hayo, *CAG* akaingilia kati katika ile *reconciliation report* na baadaye akagundua kwamba, hata kama si zile dola za Marekani milioni 18, ni kweli ziko fedha shilingi bilioni 2.1 mapato ambayo hayaonekani kama yalilipwa na kuingia Serikalini. Kwa hiyo, fedha hizi zikatakiwa zilipwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka Mheshimiwa Waziri anijulishe au alijulisha Bunge hili, je, hizi fedha zilizogunduliwa

na *CAG* sasa zimeishalipwa au bado? Kama hazijalipwa, ni kwa nini? Kama hazijalipwa katika muda wote huo ina maana pia tunawenza tukagundua jambo lingine katika mfumo wetu wa *TEITI Tanzania*, inawezekana bado hakuna sheria ambayo ina- enforce utendaji kazi wa *TEITI* ili pale upungufu unapojitokeza kwamba wale wanaotakiwa kulipa walipe na iwepo sheria inayowabana. Ningombaa Wizara ilichukulie hatua jambo hili na iwepo sheria maalum ya *TEITI* ambayo itayabana yale makampuni ambayo hayajalipa nayo sasa yalipe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna ripoti ya pili ambayo ili-*cover* muda wa kuanzia Julai, 2009 mpaka Juni, 2010. Ripoti hii pia ikaendelea kugundua madudu ya ubadhirifu au upotetu wa fedha na mara hii wakagundua kuna shilingi bilioni 727.2 ambazo pia zilikuwa ni mapato ya Serikali na hazijalipwa. Kati ya fedha hizo, shilingi millioni 543.7 zinatokana na kodi mbalimbali. Katika hii ripoti ya pili pamoja na *addendum* yake, yakagundulika mambo mengine makubwa kwamba, kuna matatizo baina ya *GGM* na *TRA* kuhusiana na shilingi bilioni 35 ambazo hazionekani. Sasa kukawa kuna kurushiana mpira; *GGM* wakawa wanasesma wameishalipa *TRA* na *TRA* wanasesma fedha hizo hazionekani.

Mheshimiwa Spika, hili limeleta mzozo mkubwa, lakini la ajabu ni kwamba, hawa watuhumiwa wawili *GGM* na *TRA*, tarehe 18 Desemba, 2012, *TRA* inaiandikia *TEITI*, barua Na. *TRA/HQ/DIA/1.1* ikieleza kwamba zile fedha shilingi bilioni 35 ambazo zilikuwa hazionekani wameshaziona na ilikuwa ni *double payment*ya VATna kodi nyingine, kwa hiyo, ni kweli *GGM* wameilipa *TRA*. Sasa jambo hili kidogo linashangaza; watuhumiwa wawili wanakubaliana, yule aliyekuwa anamwambia mwenzake kwamba nimekupa fedha na huyu anasema fedha hazijaonekana na hawa *BDO East Africa* wakagundua fedha hizi hazijalipwa, sasa *TRA* anasema nimeishaziona, mahesabu yalikuwa yamekaa vibaya, ni *double payment*, hii kidogo inatia wasiwasi. Naiomba ofisi ya *CAG* waingilie kati jambo hili waone nini kinaendelea, kwa sababu kama wewe ni mtuhumiwa huwezi kusema fedha nimeiona na kweli umenilipa wakati *chartered*

accountants waliopewa kazi hiyo waligundua matatizo hayo. Kwa hiyo, tunaiomba ofisi ya CAGkupitia kwako iingilie katika suala hili na tujue haswa fedha hizi zimepotelea wapi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mpango huu ambao unafanyika *TEITI* usiishie katika kuchunguza fedha zinazolipwa na makampuni makubwa, bali mpango huu wa uhamasishaji wa uwazi kuhusu matumizi na rasilimali za madini, unahitaji kuchunguza hata fedha inayolipwa Serikalini ionekane inatumiwa vipi, inawasaidia wananchi kwa namna gani na imelisaidia vipi taifa katika nyanja nyingine mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu ambapo ripoti mbalimbali zinaletwa Bungeni, lakini bado ripoti za *TEITI* hatuzipati hapa Bungeni. Tungeshauri kupitia ofisi yako ripoti hizi nazo zilete hapa kwa sababu zina mambo mengi ambayo yatawawezesha Wabunge kujua zaidi na kupata ufanuzi kuhusu ripoti hizi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka nije katika ukurasa wa 34 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alianza kwa kueleza kwamba, bajeti yake hii si ya porojo, bali ni ya tarakimu. Sasa katika ukurasa ule kuna habari ya zile *MW 400* Mtwara pamoja na Kv 220, fedha hii mbona hatuioni katika bajeti yake? (Makof)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Haya ahsante. Sasa nimwite msemajji mwingine, Mheshimiwa Christopher Ole - Sendeka na tutamalizia na Mheshimiwa Agripina Buyogera.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE - SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, amani ya Tanzania, ni tunu isiyostahili wala isiyopaswa iruhusiwe kuchezewa na yeoyote

yule, wakati wowote ule na kwa sababu yoyote ile. Natambua yanaweza kuwepo mahitaji na madai ya haki lakini ni vizuri yakaombwa au kudaiwa kwa njia stabili bila kuvuruga amani na umoja wa Kitaifa. Kwa sababu hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, kwa maelekezo aliyojatoa ambayo yanastahili kuungwa mkono na Watanzania wote bila kujali itikadi wala dini yoyote ile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawasihi sana wenzangu wa Mtwara waendelee kuieleza Serikali madai yao na naisihi sana Serikali yetu iendelee kuona umuhimu wa kusikiliza matatizo ya wananchi wa Mtwara, maana wale ni watu wazima na wana akili zao, hawawezi wakapiga kelele bila kuwa na sababu ya msingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, natambua sana umuhimu wa sekta ya gesi katika kuleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya nishati. Kama kuna mzigo mkubwa unaobebwa na Serikali yetu kupitia *TANESCO*, ni kuendelea na mitambo inayotumia mafuta mazito lakini zaidi mitambo ya kukodi. Ukienda kwenye taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini ya sasa na Kamati zilizopita, tuliomba sana Serikali iwekeze kwenye sekta hiyo ili kuhakikisha tunapata mitambo yetu wenyewe ili tuepukane na gharama tunazopata kutokana na mitambo ya watu binafsi. Napenda kuona sambamba na mradi wa kuvuta umeme kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam, nione mkakati wa dhati wa kuhakikisha mitambo itakayokuja kuzalisha umeme Dar es Salaam na Mtwara ni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na siyo ya watu binafsi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kutumia mitambo ya kokodi, tutaleta gesi Mtwara, tutapeleka gesi Tanga, tutapeleka gesi popote, lakini kama tunapeleka kwa mitambo ya watu binafsi tutaendelea kuumia. Taarifa ya Waziri inathibitisha kwamba, tunatumia zaidi ya shilingi bilioni tano ambazo ni zaidi ya dola za Marekani bilioni moja kwa mwaka, ambazo ni sawa na shilingi trillioni 1.6. Kwa hiyo, kama tutaendelea na mitambo hii ya kukodi maana yake ni

kwamba, tutakuwa hatujamsaidia Mtanzania wa kawaida. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninatambua jitihada na dhamira njema ya Waziri Muhongo katika kuhakikisha kwamba mzigo huu unapungua, lakini ninataka nimshauri Profesa Muhongo kwamba siku zote asikubali kuuziwa mbuzi kwenye gunia. Ni vizuri akawa shahidi, akathibitisha, akawa Thomaso, asije kuingizwa mjini kama alivyoingizwa mwaka jana wakati wa bajeti iliyopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliliambia Bunge hili kwamba kulikuwa na nguzo zinatolewa Iringa zinakwenda Mombasa, zinakwenda Afrika ya Kusini kisha zinarudi hapa nchini kwa bei ghali na ni *deal* ya watu wachache. Mheshimiwa Waziri amesema *compliance* ya shillingi billioni 16 tuliyohojî kuhusu ununuaji wa mafuta ya PUMA ambao haukuzingatia Sheria ya Manunuzi, nikahoji kwenye Kamati ya Nishati na Madini na amezungumzia habari ya misumari. Nataka nilihakikishie Bunge lako hili kwamba kauli zake hizo zimethibitishwa na ripoti ya *Controller and Auditor General* kwa kutumia kampuni ya *Ernest & Young* iliyothibitisha kwamba hoja zile Mheshimiwa Waziri alizoletewa na wasaidizi wake na ye ye kuzitamka Bungeni ni za uongo kwa kiwango ambacho hakiwezi kuonewa haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitibitishe, ripoti hii hapa ya *Ernest & Young* na nitaiweka Mezani ili kama kuna mtu anabisha, kuthibitisha wazi kwamba, kauli ya Waziri alioambiwa na wataalam wake ni ya uongo. Tena naitamka vizuri na akitaka aende kwenye ukurasa wa 79 wa ripoti hiyo kwa upande wa nguzo, ukurasa wa 211 na aendee kwenye ukurasa wa nane (8) kwa upande wa shillingi billioni 16 ambazo Maswi alizitumia bila kushirikisha Bodi ya Zabuni ya Wizara, wala kushirikisha Bodi ya Zabuni ya TANESCO. Ripoti ya *CAG* iliyokaguliwa na kampuni ya *Ernest & Young* ipo kwenye Bodi yake ya *TANESCO*, imefungiwa na haitakiwi kutolewa hadharani kwa sababu Katibu Mkuu wake anahuksika. Leo tena Mheshimiwa Waziri anaingizwa mjini kwa mara ya pili katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, tulipitisha Sheria hapa ya Madini tukasema vito vichimbwe na Watanzania kwa asilimia 100. Tukasema leseni itolewe kwa Mtanzania na yeye aombe kumleta mgeni, kama anahitaji teknolojia au mtaji zaidi, kwa ushauri wa Bodi ya Ushauri wa Madini. Kana kwamba hiyo sheria hawakuisoma wataalam wako, Kamishna juzi ametoa leseni kinyume cha sheria. Nazungumza kinyume cha sheria na nitatamani na nitaleta maelezo hapa kwa sababu dakika 10 hazitoshi. Kwanza sheria iko hivi, leseni imetolewa kwa *STAMICO* ikishirikiana na *Tanzanite One Mining Ltd*, wakati ambapo ninazo *certificates* zao hizi hapa, wamebadilisha majina mara kadhaa kwenda *Richland* kutoka *Tanzanite One*. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri nitampa nyaraka hizi ili athibitishe kwamba hata hicho walichoingia mkataba huenda hakiishi kwa mujibu wa uhalali wa kisheria. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimesema hili na waangalie pia suala la Buhemba. Hakuna sababu ya baba kugombana na watoto wake, wapeni wachimbaji wadogo maeneo fulani pale Buhemba. Mtasema *STAMICO*, leo mnaleta *STAMICO* pale Mererani, mtaletaje *STAMICO* Mererani? Ni sawasawa na mama kunogewa na uji wa watoto akaunywa yeye badala ya kuwapa watoto.

Mheshimiwa Spika, nataka Mheshimiwa Waziri anipe majibu, hii ni nakala ya gazeti la Mwananchi la tarehe 26 Oktoba, mwaka 2010, ambapo Mheshimiwa Kikwete, alipokuwa Olkesemet alisema, mara baada ya leseni ya *Tanzanite One* kwisha nitawagawia wachimbaji wadogo. Mheshimiwa Rais Kikwete amesema, Mheshimiwa Waziri asome gazeti hilo na nitaweka Mezani kama anahitaji maana ninaona anatikisa kichwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie jambo moja, anasema hivi mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Jakaya Kikwete, amewahakikishia wakazi wa Wilaya ya Simanjiro, Mkoani Manyara kuwa wachimbaji wadogo watapatiwa maeneo kwenye mgodi wa madini wa *Tanzanite One* mara leseni ya kampuni hiyo itakapomaliza

muda wake. Hii ni kauli ya Rais Kikwete, Wizara inakwenda kinyume na kauli ya Rais! Nataka kujua Rais ni Muhongo au Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete? Kama kauli ya Rais haiheshimiwi, nathibitisha magazeti ya tarehe 26 Oktoba 2010 someni, lakini ukitaka hata mikanda ya video, waulize wasaidizi wa Rais wakwambie. Nilimwambia Mheshimiwa Waziri, tatizo lake ni kwamba hawataki kusikiliza hili, lakini zaidi msiingize mwamvuli huo mnajua kuna mgogoro. Tume ya Boman, Tume ya Jenerali Mboma ilisema baada ya leseni ya kampuni kubwa kwisha wapewe wachimbaji wadogo, leo mnailleta *STAMICO*, *STAMICO* inakwenda kwenye *strategic minerals*, wapelekeni kwenye urani. Leo hata kwenye urani yenye pale bado hamjawapa, mnaendelea kuzungumza, hata ushauri wa Bodi yenye ilisema kwamba, msitoe leseni mpaka pale ambapo wawekezaji wale watakapoweza kutoa ile *free carried ya shares* zile kwenye kampuni ya *STAMICO*. Hilo nalo bado halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu tuna kazi ya umeme wa *REA* vijijini. Waheshimiwa Wabunge wote mnajifurahisha hapa, kama hamjatatua tatizo la uhamishaji wa fedha kutoka kwenye *REA* kwenda kwenye mitambo ya kukodi ya watu binafsi, hamwezi mkapata fedha za umeme vijijini. Vijiji villivyoorodheshwa pale, leo mimi ni faraja

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Muda umeisha.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, sitaunga mkoно hoja mpaka hapo itakapopata maelezo stahiki. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Buyogera!

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba wa kuwasemea wananchi wa Jimbo langu la Kasulu Vlijijini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwanza niishukuru Kamati ya Uongozi ya Bunge, inayoongozwa na wewe kama Mwenyekiti, kwa kuahirisha Bunge kwa muda wa siku mbili ili tuweze kupata utulivu wa kutosha kulingana na tatizo kubwa lillolokuwa limetokea kule Mtwara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba niungane na Wabunge wote wanaosema *REA* iongezewe fedha. Kwa kuwa mimi ni Mbunge wa Vijijiini, ninaunga mkono kwa asilimia mia moja, Serikali isikie na ihakikishe inatafuta fedha za kuwapatia *REA* ili wananchi tunaotoka vijijiini tuweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, nikiwa naendelea na *REA*, naomba niwashukuru na kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya vijijiini. Nimekuwa nikilalamika humu Bungeni tangu niimeingia kwamba, Jimbo la Kasulu Vijijiini lenye kata 19 hakuna kijiji hata kimoja ambacho kina umeme, lakini kwa kupitia *REA* angalau wameweza kupeleka umeme kwenye zahanati ambapo nafikiri wataweza kufikisha umeme wa *solar* kwenye zahanati zote za Jimbo la Kasulu Vijijiini na vituo vy'a afya. Niombe zoezi hili linalofanyika huko wajitahidi kufikisha hizo *solar* kwenye shule za sekondari katika jimbo la Kasulu Vijijiini ili vijana wetu waweze nao kuiona dunia mpya baada ya uhuru wa miaka 50.

Mheshimiwa Spika, katika salamu hizo njema kwa Jimbo la Kasulu Vijijiini, ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotaja vijiji vilivyopata neema ya kuingizwa kwenye ramani ya Mheshimiwa Waziri na mimi nivitaje ili na wananchi wangu huko waanze kujiandaa. Kijiji cha kwanza ni Nyachenda, cha pili ni Nyakintonto, cha tatu Makele, cha nne Mvugwe, Nyamidaho, Nyumbigwa, Lungwe Mpya, Titye, Nyenge, Kasengezi, Lusesa na Kwaga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huu ni mwanzo mzuri, Waswahili wanasema asiyeshukuru kwa kidogo hata kikubwa hawezu kushukuru. Mimi ni mungwana, naomba nishukuru, lakini nashukuru kabla umeme haujawaka, shukrani zangu

naomba zisipotee bure. Tafadhali mhakikishe umeme umewaka katika vijiji nilivyovitaja ili kuwapa matumaini wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwamba hata vijiji vilivybaki vina uhakika wa kupata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye madini. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini amewahi kutembelea Kasulu na alipotembelea Kasulu, alitembelea kijiji cha Makere, aliongea na vijana wachimbaji wa chokaa. Pale kuna mgogoro ambao kwa akili za kawaida sioni kwa nini mgogoro ule unaendelea. Wizara ya Nishati na Madini imewapa leseni watu wachimbe chokaa lakini Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Mazingira wanawakimbiza kila siku wanasema kwamba wasichimbe hawaitambui leseni. Sasa mimi ninashindwa kuelewa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Baraza la Mawaziri ni moja, iweje Wizara hii inatoa leseni halafu Wizara nyingine inaenda kuwakimbiza Watanzania kama wakimbizi? Naomba suala hili Mheshimiwa Waziri muwasiliane na Wizara nyingine muweze kulitatu.

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu wa kulimbikiza matatizo madogo madogo na kuyaacha yakawa makubwa, Wabunge tunakuja hapa kutimiza wajibu wetu wa Kikatiba, lakini viongozi hamtaki kutusikia, haya ndiyo mambo ambayo mnayalimbikiza na baadaye yanaleta matatizo makubwa bila ya sababu ya msingi. Ukienda Kasulu pale Jimbo la Kasulu Vijijini mimi ndiyo ninayemsaidia Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Mheshimiwa Rais amepigwa kura pale na mimi nimepigwa kura na wananchi wale. Kwa hiyo, kilio chao ni wajibu wangu mimi kukifikisha hapa Bungeni. Sasa kama ninakifikisha hapa Bungeni ili kumsaidia Mheshimiwa Rais siku akitembelea kule asihojiwe maswali yasiyokuwa na maana nyie hamtaki kunisikia. Naomba hili walichukue na tatizo la wachimbaji wadogo wa Makere litatuliwe. Naomba nisisitize msikubali kabisa kupambana na Majimbo yanayoongozwa na akinamama, ni hatari, kwa sababu hakuna mwanamume yejote aliyepo duniani ambaye hajazaliwa na mwanamke.

Sasa usifike mahali ukankasirisha, nikikasirika hata mama yako aliyezuzaa atakasirika, awepo au awepo kaburini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaongea maneno haya kwa uchungu kwa sababu tangu nimeingia Bungeni ninaillilia Makere. Chokaa iliyopo kijiji cha Makere inatumika tangu wakati wa mkoloni. Majengo yote wanayoishi viongozi wa Serikali katika Mkoa wa Kigoma tangu enzi za mkoloni yamejengwa kwa chokaa inayochimbwa Makere. Iweje tusiwaandalie mazingira mazuri hawa wananchi wa kijiji kile na wao wakanufaika, wakajidai kupata maisha bora kwenye nchi yao kama mnavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, la pili na nadhani ni la mwisho. Naomba Wizara iandae wataalam waende kutembelea kijiji cha Nyenge. Kule kuna madini ambapo wananchi kule wanayachimba kwa kienyeji na wanauza kwa bei ya kutupa shilingi 3,000 mpaka 5,000. Mheshimiwa Naibu Waziri hizi taarifa unazo, ninaomba ulifanyie kazi. Kwanza, itasaidia pato la Taifa, lakini pia itasaidia kuwaondolea umaskini. Juzi nimezungumza hapa, nikasema wananchi wa Mkoa wa Kigoma hatuna sababu yoyote ya kuitwa maskini kwa sababu tuna utajiri wa kutosha. Sasa wakati umefika mtuandalie wataalam waende wakafanye utafiti, waangalie madini yanayopatikana katika kijiji cha Nyenge ili yaweze kuwasaidia wananchi kule, lakini pia yasaidie kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, nimesema ninawasilisha hoja za wapiga kura wangu na nimefikisha ujumbe, ninashukuru. Ninaomba majibu kwa maslahi ya Taifa, ahsanteni. (*Makofi*)

MICHANGO YA MAANDISHI

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, naomba nipongeze juhudii kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Waziri na Manaibu Mawaziri katika Wizara hii, kwa kweli wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. Mchango wangu katika Wizara hii ni mfupi kama ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, *REA*. Katika mipango iliyopo ya kupeleka umeme katika Jimbo la Manyovu/Wilaya mpya ya Buhigwe, tunaomba nasi tupewe kipaumbele kwani tumeachwa na sekta mbalimbali kwa muda mrefu. Ombi langu ni kwamba Wizara hii tunaimani nayo na nimewaaminisha wananchi wangu kwamba kwa *team* hii ya watendaji itafanya. Vijiji vya Manyovu vimesubiri umeme kwa muda mrefu sana na ni vizuri mipango hii itekelezwe. Je, ni lini mradi huu utakamilika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *solar*, niipongeze sana Serikali kwa kuweka umeme wa jua katika zahanati zetu na baadhi ya shule za sekondari na masoko yaliyoezekwa. Tunaomba kuwekewa umeme kwenye shule za sekondari kwa shule ambazo zimebaki mfano shule za sekondari zote za Tarafa ya Muyama, zahanati ya Mlela Mission/Buhigwe na shule ya sekondari ya Janda na nyingine ambazo hazijawekwa.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Sospeter Muhongo (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa George Simbachawene (Mb), Naibu Waziri Stephen Maselle (Mb), Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuinua uchumi wa Watanzania kupitia madini na nishati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kukomesha tabia za wanasiasa wanaopotosha wachimbaji wadogowadogo. Inasikitisha sana ninapoona baadhi ya wanasiasa wakiwapotosha wachimbaji wadogo huko kwenye migodi kupuuza sheria za nchi. Naiomba Serikali kufuatilia tabia za baadhi ya wanasiasa wanaojingiza kupotosha wachimbaji wadogo ili kujua wanafanya hivyo kwa maslahi ya nani na kwa sababu gani, hawajui sheria au wanafanya hivyo kwa makusudi. Nitafarijklaka sana endapo Waziri atalieleza hili wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninaipongeza Wizara kwa kuendelea kutoa semina mbalimbali kwa lengo la Wabunge kuendelea kupata uelewa. Naomba semina hizi zitolewe kila mara ili kukuza uelewa wa wanasiasa, wachimbaji wadogowadogo na wananchi kwa ujumla. Nitafurahi kupata kauli ya Serikali wakati wa kuhitimisha bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo. Utaratibu wa kuwapatia wachimbaji wadogowadogo maeneo yao ya kuchimba kabla ya kutoa leseni kwa wachimbaji wengine ni muhimu sana. Kwa kuwa kumekuwa na migogoro ya wachimbaji wenyewe leseni na wachimbaji wadogo wadogo, naiomba Serikali kufuatilia kwa karibu maeneo yote yenyewe migogoro na kuimaliza ili kuzuia matatizo makubwa yanayoweza kujitokeza. Naomba maelezo ya Serikali yatolewe wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa wachimbaji wadogo na mchimbaji mwenye leseni Mgodi wa Mgongo – Shelui – Iramba. Naomba Serikali kufuatilia mgogoro huu ambaو umesababisha mgodi kufungiwa. Mimi naona kulikuwa na uchochezi wa baadhi ya viongozi. Kwa kuwa wachimbaji wadogo sasa inaelekea wanajutia, naomba kazi ya kuunganisha wachimbaji wadogo na mwenye leseni ufanyike, wameshaonja joto ya jiwe.

Mheshimiwa Spika, maombi ya umeme kuititia umeme vijiji. Napenda kutuma maombi Serikali kupeleka umeme kutoka Shelui kwenda Mtoa, Msai, Tyeme, Mtekente na Urughu pia kupeleka umeme kutoka Shelui hadi Mgongo, Sekenke, Ntwike, Mingela, Tulya, Doromoni na Kidani. Nasubiri majibu mazuri ya Waziri maana Wilaya hii ya Iramba bado ina vijiji vingi sana ambavyo havina umeme.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii, Mungu awatangulie, utekelezaji wa bajeti uende vema.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ombi muhimu kwa Wilaya yangu ni kusambaza umeme katika Mji wa Namanyere maana mpaka sasa ni asilimia 30 tu ya wananchi wa Mji wa Namanyere ndio wanaopata huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme katika Mji wa Kirando na Swaila. Maombi ya kupeleka umeme Kirando na Swaila yako kwenye mpango wa *REA*. Nashukuru sana tena sana maana Engineer Msofe wa *REA* amenieleza mpango wa kupeleka umeme Kirando na Swaila katika Wilaya ya Nkasi umo katika mpango wa *REA* awamu hii ya pili. Kwa hiyo, ombi langu ni kupewa kipaumbele tu kwa huo mpango wa kupeleka umeme pia katika vijiji vya Londikazi, Miyombo, Mashete, Mtega Mwai na Paramawe.

Mheshimiwa Spika, Wizara ione kuwa umeme kufika katika Mji wa Kirando ni ukombozi kwa wavuvi wa samaki na dagaa, yaani wakazi wote wa mwambao wa ziwa wanategemea sana uvuvi wa samaki aina ya migebungu na hakuna hifadhi, huwa wanaoza na kufukiwa na kuendeleza umaskini kwa wavuvi wa ziwa Tanganyika. Umeme utakuwa ukombozi wao kwa vile wataweza kuhifadhi migebungu. Nashukuru kwa umeme kufika Namanyere na vijiji vyote barabarani.

Mheshimiwa Spika, katika mji wa Namanyere sehemu muhimu ambazo umeme haujafika ni pamoja na shule nne za sekondari, shule nne za msingi, eneo la viwanda vidogo na visima vya maji vinne ambavyo vilikwishaunganishwa na umeme wakati tunatumia *generator* ili wananchi wapate maji kwa urahisi na nafuu.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, kikao cha wachumi duniani kilichofanyika Marekani miaka miwili iliyopita, walikubaliana kwamba nchi nyengi zenyе rasilimali (madini na gesi) na kadhalika zinaingia katika migogoro (vita) vya wenyewe kwa wenyewe kutokana na mgawano mbaya wa rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumeanza uchimbaji wa

dhahabu na madini mengine kwa muda mrefu sasa na bado kuna malalamiko makubwa kwa wananchi walio katika yale maeneo yallyozunguka migodi na pia kuna kutokuelewana kati ya wananchi na wachimbaji (wawekezaji) kwa kiasi cha hata kupeana majina ya kiuadui kutokana na hasira za kukosa maslahi stahiki kama vile wenyeji huwaita wawekezaji kwa majina ya makaburu, wanyonyaji, wezi na kadhalika lakini pia wawekezaji huwaita wananchi kwa majina ya wachimbaji haramu, wavamizi, majambazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa tumezoea kusikia ama watu wameuawa au kuna vurugu kati ya wananchi waliozunguka maeneo ya migodi na walinzi, polisi na au wawekezaji wenyewe katika migodi ya Mererani, Mwadui, Buzwagi, North Mara, Isanga na kadhalika. Hii si dalili nzuri kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Afrika, Algeria ndio nchi ya kwanza inayotoa gesi kwa wingi na inachangia asilimia 3% ya pato la Taifa lakini pia inapunguza tatizo la ajira kwa 10%. Tanzania tumegundua gesi na pia inasadikika kwamba tunaweza tukawa pia na mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mtwara na Lindi ni Watanzania na wamejifunza kutoka katika yale maeneo ambayo yanatoa madini (dhahabu) kwa muda mrefu na ndio maana nao walichachamaa vile. Naiomba Serikali ije na sheria na kanuni zitakazoonesa au kutoa matumaini kwa Watanzania inayoonesha ni kwa kiasi gani gesi hii itaongeza pato la Taifa, lakini pia ni vipi itawenza kujibu tatizo sugu la ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe angalizo na pia niishauri Serikali kwamba, tuisipokuwa waangularifu juu ya gesi hii, Taifa linaweza likaingia katika matatizo makubwa na tukajikuta kwamba badala ya neema imekuwa kama laana kwa Taifa. Kwa pamoa tumwombe Mwenyezi Mungu ajaalie iwe ni neema na isijekuwa laana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kwa kazi nzuri anayofanya ya kuleta matumaini kwa wananchi ili wafaidike na rasilimali zao. Pia niwapongeze Naibu Mawaziri kwa kumshauri vizuri Mheshimiwa Waziri. Bila kumsahau Katibu Mkuu Eliakim Maswi, kwa umahiri na uadilifu wake. Pia nawapongeza timu yote ya wataalam.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati na madini ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wetu na ni moja ya vipaumbele vya kutuvusha katika jangwa na kufikia nchi ya ahadi, nchi yenye uchumi wa kati. Bila umeme uliosambazwa nchi nzima hakuna maendeleo, lazima wananchi wafaidike na madini yetu. Madini yaliyoko ardhini ni mali ya Watanzania wote. *Nickelya Kabanga* iliyoko Ngara siyo mali ya watu wa Ngara ni mali ya Watanzania. Ni upuuzi kuwaendekeza wananchi wa Mtwara na Lindi kwamba gesi ni yao. Bomba la gesi Mtwara Dar es Salaam ni lazima.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Tanzania ilikuwa na umeme mwangi kuliko Kenya na Uganda. Sasa hivi Kenya inatuzidi sana. Kenya inazalisha *MW 1,400*, Tanzania inazalisha *MW 700* na Uganda inazalisha *MW 400*. Utafiti nilioufanya unaonyesha kwamba Kenya wanatuzidi kwa sababu walikuwa wepesi wa kutekeleza wazo lilioanzishwa na *PSRC* la kutenganisha *Generation, Transmission* na *Distribution*.

Mheshimiwa Spika, Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Ngaka yatazalisha umeme mwangi. Basi umeme huo uwekwe kwenye *National grid* ili Wilaya zote ikiwemo Wilaya ya Ngara waweze kupata umeme wa *grid*.

Mheshimiwa Spika, Ngara ni Wilaya yenye madini mengi ambayo hayajachimbwa. Hii inatokana na taarifa ilioachwa na Wajerumani. Ngara imejaa *Nickel*/na dhahabu. Madini haya yafanyiwe utafiti.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa *Kabanga Nickel* umekuwa sasa ni hadithi. Hadithi hii imekuwepo tangu

miaka ya 1970. Wawekezaji wamekuwa wakibadilikabadi. Tunaambiwa kwamba mgodi huu ni wa pili duniani katika utajiri wa *deposits* baada ya ule wa Canada. Wakati tumeanza kuamini kwamba sasa wataanza kuchimba, mwekezaji mmoja *Barrick Gold* ameamua kujiondoa. Anatafuta mwekezaji mwininge wa kununua hisa zake ambazo ni 50%. Mwekezaji wa pili ni *Extrata*.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa sijaona dalili za Serikali kuwa *serious* na mgodi huu. Mheshimiwa William Ngeleja alipokuwa Waziri aliwahi kuutembelea mradi huu. Mheshimiwa Waziri nakukaribisha uutembelee mgodi huu ili wananchi wawe na imani kwamba Serikali iko *serious*.

Mheshimiwa Spika, *Nickel* itakayochimbwa kwenye mgodi wa Kabanga – Ngara inangojewa kwa hamu ili ichanganywe na chuma cha Liganga kupata chuma cha pua. Kabanga *Nickel* inahitaji vibali kutoka Wizara hii kama Leseni ya uchimbaji, Kibali cha Mazingira (*EIA*), *MDA*. Naiomba Wizara iharakishe vibali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa *REA* – Rulenge. Naomba nitoe shukrani za pekee kwa uongozi wa *REA* na hasa Dkt. Lutengano Mwakahesya na Msaidizi wake Eng. Msofe kwa kazi nzuri wanayoifanya. Watendaji hawa ni wachapakazi na ni waadilifu sana. *REA* imeshatengeneza *transformer* ya Rulenge bado kuweka *line*. Nina imani kwamba nguzo zitaanza kuwekwa kuanzia Djuokuligwa hadi Rulenge mwezi wa saba kama nilivyoahidiwa. Naiomba Wizara izidi kuiongezea *REA* bajeti kwa sababu watendaji wake ni waadilifu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa *Orio – Holland*, mpaka sasa Wizara haiko wazi ni lini mradi wa umeme wa *Orio* kwa Wilaya za Ngara, Biharamulo na Mpanda utaanza kutekelezwa. Naiomba Wizara ianze kutekeleza mradi huu kwa kuweka *generator* mbili kwenye kituo cha *TANESCO* Ngara ili umeme usambazwe kwenye vijiji vya Mugoma, Benaco, Rusumo, Kabaheshi, Nyamahwa na Kashinge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa *solar*, naiomba Wizara ifikirie mpango wa kuweka umeme wa *solar* katika shule za sekondari na vituo vya afya katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa Rusumo. Naiomba Wizara iharakishe mchakato wa umeme wa maporomoko ya Rusumo kwa kushirikiana na nchi za Rwanda na Burundi.

MHE. LUCY P. OWENYA: Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya maendeleo vijijini, Serikali ilipunguza bei ya nguzo na kuunganisha umeme ili kila mtu aweze kupata umeme. Cha kusikitisha haswa *TANESCO* Moshi unakuta watu wanaenda kwa ajili ya kulipia nguzo lakini wakifika pale ofisini wanaambiwa hakuna *form* za kujaza na wale waliobahatiwa kulipia na kupata *form* hawaunganishiwi umeme ule kwa kisingilio vifaa hakuna kama nguzo, *wire*, mita, luku, hii ni mbaya sana kushikilia fedha za watu kwa muda mrefu wakati wangeweza kutumia fedha hizo kwa ajili ya mambo mengine? Je, ni sababu zipi zinapelekea *TANESCO* Moshi kutopelekewa vifaa kutoka Makao Makuu ya *TANESCO* na kupelekea wananchi kupata usumbufu wa hali ya juu?

Mheshimiwa Spika, Bunge la Novemba 2012, nilimuuliza Waziri swali hapa Bungeni kuhusu nguzo zilizopo chini kwa zaidi ya miaka miwili kule katika Jimbo la Hai, Kata ya Machame Kaskazini na Hai Mjini. Mpaka sasa hivi nguzo zile bado hazijasimamishwa na mvua zinazoendelea sijui zitakuwa kwenye hali gani? Utakuta tunalalamika *TANESCO* ipo kwenye hali mbaya kifedha, je, kwa kuziacha nguzo hizo si upotevu wa fedha za umma na kuwakandamiza wananchi?

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* wamekuwa waki-*print bill* za wenye mita kuanzia tarehe 18 – 19 ya kila mwezi lakini ikifikia tarehe 25 -27 ya mwezi kwa wale ambao hawajalipa *TANESCO* wanawakatia umeme wateja hawa. Huu ni unyanyasaji ukizingatia watumishi wengi unakuta hawajapata mishahara. Nashauri *TANESCO* *wa-print bill* hizo mwisho wa mwezi tu utakuta watumishi wameshapata mishahara.

Mheshimiwa Spika, Moshi Vijijini, Old – Moshi, Uru, Kibosho, Mbokomu, Mabogini ni kama hakuna umeme ikifika jioni na watu wote wakishawasha umeme hauwaki kabisa, ni mdogo sana, inabidi watu watumie mishumaa au vibatari? Ni lini wananchi wa Moshi Vijijini watapata umeme wa uhakika? Waziri anasema umeme ndio uchumi, kwa hali hii kuna maendeleo?

Mheshimiwa Spika, Shirika linaidai Serikali na Taasisi zake Sh.83,773,824,632, ni lini fedha hizi zitalipwa? Ni rahisi kuwakatia umeme wananchi wasiolipa Sh.10,000 lakini wadaiwa sugu hawakatiwi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, wawekezaji wengi wanakuja Tanzania kutafiti ni wapi madini yanaweza kupatikana hata wengine kuondoka na michanga kwa kisingizio cha utafutaji lakini tukumbuke wakoloni hawa kwenye maktaba zao tayari wanajua kila eneo la nchi hii madini ya aina gani yanapatikana wapi. Mfano gesi ilishagunduliwa siku nyingi sasa, kwa nini watu hawa wasamehewe kodi za mafuta wakati tayari ilishajulikana madini yapo wapi.

Mheshimiwa Spika, je, hii gesi iliyogundulika tunayo Sera ya Gesi? Serikali inajua hatuna Sheria ya Gesi lakini wanasema watatumia Sheria ya Mafuta ya 1980. Je, sheria hii inakidhi mahitaji ya sasa? Je, pakitokea kutokuelewana kati ya Kampuni na nchi, kesi hiyo ni lazima ikafanyikie nje ya nchi na mikataba hii itakuwa ni ya muda gani?

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo na malalamiko kwa wawekezaji wa ndani hawatendewi haki katika ulipaji wa leseni, huwa hawashirikishwi na inachukua muda kuwalipa fidia pindi eneo linapokabidhiwa kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, madini yote ya vito yanatakiwa yamilikiwe na wazawa. Je, madini ya *Tanzanite* ni kwa kiasi gani Watanzania wanamiliki madini haya?

Mheshimiwa Spika, je, mchakato wa kuanzisha

kiwanda cha kukata *veto* pale Kilimanjaro *International Airport* umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, uchangiaji wa sekta ya madini kwa pato la Taifa ni 3.5%, asilimia hii ni ndogo sana ukilinganisha na aina ya madini yanayopatikana nchini. Tunapoteza fedha nyingi sana kwa kutoku-*process* madini haya hapa nchini.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kusambaza umeme nchi nzima. Niwapongeze kwa kukamilisha mradi wa *MCC Wilayani Misungwi*. Vilevile nishukuru kwa niaba ya wananchi wa Misungwi kwa mradi wa Benki ya Afrika katika maeneo ya Wilaya ya Misungwi. Ni matarajio yangu kwamba mradi huu utatekelezwa kwa muda uliopangwana kuapatilia wananchi nishati hii muhimu kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile niombe Wizara kupitia *REA* iongeze kasi ya kutekeleza mradi wake katika Wilaya ya Misungwi kwani maeneo husika viongozi mbalimbali wameahidi kwamba umeme utakuwa umepatikana kabla ya mwaka 2015. Vilevile wataalam walipita katika maeneo hayo na wananchi kuweza kujandaa kwa kufunga nyaya za umeme kwenye nyumba zao kitu ambacho kinasababisha malalamiko kwamba wamedanganywa na kuwasababishia hasara. Naiomba Wizara kupitia *REA* kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili kupunguza manung'uniko kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Wizara hii kwa kazi kubwa inayofanya katika maeneo yake makuu mawili ya nishati na madini. Hata hivyo, napenda kuchangia kidogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais kuhusu umeme. Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika nyakati mbalimbali na maeneo mbalimbali Mbozi ikiwemo aliweka ahadi za utekelezaji wa miradi ya umeme. Ili kuendeleza imani ya Watanzania kwa Rais, Chama cha Mapinduzi na Serikali, nashauri Wizara hii itekeleze ahadi zote zilizowekwa na Rais kuhusu usambazaji wa umeme. Kwa Wilaya ya Mbozi Mheshimiwa Rais aliahidi kupeleka umeme Taraifa ya Itaka na katika Kituo cha Afya cha Itaka. Ni matumaini yangu kwamba ahadi hii ya Rais itatekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji miradi ya umeme katika vijiji vinavyopitiwa na Gridi ya Taifa ya umeme – Mbozi. Mwaka 2009 niliandikia *REA* barua kuhusu kupeleka umeme katika vijiji vya Nanyala, Senjele, Ivwanga na Old Vwawa. Katika majibu yake *REA* ilikubali kuvipatia vijiji hivyo umeme kwa kuweka '*transformer*' hata hivyo tangu wakati huo (mwaka 2009) hakuna kitu kilichofanyika. Hata hivyo, hivi karibuni niliongea na viongozi wa *REA* ambao kimsingi, baada ya kuwakumbusha kuhusu ahadi yao sasa wamekubali kuvipatia vijiji hivyo umeme. Ni matumaini yangu kwamba *REA* watakuwa waaminifu kwa kutekeleza ahadi yao ya muda mrefu sana kama tulivyokubaliana.

Mheshimiwa Spika, aidha, naiomba *REA* ifikishe umeme katika Kituo cha Afya cha Isanza. Naomba pia ikumbukwe kwamba moja ya madhumuni ya kupeleka umeme Isanza ilikuwa ni Kituo cha Afya. Bahati mbaya sana umeme huo umefika Isanza, lakini siyo Kituo cha Afya Isana. Umbali uliobaki kufikisha umeme Kituo cha Afya cha Isanza ni kama kilometra $1\frac{1}{2}$ hivi.

Mheshimiwa Spika, nilishafanya mazungumzo na viongozi wa *REA* kuhusu kufikisha umeme katika kituo cha afya Isanza. Kimsingi *REA* walikubali kufikisha umeme katika Kituo cha Afya kwa kumtumia mkandarasi aliyejenga mradi huo. Mkandarasi bado hajakabidhi mradi huo. Naomba *REA* wahakikishe ahadi hiyo inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya kusambaza

umeme vijijini, nashauri Serikali ihakikishe pesa zote zinazoidhinishwa kwa REA zinatolewa zote na kwa wakati. Vinginevyo ahadi/lengo la Serikali la kusambaza umeme vijijini kufikia asilimia 30 hadi mwaka 2015 itakuwa ndoto.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa makaa ya mawe Magamba – Mbozi. Iko kampuni ambayo inajihuisha na utafiti wa makaa ya mawe katika eneo nililolitaja hapo juu. Utafiti huo umechukua muda mrefu sana zaidi ya miaka saba sasa. Wananchi wa maeneo hayo pamoja na viongozi hawajui kinachoendelea hadi sasa. Kampuni hiyo imekuwa ikisomba makaa ya mawe mengi sana kwa maelezo kwamba ni katika mchakato wa utafiti. Tunaomba Serikali itueleze ni lini utafiti huo utakamilika na nini faida ya makaa hayo kwa uchumi wa maeneo hayo. Maana kilichoendelea ni uharibifu wa barabara zetu kunakofanywa na kampuni husika kupitisha magari yake ambayo ni mazito sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makaa ya mawe Kiwira. Kwa nyakati tofauti aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Ndugu Ngeleja na Waziri wa sasa Profesa Muhongo waliahidi kwamba mradi huo ungeanza kazi mapema sana. Hadi leo haijulikani kinachoendelea. Sasa nataka kujua ni lini mradi wa Makaa ya Mawe Kiwira yatafunguliwa na kuanza uzalishaji na hivyo kuongeza uzalishaji wa umeme nchini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono na nawasilisha.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kutokana na adha au changamoto tunazozipata Lindi na Mtwara za kupigwa viongozi, kuchomewa nyumba moto, maandamano ya wananchi, kunyanyaswa kwa viongozi wakiwemo Wabunge na Madiwani wa Lindi na Mtwara, tunaiomba Serikali kuanza uwekezaji wa viwanda mbalimbali Mikoa ya Lindi na Mtwara kabla ya kuendeleza miradi mingine. Viwanda kwanza kwa kutumia *gas* iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi asilia Tanzania, Serikali iandae Sera ya Gesi asilia haraka iwezekanavyo ili kuondoa changamoto zilizopo za gesi Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, madini yaliyopo Wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Lindi ambayo yanachimbwa bila utaratibu. Serikali ianzishe utaratibu rasmi wa uchimbaji huo ili wachimbaji wadogowadogo waweze kufaidika na pia Halmashauri za Wilaya ziweze kupata mrabaha.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Mchuchuma na Liganga unaendeleaje? Naomba tupate taarifa.

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati ni moyo wa Tanzania kimaendeleo. Nchi zote zilizoendelea duniani ziliwekeza sana kwenye umeme, sasa sisi Tanzania kama tusivyowekeza vyaa kutosha kwenye suala la umeme basi lengo letu la 2015 kuwa nchi yenye pato la kati haitowezekana.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2011/2012, tulipendekeza kuongeza bei ya mafuta ya taa na ongezeko la fedha ilikubaliwa Bungeni kupelekwa *REA* lakini hadi leo fedha hizo hazijapelekwa *REA* na mwaka jana 2012/2013 niliuliza katika mchango wangu kipindi cha Bajeti lakini sijajibowi.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO*, Shirika hili linahitaji uwekezaji mkubwa ukizingatia kwamba linajientesha kwa hasara. Serikali iwekeze hasa katika kununua mashine za kufua umeme kwa kutumia gesi asilia na ziwe mali ya *TANESCO* kwa 100% ili kupunguza utegemezi mkubwa wa kununua umeme kwenye makampuni ya nje. Tanzania tumejaliwa lakini sisi (Serikali) haijali. Tumejaliwa upepo, maji, jua, joto ardhi, gesi asili ambapo vyote vinaweza kusaidia kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, katika mchango wangu Bungeni nilisema ili kuokoa mazingira, *TANESCO* waanze kutumia nguzo za *concrete* badala ya nguzo zilizopo za kusambaza umeme. Nguzo za *concrete* zina maisha marefu zaidi kuliko nguzo za miti zilizopo, ambazo ni aghali na adimu kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *uranium*, Serikali sasa ianze kufikiria kutumia *uranium* kwenye kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi asilia, gesi hii ni mali ya Taifa, ni bora wenzetu wa Mtwara waelimishwe vya kutosha, vurugu zinazoendelea ni uchochezi wa nguvu za kutoka nje ili sisi tuendelee kumalizana na hao wageni wanufaike kama jinsi ambavyo imekuwa ikifanyika nchi nyingine duniani.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, nchi yetu imezungukwa na madini lakini pia kuna maeneo wananchi wanalala juu ya madini. Tatizo ni vipi rasilimali hii itawanufaisha Watanzania wote. Badala ya kuongeza kipato tumekuwa tukiongeza migogoro katika maeneo ambayo yana madini.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie upya suala la wachimbaji wadogowadogo aidha kwa kuwapa maeneo yao wenyewe na si kuwaacha kama yatima, kwani na wao kama madini yao yakikusanywa vizuri yanaweza kuliongezea pato Taifa. *TMAA* wamekuwa wakijishughulisha na migodi mikubwa mikubwa na kuwaacha wachimbaji wadogo wakiamua wao wafanyeje kuhusu madini wanayopata na wengi wao wamekuwa wakidhulumiwa na wafanyabiashara wajanja.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Serikali ilisema inatarajia kuanzisha au kukamilisha taratibu za mfuko rasi mi wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo. Ninaomba sasa jibu la Serikali, ni lini sasa mfuko huu utakamilishwa ili wachimbaji hawa waweze kupatiwa mikopo na nyenzo/vifaa vya kuchimbia vya kisasa ili wajikwamue na waondokane na uchimbaji wa kienyeji ambao ni hatari kwa afya zao?

Mheshimiwa Spika, bado kuna migogoro katika maeneo yenye madini ambapo wachimbaji wadogowadogo aidha wao kwa wao au na wachimbaji wakubwa wakiwemo watafiti wa madini, wamekuwa

wakigombana mara kwa mara. Tatizo ninaloliona mimi ni kuwa Serikali iangalie upya utaratibu wa kutoa leseni za utafiti kutokea Makao Makuu ya Wizara, kwani watendaji wamekuwa wakigawa maeneo ya utafiti huku wamekaa kwenye *computer* zao bila kujua kuwa tayari eneo walilogawa lina wananchi ambao pengine tayari wameshaanza nao shughuli za uchimbaji. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuhamisha kitengo cha utoaji leseni za utafiti kwenda Mikoani ambapo ni rahisi sasa kwa Afisa kufika eneo husika kabla ya kutoa leseni kwa mtatifi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna tatizo la watafiti kupewa leseni mbili yaani ya kuchimba na hapo hapo anatafiti na kama si hivyo basi wanapofanya utafiti wengine wanachimba kabisa madini. Hili hapa ni tatizo, naiomba Serikali iangalie tena kwa kukagua maeneo yenye leseni za utafiti ili kuona kama kweli hakuna uchimbaji unaofanyika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuweza kuokoa kiasi kikubwa cha madini yaliyokuwa yanasa firishwa nje kwa wizi, bado inahitaji kuongeza nguvu za ziada ili kuziba mianya ambayo inasababisha wizi huu ufanyike kwenye viwanja vyetu vya ndege. Tumeona ni jinsi gani Taifa linapoteza mapato yake kutokana na watumishi wasio waadiliflu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo sugu sana la migodi mikubwa kutolipa “*service levy*” kwenye Manispaa husika kulingana na mikataba yao lakini Serikali hailioni hili na bila Mbunge wa eneo husika kufuatilia migodi hii haishtuki na wala haitoi “*service levy*” hiyo. Ninaomba kuuliza tozo hizo ni hisani au ziko kwenye mikataba? Kama zipo kwenye mikataba yao kwa nini sasa mpaka wafuatiliwe ndio walipe tozo hizo?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wafanyakazi wazawa waliopo migodini, wamekuwa wakidhalilishwa sana, sijui kama Serikali haina taarifa kuhusu unyanyasaji wa Watanzania unaofanywa katika migodi nchini. Nina taarifa kuhusu Mgodi wa Mwadui ni moja ya migodi ambayo inanyanyasa na kudhalilisha

Watanzania. Kama Serikali inaona na inasikia, kwa nini basi isikemee vitendo hivi vinavyofanyika katika migodi yetu yaani waje wachukue rasilimali zetu lakini bado watunyanyase? Mie nasema si haki hata kidogo. Ninaomba Serikali ione sasa kuna haja ya kutembelea migodi yote na kuongea na wafanyakazi ili wasikie vilio vyao ikishirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie nishati. Kumekuwa na changamoto kubwa sana katika maeneo mengi ya kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara hali ambayo inaleta kero sana na hofu kubwa kwa wananchi. Wapo wanaodiriki kuhoji kama ni mgao au ni hitilafu tu. Naomba Serikali kuititia Wizara ije na majibu, je, tatizo ni nini hasa linalofanya umeme ukatikekatike katika maeneo mengi bila hata taarifa?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kukiendelea na matukio ya hujuma ya miundombinu ya umeme zikiwemo nyaya, pamoja na mafuta ya transfoma, hivyo kusababisha maeneo husika kukosa umeme. Pamoja na kukosa umeme, Shirika la Umeme linapata hasara kubwa sana kutohana na hujuma hizo. Naomba sasa pamoja na baadhi ya watuhumiwa kukamatwa na kufikishwa Mahakamani, adhabu kali sana zichukuliwe ili iwe fundisho kwa wananchi wote ambao wamekuwa wakilihujumu shirika hili.

Mheshimiwa Spika, bado kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa mita za luku katika maeneo mengi. Ninaomba zoezi la uunganishwaji wa umeme katika maeneo uende sambamba na upatikanaji wa mita za luku. Aidha, imeonekana nguzo za umeme bado ni tatizo hasa maeneo yaliyoko pembezoni. Kuna haja sasa ya Serikali kuhakikisha nguzo zinapatikana kila Mkoa lakini hata bei yake iwe nafuu ili idadi kubwa ya wanaoomba kuanganishiwa umeme waweze kupata umeme kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zote zinazoikabili *TANESCO*, naiomba Serikali iliangalie Shirika hili kwa macho manne (4) ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi

kabisa na kuwachukulia hatua Maafisa wake ambao kwa njia moja au nyingine wanalisababishia Taifa hasara.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijiini (*REA*) ina lengo zuri sana la kupeleka huduma za nishati bora vijijiini kwa lengo la 30% ifikapo 2015, nilitaka kujua ni vijiji vingapi ambavyo viko katika lengo hilo katika Mkoa wa Shinyanga?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya, naomba kuwasilisha.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, ukiangalia hotuba ya Waziri, ukurasa wa 78, aya 147, imezungumzia vyatubu kuhusu uwezo wa rasilimali watu kwa kuapeleka Watanzania nchi mbalimbali kwa maneno. Wako watakaokwenda kusoma Brazil, China na Uingereza. Mpaka sasa suala la mafuta ni la muungano na hata elimu ya juu ni muungano, katika wanafunzi hao wanaokwenda kusoma nchi za nje, ni wanafunzi wangapi wanatoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mawazo yanayotofautiana juu ya hali ya *TANESCO*. Wako wanaofikiria kuwa *TANESCO* ipunguziwe majukumu. Mimi navyohisi majukumu ya *TANESCO* si tatizo bali ni changamoto zinazolikabili shirika hili, ndio tatizo kubwa. Iwapo changamoto zitaondoshwa basi Shirika linaweza kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, changamoto moja kubwa inayolikabili Shirika hilo ni bei ya umeme. *TANESCO* inauziwa Sh.495/= mpaka Sh.808/= kwa *unit* moja, wao wanauza kwa Sh.198/= kwa *unit* moja. Katika hali hiyo, hata *TANESCO* ikipunguziwa majukumu basi utendaji wake utakuwa hauna ufanisi. Pia changamoto nyingine ni madeni ya Shirika wanayoidai Serikali na taasisi nyingine zinazohusiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi yetu imeshavumbua takribani futi za ujazo triliioni 41.7 za gesi asilia. Hii ni neema kubwa kwa nchi yetu kama nchi yetu itatumia vizuri mali hii,

vinginevyo kama fursa hii haitatumiwa vizuri inaweza gesi hii ikaleta maafa makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida nyingi zitazopatikana kwa kupata gesi asilia, faida moja ni kupata gesi ya kupikia katika nyumba zetu. Hili ninaliona katika kulinda mazingira ya nchi yetu linachukua nafasi ya pekee. Iwapo wananchi hawatakuwa na uwezo wa kuweza kutumia gesi hii kwa kupikia basi tuelewe nchi yetu itakabiliwa na janga kubwa la uharibifu wa mazingira kwa ukataji wa misitu yetu kwa ajili ya utengenezaji wa mkaa. Ili gesi hii ilete manufaa ya kimazingira, ni lazima bei ya gesi ya kupikia iwe rahisi kuliko kutumia mkaa. Hapo ndipo wananchi wataweza kuhama kutumia mkaa na kutumia gesi. Naomba Serikali inieleze watachukua hatua gani ili kuhakikisha kuwa bei ya gesi ya kupikia itakuwa ni rahisi kuliko mkaa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kuiunga mkono hoja na kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambazo zimeshafanyika na zitakazofanya.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa kusimamia na kutimiza ahadi zake baadhi kama vile uletaji wa umeme katika Jimbo la Nyang'hwale, nguzo na nyaya zinaendelea kusambazwa. Je, ni lini sasa kazi hiyo itakamilika na umeme kuwashwa?

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kufuta leseni 161 za utafiti wa madini na moja moja ya uchimbaji. Je, katika leseni hizo zilizofutwa na eneo la Wilaya ya Nyang'hwale zimo? Kama zipo ni maeneo gani? Kama hakuna je, Wizara ina mpango gani wa kuwatengea maeneo wachimbaji wadogowadogo Wilaya ya Nyang'hwale sababu maeneo mengi ya Nyang'hwale yana madini aina ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupata ufanuzi wa malipo ya mgodi wa Bulyang'hulu yaani (*service levy*) kwa

Halmashauri ya Wilaya ya Kahama maana ni haki yao. Je, ni lini sasa Wilaya ya Nyang'hwale itaanza kulipwa? Sababu uchimbaji wa mgodi huo unelekeea Jimbo la Nyang'hwale na madhara mengi kujitokeza kama milipuko na kupasuka baadhi ya nyumba na ardhi na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufafanuzi kuhusu ni namna gani Wizara imejipanga kuwasaidia wachenjuaji kupatikana kwa *chemical* aina ya (*cyanide*) kwa bei nafuu sababu hivi sasa inapatikana kwa njia ya panya tena kwa bei kubwa sana. Wachenjuaji wote wanasubiri majibu ya Waziri kwa hamu sana kusikia Wizara yao inawasaidiaje kwa sababu nao wanachangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini nikijikita katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuchelewa utekelezaji mradi wa umeme vijiini kuititia *REA*. Nilianza kwa kuandika barua ya maombi mwaka 2011 kuomba kupeleka umeme vijihi vya Kidudwe, Kunke, Lusanga Ng'ambo, Kisala, Mjudeni, Makuyu na kata za Doma, Melela, Kanga na Kibati. Nilikubaliwa maombi yangu kwa barua, nimeshaandika barua mbili kwa Waziri, Profesa Muhongo na zote ameniahidi mradi huu utatekelezwa. Mwaka jana bajeti 2012/2013, zilitengwa fedha lakini mpaka sasa hakuna kinachotekelzwa. Nashukuru tena mwaka huu 2013/2014, vijihi hivyo na kata hizo zipo katika mpango wa kupelekwa umeme. Naomba sana *REA* itekelze maombi yangu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *MCC*. Naomba Wizara ikamilishe miradi ya *MCC* ikiwepo kupeleka umeme (Mgeta, Mbogo, Sokoine, Dihombo, Mji Mpya (Madizini) na kitongoji cha Mtakuja, kijiji cha Dakawa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya kupeleka umeme Kijiji cha Msufini, Mlaguzi, Dibamba, Lukenge, Mlumbilo na Lungo.

Naomba Wizara ipokee maombi ya kupeleka umeme katika vijiji nilivyovitaja. Nilishaandika barua kwa Meneja *TANESCO* Mkoa ya kuomba vijiji hivyo kupelekewa umeme kutokana na mahitaji muhimu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba nijibiwe.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, umeme vijiji. Umuhimu wa upatikanaji wa umeme vijiji ni haki ya kila Mtanzania. Hata hivyo, asilimia 80 ya Watanzania wanaishi vijiji huko ambako hawana matumaini ya kupata umeme kutokana na gherama kubwa za kufungiwa umeme, malipo makubwa yenyewe makato lukuki kila mwezi, uhaba wa umeme wenyewe na changamoto ya kutofungiwa umeme kwa wakati na kadhalika. Kwa kuwa matatizo hayo yameendelea kuwa kikwazo cha wananchi wengi kukosa umeme jambo ambalo ni haki yao, je:-

(a) Ni kwa nini wananchi waliomaliza kufanya *wiring* katika nyumba zao inawachukua muda mrefu kuwashisha umeme?

(b) Je, ni kwa kiasi gani Wizara inahakikisha nguzo za umeme zinapatikana katika ofisi za *TANESCO* Wilayani ili wananchi wapate umeme?

(c) Wananchi ambao wanatumia umeme wanakatwa fedha nyingi kila wanaponunua umeme mwisho wa mwezi, kwa nini wananchi hawa wanapata gherama kubwa kila mwisho wa mwezi pindi wanaponunua umeme?

(d) Je, ni kwa nini wananchi walio maeneo ambayo nguzo za umeme zimefika hawajawashiwa umeme mpaka leo, ikiwa ni Wilaya ya Karatu – Kata ya Endamararie.

(e) Je, ni lini sasa umeme utapelekwa katika Kata za Mang'ola na Mbulumbulu Wilayani Karatu? Je, katika mpango ujao wa *REA* 2013/2014, kata hizo zipo katika orodha ya kupata umeme?

(f) Gharama za kufungiwa umeme zimeendelea kuwa kubwa hivyo kuwanyima wananchi hao haki ya kupata umeme. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama hizi ili kuwafanya wananchi kumudu gharama hizo?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio roho inayosukuma damu iliyojaa virutubisho vya uchumi wa Taifa la Tanzania. Nishati ya umeme ulimwenguni kote imekuwa ni chimbuko la mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, Mwenyenzi Mungu ametujalia kuwa na vyanzo vingi vya uzalishaji wa umeme ikiwemo maji, gesi, jua, joto ardhi, upepo, makaa ya mawe. Vyanzo hivi vya uzalishaji wa umeme vinaiweka nchi yetu katika nafasi nzuri sana ya kuwa mzalishaji mkubwa wa umeme na kwa vyovytote vile baada ya muda mchache ujao, Tanzania itakuwa na uwezo wa kuwa na umeme wa ziada ambao unawenza kuuzwa hata nchi jirani hasa katika nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki. Kwa vyovytote vile iwavyo, upatikanaji umeme wa gharama nafuu utavutia uwekezaji katika sekta ya viwanda na hivyo kuchochaea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kuwepo kwa umeme wa uhakika kutachochaea uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo na hivyo kuboresha tija kwa wakulima wa nchi hii. Ni imani yangu kuwa zao la pamba ambalo limekuwa linakumbwa na tatizo la kupanda na kushuka kwa bei, kwa kuwepo kwa umeme wa uhakika kutachochaea nguvu zaidi kuelekezwa katika uwekezaji katika viwanda vya nguo ambazo zitauzwa ndani ya nchi na hata nje ya nchi na hivyo kuingiza fedha za kigeni na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na kupandisha hata bei ya zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, aidha, naipongeza Serikali kuitia

Wizara hii ya Nishati na Madini kwa kuendelea na mpango wake wa kuipatia Wilaya yangu ya Mbogwe huduma ya uhakika ya umeme kupitia mradi wa *Electricity V unaofadhiliwa* na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na kutekelezwa na mkandarasi wa ujenzi M/S *Eitel Networks TE AB* kutoka Sweden na kwamba utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi ujao wa Juni, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala wa Umeme Vijiji ni *REA*, Mbogwe tunanufaika pia katika mwaka huu wa fedha na vijiji vya Bwendumwizo, Bwendanseko, Nambubi, Ilolangulu, Bugalagala, Kashelo na Lulembela. Nachoomba hapa ni Serikali kuongeza fedha zaidi *REA* ili asilimia kubwa ya Watanzania ambao wanaishi vijiji ni wapate umeme. Naiomba Serikali iongeze fedha ili Watanzania wengi zaidi wapate huduma hii. Kusambaza umeme vijiji ni kutasaldla sana kukuza uchumi na kuokoa uharibifu wa mazingira kupitia ukataji hovyo na miti kwa lengo la kupata mkaa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Hata hiyo, zipo changamoto nyingi hasa katika sekta ya wachimbaji wadogo na jinsi Wizara kwa niaba ya Serikali kuona ni jinsi gani Serikali itakavyomiliki angalau asilimia hamsini 50% katika migodi ya madini na sekta ya gesi.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Mbogwe kuna taarifa za uwepo wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Bukandwe, Lugunga, Shenda, Nyakafuru na kadhalika. Naiomba Wizara ione ni kwa namna gani itakavyowasaidia wachimbaji wadogo wa maeneo tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kuja na bajeti ambayo ina lengo la kuiweka nchi yetu katika nafasi ya mataifa yanayokuza uchumi kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha nami niseme machache juu ya bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi ngumu anayoifanya na kuhakikisha usimamizi wa sheria katika sekta ya madini unasimamiwa vizuri. Bajeti hii imelenga kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi lakini changamoto bado ni nyangi sana katika sekta hii, inabidi ifanyike kazi ya ziada ili wananchi waridhike na utendaji wa sekta hii ya nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo kubwa linalolalamikiwa sana na wananchi ni sekta ya umeme. Kila kukicha umeme umekuwa tatizo kubwa kwa wananchi. Napenda kuipongeza Serikali kwanza kwa kupunguza ada ya kuunganisha umeme ambayo hapo awali ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi na hata kuleta mianya ya rushwa kwa baadhi ya wafanyakazi wa *TANESCO*. Tatizo la kukatikakatika kwa umeme limekuwa la kudumu, bado halijapatiwa ufumbuzi, mpaka karne hii imekuwa ni aibu kwa Taifa letu kuwa na migao ya umeme isiyokuwa rasmi na kukatikakatika ovyo kwa umeme kusikokuwa na taarifa yoyote kwa watumiaji. Hali hii inaonyesha kama hatutaki kubadilika, kujifunza kutoka kwa wenzetu mbinu walizotumia kuepukana na adha hii. Ikumbukwe umeme ni kila kitu, bila umeme, maofisini kazi zinazorota, mahospitalini wagonjwa huhatirisha maisha yao, viwanda havitazalisha, ama uzalishaji utapungua na kushusha uchumi wa nchi. Naomba tutille mkazo katika hilo ili tuondokane na matatizo haya na hata iklonekana njia hii ya uzalishaji umeme wetu ndio tatizo basi zifanyike juhudzi za makusudi kupata njia mbadala. Leo hii tumesikia *TANESCO* imeshindwa rufani ya kesi iliyokuwa inapinga kuilipa kampuni ya *DOWANS*, kwa maana hiyo *DOWANS* inatakiwa ilipwe. Naishauri Serikali kuliangalia hili kwani *TANESCO* haina uwezo wa kulipa hizo fedha vinginevyo mzigo huu watatupiwa wananchi katika njia ya kupandishiwa bei ya umeme na kugeuka kuwa mzigo kwao, kwa hili Serikali haina budi kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini imekuwa ikilalamikiwa sana hapa nchini, zaidi mikataba tunayoingia na hawa wawekezaji ambao mwisho wa siku naamini wanatunyonya tu. Kuna baadhi ya maeneo kuna migogoro mingi sana kati ya wananchi na hawa wawekezaji, lakini Serikali imeonekana kuwalinda ama kuwabeba hawa wawekezaji ili hali wananchi wanauawa kwa kupigwa risasi na wawekezaji hao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali irekebishe hii Sheria ya Madini ili itunufaishe wazawa kwani mikataba tunayoingia ni ya muda mrefu na haitunufaishi kitu wazawa. Pia Serikali iwaafuatilie hawa wawekezaji kuhusu utekelezaji wa ahadi walizokubaliana kwenye hiyo mikataba kwani imegundulika utekelezaji wake kwa jamii umekuwa mdogo mno. Vilevile usimamizi wa madini yapatikanayo hapa nchini uongezwe kwani inasemekana kuna madini hutoroshwa bila Serikali kujua na kupoteza fedha nyangi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kufuta misamaha ya kodi kwa wawekezaji hawa pale wanapokuja kuwekeza katika sekta ya madini kwani hatuna budi kuringia urithi wetu tuliopewa na Mwenyezi Mungu, kwani madini yanajitangaza yenewe na hakuna uhitaji wa kumbembeleza mwekezaji kwenye sekta hiyo. Ikumbukwe madini hayaodzi hata yakiachwa milele vizazi vijavyo vitakuja kufaidika nayo lakini si kwa hali hii ya kuingia kwenye mikataba mibovu na kupoteza rasilimali zetu kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la watumishi wanaofanya kazi katika sekta hii ya madini kupatwa na matatizo makubwa ya kiafya baada ya kutumia vifaa ambavyo vina madhara na baadaye kutokupata msaada wowote kutoka kwa waajiri wao. Naiomba Serikali kuboresha sheria ili kuwabana wawekezaji hawa ili kuwalinda wananchi wetu wanaopata athari hizo na mwisho kufikia kufariki dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda kukumbushia kilio cha wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini,

matatizo ya umeme bado ni kero na kutokujua hatma yake ni lini. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kutatua tatizo hili na kupeleka umeme Kata ya Ruvu. Ufuartilajji wa utekelezaji wa ahadi hii ulishaanza kwa Waziri wa Nishati na Madini kufanya ziara katika Jimbo hili na akaona ukubwa wa tatizo. Napenda kujua ni hatua zipi zimefikiwa na nini kinaendelea katika utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu. Kwani kupeleka umeme katika Kata ya Ruvu kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka na kupandisha uchumi wa wakazi wa Jimbo la Kibaha Vijiji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri na Naibu Mawaziri wa Nishati na Madini, Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kuandaa, kujenga na kusimamia rasilimali ya nishati na madini kwa ajili ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu Tanzania. Ushauri wangu, Serikali iendelee kutumia juhudhi na maarifa walijonayo watumishi wazalendo ya wanaosimamia sekta hii ili tuijenge nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umeme, sisi wananchi wa Wilaya ya Namtumbo tunaishukuru Serikali kwa kuwa sikuvi, niliposhauri na kuiomba kutuwekea umeme wa *generator* wakati tunasubiri mradi wa umeme wa Gridi Makambako – Songea 220KV. Leo Namtumbo Mjini umeme unawaka lakini kuna changamoto yake. Tulipokubaliana umeme uwekwe sehemu zippi, Makao Makuu ya Wilaya Namtumbo, walipofika wataalam, Wahandisi Umeme na Mipango, tulikubaliana umeme utawekwa pia katika Hospitali ya Wilaya, lakini nguzo za umeme hazikufika hospitalini, zimeishia katika maeneo ya nyumba za wananchi tu, ni umbali ambao hauzidi kilomita moja. Naiomba Serikali kupitia (*REA*) watuongezee fedha za *distribution line* ili umeme ufile pia Hospitali ya Wilaya na kukamilisha lengo tulilokusudiwa na wananchi, wagonjwa wapate huduma stahiki katika Hospitali hiyo ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwa

hatua zilizofikiwa za utekelezaji wa mradi wa umeme wa 220KV Makambako – Songea, Namtumbo ikiwa mojawapo ya Wilaya zitakazofaidika. Tunachowaomba, kwa mujibu wa taarifa mliyotusambazia wadau watakaofaidika na mradi huu na ratiba ya mradi utakavyoanza na sisi tuwahamasishe au tuwa-*sensitive* wananchi waliopo na wale ambao njia ya umeme itapita kwenye maeneo yao, waweze kutoa ushirikiano kama Serikali mlivyoomba. Sasa sisi *sensitization* tutakayoifanya ni pamoa na kuwaambia kazi hiyo itaanza lini na tunategemea pia kukamilika lini ili waweze kupisha mapema kwa maana ya kuacha kulima au kuyatumia maeneo hayo ambapo njia ya umeme itapita. Nachoiomba Serikali, mradi ufuate ratiba mliyotueleza katika taarifa mlizotusambazia. Sisi ni wanasiasa tunapoenda kuwaeleza wananchi wanaamini tuyasemayo, sasa kama bado mnafikiri mradi hautaanza kama mlivytueleza, tuelezeni mapema kabla hatujaanza kazi hiyo ili isije kutufanya tusileweke na kuanza kazi ya kuelezea kwa nini mradi haujaanza baada ya kutumia muda mwangi wa *sensitization* kwa wahusika ili watupe ushirikiano. Pia anapoacha kuitumia ardhi yake, mwananchi wa kijijini maana yake ni kwamba anapunguza eneo liilokuwa linampatia pato lake. Hivyo anatakiwa aone kazi iliyomfanya aiachie ardhi yake inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, kumekuwa na tetesi kuwa kuna baadhi ya wawekezaji wakubwa wa nje na baadhi ya taasisi wanapinga chinichini na wazi miradi mikubwa ya maendeleo yetu ya uchimbaji gesi na urani. Je, Serikali inasema nini kuhusu tetesi hizo na kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi yetu na kukamilisha lengo letu la kuja kuwasaidia wananchi maendeleo yao kiuchumi na kukuza pato la uchumi wa nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pia kumekuwa na tishio la usalama wa miradi yetu, nashauri tutumie vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kulinda miradi hii. Tusikubali hata kidogo kuruhusu makampuni ya ulinzi ya nje ya-*control* ulinzi wa miradi yetu mikubwa. Kama ikibidi ushirikiano wa ki-teknolojia basi *Head of command* lazima viwe vyombo vyetu vya ulinzi

na usalama. Hapa tutajihakikishia mambo matatu, moja, pato litakalopatikana kutokana na kazi hiyo, pili, uhakika wa ulinzi wa mali zetu bila kuhujumiwa na tatu, kama tutashirikiana na kampuni za nje vijana wetu watapata *knowledge* ya teknolojia ya ulinzi wa kisasa katika miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, napenda nami kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara hii. Naanza kuchangia kwa maandishi lakini pia kwa vile nimeomba kuchangia kwa kuongea, nkipata nafasi nitayaongea haya.

Mheshimiwa Spika, sina shaka na utendaji wa Wizara hii kwa sasa kwa maana ya viongozi wa juu Wizarani na naipongeza Wizara hii na hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, nachotaka kuanza nacho ni miradi ya umeme ya *REA* Awamu ya Kwanza ambapo katika Wilaya ya Gairo tulipewa Kata za Rubeho, Kibedya na Chakwale. Kama majibu ya Waziri ya tarehe 7/5/2013 katika swali langu namba 158.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizofika ni upimaji wa njia na kuweka alama kwa asilimia 100 lakini mpaka sasa bado hakuna kazi yoyote au (Mkandarasi) anayeendelea na kazi hiyo kwa muda mrefu toka kazi ya upimaji imalizike. Hofu yangu ni kwa vile upimaji huu ni wa muda mrefu na sehemu zilizopimwa ni mashamba ya watu. Kuchelewesha mradi huu kutasababisha wananchi waendelee na shughuli zao katika maeneo yaliyopimwa kama ujenzi na kusababisha kero zingine kujitokeza kwa vile hawakupewa taarifa. Kwa maana hiyo, nashauri mradi huu uanze mapema kutoa au kuzuia kero zozote ambazo zinaweza kujitokeza katika bajeti ya mwaka 2013 – 2014.

Mheshimiwa Spika, miradi itakayotekelezwa na *REA* katika Wilaya ya Gairo, vijiji saba tu ndio vya Wilaya ya Gairo, vijiji sita sio vya Wilaya ya Gairo. Kama Kiegea na Mtumbatu

ni Wilaya ya Kilosa na Kikunde, Kwa Maligwe, Mswaki, Mgela – ni Wilaya ya Kilindi. Vijiji vya Gairo ni Madege, Nguyami, Idibo, Italagwe, Makuyu Kinyolisi na Iyogwe. Kwa masikitiko sana Wilaya ya Gairo ina watu wengi sana kwenye vijiji vyake na watu wanaojituma na wana uwezo wa kuweka umeme katika nyumba zao na viwanda vidogovidogo vya usagaji na ukamuaji mafuta. Cha ajabu mpaka leo ni Gairo Mjini tu ndio pana umeme pamoja na hayo bado Gairo hiyo hiyo inapatiwa vijiji saba tu katika bajeti hii ya 2013/2014 ukilinganisha na Bunda vijiji 69 ndani ya nchi moja. Sielewi REA inafanyaje utafiti wake, hapa napata mashaka. Naomba angalau uwiano sehemu zilizosahaulika miaka mingi toka uhuru uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu katika vijiji vilivyopendekezwa kupatiwa umeme viongezwe vijiji vya Leshata na Kitaita, vipate umeme kutoka katika Kijiji cha Idibo ambacho kimo kwenye bajeti hii na umbali wake ni kilometra sita tu kutoka Idibo.

Mheshimiwa Spika, umeme unaoenda Chakwale upelekwe katika vijiji vya Tabu Hotel na Ihenje, umbali wake ni kilometra nne tu.

Mheshimiwa Spika, umeme wa Gairo Ukwamani uende vijiji vya Majawanga, Luhwaji, Mkalama, Meshugi na umbali wake ni kilometra saba tu.

Mheshimiwa Spika, ni ajabu katika ukanda wa tambalale katika Tarafa ya Nongwe, Kata ya Chanjale inayopakana na Wilaya ya Mpwapwa. Vijiji vyote vya Mpwapwa vimo katika bajeti hii wakati vinapakana kwa kilometra mbili na vijiji vya Jimbo la Gairo mfano, Mlembule, kijiji cha Mpwapwa kinapata umeme wakati cha jirani kwa kilometra moja na nusu kijiji cha Kumbulu, Wilaya ya Gairo hakimo. Kingine, Mwenzele (Mpwapwa) mpaka Mavisi na Chanjale (Gairo) kilometra kumi (10) havimo, inaleta picha mbaya sana kwa vijiji hivi na hata kiwilaya, kisiasa na kirasilimali za nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nieleweke,

sitopenda kупingа bajeti hii kwa mwaka huu. Naomba sehemu nilizozitaja zifanyiwe kazi.

MHE. CELINA O. KOMBANI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Wizara ya Nishati na Madini, kwa Hotuba nzuri, yenye *Facts & Figures* kwa upande wa Jimbo la Ulanga Mashariki. Tunawashukuru sana *REA* (Umeme Vijiji), kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika Mradi wa Umeme wa Mahenge hadi Mwaya. Umeme huo umeanzia Mahenge Mjini na kupitia Vijiji vya Mzelezi, Ruaha, Chirombora hadi Mwaya. Wakandarasi walifanya kazi hiyo kwa kasi na kusimamisha nguzo na nyaya katika mtandao wote.

Mheshimiwa Spika, ombi kwa Wizara; naomba Mradi ukamilike kwa sababu umeme haujawaka wakati nyaya na nguzo zimekamilika miezi saba iliyopita. Naomba Mradi huo sasa utoke Kata ya Mwaya kwenda Kata ya Mbuga ambako ni Makao Makuu ya Mbuga ya Selous, ambayo ina wawindaji wengi wanaongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mradi huo pia utoke Kata ya Mwaya kwenda Kata ya Ilonga na Ketaketa. Nitashukuru sana ombi hili likikubaliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, kwa nini umeme uishie Kibaoni na Usevya tu usifike Kata za Mizinga, Muze, Mtowisa, Milepa, Illemba, Kaoze na Kilyamatundu?

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kufikisha umeme Kijiji cha Sakalilo kwa nia ya kufunga mashine za kukoboa mpunga ili Wananchi wauze mchele badala ya kuuza mpunga na vilevile kuna Skimu ya Umwagiliaji; ni lini umeme utafika?

Mheshimiwa Spika, ni lini Mto Nzovwe ambaو ulishafanyiwa utafiti kuwa una uwezo wa kutoa megawati nane na zaidi Serikali itafanya kazi lini? Pia Mto Mombasa megawati kumi?

Mheshimiwa Spika, kwa nini umeme uishie Kamsamba uache kufikishwa Kilyamatundu wakati umbali uliopo ni kama mita mia moja? Huu ni ubaguzi naomba majibu?

Mheshimiwa Spika, Ukanda wa Ziwa Rukwa wote unahitajika kuwa na umeme kwani ni ukanda wa uzalishaji. Mawaziri tembeleeni Ukanda huu mwone fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ni tegemeo letu sote; atutendee haki nasi.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Prof. Muhongo na Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi yao nzuri ambayo imeliletea Taifa maendeleo ya aina yake.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kadhaa ambayo nataka nichangie katika hoja ya Wizara hii:-

Mheshimiwa Spika, mpango mzuri wa kusambaza umeme vijiji ni mpango wa pekee kabisa ambao umekusudia kuboresha maisha ya Wananchi vijiji, lakini Mradi huu unakumbwa na tatizo la kutengewa fedha kidogo. Hata kama zinatengwa na kuwekwa katika bajeti, lakini Wizara ya Fedha inashindwa kutoa fedha zote zilizowekwa kwenye bajeti na hivyo kuifanya Miradi yote iliokusudiwa kutekelezwa kushindwa. Hali hii huwakatisha tamaa Wananchi ambao tumekuwa tukiwaahidi tukiwa Majimboni.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo linakwamisha Wananchi wa vijiji kupewa huduma hii ya umeme ni uchache wa *transformer* zinazoletwa.

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu Mbeya Vijiji kuna viji vingi ambavyo umeme mkubwa unapita katika vijihi hivyo lakini Wananchi wanashindwa kupewa huduma hiyo kwa sababu *transformer* hazipo. Aidha, mfano wa vijihi hivyo ni

Lwanjilo, Ihango, Nsongwi Juu, Shibolya, Tembela, Iyela, Nyara, Ikocho Sekondari, Iyela Sekondari, Hatwelo na vingine vingi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vijiji hivyo huduma hiyo?

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Nsongwi Juu kinapakana na Ituha Mbeya Mjini ambako majirani zao wanapata umeme wa *MCC*. Je, Kijiji hiki hakiwezi kuunganishiwa umeme huo wa *MCC*?

Mheshimiwa Spika, naipongeza kazi nzuri inayofanywa na Wakala wa Umeme Vijiji (*REA*). Kwa kuwa sekondari nydingi za kata ziko vijiji; kwa nini Serikali isiwe na mpango maalum wa kupeleka umeme katika shule za kata? Mbeya Vijiji ina shule za kata ambazo zipo karibu kabisa na mapitio ya umeme. Mfano wa shule hizo ni Nsongwi Juu Sekondari, Igale, Isato, Mshewe, Ihango, Ikocho Sekondari, Shibolya, Mwakipesile, Iukwa na zingine nydingi. Ili kupeleka elimu ya TEKNOHAMA katika shule hizo ni vizuri pia zingefikiriwa katika mpango maalum wa kupeleka huduma hiyo. Walimu wengi pamoja na Waganga walioko vijiji, hawatakimbia wataishi vijiji.

Mheshimiwa Spika, tulielezwa katika Bunge lako Tukufu kuwa, vyanzo vingine vya mapato ya *REA* ni kutoza fedha kwenye simu. Je, huo mpango ukoje; Wananchi wanajua kwamba kila mtu akipiga simu fedha kiasi zinakatwa kwa ajili ya umeme vijiji? Tulipoelezwa katika Bunge lako tuliwaeleza Wananchi hivyo. Naomba Waziri atueleze amekwama wapi?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutafiti au kupata chanzo kingine cha mapato kwa ajili ya kuiwezesha *REA* waweze kusambaza umeme kwa haraka vijiji. Kutegemea fedha za wafadhili tutakwama, angalia Miradi ya Maji, nayo kwa kutegemea fedha za wafadhili haitekelezwi karibu miaka kumi sasa. Bila shaka Waziri atatoa majibu yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake, kwa maandalizi ya Hotuba nzuri, inayoleta matumaini mapya katika Sekta ya Nishati na Madini Nchini. Kwa kuwa Sekta ya Nishati ipo katika Mpango wa Serikali wa *Big Results Now*, tunaomba fedha ya kutosha ipatikane kwa utekelezaji wa Miradi yote iliyowekwa na pia uwepo usimamizi madhubuti zaidi ili iweze kukamilika kwa wakati. Kukamilika kwa Miradi hiyo kutasaidia sana kuondoa umaskini wa watu wetu kutokana na matumizi ya nishati ya umeme na pia kupunguza uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kuhoji mambo machache kama ifuatavyo:-

Kitaifa kunakuwa na kusuasua sana kwa Miradi inayotekelzwa na Kampuni ya *Symbion* na inaonekana kuwa Serikali haina meno ya kuwahoji wala kuwachukulia hatua. Sasa Wananchi waelewe nini kuhusu Miradi hiyo ukiwemo Mradi wa siku nyingi katika Jimbo la Busega wa Nyashimo – Kabita – Nyamikoma – Kalemela. Baadhi ya nguzo zilisimikwa tangu Aprili mwaka 2012 hadi leo hakuna kinachoendelea zaidi. Wananchi wanahitaji kufahamu hatima ya Mradi huu ambao unapita katika vijiji muhimu vya uchumi.

Viwanda vya pamba katika Mkoa wa Simiyu vimeduwa vikitozwa malipo ya umeme kwa miezi mitatu zaidi baada ya kufunga msimu wa kusindika pamba kama *KVA charges* ambazo ni asilimia 75 ya gharama ya matumizi ya kila mwezi. Hivi gharama hii ni ya kazi gani wakati mitambo huwa imezimwa? Kimsingi, gharama hii huwa inawaongezea mzigo mkubwa wasindikaji wa pamba na kuwarudisha nyuma kiuchumi. Mara kadhaa wasindikaji wameleta malalamiko kuhusu suala hili lakini wanapewa ahadi zisizotekelzwa. Gharama hii inatufanya tuhisi kuwa ni mradi wa kifisadi unaosimamiwa na watu fulani maalum ndani ya *TANESCO*. Nahitaji ufanuzi zaidi kuhusu hili na kimsingi tunataka mtindo huu ukomeshwe. Ninadhamiria kuondoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri iwapo suala hili halitapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, viwanda nya pamba vingi vilivyoko Wilaya za Busega na Bariadi havina umeme wa uhakika, kwa sababu umeme kutoka Shinyanga ni mdogo na hukatika mara kwa mara. Kulikuwa na maelezo ya kuvipatia umeme viwanda hivi kutokea Bunda ambapo *transformer* ilipelekwa Arusha kutengenezwa ili ije isaidie kuimarisha uzalishaji wa umeme wa Bunda. Hata hivyo, mashine hiyo bado hajafungwa. Matokeo yake, kwa viwanda ambavyo vimeunganishwa na umeme wa Bunda, inapofika msimu wa kusindika pamba huwa umeme unakatwa kuja Bariadi ili viwanda nya pamba nya Bunda vijitosheleze kwanza. Hali hii husababisha hasara kubwa kwa kukaa na pamba bila kusindika kwa muda mrefu vikisubiri viwanda nya Bunda vimalize. Kwa nini Serikali hailipatii uzito wa kutosha suala hili linalochangia kudidimiza Wananchi kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, kuna wakati nilimwandikia barua Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Miradi ya Umeme Wilayani Busega: Lamadi – Mkula – Mwanangi – Badugu – Busami hadi Kasolo na ule wa Nyashimo – Nyamatembe – Shigala – Busega – Igalukilo – Malili – Ngunga – Ngasamo. Majibu niliyopata yalikuwa na matumaini sana, lakini hadi sasa bado hakuna kinachoendelea. Miradi hii ipo katika hatua kadhaa za utekelezaji lakini kwa nini sasa kisifanyike kitu kamili kikakamilika? Nitaomba sana hata kwenye taasisi kama shule na zahanati ambapo miradi hii inapitia nazo zipate umeme.

Mheshimiwa Spika, ni lini kwa hakika Mradi wa Mgodi wa Dutwa – Ngasamo utaanza uzalishaji? Wananchi wamesubiri sana kujua maendeleo ya mgodi ili nao wajipange jinsi ya kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo.

Je, ni lini *TANESCO* itawalipa taasisi ya fedha iliyogharimia ujenzi wa njia ya umeme kutoka Mwanangi hadi Kiwanda cha Pamba cha *Alliance* katika Kijiji cha Kasoli? Baada ya kufanikisha ujenzi huo, sasa imekuwa ni usumbufu mkubwa kudai fedha hiyo kutoka *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, naomba nianze moja kwa moja kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini na nijikite katika suala la madini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini ni Sekta muhimu sana, inayoinua maisha ya watu na hasa vijana kiuchumi katika nchi hii. Kumekuwa na ugumu wa upatikanaji wa leseni za uchimbaji hasa kwa wachimbaji wadogowadogo wamekuwa wakihangaika na kunyanyasika sana. Kwanza, hawana maeneo ya kufanya shughuli zao za uchimbaji. Wanafanya shughuli za uchimbaji bila leseni kwani wamekuwa wakisumbuka namna ya kupata leseni.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2012/2013, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, aliongelea juu ya upatikanaji na utoaji wa leseni za uchimbaji pamoja na kuendeleza uchimbaji mdogomdogo, ukurasa wa 97/98 na Serikali iliainisha maeneo yatakayotengwa kwa ajili ya uchimbaji mdogo, lakini mpaka sasa Wananchi bado wanahangaika. Mfano, mzuri ni wachimbaji wadogowadogo wa dhahabu Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji hao wananyonywa kwa kuwa wanachimba kwenye maeneo ya watu na kwa masharti magumu, kwamba wanapochimba lazima wamuuzie mwenye eneo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atakapohitimisha bajeti yake, awaeleze Watanzania na wachimbaji wadogowadogo ni lini watapata uhuru wa masoko ya madini wanayochimba? Na ni lini watapata leseni na kupewa maeneo maalum ili waendeshe shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, pia wachimbaji wakubwa wa madini wanaotoka nje ya nchi na wanaopewa leseni ya kuchimba kama vile Wachina, Waturuki na Kadhalika, wamekuwa wakiwanyanyasa Watanzania kwa kuwafanyisha kazi kwa ujira mdogo na Wananchi wanakosa pa kulalamikia.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri mwenye dhamana, alitolee tamko suala hili ili Wananchi wasiendelee kunyanyasika ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la nishati, suala ambalo maisha ya Watanzaia walio wengi huendeshwa kutegemea nishati tofauti.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na nishati ya umeme, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa bajeti ya 2012/2013 kama Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ukurasa 75 na 76 inavyosema; lengo ni kuongeza uwezo wa kufua umeme na ujenzi wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme makao makuu na vijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa malalamiko kwa Serikali kwamba, Mkoa mpya wa Katavi tumesahaulika sana, kwani mpaka sasa tunatumia jenereta chakavu na zilizochoka. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze kuwa ni lini Mkoa wa Katavi tutaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa ili kupata uhakika wa umeme au ni lini tutapata jenereta mpya ili kuepuka adha ya umeme?

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa mpya wa Katavi kuna Wilaya mpya ya Mlele ambayo ni muunganiko wa Tarafa mbili kubwa ambazo ni Mpimbwe na Inyonga. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupe macho katika Wilaya hii ili Wananchi waweze kupata nishati ya umeme. Pia kuna Tarafa nyiningine kama Mwese na Karema, tunaomba Serikali ifikishe umeme katika Tarafa hizi ambazo zipo mpakani mwa Tanzania na Nchi Jirani za Congo, kuimarisha ulinzi na kuchochea maendeleo kibashara.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imejitahidi sana katika kutekeleza Mipango ya Serikali. Jambo kubwa ambalo ninawapongeza ni kumudu kusimamia *TANESCO* kwa kuondoa mgao mbaya wa giza ambalo lililikabili Taifa letu. Pamoja na changamoto za miundombinu lakini wamejitahidi sana.

Mheshimiwa Spika, pongezi za kipekee kwa Serikali kuboresha umeme katika Jiji la Dar es Salaam. Nikiwa Mbunge wa Mkoa, natoa shukrani nyingi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa mipango yao mizuri ya kuboresha Jiji.

Mheshimiwa Spika, kwa upekee, natoa shukurani kwa Wizara kunijengea uwezo kwa mafunzo katika nchi mbalimbali ambayo ndani ya mafunzo nimegundua yafuatayo:-

Kumbe Serikali yangu (Wizara) mnayo mipango mizuri ya Kimataifa ikiwemo ya uboreshaji miundombinu ya umeme katika Miji Mikuu.

Mheshimiwa Spika, nashauri endeleeni hivyo pamoja na changamoto za ukosefu wa fedha za kutosha, lakini juhudini zenu zinatia moyo. Umeme katika Wilaya ya Temeke umeshafika Kimbiji, sasa ufile Kata ya Pemba Mnazi.

Wilaya ya Ilala nashukuru Serikali imepeleka umeme mpaka kwa waathirika wa mabomu, naomba wanakijiji waliopo njiani ulimopita umeme nao wapewe umeme washushiwe *transformer*.

Wilaya ya Kinondoni kuna matatizo ya kukatika katika umeme maeneo ya Sinza, Kijitonyama, Mwenge na sehemu nyinginezo, tuangalie tatizo bado halieleweki vizuri kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kujengewa uwezo, nimeona Nchini Bangkok jinsi gani wana-*control* matumizi ya umeme. Unapotumia vyombo vyya umeme mfano *air-condition* hata ukiweka *high speed* inarudi kwenye matumizi ya kawaida tu. Hali hiyo inasaidia katika ku-*balance* matumizi ya umeme kila Mwananchi aweze kufaidika na huduma hiyo. Nashauri tuangalie kwa undani tuone kama inaweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunatumia sana umeme

wa juu lakini katika sehemu kubwa ya watumiaji kila mmoja anakuwa na *panel/yake*. Katika uboreshaji umeme vijiji ni bora Serikali ikaweka utaratibu wa kupata Kituo cha Umeme wa *Solar* na kuingiza katika Gridi ya Taifa kisha ukagawiwa kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi kubwa za Serikali kuendeleza upatikanaji wa umeme, lakini nyumba zinajengwa siku hadi siku Jijini Dar es Salaam mpaka maghorofa yanaanguka. Je, kuna mawasiliano baina ya wajengaji na *TANESCO*?

Nashauri Serikali isimamie majengo; vinginevyo, *TANESCO* watalaumiwa kila siku kwa tatizo la umeme kumbe na sisi Wananchi tuna makosa kwa kujenga bila utaratibu kwenda kinyume na mipango au bajeti za Serikali. *TANESCO* washirikishwe kwenye Kamati za Mipango Miji zinazotoa vibali vyta ujenzi waweze kutambua mahitaji yao mapema.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inapata hasara kwa kununua umeme wa gharama kubwa na kuuza kwa gharama ndogo. Pamoja na juhudhi kubwa za kupata gesi asilia iweze kuzalisha umeme wa bei nafuu. Tukiweza kubadili muundo wa uendeshaji wa *TANESCO* na tukaleta fedha, tunaweza kulipia umeme kwa *tariff* tofauti ya mijini na vijiji, kulingana na maeneo; mfano, Osterbay na Masaki, bei tofauti na Mbagala na Manzese. Mbona hata kodi za viwanja na *rent* za nyumba zinatofautiana kulingana na maeneo?

Mheshimiwa Spika, ushauri uzingatiwe, Uongozi wa Wizara; Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu, waendelee kuchapa kazi kama wanavyofanya; tutawakumbuka, hongereni sana tuko nyuma yenu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha ufungaji wa mashine za kukoboa mpunga wakulima wauze mchele badala ya mpunga na kukuza kipato chao; je, ni lini umeme utafikishwa Sakalilo?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamekuwa wakitambuliwa na Serikali kama wakulima stadi na wavuvi wa samaki. Pamoja na hayo yote, Serikali inaonesha kutojali maendeleo yao. Sasa tunataka kujua ni lini maendeleo ya umeme yataboreshwa Mkoa wa Rukwa ukiacha Laela na Kasanga ambapo tuliahidiwa umeme wa *REA*?

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa na sisi watu wa Rukwa mtuone tu binadamu na Watanzania wenzeni, tunaohitaji kuishi kwa kukifurahia Chama cha Mapinduzi na Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini katika Mkoa wa Rukwa maendeleo ya uwekaji umeme yanaonesha kutojali Mkoa wetu na kutufanya tuendelee kuonekana kama sisi hatuko Tanzania, wakati ukipita Mikoa mingine utaona kama kweli ni Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo gani katika Mkoa wa Rukwa ukilinganisha na Mkoa mpya wa Katavi ambao sasa unamelemeta kwa umeme hadi Vijiji vya Usevya vina umeme au katika Mkoa wa Rukwa hatuna wataalam wanaoweza kusimamia umeme kama utaongezwa katika maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Mkoa wa Rukwa yanaonesha kuzorota kwa sababu ya Miji midogo kukosa umeme na hii inasababisha Serikali kuwa na ubinafsi kwa wakubwa wenzao kupewa upendeleo wa pekee kufuatana na nafasi walizo nazo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili la kutojali wanyonge litajionesha tu hata upande wa umeme wa *REA*, Mkoa wa Rukwa kuwa wa mwisho japokuwa tuna watumishi mahiri *TANESCO* na wenyewe bidii na kazi na ujuzi pia.

Mheshimiwa Spika, jambo ninalosema hapa, naomba katika suala la umeme wa *REA* na sisi tupewe kipaumbele. Siyo hivyo tu, inasikitisha kuona Wananchi walio wengi Mkoa

wa Rukwa, Wilaya ya Kalambo Vijiji na Jimbo la Kwela hata vijiji vya jirani ya Mkao – SBA Mjini na Wilaya Nkasi, hawana huduma ya umeme. Mnajua kabisa umeme ni maendeleo, ajira, starehe, huduma, biashara, ni kinga ya uharibifu wa mazingira na pia ni ustaarabu.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kutowafikishia umeme Wananchi wa Rukwa ni kuwadumaza kimaendeleo, ni kuwafunga *speed governory* maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sumbawanga Vijiji kutokuwa na umeme hata kijiji kimoja wala Wilaya yenyewe ni Wilaya ya muda mrefu, ina vyanzo vingi, makaa ya mawe na vyanzo vingi vya Maporomoko ya mito na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kufikisha umeme Mji Mdogo wa Laela kushusha katika vijiji vya njiani katika Kata za Kaengesa, Mpanda Muungano, Sandulula, Mpui, Kalambanzite na Lusaka; je, ni lini sasa Wananchi wategemee kupata umeme huo na hata Ukanda wa Ziwa Rukwa?

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa umeme katika maeneo haya ni utayari wa watu, ujenzi wa nyumba bora, sekondari nane, vituo vya afya vinane na zahanati 40. Uchumi kwa Wananchi, wauze mchele badala ya mpunga, wauze juice na unga badala ya mahindi.

Mheshimiwa Spika, Viongozi au Mawaziri wazunguke maeneo yote ya Mkao wa Rukwa, siyo kupendelea baadhi ya Mikoa fulani ili kuona fursa zilizopo katika maeneo yote ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kwa nia ya maandishi, nichangie Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Nishati na hasa mafuta jamii ya petrol kwa uchumi na usalama wa nchi ni kama damu kwenye mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kwanza ni hali ya ongezeko la watu wanaotegemea au hata kufuatilia shughuli za tasnia ya madini ili kukidhi kiu hii na hasa kupunguza malalamiko ya Wananchi. Nashauri Chuo cha Madini Dodoma kibadilishwe muundo wake na kisukwe upya. Ijengwe taasisi itakayosimama yenyewe badala ya mfumo wa sasa inapoendeshwa kama Idara ya Wizara ya Madini. Chini ya muundo mpya, chuo kiajiri wakufunzi na walimu wa kutosha. Miundombinu iandaliwe kwa kupokea wanafunzi wengi kwa wakati mmoja. Yawepo mafunzo ya muda mrefu (miaka minne), muda wa kati na muda mfupi (majuma mawili - mtatu). Lengo hapa ni kuwa Chuo kiwekwe katika hali ya kuwafundisha vijana na kwenda kujajiri katika Sekta ya Madini. Pia wale ambao tayari wapo katika shughuli kwa mtindo wa mafunzo mafupi, wafuatwe huko na kupewa ujuzi wa shughuli. Kupitia Chuo hiki, siku zilazo, mikopo kwa wachimbaji wadogo wadogo itolewe kwa kada ya watu ambao uwezo wao unafahamika.

Mheshimiwa Spika, mchango wa pili ni tasnia ya mafuta jamii ya petrol, yaani *down stream activities*. Itoshe kusema, Serikali haija simamia vizuri Sekta hii na mambo yanaonekana yanakwenda vizuri kwa sababu daima Mungu yuko nasi, uendeshaji wa uagizaji wa mafuta kwa wingi una upungufu. Chombo – *P/C*, muundo wa au uendeshaji wake siyo sawa, narudia tena kuionya Serikali utendaji wa Chombo hiki unawenza kupelekeea kushitakiwa na kuibebesha nchi adhabu kubwa katika mamilioni ya Dola za Kimarekani. Rejea mawasilino ya matishio toka kwa wagavi kwenda *P/C*.

Nilitegemea baada ya kutoa tahadhari ya kwanza Julai, 2012, Serikali ingejiangalia na kuweka mambo sawa. Hii ni pamoja na mipangilio isiyo sawa, ambayo ilipelekeea vipindi fulani nchi kukaribia kukosa mafuta na ujanja wa kubadili *lay can unatoa* faida kwa wagavi. Kitaalamu, binafsi nasikitika wakati vyombo vinavyohusika, Serikali ikiwemo Nchi, inaposhindwa kupata faida ya kushusha *premium MR –LR*, kama ilivyoahidiwa. Nashauri kuwa, Serikali ilisimamie hili, kinyume chake inaweza kuchukuliwa kuwa ni uzembe au makusudi.

Mheshimiwa Spika, upungufu mwingine katika usambazaji wa mafuta, Serikali inashindwa kuona kuwa vituo salama vya mafuta vimerundikana mijini tu na kwenye njia kuu. Wilaya za pembezoni na vijijini, mafuta yanauzwa kwenye vibuyu, ndoo za plastic na viloba vya rambo. Udhibiti unaelekeza macho sehemu moja! Msingi wa utawala wa mafuta kwa uchumi, usalama na ustawi wa nchi ni *availability, quality & affordability of product with maximum safety*. Mafuta jamii ya petrol kwenye mfuko wa *plastic* hakuna ubora na usalama. Hii haihitaji mshauri toka Canada au Ujerumani. Tunapaswa kuwa na vituo kwa ngazi zote tatu; *petrol service station, petrol station na kebsite*. Kampuni zote za mafuta zidhibitiwe kwa kuwa na vituo mijini mpaka vijijini na asiyekubali aelezwe, huo ndiyo udhibiti. Kanuni ya kupanga bei yaweza tunzwa kutoa motisha.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ni Kampuni ya Mafuta ya Kitaifa. Faida kubwa ya Taifa letu kuwa na kampuni ya aina hii ni kuntuondoa hofu na mashaka, lakini pia kutoa fursa ya kujifunza. Ipo hali ya kutokujua mionganoni mwa jamii wakiwemo wasimamiaji wa sekta, kwa sababu moja tu kuwa na ujuzi usiokuwa na uzoefu wa kutenda. Matokeo yake ni hofu na mtu kuishia kuhesabu faida ya pale ambapo hukuwekeza mtaji. Kampuni ya Kitaifa itawezesha mkono wa Serikali kushiriki katika shughuli na kuwa na uhalisia wa mambo yanavyokwenda, yaani kuondoa hofu na mashaka. Inapotokea fursa na faida kupindukia, pato hilo linakwenda Serikalini. Sielewi king'ang'anizi cha kuanzisha kampuni hii kinatokea wapi?

Tunayo faida ya nchi jirani ambazo zitakuwa na amani ya moyo kuendesha shughuli na kampuni ya Serikali. Tunazo Halmaishi za Wilaya na Taasisi za Serikali ambazo zitageuka wateja wa kwanza. Kampuni ya Kitaifa itakuwa tayari kufungua kituo kila pembe ya nchi hii kwani ni ya Kitaifa, kampuni binafsi hata ikilazimishwa itakuwa inaonewa tu. Nashauri hoja itafutiwe muda na kuongeleva kwa kina ili tupeane uzoefu wa wenzetu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ni umeme. Kigezo

cha kupima maendeleo ya Taifa lolote ni pamoja na matumizi ya umeme. Hata hivyo, kipimo hicho kitakuwa na upungufu iwapo umeme huo utakuwa unaishia na kutumika kwa wingi katika migodi na viwanda.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuendeleza miradi ya kupeleka umeme vijiji kwa wingi, kwa faida zilizo dhahiri. Ipo mitambo midogo ya kukausha nafaka (*drier*), ambapo maharagwe yaliyovunwa saa nne asubuhi baada ya saa tatu yamekaushwa na tayari yanakwenda sokoni. Tunapoteza mazao mengi katika hatua hii ya uzalishaji. Ufugaji wa samaki katika mabwawa unahitaji mitambo ya kuongeza *oxygen*. Mitambo hii inahitaji umeme na pale inapotumika tija ni mara sita. Hii ni kwa kutaja mifano michache inayoweza kulipandisha hadhi Taifa letu, kwa kufanya vizuri kile kilicho katika uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo, hapa juu hoja yangu ni kuwa, jitihada zifanyike kukamilisha Mradi Kabambe II katika kipindi cha mwaka mmoja. Hoja ya tozo ya shilingi 100 katika kila lita ya mafuta; *diesel/na petrol*, upo umuhimu wa kuweka kiwango katika simu za kiganjani ili tupate angalau shilingi bilioni 150 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, muhimu kwa Watanzania kama Taifa ni kuelewa kuwa, misaada tunayopewa, Serikali zinazotupatia mikopo hiyo, hutoza kodi Wananchi wake. Uzuri wa Miradi ya *REA* ni kuwa tozo zinaweza kupewa muda kikomo, tuweke tozo miaka miwili au mitatu tukusanye trillioni mbili, tujenge miundombinu mambo yaishe. Naiona taswira ya Tanzania mpya pale ambapo shule zote zinapokuwa zimepata umeme ukiambatana na mtandao wa simu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ni rasilimali gasi asilia na mafuta jamii ya petrol yachimbwayo. Historia ya shughuli hii, yenye ghamama kubwa, inahusisha imani kwa wale waliomwacha Mungu wakati unapotafuta rasilimali yenye thamani kubwa kama hii na hasa unapotumia ghamama kubwa hapana budi kuomba.

Mheshimiwa Spika, kama niliviyowahi kusema katika Bunge lako Tukufu, imani yangu inanituma kuwa, ipo siku mimi nikiwa Mbunge bado na Rais wa Nchi akiwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tutasherehekea Bungeni uvumbuzi wa mafuta mengi tu. Imani yangu inanituma pia kuwa, waasisi wa tasnia ya utafutaji wa mafuta kama hawataalikwa katika jukwaa la Spika na kutambuliwa, juhud zetu zitachelewa zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mengi hoja hapa ni kulenga kwenda pamoja kama Taifa hasa tunapofanikiwa kuhusisha rasilimali iliyotumika hapo mwanzo na kuleta mafanikio kwa ajili ya kuazima uzoefu, lakini pia kuwaenzi. Tunapofikiria kuanzisha Kampuni au Idara ya *TPDC* ya kwenda kuchimba mafuta au gesi ni busara wastaifu wenye nguvu bado wakarudi na kufanya kazi kwa mkataba.

Inasikitisha mfanyakazi aliyeshiriki zoezi gumu la hatua za mwanzo, asishiriki katika hatua za kuona matunda. Kundi hili nashauri lihamasishwe kuanzisha kampuni na vijana toka vyuoni katika kushiriki shughuli nytingine zitokanazo na tasnia za gasi asilia. Kundi hili ambalo nategemea kuona Serikali ikilitumia kuelimisha jamii juu ya gasi asilia na mafuta badala ya makundi ya wavizajji wanaojitokeza kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, tusingoje hao wastaifu waombe tuwafuate. Kimsingi, Serikali iwafuate. Katika mazingira ambapo wahamasishaji wanadai Wananchi waruhusiwe kuchota gasi kwa ndoo au basi walipwe dola 2,000 kwa kila juma, ni nafuu kuangalia matumizi ya kundi hili ambalo kufikisha miaka 60 kumewatoa ofisini.

Mheshimiwa Spika, gasi asilia Mikoa ya Lindi na Mtwara, Gazeti la Raia Mwema, toleo la tarehe 16 Januari, 2013 lilikuwa na makala yangu juu ya rasilimali hii. Makala hii imesambazwa kwa watu wengi, ikiwemo Watendaji Waandamizi wa Serikali. Gasi asilia ina faida kwa Taifa na mahali inapochimbwa. Huo ndiyo mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, Rasimu ya Sera ya Gasi Asilia

tuliyopewa ni ya *downstream*, lakini wawekezaji wakubwa wanaotia hofu inaanzia *upstream*. Pamoja na hali hiyo, nashauri Sera itamke kwenye *specific objective* yafuatayo:-

- Pato la gasi asilia litawekezwa kwenye shughuli za asili za Watanzania ili wazalishe kwa tija kubwa na wasitegemee gasi asilia (wasibweteke); na

- Pato la gasi asilia litawekezwa kwenye elimu ya Wananchi ili kuwapa ujuzi wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kutoka kwa Wananchi ambao wanazungukwa na migodi ya madini. Wananchi hao hawanufalki na migodi hiyo. Wawekezaji wengi ambao wamezunguka migodi, wamekuwa hawatimizi ahadi zao ambazo wamekuwa wakizitoa kwa Wananchi. Kwa mfano, kuwajengea Wananchi shule, zahanati na visima vya maji safi; ahadi hizi wamekuwa hawazitimizi kwa wakati mwafaka. Wamekuwa wakijinufaisha wao wenyewe (wawekezaji). Je, ni lini Serikali itahakikisha inawadhibiti wawekezaji waliowekeza kwenye migodi ya Madini ili kuhakikisha wanatekeleza ahadi za maendeleo walizozitoa kwa Wananchi?

Mheshimiwa Spika, hawa wawekezaji katika migodi; kwa mfano, Mgodi wa Geita (*Geita Gold Mine*); katikati ya huu mgodi kuna uwanja mkubwa wa ndege, ambao ndege zinaruka na kutua usiku na mchana kwa ajili ya ubeabajji wa dhahabu kupeleka nje ya nchi. Je, Serikali ina udhibiti gani kuhakikisha dhahabu haitoroshwi kwenda nje ya nchi?

Je, Serikali ina udhibiti gani kuhakikisha kila dhahabu inayotoka pale kwenye Mgodi wa Geita inalipiwa kodi?

Kumekuwa na tabia ya kufichwa kwa mikataba mikubwa mikubwa inayofanywa baina ya Serikali na wawekezaji wakubwa wakubwa na kuwafanya Wananchi

wawe na maswali ya kujiuliza, kwa nini mikataba hiyo ifichwe kama haina matatizo. Je, ni lini Serikali itakuwa inaweka mikataba wazi ili kuwaondolea washwasi Wananchi?

Mheshimiwa Spika, gesi asilia inaleta matatizo katika Mkoa ilikogunduliwa gesi hiyo. Mkoa huo umekuwa hauna amani na kabla gesi hii haijachimbwa, Wananchi wa Mkoa huo ni lazima wapatiwe elimu ya kutosha na Serikali. Vilevile Serikali iwanufaishe Wananchi wa Mkoa huo kabla gesi haijasafirishwa kwenda Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, kwenye Mkoa huo pajengwe kiwanda cha kusafishia gesi ili kutoa ajira kwa Wananchi wa Mkoa huo na kuepusha migogoro baina ya Serikali na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka 52 tangu tupate Uhuru, lakini cha kushangaza vijiji vingi havijapata umeme na vilivyokuwa na umeme, umeme wake ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenye bajeti ya kutosha ili Wananchi wa vijiji wapate kunufaika na umeme.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Muhongo, Manaibu wake na Katibu Mkuu, kwa kazi yao nzuri, pamoja na ugumu wake.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ya kisasa katika nyanja zote inahitaji nishati ya aina moja au nytingine. Kwa hiyo, umuhimu wa sekta hii katika uchumi wetu haina mjadala. Tatizo linakuwa ufinyu wa bajeti. Ninashauri tutambue kwamba, Sekta ya Nishati tukielekeza ndani yake italipa yenyewe. Tutazalisha zaidi.

Wilaya ya Muleba ina wakulima, wafugaji na wavuvi. Wakiwa na umeme katika vijiji na nyumba, wataweza kuzalisha zaidi; ni jambo linalohitaji kuangaliwa na REA kwa umakini. Visiwa vyta Mazinga na Ikuza ndiyo wazalishaji wa samaki, lakini wengi huharibika au kulazimika kukaushwa na

kupungua thamani, kwa sababu hakuna umeme. *REA* wafanye jitihada maalum kupeleka umeme katika Visiwa hivi. Aidha, *REA* watambue Kata za Muleba ambazo zimeomba kwa muda mrefu lakini hadi leo hawajapata umeme. *TANESCO* imekuwa ikitoa vikwazo mbalimbali, ninaomba sasa kati ya *TANESCO* na *REA*, suala hili na ahadi za Mheshimiwa Rais zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kero kubwa iliyoenea katika maeneo ya madini na migodi ni Wananchi kutopewa fidia stahiki. Ninaomba Wizara ya Madini ishirikiane na Wizara ya Ardhi, kutekeleza sheria ambazo ziko wazi katika suala hili. Anayepewa *Mining Rights*, huwezi kuanza kuchimba kabla hujafidia na kuwahamisha (*resettle*), wakazi wa pale inapohitajika. Haikubaliki kwamba, sheria hii inavunjwa. Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani juu ya tatizo hili katika Mikoa ya Madini?

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Waziri kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo, lakini kodi iliyowekwa kwenye *PML* ni kubwa na wengi hawamudu. Mheshimiwa Waziri anafuatilia madeni ili *STAMICO* iweze kuwasaidia vyema zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza na kuunga mkono hoja hii.

MHE. MATHIAS M. CHIKAWE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia hoja moja tu; umeme katika Vijiji vya Nachingwea. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri alitoa orodha ya vijiji ambavyo vingepatiwa umeme. Orodha hiyo haina tofauti na orodha ya mwaka huu; yaani ni kusema kuwa, kwa mwaka jana hakuna hata kijiji kimoja kilichopatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba mwaka huu umeme huo upatikane kama ilivyopangwa. Aidha, vijiji viongezwe ili

angalu vijiji vile vikubwa vyenye miradi ya uzalishaji vipatiwe umeme. Vijiji vya Mnero, Lionja na Marambo, viongezwe katika orodha hii. Umeme uliopo unapita karibu sana na vijiji hivi. Gharama haitakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia mgogoro mkubwa uliopo katika Kijiji cha Ikungu na *Ntaka Hill*, baina ya wachimbaji wadogo wadogo wenyewe kwa wenyewe na wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wadogo. Mgogoro huu ni wa siku nyingi na Maafisa wa Madini wa Kanda wameshindwa kuutatua kwa sababu wenyewe wana maslahi katika sehemu hizo. Aidha, kila wakati wachimbaji wadogo wanapogundua madini, wakienda kuomba leseni wanaambiwa kuwa sehemu hiyo tayari imeshachukuliwa. Mara nyingi hii siyo kweli bali wale maafisa wakishapata taarifa hizo, huwa wanawapa leseni ndugu zao na hii huzalisha migogoro ambayo haina sababu za msingi. Waziri achukue hatua dhidi ya maafisa hawa wasiotimiza wajibu wao.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inisaidie njue ni lini Wilaya mpya ya Chemba Mkoani Dodoma itapata umeme?

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka jana, inayomalizika Juni mwaka huu, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme, tathmini tayari imeshafanyika kilichobaki sasa ni kupeleka nguzo tu.

Mheshimiwa Spika, pili, Kijiji cha Tandala chenye idadi kubwa ya watu, nyumba nzuri na barabara ya *TANROAD* kitapewa umeme lini? Umeme upo kilomita nne tu jamani, jitahidini basi wapate umeme.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, umeme ni nyenzo muhimu katika maisha ya binadamu, lakini la kusikitisha baada ya miaka 50 ya Uhuru, bado upatikanaji wa umeme ni mdogo sana hasa vijijini. Kwa kuwa

Mheshimiwa Waziri amesema kwenye Hotuba yake kwamba, atasambaza umeme vijiji na mjini, basi tunataka tuone kwa vitendo na siyo kwa maneno.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme hapa nchini unachukua muda mrefu kutokana na sababu nyingi kama vile ghamama za usambazaji umeme kuwa kubwa, ughali wa nguzo za umeme, pamoja na watendaji wabovu wa Wizara hii. Naiomba Serikali ilione hili na ilipatie ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walifurahi sana kwa upatikanaji wa gasi Mkoani Mtwara na Lindi. Furaha ile imekwishatoweka baada ya kuona jambo zuri kama hilo limeleta chuki, uhasama, fujo na uchonganishi katika nchi yetu. Baadhi ya watu ambao hawaitakii mema nchi yetu, wameanza kupotosha Wananchi na kusababisha mauwaji na uharibifu wa mali.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa Hotuba yake aliyosema wahusika wakamatwe bila kujali ni nani. Naamini kuwa, ujumbe umefika na wahusika wa kusaka wahalifu wafanye kazi hiyo mara moja na ni lazima watuhumiwa wote wapatikane na wafikishwe mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nataka kuiuliza Serikali; kwa kuwa fujo hizi ziliwahi kutokea mwaka jana; je, hatua gani zilichukuliwa kwa wale waliofanya fujo na kusababisha vifo na uharibifu mali nyingi zikiwemo za Wabunge?

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, naomba majibu kutokea kwa Mheshimiwa Waziri, kwa maswali yafuatayo:-

(i) Tunduru itapata umeme wa uhakika wa Gridi ya Taifa kutokea wapi; Namtumbo au Masasi?

(ii) Umeme huo utafikishwa Tunduru lini?

(iii) Hivi mnajua kwamba Wananchi wa Tunduru tumechoka kuona umeme ukisambazwa kwenye vijiji vya

Wilaya za wenzetu huku sisi tukiwa tunaendelea kutumia vibatari?

(iv) Mnafahamu kuwa binadamu huwa anafikia kiwango cha mwisho cha kuvumilia na kusubiri?

Mheshimiwa Spika, Bajeti ijayo tunataka majibu kwa vitendo na si maneno tena.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu, kwa kuwasilisha Hotuba nzuri Bungeni na yenye kutoa matumaini makubwa kwa maendeleo ya nchi iwapo yaliyomo yatakekelezwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwapongeza zaidi kwa kutoa vielelezo vingi vya utekelezaji wa upelekaji umeme vijijiini na maeneo mbalimbali ya utafutaji na uchimbaji mafuta au gesi asilia na madini sawia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nasikitishwa na ucheleweshaji wa upelekaji umeme vijijiini. Kwa mfano, umeme ulivutwa kutoka Tagamenta – Iringa hadi Kidabaga Wilayani Kilolo tangu mwaka 2009 na ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 27 Oktoba, 2009. Inasikitisha kuona vijiji mbalimbali kama vile Kilolo kibaoni, Luganga, Ilamba na Shule za Sekondari za Udzungwa, Maria – Consolata na Dabaga, hazijafikishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka 2011 umeme ulivutwa kutoka Ilula hadi Ruaha – Mbuyuni, Wilayani Kilolo. Inasikitisha kuona kwamba, umeme huo haujashushwa katika Shule ya Sekondari ya Lukosi na Vijiji vya Kidika na Msosa; hivyo, kupunguza kasi ya maendeleo katika Wilaya

ya Kilolo. Je, ni lini hasa umeme sasa utafikishwa katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Umeme katika Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2012/2013, Wizara ya Nishati na Madini, inipatie majibu juu ya hatua ilizochukua kupitia maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya tarehe 27 Julai, 2012 na michango yangu ya maandishi tarehe 27 Julai na 28 Julai, 2012. Pia nipewe majibu juu ya hatua ambazo Wizara ya Nishati na Madini kupitia kabrasha lenye barua za muda mrefu za Wananchi kwenda kwa TANESCO za matatizo ya umeme katika maeneo yao, ambayo nilikabidhi kwa Wizara wakati ilipoitisha mukutano na ziara na Viongozi wa Jiji la Dar es Salaam kuhusu Miradi ya Umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini itambue kuwa, kwa upande wa Jimbo la Ubungo, yapo maeneo ambayo nguzo zinaanza kuwekwa. Hata hivyo, kumekuwa na uhaba wa vifaa mbalimbali kama nyaya na vifaa vingine. Hii ni kwa sababu mfumo wa ununuzi wa vifaa ambaao unaratibiwa na TANESCOMakao Makuu, unahuishisha kupeleka katika Mikoa na kwenye Miradi, vifaa vichache badala ya kupeleka vifaa vyote vinavyohitajika (*Complete Package*). Katika kuhakikisha kwamba, vifaa vinapatikana, Wizara iweke mkazo katika miradi ya maeneo yafuatayo ambayo ilipangiwa fedha miaka ya nyuma, lakini utekelezaji wake haujakamilika mpaka hivi sasa: Malamba mawili, Msingwa, Msikititi kwa Mtoro, Msakuzi Loperanya kwa Bibi, kwa Masista Hondogo, Kibwegere Mloganzila, Goba Kulangwa na Goba Matosa Darajani.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara tofauti na miaka iliyotangulia, itekeleze kwa wakati miradi ya kusambaza umeme maeneo ya pembezoni, ikiwemo katika maeneo ya Msumi. Hatua kama hizo zichukuliwe kuhusu maeneo ya Miradi ya Maji inayohitaji umeme; mfano, katika Kata ya King'ongo.

Mheshimiwa Spika, Wizara itoe maelezo juu ya sababu za kutokamilisha mchakato wa kulipa fidia kwa Wananchi walio eneo la karibu ya mitambo ya umeme, maeneo ya Ubungo, Kibo na Kisiwani, pamoja na bajeti kutengwa katika mwaka 2012/2013. Aidha, Wizara na TANESCO, wamshirikishe Mbunge katika makubaliano yanayofikiwa na Manispaa ya Kinondoni kuhusu tathmini ya fidia kwa Wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata pia majibu kuhusu hatua ambazo Wizara ya Nishati na Madini imechukua juu ya mapendekezo niliyotoa kuhusu miundombinu ya usambazaji na matumizi ya gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Wizara ishirikiane na Wakala wa Vipimo (*WMA*), katika kuhakikisha Wananchi wanapata thamani halisi ya fedha (*value for money*) ya gesi ya mitungi na *EWURA* longeze ufanisi katika udhibiti wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo yaliyomo katika Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, katika majumuisho, ni muhimu Waziri akatoa maelezo ya ziada kuhusu masuala yafuatayo:-

Uchimbaji wa madini ya urani: Sababu za Waziri kutoa leseni ya Kampuni ya Mantra kwa ajili ya uchimbaji wa madini hayo katika eneo la Mkuru River, Namtumbo, bila kuzingatia maoni tuliyotoa mwaka 2011/2012 na bila kujali kwamba hatua hiyo ingeweza kutumika kuibana Kampuni hiyo kulipa kodi inayodaiwa na Mamlaka ya Mapato (*TRA*). Aidha, Wizara ipitie Kanuni (*Regulation*), ambayo ilitungwa na Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2010 na Kanuni za mwaka 2011, kubaini mgongano wa kimajukumu baina ya Wizara na chombo chenye dhamana ya masuala ya mionzi ya kiatomiki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara izingatie kuwa chombo hiki ndicho kimepewa mamlaka pia na vyombo vya kimataifa, kuhakikisha usalama katika uchimbaji na usafirishaji wa madini hayo na pia kuepusha madini hayo kuuzwa kwa nchi zenyenye mipango ya kuandaa silaha za nyuklia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Tanzanite*; Wizara ya Nishati na Madini itoe maelezo ya sababu za kwenda kinyume na ahadi za Mheshimiwa Rais Kikwete za mwaka 2005 na 2010 katika eneo la Mererani, ambapo aliahidi leseni ya Kampuni ya *AFGEM/Tanzanite One*, ikifika ukomo eneo hilo lingetolewa kwa wachimbaji wadogo ama umiliki wa wazawa kwa ujumla. Uamuzi wa Wizara ya Nishati na Madini kupitia *STAMICO* kuingia ubia na kuwa na hisa asilimia 50 kwa 50, hauendani na ahadi zilizotolewa na Rais. Aidha, Wizara na *STAMICO* kwa pamoja hawakuzingatia baadhi ya masuala muhimu kwa mujibu wa nyaraka za makubaliano yaliyofikiwa mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke wazi makubaliano hayo yaliyofikiwa na hatua zinazochukuliwa kurekebisha kasoro zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini (*MRI*); Wizara ya Nishati na Madini ieleze hatua ilizochukua kutekeleza mapendekezo tuliyotoa mwaka 2011 kuhusu Chuo husika. Mwaka 2011 tulipendekeza kuanzishwe Chuo Kikuu cha Mafuta na Gesi Mtwara, Serikali ikakubali. Hata hivyo, suala hilo halikuwa kwenye utekelezaji mwaka 2012/2013 na haliko kwenye Bajeti ya 2013/2014. Hivyo, kwa kuanzia katika mwaka 2013/2014; Chuo cha Madini kianzishe Kampasi (*Campus*) Mtwara.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iweke wazi Ripoti ya Kamati iliyoundwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Madini (*MRI*), Profesa Mruma, kufuatia malalamiko ya Wananchuo. Pia Waziri wa Nishati na Madini aeleze hatua zilizochukuliwa kufuatia barua iliyoandikwa kwake na wananchuo mwanzoni mwa mwaka 2013, yenye madai juu ya matumizi mabaya ya fedha na madaraka yenye athari kwa Wananchuo na Umma kwa ujumla.

MHE. ABDALLA HAJI ALI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyekiti Mungu, muweza wa mambo yote. Aidha, nakupongeza Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wako wa busara na hekima kubwa juu ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa ufupi sana, nizungumzie mambo makubwa yanayoikabili nchi yetu kwa sasa, nalo ni kuhusu vurugu za Mtwara zinazohusishwa na gesi asilia iliayogunduliwa huko Mtwara.

Mheshimiwa Spika, jambo hili Serikali isilichukulie urahisi hata kidogo, kwani tayari limekwisha gharimu maisha ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, mambo mawili napenda kuishauri Serikali, kama yatafanywa huenda yataisaidia Serikali na kuondokana na vurugu za Mtwara na mfano wa hizo katika sehemu nyine ambazo zinaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kwamba, watu waelimishwe juu ya rasilimali za nchi kwamba, popote patokeapo maliasili nchini ni ya Watanzania wote. Kinyume na ufahamu wa watu wengine kwamba, kilichoonekana Mtwara ni cha Mtwara pekee. Elimu hii watu hawana na ndiyo wengi wakadhani kwamba, wanaporwa rasilimali yao na Serikali ili ikatumike sehemu nyine. Naishauri Serikali itoe elimu kiasi cha kutosha hadi watu waondokane na fikra mgando kwamba kitokeacho kwao ni cha kwao tu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, naishauri Serikali ikae na Wananchi wa Mtwara, iwasikilize wanataka nini juu ya suala zima la rasilimali ya gesi. Serikali ifahamu kwamba, suala la vurugu za Mtwara kwa kiasi fulani linapigiwa debe kisiasa, lakini kwa nia njema ya Serikali juu ya Wananchi wake, nashauri kwamba, Wananchi wa Mtwara wasipuuzwe. Vyombo mbalimbali vitumiwe kufanya mazungumzo na Wananchi hawa na ili nchi itulie, basi Wananchi washirikishwe katika mazungumzo waseme wanataka nini juu ya rasilimali hii na Serikali isiwe kaidi katika hili na iwape matumaini mazuri kiasi kwamba tuondokane na balaa ya fujo ambayo haina tija yoyote katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa mara nyine tena, ijaribu kutumia mbinu shirikishi kwa maslahi ya nchi.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, kwa kifupi kabisa, napenda kuchangia maeneo makuu matatu:-

Tathmini zinazofanywa kwa ajili ya Wananchi kupisha shughuli za mgodi, zoezi hili kwa sasa limegubikwa na rushwa na dhuluma kubwa sana. Wananchi wanafanyiwa mambo kama vile siyo watanzania. Zamani tathmini ilikuwa ikifanywa baina ya Mgodi na Wananchi, ambapo *Barrick* walikuwa wakitoa fidia ya dola 25,000 kwa heka na hii ilikuwa pamoja na fidia nyingine kadiri itakavyompendeza *Barrick*. Sasa hivi Uongozi wa Wilaya pamoja na Mkoa kwa maana ya *Task Force* ambapo huenda kwenye tasnia bila hata taarifa, kuweka alama na wakati mwingine huvunja nyumba na mali zingine. Vilevile hudai walipwe fedha kati ya shilingi 100,000 na 300,000 au wengine huombwa watoe sehemu ya maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ombi la Wananchi wa Nyamongo na hasa Kijiji cha Nyakunguru ni kufanyiwa tathmini na Mgodi. Kwa maana Serikali isitwae ardhi kwa niaba ya Mgodi. Hii siyo haki kwani hutia mwanya wa ukandamizaji; iwe *negotiation* kati ya mthaminiwa na mgodi. Pia kwa mujibu wa *Mining Act*, inatakikana Mgodi uwape makazi mbadala wale wote wanaohamishwa sambamba na kuwapa fedha; hivyo, naomba Wizara yako pamoja na Wizara ya Ardhi kustopisha zoezi la *Task Force* mara moja, kwani sasa hali ni tete.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu wachimbaji wadogo wadogo. Mwaka 2011 yalipotokea mauaji ya wananchi watano, Mawaziri wa Nishati, Mahusiano na Uwekezaji, walienda kuongea na Wananchi na kuwaahidi kuwa, watatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo, ikiwa ni moja ya utatuzi wa Wananchi kwenda kuokota mawe kwenye vifusi, kwani kabla ya uwekezaji na ubinafsishaji, Wananchi wale walitegemea mgodi ule kama chanzo muhimu cha fedha, hamna shughuli za ufugaji wala kilimo kule. Serikali ilituahidi kutenga maeneo, kutoa elimu pamoja na vifaa na mtaji kwa Wananchi, vilevile Mgodi wa *Barrick* walikuwa tayari kuwapa na kuwezesha *artsan miners*,

Iakini *Barrick* wapo tayari na wanasesma Serikali ndiyo wanachelewesha.

Mheshimiwa Spika, vilevile tulishauri juu ya kuwekwa maeneo muhimu kwa ajili ya kumwaga vifusi ili Wananchi waweze kwenda kuokota *left-over*. Vilevile vifusi na kokoto vingetumika katika kujenga nyumba za kudumu au kujaza kwenye barabara. Tunaomba sana haya yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya Askari wa Jeshi la Polisi kutumika kulinda Mgodi. Hili ni jambo lisilokubalika na mwaka jana aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alisema, kuanzia mwaka ule polisi hawaruhusiwi kulinda Mgodi. Hadi leo polisi bado wapo na wameendelea kuuwa raia. Wao ndiyo wachonga *deal*, wakikosa wao wanafukuza Wananchi kwenye vifusi na hata kuwapiga risasi. Serikali pia isiruhusu Mgodi kufanya kazi wakati bado Wananchi wapo, hii siyo halali na hupelekea athari kubwa.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, Wananchi waishio Buhemba wanaishi kwa tabu sana. Wawekezaji mbalimbali wamekuwa wakija Buhemba kuchimba dhahabu tangu enzi za Ukoloni hadi enzi za MEREMETA. Wawekezaji hao wamepora mali zote pale na kuacha Wananchi bila barabara, shule, zahanati, maji na kadhalika.

La aibu kabisa, hata baada ya Waziri Mstaafu kutuma Mawaziri watatu; Mheshimiwa Wasira, Mheshimiwa Ibrahim Msabaha na Mheshimiwa Profesa Mwandyosa, kuona hali mbaya ya Butiama, Serikali imeitelekeza Buhemba. Hivi sasa *Buhemba is an environmental disaster, a national disaster*. Dhahabu yote iliyochimbwa hapa hakuna fedha zozote zilizolipwa kwa kuboresha huduma za jamii. Badala yake, majitaka yaliyokuwa yapo kwenye mashimo ya kuoshea mawe kwa kutumia *cynide* yameachwa ovyo na mvua zinaponyesha husambaza uchafu wote kwenye vyanzo vyote vya maji wanayokunywa Wakazi wa Buhemba. *Cynide* ni sumu, Serikali imewaacha Wananchi wanywe maji hayo.

Ng'ombe na mbuzi wanakufa, Wananchi wanaishi kwa hofu na Serikali imekaa kimya.

Mheshimiwa Spika, niliomba Serikali ilete *STAMICO* kurithi MEREMETA. *STAMICO* wamefika bila kuwa na mtaji wa kutosha. Wametegemea wabia wenzao ambao naambiwa wao pia hawataki kuwekeza katika uboreshaji wa mazingira. Mheshimiwa Profesa Mhongo, amesikika akiwaambia wapiga kura wangu kwamba, hatafika Buhemba kamwe. Mimi pia naambiwa sina haki ya kuzungumza humu Bungeni maana niko *conflicted*. *Conflicted* eti kwa kuwa nimekuwa nikililia Serikali ilete *STAMICO*, Chombo cha Serikali kiwasaidie Wananchi wangu wapate huduma bora Buhemba. Mimi sina biashara yoyote ninayofanya Buhemba, badala yake naombaomba marafiki na jamii watusaidie ujenzi wa huduma mbalimbali kama vile shule, zahanati, barabara, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Butiama hawaishi kama Watanzania wenzao, Wananchi hawa hawana maisha bora na hawako huru. Juzi Wizara ya Nishati na Madini imekwenda Buhemba na kutoa amri ya kuwafukuza wachimbaji wadogo wadogo, sasa kuna vurugu kubwa. Hakuna usalama tena Buhemba. Nataka kujua ni lini Mheshimiwa Waziri Mkuu au Mheshimiwa Rais ikiwezekana, watafika Buhemba na kutuliza hali tete iliyopo Buhemba?

Mheshimiwa Spika, bila kupata kauli ya Serikali kuhusu hali hii, sitaunga mkono hoja hii.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, maeneo mengi nchini yaliyopatikana na madini, badala ya kuwa na furaha imekuwa ni kilio na kusaga meno. Mfano mdogo ni katika Mkoa wa Singida, maeneo ya Mang'onyi, Sumbaru, Londoni na kadhalika; kumekuwa na kilio na kusaga meno baada ya maeneo hayo kugundulika kuwa yana dhahabu.

Kampuni ya *Shanta Mining* ilipewa uhalali wa kuchimba dhahabu baada ya wachimbaji wadogo wadogo

kufukuzwa na Wananchi wengi kunyang'anywa mashamba na makazi yao ili kupisha mwekezaji huyu. Mpaka leo kuna kilio na watu bado wanalamikia fidia zao. Nilitaka Serikali iangalie umuhimu wa kuyainua kimaisha maeneo yenye rasilimali hizi za madini kwa kuwapa vipaumbele vya huduma bora za kijamii kama shule, hospitali, barabara, maji na kadhalika ili nao wafaidike na ambavyo Mwenyezi Mungu amewajalia.

Mheshimiwa Spika, suala la wachimbaji wadogo wadogo limekuwa ni kero nchi nzima hasa kwa kutokupewa uwezo na maeneo yanayoeleweka ili nao wafaidike na mali zilizopo kwenye maeneo yao. Wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyaswa wa wawekezaji wakubwa kana kwamba wao hawana haki ya kunufaika na mali na madini yaliyopo. Serikali kama ilivyokwishaanza kuonesha nia ya kuwajali, basi Iisiachie hapa ila mkazo mkubwa uwepo kuwasaidia hawa Watanzania ambao wanatakiwa kunufaika na mali zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Singida Kaskazini (Singida), katika Kijiji cha Khanoda, lilipata bahati ya kuwekewa nguzo za umeme katika Kijiji hicho tangu mwaka 2002; lakini kwa masikitiko makubwa, mpaka sasa hakuna *transformer* iliyowekwa na mpaka ninapoandika mchango huu, nguzo mbili zimeshaanguka! Hii ni hasara kubwa sana, kwa sababu nguzo hizi ni ghali na kabla ya kuanza kufanya kazi yake, tayari zimeshaanguka. Je, Serikali itakamilisha lini kufunga *transformer* katika Kijiji hiki na kuwapelekea Wananchi hawa umeme? Suala hili ni la muda mrefu sana na limeshaongeleta sana Wizarani, naitaka Serikali inipe majibu kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali; ifike mahali sasa nchi yetu itumie vizuri rasilimali za madini, mafuta na gasi asilia katika kuwanufaisha Wananchi wa Tanzania ipasavyo. Ni aibu kwa nchi hii kuwa maskini na ombaomba kwa nchi za wenzetu ilihali tuna mali za kutosha. Lazima sasa tuepushe vita kwa kuingia mikataba isiyo na tija kwa nchi bali kwa wachache wenye roho ya ubinagsi hawatufai katika

nchi yetu ni wasaliti. Tujifunze toka Afrika Kusini, nchi ambayo inaongoza kwa kutoa dhahabu, ilipoamua kuwapa wawekezaji eneo la Egol liliokwu limesheheni dhahabu, baada ya kuchimba dhahabu hiyo wawekezaji walijenga Mji huo ambao ni wa kisasa sana na wakauita '*Egol the place of Gold*' kama kumbukumbu ya dhahabu iliyokuwepo pale.

Afrika Kusini hawakuachiwa mashimo na vifusi vyatumbi kama ilivyo Nyarugusu, bali Mji mzuri wa kupendeza. Kwa nini sisi Tanzania tusiige yale mazuri wanayofanya jirani zetu na badala yake tunauza mali zote kwa wageni bila mrejesho unaolingana? Ni wakati wa Taifa kufanya maamuzi magumu sasa na si kesho!

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ni nzuri na yenye ufanuzi. Inaonesha mipango ni mizuri, lakini utekelezaji utakwama kwa kutokuwa na fedha ya kutosha. Naomba Serikali ikubali kukusanya fedha kwenye mafuta na simu kama Bunge liliwyokwisha kuishauri.

Mheshimiwa Spika, tangu tusikie mradi wa kuzalisha umeme kwenye maporomoko ya Rusumo ni muda mrefu sana. Je, ni lini hasa utaanza? Umeme huo ungeweza kusambazwa na kuleta maendeleo katika Wilaya za Ngara na Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo au ubaba wa nguzo za umeme Mkoani Kagera (*TANESCO*). Nguzo zinazalishwa hapa hapa nchini sasa tatizo linakujaje? Naomba majibu katika haya yote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuelekeza mchango huu kwenye suala zima la Mradi wa Umeme Vijijini (*REA*). Hakika asilimia 80 ya wananchi wanaishi vijijini sehemu ambazo uzalishaji hakika ukipewa

msukumo wa nishati ya umeme utakuwa wa hali ya juu sana. Hakika wafanyabiashara wadogo kwa wakubwa wanahitaji nishati hii muhimu sana kwa ajili ya uzalishaji na uchochezi wa shuguli za maendeleo. Katika mradi huu kuna vijiji ambavyo vimewekwa kwenye mradi huu Jimboni Biharamulo Magharibi ambavyo ni Kabindi, Runazi, Rwagati, Katohoka, Nyamahanga, Ntungamo, Kibale, Nyambale, Lusahunga, Nyakahura na Nyakanazi, lakini pamoja na maeneo hayo kuainishwa bado yapo maeneo mengi ambayo mradi huu wa *REA* unapaswa kuharakishwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna Kata ya Nyabusoz pale kuna *Centre* kubwa ya Isambara, Nyabusoz yenye, Nyabusoz sekondari, Mwanga zahanati, Kabangani, Kata ya Nemba hususan Nemba sekondari, Nemba *centre*, Kisenga, Kazilambwa, Kata ya Nyantakala; Nyantakala *centre*, Iyengamulito, Nyantekara sekondari, Mgera, Mtunduni mpaka Nyakanazi, hakika maeneo haya yote niliyoyataja yana makundi mengi ya vijana wanawake na makundi mbalimbali ya jamii ambayo kweli kama yangeta umeme huu wa *REA* hakika tungepunguza umaskini ambao unazidi kukithiri katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la wananchi kuomba kuunganishiwa umeme, lakini mamlaka zinazohusika kuwanyima wananchi fursa hiyo. Hakika kuna maeneo ambayo kuna nguzo zinazipita na wananchi wana ushuhudia umeme kwenye waya ukipita na wao wakibaki gizani. Hakika hii si sahihi hata kidogo, *TANESCO* kupuuza nguvu za wananchi. Pale wanapopeleka maombi wanaambiwa wapeleke mihtasari kitu ambacho tayari wamekwishafanya, lakini hakika hata wakipewa bado hakuna utekelezaji. Naomba mamlaka zinazohusika zifikirie wananchi hawa kilio chao.

Mheshimiwa Spika, niombe suala hili la umeme lifanyiwe kazi haraka sana ili kuweza kuchochaea maendeleo ya wananchi na hakika umeme ndio nguzo ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote

zilizoainishwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo hakika imeainisha mianya yote ya ubadhirifu baina ya mikataba mibovu. Upotoshwaji na uporwaji wa madini yetu katika migodi yetu. Hakika maendeleo hayana itikadi, hayana chama na wala hayawezi kuwa ya mtu mmoja mmoja tu, bali yanategemea nguvu ya pamoja. Ni imani yangu kama wote tutasimamia nguvu ya pamoja tutafanikisha adhma hii ya kupata kile tunachokihitaji kutokana na rasilimali tulizonazo. Zawadi ya Watanzania wote toka kwa Mwenyezi Mungu.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu na viongozi wa Taasisi chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kusimamia dira ya *TANESCO* ili ifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara na *TANESCO* waweke dhamira ya kweli kuondolea Taifa mzigo wa ghamama za kampuni za umeme na dharura *IPTL AGGREKO* na *Symbion*. Jitihada zilizofanyika kuwezesha *Aggreko* kupunguza ghamama za *Capacity charge* kwa asilimia 34% ni mfano mzuri.

Mheshimiwa Spika, tatu, napongeza jitihada za kuungeza uzalishaji kwa miradi mipya ya Mwanza *mw* 60; Kinyerezi (1+2) *mw* 390; Somanga fungu *mw* 320; Mchuchuma *mw* 660; Makaa ya mawe Ngaka *mw* 400; makaa ya mawe Kiwira *mw* 20; Murongo na Kikagati *mw* sita; Mtwara – *Symbion mw* 400; jumla *mw* 2,386.

Mheshimiwa Spika, ni vema mradi wa Mtwara *Symbion* 400 *mw* ukapewa kipaumbele na kuwatambulisha hivyo wananchi wa Mtwara ikiwepo ziada ya miradi ya *REA*, huko Masasi, Nanyumbu, Newala na Tandahimba na pia miradi chini ya Mfuko wa Umeme Vijijini (*REA*).

Mheshimiwa Spika, maombi niliyopitisha *REA*,

nimeomba na narudia kuomba umeme kwa vijiji vinne vifuatavyo:-

(a) Kiwanda; hapa kipo Chuo cha Maendeleo ya Ufundı, Zahanati na Nyumba za Walimu na Daktari na mabweni ya wanafunzi.

(b) Tongwe; ili kufikisha umeme Kiwanda, umeme upo sasa Kijiji cha Bombani; hivyo ukitoka Bombani lazima upite Tongwe ili kufika Kiwanda.

(c) Tingeni; hapa upo uchaguzi wa Diwani, baada ya aliyekuwepo kufariki. *TANESCO* Muheza walishapima na kufanya makadirio ila hawajathibitisha kuingizwa katika mpango wa 2013/2014. Umeme kwenda Tingeni unaweza kutoka Muheza Mjini, Kata ya Kwamkabara au kutoka Kerenge, Kijiji ambacho kipo ndani ya Kata hiyo ya Tingeni.

(d) Kwakifua; hapa ni Makao Makuu ya Kata ya Kwakifua na ipo zahanati na nyumba za Walimu shule ya msingi Kwakifua.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Wizara ya Nishati na Madini, Bungeni 2012/2013, mara kwa mara imetolewa kauli kwamba, pale waya za umeme zikipita juu ya eneo la kijiji kuelekea kijiji cha mbele ya kijiji au kitongoji hicho umeme utashushwa ili kijiji hicho kipate umeme. Kwa maeleo hayo, naomba muiagize *TANESCO* Muheza kuteremsha umeme kwenye kijiji na kitongoji cha Mabungu.

Mheshimiwa Spika, nguzo na waya za umeme zimepita hapa Mabungu, sasa miaka 18 imepita wakati umeme ukipelekwa katika Kijiji cha Misozwe. Nilisaidia *TANESCO* miaka hiyo 18 iliyopita kuwezesha umeme kufika Misozwe bila gharama yoyote ya fidia na wananchi walishiriki kusaidia kazi ya kuchimba mashimo kwa ajili ya nguzo za umeme, pamoja na jitihada hizo kwa miaka 18 *TANESCO* haikuwezesha kusogeza umeme hata kwa kitongoji kimoja cha ziada! Hata nilipoomba umeme usogezwe kwa nguzo

nne tu kuingizwa katika nyumba ya Mapadre ndani ya Kijiji cha Kwemingoji ambapo ndio ulipoishia umeme wa Misozwe, nimetakiwa kulipia gharama zote kuwezesha umeme kufikishwa hapo! Nashukuru leo kwa mpango wa REA vijiji ndani ya Kijiji cha Misozwe vimekubaliwa katika orodha iliyopo na kuondoa kero hiyo ya miaka mingi (Vijiji vya Matogoro, Amtakae na Soweto) ila kimebaki Kijiji kimoja cha Kisinga”

Mheshimiwa Spika, mwisho, natoa ushauri wa ziada ufuatao; mchango katika Mfuko wa Umeme Vijiji ni uongezwe na kuongeza usimamiaji wa matumizi ya fedha hizo na kuhakikisha makusanyo yanasmamiwa vizuri na kuingizwa katika mfuko kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, *REA (Rural Energy Authority)*, chombo hiki ni mamlaka ya umeme vijiji ni hivyo sio busara kuendelea kuwa kitengo ndani ya TANESCO. *REA* iwe chombo huru na kiutawala katika kujidesha, hii itasaidia kuwa na chombo cha pili muhimu katika usambazaji wa umeme vijiji ni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, nimechangia kwa kusema, lakini hili sikulifikia kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kuitia Wizara kwamba, kwa kuwa Watanzania wanaonekana wamekata tamaa na manufaa yatokanayo na rasilimali zao. Hivyo basi, Wizara ije na sera itakayowapa matumaini Watanzania wote popote walipo.

Mheshimiwa Spika, mambo matatu sera ioneshe sera igawe pato lote litokanalo na madini kwa ujumla kama ifuatavyo:

(a) Sehemu moja iwe inakwenda kulipa madeni ili kuliondolea Taifa na vizazi vijavyo mzigo wa madeni;

(b) Sehemu nyingine ioneshwe kwamba, inakwenda kujenga miundombinu ya barabara, maji, reli, shule, zahanati na kadhalika; na

(c) Sehemu nyingine hii igawanywe kwa Watanzania wote kuanzia aliyezaliwa leo hadi yule wa miaka 100.

Mheshimiwa Spika, huo ndio ushauri wangu kwa Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi yao ambayo kweli ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe machache kama taarifa na maombi kwa Serikali kuhusiana na hali ilivyo na inavyoendelea Mtwara. Taarifa za uhakika ninazopata ni kwamba, wananchi madai yao ni kwamba, wanataka viwanda vijengwe kwanza ili wawe na imani ya kweli, ndipo yale ya kupeleka Kinyerezi yafanyike. Hofu yao ni pale wanapoona unaharakishwa utaratibu wa kusafirisha kabla ya kiwanda, isije ikawa ya Songsongo.

Mheshimiwa Spika, amini usiamini fujo kubwa zinafanywa na Polisi, hawa Polisi imezoleka mahali pengi penye matatizo, wao huwachokoza wananchi ili wafanye fujo ili wao wafaidike. Huwa wanavunja maduka na kubeba mali, juzi Polisi walishukiwa na askari wakiwa na majokovu (frijji) nne, walinyang'anywa na kupeleka kwenye Kambi ya Jeshi. Pamoja na hayo wao huwa wanavunja nyumba na kuwakamata watu usiku na kuwapiga wanawake. Mabwana kupelekwa kituoni wakiona kitu kizuri mle ndani wao wanachukua.

Mheshimiwa Spika, watu waliovunjiwa nyumba zao, vibanda vyta biashara hivi sasa wanahangaika na watoto

kwa kukosa chakula na kadhalika. Ileleweke wananchi, wao ndio wadai wasingeweza kujuumiza wenyewe (kujivunjia majumba).

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, Serikali isilalie upande mmoja wa kuwa waletao fujo ni Wapinzani, wale wote kule sio Wapinzani, CCM wapo na ndio wengi. Hao Wapinzani wana nguvu gani ya kuweza kuwashawishi vigogo au makada wa CCM wakakubali kurubuniwa? Tafadhali sana wapiganapo ndovu ziumiazo ni nyasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mzazi anapomwona mtoto analia, humhoji analilia nini. Ikibidi kumpatia kama kipo na kama hakipo humtuliza kwa lugha nzuri ili anyamaze na sio kushika bakora na kumchapa, matokeo yake kitakachotokea pale kinaweza kikawa kibaya. Kumbuka *lahaula haitangulii*. Serikali illiangalile hill kwa mapana hasara zinazopatikana ni kazi ya Serikali kugharamia matengenezo. Vile vile nchi inapoteza sifa yake ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, hali iliyopo hadi hivi usiku nilikuwa naongea na mwanangu wakati na majira ya saa tatu, niliisikia milio miwili ya mabomu. Asubhi hii nikaambiya liliisikika la tatu. Ikumbukwe kwamba ushauri mwengine unaotolewa na baadhi ya viongozi kwa Serikali unachochea mambo kuzidi kuwa mabaya. Hivyo, naiomba Serikali ikae chini na kutafakari kwa kina ili amani ipatikane.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa machache juu ya suala la umeme vijiji. Shule nyingi za sekondari za Kata zipo vijiji ambako hakuna umeme, humo mashulenii mna mahitaji makubwa hasa kwa somo la sayansi. Somo hili linatakiwa vitendo hasa kwenye somo la kemia karibu shule nyingi wanafunzi hawapati na matokeo yake wanafeli mtihani. Hivyo, Serikali ione umuhimu wa kupeleka umeme ili kuwasaidia wanafunzi kupata somo hilo la sayansi.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vile ambavyo hakuna umeme, kuna vituo vyta afya na zahanati pia. Pamoja na

sehemu zingine kuweka *generator* kunakuwa na ukosefu wa mafuta na shughuli zingine za uendeshaji wa kazi kukwama. Vile vile pale palipopelekwa *solar* kama mvua zinanyesha mfululizo na kupelekeea ukosekanaji wa mwanga wa jua nako huleta matatizo pia. Hivyo umuhimu wa umeme ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, umeme ni kila kitu, shughuli nyingi za uzalishaji wa uchumi zikikosa umeme hakuna maendeleo. Hivyo, naiomba Serikali izingatie sana juu ya upatikanaji wa umeme, sio mijini tu bali na vijijini. Maana katika kufanya hivyo kutasaidia utunzaji wa mazingira pia kukatwa miti hovyo kwa ajili ya mkaa kutakoma au kutapungua.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (*Subhanah Wataala*) kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kila alichokiumbwaa Mwenyezi Mungu (*Subhanah Wataala*) katika ulimwengu huu ni kwa madhumuni ya kumnufaisha mwanadamu. Kila alichopewa mwanadamu kama afya, elimu umasikini au utajiri ni mtihani kwake. Ni wajibu wa mwanadamu huyo kutumia akili yake, elimu yake, busara yake na hata ushauri ili aitumie vizuri neema aliyopewa. Nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi na zenyet thamani sana, hivyo basi ni wajibu wa Serikali kuzisimamia vizuri rasilimali hizi ili zilete neema kwa nchi yetu na isiwe kinyume chake! Naiomba Serikali iendane na ushauri ili dhahabu, almasi na hata gesi zinufaishe nchi kama dhahabu iliyonufaisha Afrika ya Kusini hadi Mji wa Egoli ukaitwa *the place of gold* kama Oman iliyonufaika na mafuta, Abudhabi na nchi nyingi za *Middle East!*

Mheshimiwa Spika, naiomba na kuisihi Serikali yetu iwe wazi katika mikataba ya Madini na *Gas* ili kuondoa fitina na wasiwasi uliotanda katika nchi. Nguvu sio suluhisho la matatizo la kuendeleza rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, tusipoziba ufa sasa tutashindwa kujenga ukuta baadaye wakati ni huu! Ni bora lawama kuliko fedheha. Tukiogopa kulaumiwa hivi sasa kwa kurekebisha mikataba na Sera ya Gesi na madini tutapata fedheha baadaye ya kuendelea kuwa maskini bila msaidizi. Wanaochota rasilimali zetu sasa watakuwa wa mwanzo kutucheka na kutukejeli kuwa ni wapumbavu.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana inawezekana, timiza wajibu wako, Mungu ibariki Tanzania na mali zake.

MHE. MOZA ABEDI SAIDY: Mheshimiwa Spika, niungane na watanzania wenzangu kuwapa pole wale wote waliopoteza ndugu na jamaa zao waliopoteza maisha kwenye migodi na hasa huko Mererani, Arusha.

Mheshimiwa Spika, napinga kauli ya kubezana ndani ya Bunge hili kwani kila mtu anayo fursa ya kuongea na kutoa mawazo yake na mchango wake na ukathaminiwa kama mchango kwa Serikali au kuishauri na hata kuikosoa Serikali hasa upande wetu Wapinzani imekuwa kila kitu kwetu hakifai, inavyoonekana kwa wenzetu wa utawala, jambo ambalo linaleta mtafaruku kila mara hapa Bungeni. Naomba mambo haya si mazuri, Serikali ikubali kukosolewa na ikubali kupokea mawazo ya upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, nianze na mchango wangu wa madini; madini ni uchumi, madini ni utamaduni wa rasilimali, lakini madini hayalimwi useme yataota tena kama mimea, ukiyachimba na kuyatoa hayarudi tena. Sekta hii ni mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika sekta hii ya madini imepoteza ndugu zetu kwa kufia kwenye machimbo bila kuwepo uangalizi wa uchimbaji hasa wachimbaji wadogo wadogo hata wengine kukosa kifuta machozi wanapopata madhara. Swali Mheshimiwa Waziri naomba kwenye majumuisho yake aeleezeo nini hatima ya vijana wetu wanaojajiri kwenye migodi pindi wamalizapo kuchimba au kuachishwa na hata kufa, Serikali inawasimamiae?

Mheshimiwa Spika, madini yapo sehemu kubwa ya Tanzania, Serikali mbona inaachia uchumi huu unatoweke bila vipaumbele vinavyosemekana, maeneo husika havikamilishwi kama makubaliano yalivyo? Nini tatizo la wawekezaji hao je, ni elimu gani itolewayo na Serikali hasa kwa wale wanaovumbua madini hayo wananaufakaje? Kwani tunaona matatizo yapo kwa waendesa migodi hiyo kutokuwathamini Watanzania wanaowaajiri, naishauri Serikali ipitie mikataba upya na iangalie mikataba ya waajiriwa kwenye migodi iko sahihi?

Mheshimiwa Spika, nimalizie, sekta hii bado hajakaa vizuri, kwa kiasi kidogo ifanye marekebisho ili uchumi wetu huu usiwe mateso kwa Watanzania na wafukie yale mashimo kama kuna makubaliano haya na udongo usitoke kwenda kwingine kokote na wananchi wapewe fursa ya kutafuta riziki ndogo ndogo pemberi mwa migodi ili waweze kujikimu kimaisha kwani ndiyo rasilimali zao, wasinyanyasike hasa huko Geita na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara hii ni ndogo haikidhi mahitaji na Maafisa Madini wa Kanda na wasiwe na upendeleo na watekeleze kazi zao ipasavyo. Hivyo, sitolunga mkono hoja hii kwani ina upungufu mwingi ikiwepo na bajeti yenywewe.

Mheshimiwa Spika, nichangie tena Wizara ya *TANESCO* Wizara hii imepata bajeti ya kutosha, lakini bado ina mapato mengi, mengine ni kuwakandamiza wananchi hasa kwenye nguzo limbikizo lisilojulikana makosa ya ongezeko la bilioni na kutoainisha mteja kwa makundi na kuwatoza bili kubwa kuliko matumizi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepanga makundi ya matumizi kwa makundi mbalimbali ikiwemo kundi la matumizi madogo ya nyumbani wastani wa *kw/hr⁵⁰*, angalia matumizi haya yamepewa ruzuku na shirika. Sasa mteja atajuaje hiki ni kiwango chake halali, mbona hailingani na tozo yake nini tatizo? Pia shirika wakati linafunga umeme kwa mteja huwa hawaambii au hayo huja tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ana uhakika na meneja wa Shirika kasomea utawala au ni injinia katika sehemu zake zote za mashirika yaliyopo, naomba ufuatilie hilo ili kuepuka malimbikizo na kulipiza wananchi bili kubwa, kuliko hitaji na kuwaambia walipe tu watakuja fidiwa au *Computer* ndiyo imesema hivyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na rasilimali za asili zilizokuwepo nchini ambazo ni vyanzo vyatya asili vyatya nishati vikiwemo gasi maji ya mito na kadhalika mtumiaji wa umeme wa Tanzania analipa bili kubwa.

Mheshimiwa Spika, bei kubwa ya umeme; huduma hii pamoja na bei zake zinadumaza ukuaji wa uchumi wa Tanzania, naiomba Serikali itoe agizo kwa *TANESCO* iweze kurekebisha bili za umeme kufuatana na makundi, naweka mfano huo.

Mheshimiwa Spika, *DI* watumiaji wadogo kiwango cha 0 - 50 ni ndogo angalau watoke mpaka *unit* 0 - 100, wanafunzi wanashindwa kujisomea wakati wa usiku.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya *power fact* ambapo mtumiaji analipa mara mbili ya gharama hasa kwa wachomeleaji wa pembejeo za kilimo, moja eneo la mrijo chini ya Wilaya ya Chemba sasa *EWURA* ipitie bei hizo na kurekebisha umeme kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo kuna nguzo na transfoma, lakini hakuna umeme katika Kata ya Dalai, Serikali inasemaje kuwapa umeme wananchi hao na mnara huo wa simu upo pale Pilui? Ina maana minara miwili yote ipo hapo Pilui mafuta ya taa hayapatikani na yana gharama kubwa sana.

MHE. DUSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono bajeti ya Wizara hii, nikitambua kuwa umeme ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono bajeti

ya Nishati na Madini ni ukweli usiopingika kuwa fedha tulizotenga hazitatuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea hususan katika kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa suala la umeme vijijini limekuwa likipata fursa ya kuzungumziwa sana, lakini kwa bahati mbaya sana uungwaji mkono huu umekosa vitendo thabiti. Hali hii inaweza kuthibitishwa na upuuziaji au kutokutekelezwa kwa uamuzi wa Bunge wa kupeleka *REA* fedha za tozo la mafuta ya taa, ili fedha hizo ziweze kutumika kupeleka umeme vijijini. Hali hii ni sawa na kosa tulilofanya katika miaka ya 1970 tulipositisha uanzishwaji wa *Tanzania rural electrification company (TARECO)*. Uamuzi ule ulidumaza kasi yetu ya kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijijini wanasubiri huduma ya umeme kutokana na ukweli kuwa, tumewaahidi kwa muda mrefu. Mafanikio tuliyoyapata katika ujenzi wa zahanati na shule katika Vijiji na Kata lazima yaende sambamba na upatikanaji wa huduma ya umeme. Wananchi wa Mkinga katika Vijiji vya Daluni, Gombero, Vuga, Mapatano, Bwiti, Manga, Bosha, Mhimbiro na Mwakijembe, wamesubiri kwa muda mrefu sana kwa bahati mbaya licha ya ahadi za mara kwa mara kwa mwaka huu vijiji vitatu tu ndio vimejitokeza kwenye orodha tofauti na miaka iliyopita, wananchi hawatatuelewa katika hili.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mikataba inayosainiwa hapa nchini kuna *component* ya mafunzo kwa Watanzania. Mchango huo ni katika dola laki moja mpaka dola laki mbili. Je, ni Watanzania wangapi wamekwishapata fursa hizo za mafunzo na ni wa kada zipi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo kwa niaba ya wana Katavi, napenda kuiomba Serikali iwapatie wananchi na wachimbaji wadogo wadogo maeneo waliyoomba na si kuwapa maeneo mapya ambayo

hawayafahamu, kwa mfano, wana Mpanda wameomba maeneo haya yafuatayo:-

- (i) Ibindi.
- (ii) Kampuni.
- (iii) Kakese.
- (iv) Kasinde.
- (v) Singililwa.

Mheshimiwa Spika, pia maeneo ambayo kampuni ya *GBA* ya Kirusi ina maeneo ambayo haiyafanyii kazi. Hivyo basi, maeneo hayo ni vema wakapewa wananchi ama wachimbaji wadogo wadogo wa Mpanda wa maeneo yaliyopo pembezoni ya kampuni hiyo ya *GBA*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. DALALY PETER KAFUMU: Mheshimiwa Spika, wakati nachangia kwa maneno niliipongeza sana Wizara katika kutekeleza mabadiliko ya sera za uchumi zinazohamasisha na kukuza uwekezaji nchini. Zilizoanzishwa miaka ya 1990, sera hizi zililenga kuzifanya Sekta za Nishati na Madini kuwa mhimili mkubwa na injini ya uchumi wa nchi. Nilisema lazima tuhakikishe sekta hizi zinafungamanishwa na sekta nyingine za uchumi ili kuwafanya wananchi wengi washiriki katika uwekezaji huu na kupata manufaa zaidi kulingana na Sera ya Nishati ya mwaka 2003 na Sera ya Madini ya mwaka 2009, sasa naomba kuchangia kwa maandishi kutoa ushauri kadhaa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nishati; wananchi wa Vijiji vya Kata za Mbutu, Mwamashimba na Igunga waliopitiwa na laini ya umeme wa gridi inayotoka Singida hadi Shinyanga walipewa fidia hivi karibuni. Fedha zilipelekwa na wananchi wakalipwa fedha taslimu. Kuna malalamiko mengi kuwa baadhi ya wananchi walilipwa fidia kwa kupunjwa, wengine walilipwa zaidi na wengine hawakulipwa kabisa. Suala hili nimelishughulikia kwa kushirikiana na *DC* na kulifikisha *TANESCO*, nao wakaahidi kulishughulikia. Namwombwa Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo stahiki kwa uongozi wa

TANESCO ili malipo haya yapitiwe upya na malipo kufanyika kadri ya haki ya kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kuleta miradi ya umeme vijiji ambapo Vijiji nya Kata za Itunduru, Igurubi, Itumba na Mbutu zitapatiwa umeme kutoka kwenye Mfuko wa REA naiomba Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi hii ili wananchi wa maeneo haya watambue kwamba, Serikali yao ya CCM inawajali.

Mheshimiwa Spika, madini; katika usimamizi wa sekta ya madini jambo kubwa ni kuhakikisha uwekezaji wa ndani na nje unasaidiwa kukua na kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wa Tanzania. Katika kufanya hivyo, kumekuwepo mchanganyiko na mwingiliano wa majukumu ya taasisi na idara za Serikali, jambo ambalo limeanza kuidumaza Sekta ya Madini. Mwingiliano huu umewasumbua sana wawekezaji, lakini pia umeifanya Serikali itumie fedha nyingi sana kufanya jambo lile lile.

Mheshimiwa Spika, msimamizi Mkuu wa sekta ya madini ni Kamishina wa Madini kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na kanuni zake akisaidiwa na makamishina wa Madini Wasaidizi wa Kanda nane nchini; Mkaguzi Mkuu wa migodi na Makamishina wa Madini Wasaidizi watano waliopo Makao Makuu ya Wizara wanaoshughulikia Ukaguzi wa Migodi; matumizi ya Baruti; uchumi na biashara; uongezaji thamani ya madini utoaji wa leseni na usimamizi wa uchimbaji mdogo. Lakini ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonekana dhahiri kuwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini. *Tanzania Mineral Audit Agency (TMAA)* imechukua kazi na mamlaka ya Kamishna wa madini. Baadhi ya mifano ya mwingiliano huo inaelezwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kazi ya kukusanya maduhuli kutoka kwenye madini yote yakiwemo madini ya ujenzi ni ya Kamishna wa Madini kwa kutumia ofisi za Makamishna Wasaidizi wa Kanda na Maafisa Wakazi waliopo mikoani katika Kanda nane za utawala wa Wizara. Lakini

ukiangalia ukurasa wa 69 wa hotuba, kifungu cha 131 inaonekana wazi kuwa *TMAA* imechukua kazi ya ukusanyaji wa maduhuli kinyume cha sheria. Maafisa Madini wanaopaswa kufanya kazi hii kwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 wanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tena ukurasa wa 70, kifungu cha 133, *TMAA* sasa imeweka madawati ya kukagua usafirishaji wa madini kwenda nje, kazi ambayo kwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, inapaswa kufanya na Kamishna Msaidizi wa Uchumi na Biashara ya Madini. Pamoja na Ofisi za Makamishna wa Madini Wasaidizi waliopo karibu na maeneo ya mipakani na Viwanja vya Ndege vya Kimataifa. Hivi kumetokea nini kiasi kwamba, Wakala ulioundwa kwa nia njema ya kushughulikia ukaguzi wa migodi kwa ajili ya udhibiti yaani *auditing*. Sasa Wakala unafanya kazi za usimamizi yaani *Inspection* kwa ajili ya utunzaji wa mazingira. Ukusanyaji wa maduhuli na biashara ya madini. Hii siyo sawa ni *ku-duplicate* shughuli za Serikali na kuzifanya kuwa na gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 71, kifungu 134 kinaonesha dhahiri kuwa *TMAA* inafanya kazi ambazo zingeweza kufanya na *NEMC* wakisaidiwa na Kitengo cha Mazingira cha Wizara ya Nishati na Madini na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Migodi kwa ufanisi. Kulingana na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, pia ukiangalia maelezo ya ukurasa wa 68 hadi 69, vifungu namba 129 na 130 vinaonesha kana kwamba mafanikio ya ulipaji wa kodi ya mapato (*corporate tax*) yanatokana na tathmini ya kodi kwenye migodi yametokana na kazi ya *TMAA* pekee. Lakini kwa uhalisia wa jambo hili *TRA* inao mchango mkubwa zaidi na ni kazi ya *TRA* kwa sheria ya *TRA* kufanya kazi za ukaguzi wa uwekezaji kwa lengo la kutathimini kodi. Hapa tena *TMAA* inafanya kazi ya taasisi nytingine kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, ukiongea na wawekezaji na

wadau wa sekta ya madini wanalamika sana kuwa ukaguzi wa jambo lile lile unaofanywa kwenye migodi na taasisi zaidi ya moja linawapotezea muda, ni gharama kubwa sana kwao. Kiashiria hiki siyo kizuri kwa mustakabali wa kuinua uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote, nimesoma pia mapendekezo ya Kamati ya Nishati na Madini inayopendekeza *TMAA* iwe Mamlaka, inaonekana Kamati haijaelimishwa vema juu ya kazi na majukumu ya *TMAA*.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kuwepo kwa Mamlaka ya Madini na pia Idara ya Madini, itakuwa ni kutengeneza Taasisi mbili zenye kazi sawa. Taifa changa linalotaabika kujaribu kujenga uchumi wake halipaswi kutumia rasilimali nyingi kiasi hicho kufanya kazi zinazofanana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Kamati ya Bomani ilipendekeza kuwa Idara ya Madini ibadilishwe na kuwa mamlaka ili kuipa nguvu ya kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Idara hiyo yenye mamlaka na madaraka ya kisheria kusimamia Sekta ya Madini iwe na uwezo wa kitaasisi, kirasilimali watu na fedha na kiteknolojia kama ambavyo nchi ya Ghana ilivyobadili Idara ya Madini kuwa Mamlaka huru iitwayo *Mineral Commision of Ghana*.

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati inatekeleza baadhi ya mapendekezo ya Kamati ya Bomani ilisema uundwaji wa mamlaka usubiri wakati muafaka. Kwa nini sasa tunazungumzia *TMAA* badala ya Idara ya Madini?

Mheshimiwa Spika, nchi zingine kama Australia, Afrika Kusini, Canada, Botswana na nyingine nyingi zimeimarisha Idara za Madini zinazofanya kazi za ukaguzi na usimamizi wa migodi kwa ufanisi mkubwa. Marekani inayo idara inayojitegemea inayoitwa *Mineral Bureau*. Idara hizi na taasisi katika nchi hizi hufanya kazi zote za usimamizi wa Sekta ya Madini, lakini shughuli za ukaguzi wa uwekezaji (shughuli ambazo zilitengwa zifanywe na *TMAA* hapa kwetu, hufanywa na mamlaka za mapato za nchi hizo. Nchi hizo

zimeimarisha Mamlaka za Mapato kuweza kukagua na kusimamia masuala ya uwekezaji katika sekta ya madini ili kodi stahiki ziliipwe.

Mheshimiwa Spika, tuliunda *TMAA* kufanya kazi za ukaguzi wa madini (*Auditing*) kazi ambazo hazitoshelezi kulingana na ukubwa wa taasisi tuliyounda matokeo yake *TMAA* ikaanza kujichukulia kazi za taasisi zingine. Viongozi wa Wizara wamefunikwa na kukosa kujua ukweli na hivyo kuamini kuwa *TMAA* ni taasisi yenye faida kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wangu wa kuwa Msimamizi wa Sekta ya Madini kwa miaka sita suala hili linaidumaza sekta ya madini na pengine laweza kuiua kabisa, na hasa pale ambapo *TMAA* inajionesha kama kwamba, imegundua wizi mkubwa katika migodi na kutangaza kwa umma hali inayoweza kuondosha wawekezaji wengi sana nchini. Serikali inao wajibu wa kushughulikia ukiukwaji wa sheria kwa hekima. Badala ya kutangaza uovu huo kwa umma.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la kuundwa kwa *TMAA* linatokana na baadhi ya viongozi wa Serikali hususani Wizara ya fedha na Benki kuu wakati huo katika miaka ya 2003 waliunda kampuni binafsi iitwayo *Alex Stewart Assayers Government Business Corporation (ASAGBC)* ili kufanya kazi ya kukagua uwekezaji na uzalishaji wa migodi. Kampuni hiyo ilifanya kazi hadi mwaka 2007 ambapo wananchi walilalamika kuwa kampuni hiyo ilikuwa inaiibia Serikali kwa kufanya kazi ya ukaguzi kwa bajeti kubwa (takriban shilingi bilioni 13 kwa mwaka) inayokaribia bajeti ya *TMAA* ya karibia shilingi bilioni 10.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Kamishna wa Madini nilimshauri Waziri wa Nishati na Madini wakati ule kuwa kampuni hiyo iondolewe na uwezo na utaalam ilioujenga uwekwe chini ya Idara ya Madini kwa muda ili Serikali itafakari namna bora ya kukagua uwekezaji katika sekta ya madini kwa kujifunza kutoptana na uzoefu wa nchi zingine. Kitengo cha *Gold Audit Program (GAP)* kikaundwa chini ya Idara ya

Madini. Kitengo hiki kilipata fedha nyingi kuendeleza ukaguzi huo ilipofika wakati wa kutafakari hatima yake baadhi ya viongozi wa Wizara bila kuzingatia maslahi mapana ya Taifa waliendesha mchakato wa haraka sana kuunda *TMAA*, mchakato uliharakishwa kiasi kwamba, kazi za *TMAA* zikaorodheshwa nyingi zikiwa ni zile zile za *TRA*, *NEMC* na Idara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, maoni ya *TRA*, *NEMC* na Idara ya Madini yalikuwa ni kwamba, kutakuwa na mwingiliano wa majukumu, hayakuzingatiwa na Serikali ikaaminishwa kuwa hili ni jambo zuri sana. Nilishauri tufanye mchakato wenye tija kwa kuwasiliana na wadau muhimu wa Sekta za Nishati na Madini na wataalam wa kodi na *financial* na *environmental auditing* kutoka *TRA* na *Controller and Auditor General (CAG)* na Baraza la Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira (*NEMC*.) ushauri huo haukukuballika na matokeo yake mwaka 2009 *TMAA* ilianzishwa.

Mheshimiwa Spika, wengi pia walishauri *GAP* iwe sehemu inayojitegemea chini ya *TRA* ili kufanya kazi za *auditing* kwa ajili ya kuhakikisha Makampuni ya Madini na Mafuta hayakwepi kodi. Wengine walipendekeza *GAP* iwe sehemu chini ya *CAG* ili kufanya *auditing* kwa ajili kuhakikisha mapato yatokanayo na kodi yanapatikana ipasavyo. Ushauri huu haukuzingatiwa na *TMAA* ikaundwa tena kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TMAA* iliundwa kufanya kazi za ukaguzi unaofanana na ule wa *TRA*, *CAG* na *NEMC* na kwa kuwa kazi hizo hazikuweza kutosheleza au *ku-justify* uwepo wake harakati za kujitanua na kuchukua kazi za Idara ya Madini zilianza na sasa kazi nyingi za Wizara ya Nishati na Madini zinazohusu sekta ya madini zinaonekana kufanywa na *TMAA* bila kuzingatia Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kabisa kuona kuwa suala la *TMAA* limeonekana kuwa na mafanikio sana na kuisahau kabisa Idara ya Madini. Nimeshuhudia *TMAA* ikifadhili shughuli za Idara ya Madini kwa vile idara hiyo

haipewi fedha za kutosha kulingana na wingi wa rasilimali watu. Miundombinu na shughuli zake. Kwa mfano, kwenye bajeti ya 2013/2014, ofisi zote za Kanda nane zenye ofisi 22 mikoani na watumishi zaidi ya 260 zimepewa shilingi milioni 10.25 na *TMAA* inapewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 9.5 zisizolingana na uwingi wa watumishi wake wasiozidi 30 na miundombinu yake, hivi kuna taabu gani kuzitengea fedha za kutosha Ofisi za Kanda za Madini chini ya Kamishna wa Madini zikafanya kazi zote hizi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu nikiwa Kamishna wa Madini haukizingatiwa, mwaka jana pia nikiwa Mbunge nilandika suala hili mara kadhaa, lakini hakuna aliyeonekana kulitilia maanani. Nimeamua kuandika haya tena kwa kirefu kuishauri Wizara ifanye mapitio mapya ya majukumu ya *TMAA* na umuhimu wake kwa kushauriana na wadau wa Sekta ya Madini ili kuhakikisha kuwa ujuzi ullojengwa na *TMAA* unawekwa mahali muafaka ili kazi za *TMAA* zilete thamani yake ya kifedha, *value for money*.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe nafasi ya kujadiliana na wadau juu ya mwingiliano huu ili kuondoa matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa kuwa na Taasisi nyingi zinazofanya shughuli ile ile. Wadau wa sekta ya madini ni pamoja na mamlaka za Serikali za *TRA*, *CAG* na *NEMC* wakihuishwa wawekezaji chini ya *Tanzania Chamber of Minerals and Energy (TCME)*, ni jambo jema pia kuiwezesha Idara ya Madini yenye Ofisi nchini kote kuweza kufanya kazi zake kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 badala ya *TMAA*.

Mheshimiwa Spika, kuiacha hali hii ya sasa ya mwingiliano mkubwa wa majukumu ambayo siasa inaonekana kutawala kutaendelea kudumaza sekta ya madini. Naishauri Wizara ilishughulikie suala hili kwa umuhimu wake ili kukuza uwekezaji mkubwa kwenye Sekta ya Madini nchini. Kama ushauri huu bado utaangukia kwenye masikio ziwi, natarajia kuleta Muswada binafsi Bungeni ili suala hili lieleweke kwa Wabunge wote na Serikali ishauriwe ipasavyo kwa manufaa ya nchi na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na ngumu wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika masuala yote ya utafutaji, uchimbaji wa madini hapa nchini naiomba Serikali iwe makini katika mikataba inayoingia na Makampuni mbalimbali. Siku zote jitahidini kuiweka Tanzania mbele katika mikataba hiyo. Aidha, wachimbaji wadogo wawezeshwe na wapewe kila aina ya msaada.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya gesi, naiomba Serikali ili kuondoa hofu ambayo inawaingia wananchi sehemu mbalimbali hapa nchini mikataba iwekwe wazi, manufaa yatakayopatikana yaelezwe kwa uwazi, mapato ya nchi yetu yatokanayo na gesi yawekwe wazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kusambanza umeme kwa wananchi vijiji (REA) iwezeshwe, ikiwezekana wananchi wote wanaotumia simu za mikononi wawe wanachangia asilimia fulani kutoka kwenye matumizi ya simu zao za mkononi.

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na mimi kuwa mionganini mwa wachangiaji katika Hotuba ya bajeti hii muhimu ya Wizara ya Nishati na ya Madini na moja kwa moja naanza kuzungumzia sula la gesi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mwenyezi Mungu katujaalia neema hii muhimu, ni vizuri tukajenga mshikamano na kuepuka chuki na fitina ambazo zimeanza kijitokeza katika nchi yetu. Hivyo, ni wajibu wa Serikali kuwapatia elimu ya kutosha wananchi ambao wamezungukwa na rasilimali hizi.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu kutolewa na

kufahamishwa wanachi kwamba rasilimali za Tanzania ni kwa ajili ya Tanzania na hajatokea duniani kote kwa nchi yoyote ambayo rasilimali ya eneo moja inatumika kwa eneo hilo tu.

Mheshimiwa Spika, imeanza kujitokeza huko Mtwara sasa hivi, Mheshimiwa Spika naiomba Serikali ikae na isichoke kuwapa maelezo juu ya umuhimu wa wananchi kukabiliana na uamuzi wa Serikali na kujenga bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam kwa maendeleo ya Taifa na pia wana Mtwara kwa ujumla na kuwaondolea hofu iliyotanda kwamba, kujengwa kwa bomba hilo ni uhamishaji kwa ujumla wake, jambo ambalo litawaacha wao mikono mitupu.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali ifanye uchunguzi kwa umakini illi kuwapata wale wote waliojificha nyuma ya mgongo wa gesi na kufadhili ghasia kwa ajili ya malengo yao mbalimbali, aidha, iwe ya kisiasa au kibiashara.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unatuonesha kwamba, kuna watu ambao hawaitakii mema nchi yetu na hawaridhiki kuona amani ya nchi yetu hii iendelee kuimarika, hivyo, wamekaa tayari kujipenyeza katika eneo lolote ambalo wataona wanafanikiwa kutimiza nia zao mbaya. Hivyo, naiomba Serikali iwe makini zaidi kukabiliana na hali yoyote inayojitokeza na kudhibiti amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, naanza na kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo naomba kupata ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini ya vito; Sheria ya Umiliki wa Migodi inasema Madini ya Vito imilikiwe na wazawa kwa 50% au zaidi. Leseni itolewe kwa mzawa na mwekezaji anaingia ubia 50%.

Mheshiwa Spika, jambo hili ni jema sana, naipongeza Serikali kwa hilo. Lakini Serikali imepandisha sana ada na tozo za leseni kwa wamiliki wazawa na pia hata kwa wachimbaji wadogo. Hii inaleta adha kubwa sana badala ya kumsaidia inamuumiza na kushindwa kutimiza azma waliyojiwekea kwa ajili ya wazawa.

Mheshimiwa Spika, ni vigezo gani vinatumika kwa upandishaji tozo hilo kwa sababu zimepandishwa zaidi ya asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ada za mwaka na ada za kuhamisha leseni za ufuutiliaji madini, zimepandishwa sana katika Sekta ya Madini nchini Tanzania ukilinganisha na nchi nydingine.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa ada na tozo za leseni kwa wachimbaji wadogo:-

- (i) Ada ya maombi kutoka 0.00 mpaka 50000.
- (ii) Ada ya kutayarisha leseni kutoka 20,000 – 50,000/=.
- (iii) Ada ya mwaka ya leseni.
 - Madini ya vito, almasi na dhahabu kutoka 20,000-80,000/=.
 - Madini mengine 10,000/= mpaka 50,000/=.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya upandishaji huu, wachimbaji wengi wadogo, wameshindwa kulipia leseni zao na kunyang'anywa na wenye pesa. Badala ya kuwasaidia wananchi wadogo kufanya tathmini ya mazingira na upembuzi yakinifu ili wachimbaji wadogo wapate andiko na kuweza kukopa Benki inawapandiswa ada na tozo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Nishati na

Madini anao uwezo na mamlaka ya kuandaa kanuni za Madini zinazorekebisha viwango vya tozo na ada za leseni mbalimbali kwenye Sekta ya Madini kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 (kifungu 112) ada hizi ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Umeme Vijiji; naiomba Serikali iongeze juhudhi kwa ajili ya kuhakikisha vijiji vinapata umeme, pia Serikali imewekwa kuhakikisha vijiji vingi vinafikiwa? Mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kuwa Shule zote zisizokuwa na umeme zinapatiwa? Sababu hili ni tatizo kubwa sana, ni vema ukaandaliwa mpango mkakati wa kuhakikisha Shule zote za Sekondari zenye maabara zinapatiwa umeme. Pia hata Makambi mengi ya Jeshi hayana umeme, ipo haja ya Serikali pia kuweka mkakati huo. Pia bila kusahau vituo vya afya, wananchi wengi wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, nampa hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye kuonesha mwelekeo. Nimeona mipango mizuri ifuatayo:-

(1) Kinyerezi II na Kinyerezi III. Miradi hii isimamiwe vizuri ili kuongeza *capacity* ya umeme wetu kufikia 350 Mw.

(2) Bomba la gesi lisimamiwe vizuri ili tuweze kupata gesi ya kutosha kuendesha *Turbine* hizo za Kinyerezi, lakini gesi hii isiwe ya kuchoma kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda kufufua na kuongeza Viwanda vinavyotumia gesi, kama plastiki na kadhalika Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri a- *speed up* matumizi ya gesi majumbani ili umeme uende viwandani.

(3) *Hydro scheme;* umeme wa maji ni nafuu, angalia miradi ambayo ilikuwepo, lakini hajatekelezwa. Anzeni kufikiria miradi Ruhudji, *Stiglers George* na maeneo mengine. Wizara iweke mkakati.

(4) Gesi pipeline; extend the pipeline to Tanga and Kenya as well. We can earn foreign exchange by selling the gas to Kenya.

(5) Umeme Vijijini; this will stimulate rural transformation. Nashukuru kwa umeme wa Mkalamo – Mbulizaga, Jimbo la Pangani. Bado kuna Vijiji vya Choba, Kigumesimba na Kimang'a ambavyo havina umeme navyo viingie katika REA.

(6) Miradi mingine ya madini; malizeni suala la Kabanga Nickel and other metals, shaba, chuma na kadhalika.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini na Manaibu wake kwa kazi nzuri, kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO anavyotatua matatizo ya umeme Vunjo. Transfoma zilipoungua katika Kata ya Kilema Kusini, Kilema Kaskazini, Makuyuni na Kirua Vunjo Magharibi alihangaika sana mpaka Transfoma zikapatikana.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ufumbuzi wa umeme katika vijiji vya Lotima, Kata ya Himo, Makuyuni, Vijiji vya Rau River, Ngasini, Oria na Kisangesangani, Kata ya Kahe.

Mheshimiwa Spika, kutohana na kupungua kwa nguvu za umeme katika Jimbo la Vunjo, naishukuru Wizara kwa kufunga mitambo mipyä katika Kijiji cha Makuyuni. Mitambo hiyo itasaidia kusambaza umeme katika Kata zote za Jimbo la Vunjo. Ningependa kujua mradi wa Makuyuni utakamilika lini ili kuondoa kabisa tatizo la umeme kukatikakatika Jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namshukuru sana Mheshimiwa Muhongo Waziri wa Nishati na Madini kwa

kukubali kumpokea Bwana P.J. Mining wa Namibia na Bwana Jac Lee, Mkurugenzi wa Kampuni hiyo alifurahi sana.

Mheshimiwa Spika, Naomba kujua hatima ya kampuni hiyo kama itashiriki katika uwekezaji wa gesi na mafuta.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, Shule za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Bukombe, hazina umeme. Kutokuwepo umeme kunapunguza ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Shule za Msingi na Sekondari Bukombe? Aidha, hakuna umeme katika vituo vya huduma za afya. Hali hii inasababisha huduma zisitolewe kwa kiwango pungufu. Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme wa mionzi ya jua katika vituo hivyo ili kuinua viwango vya huduma?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Umeme iliyopangwa katika Bajeti ya 2011/2012 ambayo haifahamiki itatekelezwa lini.

(1) Mheshimiwa Spika, Ukurasa wa 155; Miradi ya Taa za Mwanga Bora, Vijijiini (*Community Based Solar Power Trading*); Mradi huu ulipaswa kutekelezwa Chato, Biharamulo, Kahama na Bukombe, lakini hadi sasa hakuna dalili utatekelezwa lini. Je, utaanza kutekelezwa lini?

(2) Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 117; Tanzania *Affordable Rural Electrification Plan (TAREP)*. Mradi huu ulipaswa kutekelezwa Kibondo na Bukombe, lakini hadi sasa haujatekelezwa. Serikali inawaambia nini kuhusu Mradi huu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini; kwanza kuna kilio cha wachimbaji wadogo cha kutokuwa na maeneo ya uhakika ya kuchimba Madini na pia kutokuwa na zana stahiki za kuchimba. Serikali ina mipango gani ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wa Bukombe? Jambo la pili linahusu Makampuni ya Utafiti wa Madini ya nje ambayo yamekuwa

yakifanya utafiti Bukombe, mathalani *TANCAN*, yapo maswali mawili kuhusiana na utafiti wa *TANCAN*.

- (1) *TANCAN*imefikia hatua ipi katika utafiti wake?
- (2) *TANCAN* inafanya utafiti kwenye Hifadhi. Je, ni Sheria ipi inaruhusu utafiti wa Madini ya Dhahabu katika Hifadhi hii? Ni athari zipi za kimazingira zitasababishwa na Mgodi mkubwa wa dhahabu kama ukifunguliwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala yanayohusiana na Mgodi wa Ng'anzo. Wananchi wa Kijiji cha Ng'anzo, Kata ya Ng'anzo wanalamakia utaratibu uliotumika katika kuendeleza Mgodi wa Ng'anzo. Mgodi huo ulio katika eneo la Shule ya Msingi, ulianza miaka iliyopita, lakini kwa kuwa uko katika eneo la Shule ya Msingi (Mali ya Kijiji) Serikali Kuu ilipendekeza Kijiji kianzishe ushirika na kisha kimtafute mwekezaji ili aihamishe Shule ya Msingi na kuendeleza Mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, mambo yanayolalamikiwa ni kama ifuatayo:-

(1) Ushirika ulioundwa hauku fuata mchakato shirikishi. Hakuna mukutano Mkuu wowote wa Kijiji ulioitishwa. Hakukuwa na uwazi wa aina yoyote na orodha ya wana ushirika imebaki ni siri.

(2) Mheshimiwa Spika, eneo lililotengwa kuhamishia Shule ya Misingi halilingani na eneo la sasa la Shule ya Misingi. Eneo lililotengwa linadaiwa kuwa eka 20 wakati eneo la Shule ulipo Mgodi ni takribani eka 60.

(3) Mheshimiwa Spika, wana ushirika hawafahamiki wote, inadaiwa wapo wengi ambao wameingia kwa kutumia nafasi zao katika Uongozi wa Wilaya, lakini si wana Ng'anzo.

(4) Mkataba baina ya Ushirika na Mwekezaji hauko wazi kuhusu Kijiji cha Ng'anzo kitanufaika kutokana

na Mgodi huo. Nashauri Serikali ichukue hatua za haraka kurekebisha hali hii ambayo inaweza kuwa chimbuko la mgogoro usio na kikomo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la leseni Na. 0014769 (*PML*) ya Mkombozi *Mining Cooperative Society Limited*. Ushirika huu wa uchimbaji madini uliomba leseni ya uchimbaji mahali paitwapo Kurugwete, Wilaya ya Biharamulo. Ilipata leseni Na. 0014769 ya 9 Juni, 2009, lakini eneo walilopewa *Coordinate* namba zake zilionesha kuwa liko Geita na si Biharamulo. Hakuna eneo linaloitwa Karugweta, Geita. Mimi binafsi nilipeleka barua yao kwa Kamishna wa Madini mnamo mwaka 2011, lakini hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Nyaraka husika zimeambatishwa, nashauri Serikali itatue tatizo hili kwa sababu ni la muda mrefu.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Spika, kuhusu Jiji la Dar es Salaam limeendelea kuwa na umeme wa kukatikatika mara kwa mara, wakazi wengi wa Dar es Salaam wameharibikiwa na vifaa vyao vya ndani kama friji, *Microwaves* na kadhalika, ingawa Wizara katika hotuba yake inasema *Transfoma* mpya 15 zimefungwa Dar es Salaam, lakini ukweli ni kwamba, bado hali ya upatikanaji wa umeme majumbani siyo wa kuridhisha. Nguvu zaidi ielekezwe Dar es Salaam ili kupunguza usumbufu mkubwa uliopo wa umeme usio *constant*.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupata umiliki wa maeneo ya ujenzi wa Viwanda (*Industrial Park*) kwa ajili ya gesi huko Mtwara unaendelea, kwa maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ujenzi ambao utaongeza fursa za ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, je, ni viwanda vya aina gani na vingapi vitakavyojengwa? Pia tutegemee ajira za aina gani kwa Watanzania? Tusiwe tukaishia kuwa wafagizi, wabeba mizigo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wa nchi yetu bado hawapati *fovor* kutoka Mamlaka husika,

wengi hawana leseni na hata wenye leseni ni wachache sana. Wizara iangalie jinsi ya kuwasaidia wananchi wadogo wadogo kuwapatia maeneo na leseni bila kuwasumbua.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingi hapa Tanzania viko gizani, Programu ya umeme vijjjini (*REA*) itengewe fedha za kutosha ili kuendeleza umeme vijjjini kwa kasi inayoridhisha. Wilayani Arumeru – Arusha kijiji cha Mkoasenga, Ngarenanyuki, Kilinga na kadhalika, umeme upelekwe katika vijiji hivyo ili Watanzania/wananchi waishio maeneo hayo waweze kufaidika na hivyo wanawake kuondokana na adha kubwa waliyonayo ya ukosefu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Sospeter Mwitarubu Muhongo, alisema ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba, wananchi wa Mtwara wataunganishwa umeme kwa bei nafuu, ukilunganisha na wananchi wengine wanaoishi katika maeneo yenyenye madini (almasi, dhababu, *tanzanite* na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi Mererani eneo lenye Madini ya *Tanzanite*, madini ambayo hayapatikani mahali pengine popote duniani ila hapa Mererani, Je, wao walipewa *incentive* gani? Je, Wizara haioni kwamba kuwapendelea wananchi wa Mtwara kwa kuwaunganisha umeme kwa bei ya chini/nafuu ni kuleta maswali/ manunguniko kwa Watanzania wenzao?

Mheshimiwa Spika, endapo sisi ni Taifa moja lenye umoja, basi ni muhimu sana Watanzania wote wakanufaika na rasilimali zilizopo katika usawa bila kusema au kuruhusu wachache kunufaika kwa kigezo cha kuishi katika eneo lenye rasilimali fulani.

Mheshimiwa Spika, suala la *production* ya Gesi liangaliwe kwa umakini mkubwa, sera ya Gesi iandaliwe vizuri na kwa haraka kwani ndio mwongozo wa jinsi ya kuendesha

shughuli zote zinazohusu suala la uchimbaji na usambazaji wa gesi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia niipongeze Wizara ya Nishati na Madini kwa kuleta Bajeti yenye matumaini makubwa na hasa kwa wananchi wa Vijiji.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuamua kufanya mapinduzi ya nishati bila kukatikatika. Inaleta matumaini na kuboresha uzalishaji katika Viwanda. Naomba nichangie kwa kushauri katika Wizara hii nyeti katika maeneo machache:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu Nishati; naomba nishauri Serikali katika maeneo yote ambako kutakuwa na Miradi ya kupeleka umeme, izingatie maeneo yote ya wananchi na maeneo yenye sifa au uwezo wa kiuchumi na huduma kijamii gesi iachiwe. Huduma ya umeme ufuate maeneo ya wananchi katika Miradi ya Babati kupitia REA. Nashauri mradi wa kupeleka umeme kutoka Bonga hadi Beseko ambao sasa unategewa kupita barabara kuu na hakuna vijiji maeneo hayo. Nashauri umeme ungepitia Tarafa ya Gorowa katika Kata ya Ayazenda, Vijiji vya Ayasanda na Endanashan, Kata ya Gidai vijiji vya Endadimet na Kata ya Boay vijiji vya Gidefaboska kuelekea Bereko itakuwa imenufaisha Tarafa ya Gorowa ambayo kwa sasa haina kabisa nishati ya umeme na hapo baadaye Kata nne kupata umeme na vijiji 10 kunufaika. Ni Tarafa muhimu kama nishati kukosekana.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri mradi wa umeme wa Kash – Endadosh uende hadi Hurui kama kilometra mbili mbele ambako kuna kijiji kikubwa na pia ni eneo ambapo Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa ahadi kufikisha huduma hiyo pamoja na maji na barabara ambao sasa unatekelezwa. Pia Mradi wa Babati (VETA) ufile katika eneo

ambalo tunajenga Chuo cha Ualimu na Mafunzo ya Kilimo pamoja na Sekondari iliyoko jirani. Pia iende kilomita 2.5 kuelekea Kijiji cha Mwinkatsi yenye makazi na huduma ya jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nishauri kuwa mradi wa umeme unaotegemewa kwenda Magara kutoka Shaurimoyo (shamba la *Vicky Estate*), nashauri umeme upite Kijiji cha Shaurimoyo na Kisangaji ambayo iko pembeni kidogo na njia ya umeme kilomita 2.5 na mahali inapoishia sasa usogezwe mbele hadi Shule ya Sekondari na shamba la *Rift Wall* kuelekea geti ya Iyambi katika hifadhi ya Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Spika, lingine katika upande wa nishati, naomba Serikali ijitahidi kuhakikisha maeneo yate yaliyopitiwa na umeme, umeme huo uteremshwe katika vijiji husika. Naomba pia Wizara kwa kupitia *TANESCO* iangalie suala la kuanza kutumia nguzo za Saruji (*Cement/Concrete blocks*) mapema kupunguza uhaba wa nguzo za miti na pia kupunguza uharibifu wa mazingira. Pia itaongeza ajira na nguzo hizo zinadumu kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Wizara iangalie suala la kupata mikopo kutoka vikundi muhimu vya uzalishaji ambako hakuna bajeti iliyopangwa kuendeleza mradi, kikundi kikope katika Taasisi za fedha na kulipa gharama za mradi na baadaye fedha hizo zirudishwe kwa makato katika bili za umeme. Pia Wizara iandae mpango wa kukopesha wananchi gharama za kuunganisha umeme na waweze kulipa kwa mkataba maalum.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Wizara iendelee kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya umeme na namna ya kupunguza matumizi mabaya ya nishati hiyo. Pia itoe elimu ya namna bora ya kupata nishati ya umeme kwa njia mbadala mfano *solar, biogas*, upepo kwa maeneo yote nchini ambako hakuna uhakika wa kupata nishati hiyo kwa kupitia gridi ya Taifa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie namna ya kupata mradi wa uzalishaji wa nishati kwa kuptitia *solar* kama nchi za Asia zinavyofanya, wanazalisha umeme mwangi kuptita *solar* kwa sasa, gharama ya uendeshaji kwa baadaye inapungua sana.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Madini naomba nishauri kuwa kwani Sera na Sheria ya Usonara iharakishwe. Itasaidia Sekta hiyo kukuwa na pia kuongeza thamani na ajira. Pia kuboresha uthamini huo (*Art and Craftmanship*). Pia kushauri Serikali kuboresha kituo cha Madini Kanda ya Kaskazini (Arusha) kwa kuongeza vifaa vyta mafunzo vyta kuchonga vito. Arusha inaweza kuwa kituo kikubwa cha Vito Barani Afrika. Napongeza kupanga mipango mizuri mliyoweka inayotarajiwa kuanza 2014/2015, lakini nashauri wakati tunaposubiri tuanze angalau na mashine 100 kwa sasa ambayo haitagharimu Dola za Marekani laki mbili. Itaongeza ajira, tutakuwa na waatalam wengi watakaotoka kwa awamu ambayo tukifika kipindi cha kituo kukamilika, basi watakuwa wameshajifunza kiasi na watakuwa wanakuja kujiboresha na kupata mafunzo ya muda mfupi tu kuongeza taaluma kazi hii tusiachie Sekta binafsi tu. Serikali ichukue jukumu la kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kabisa kuipongeza Serikali kwa maana ya Wizara hii chini ya Mheshimiwa Waziri Prof. Muhongo na Manaibu Waziri wake, Mheshimiwa Maselle na Mheshimiwa Simbachawene. Bila ya kuwasahau Katibu Mkuu, Manaibu wake na Wakurugenzi, Mameneja na Vitendo vyote vilivyo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Mafia ni Kisiwa na hivi sasa Kisiwa hiki kipo katika kuinuka kwa kasi kimaendeleo. Naamini kama miundombinu yake ikikamilika, kama Gati, Uwanja wa Ndege, barabara za ndani na kuptitia *REA* umeme ukishasambazwa vijijini, Mafia itakuwa ni sehemu nzuri ya

Kitalii na sehemu nzuri ya mapumziko. Umeme huu ukifika vijijiini uchumi wa wananchi utakuwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri. Hivi sasa mashine zinazotumika kule Mafia ni mbili zenye uwezo wa kuzalisha Kilowatt 900. Mashine hizi hutumia mafuta ya Dizel lita 3550 kwa siku. Hivyo kwa mwaka huu hutumia wastani wa lita 1,286,250 ambazo gharama yake ni Sh. 3,235,913,612.15 na ukijumlisha na lita 10,980 za mafuta ya vikimisho (*LUB OIL*) zilizokuba na gharama ya Sh. 57,513,323.40. Ukijumlisha gharama zote kwa mwaka ni Sh. 3,293,426,935.50.

Mheshimiwa Spika, uhai wa Kebo ya kuzamisha bahaarini ambayo ina uwezo wa kukaa bahaarini kwa zaidi ya miaka 25 mpaka 30, nafikiri ndiyo suluhisho pekee kwa wananchi wa Mafia na pia itaipunguzia Serikali/Shirika la *TANESCO* gharama kubwa sana na hizo pesa zitaweza kufanya shughuli nyingine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ukichukua gharama za kuendeshea mitambo, hivyo tena sasa imeongezeka mingine miwili yenye uwezo wa kuzalisha Megawatt 1.2 (Kilowati 1,280) kwa miaka 25 bila ya bei ya mafuta kupanda kwa Kipindi hicho. Naamini siyo kweli kuwa bei haipandi, ni lazima ipande. Gharama yake ni zaidi ya Sh. 164,671,346,776/= na wakati ukilaza Kebo hiyo sifikiri kama itazidi Shilibi bilioni 60. Naomba sana Serikali ifikirie jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mfano huo kuititia jarida la Zanzibar linalochapishwa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhii ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambayo imesema kuwa imelaza Kebo hiyo kutoka Manyanyani, Tanga mpaka Pemba kwa gharama ya Norwegian Krone milioni 400, sawa na Shilingi zetu 111,712,910,400/= na gharama hii ni kwa kilomita 72 kwa kila kitu mpaka umeme unaweka Pemba kwa Mafia ni kilometra 36 tu toka Nyamisati Rufiji hadi Mafia, ndiyo maana naamini Shilingi bilioni 60 zinatosha kulaza Kebo. Naomba mlione hilo wataalam wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Prof. Muhungo pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi safi wanazofanya katika kuongeza Wizara hii. Naomba kuunga mkona hoja hii ambayo naamini utekelezaji wake utafikisha nchi hii mahali tunapotarajia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TANESCO*, Njombe hawana umakini katika kufanya kazi zake. Zaidi ya miaka miwili sasa wamepeleka nguzo Shule za Sekondari za Igima na Wanike lakini mpaka leo kazi imesimama na ukiwaliza, hawakupi jibu la maana. Zaidi ya miaka 15 nguzo zipo karibu na Shule ya Sekondari ya llembula lakini hakuna *wire* wala mwendelezo wowote wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, pia *TANESCO* Njombe wanalalamikiwa na wananchi vijiji vya Mhaji, Mdandu, llembula ambao wamelipia kuingiziwa umeme lakini ni zaidi ya miaka 2 hawajapewa umeme. Nimefuatilia na Ofisi za *TANESCO* Njombe na Makambako lakini inaelekea kuna dalili ya utapeli unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kuna Wilaya yangu ya Wapigangebe kwa kupitia *REA*, kuna baadhi ya vijiji vimeorodheshwa. Naomba maelezo: Kwa nini vijiji vingine havijaorodheswa kulingana na Tangazo la Zabuni lilitangazwa gazetini na *REA* vikiwemo Mwilamba, Uhekule, Ujindile, Kijinte, Lyndebwe Lyanduki, Ujwala, Mungelege, Itemi Usuka, Wingilwa , Bonawamu na Kanawalenga?

Mheshimiwa Spika, katika kupeleka umeme Wilaya mpya, sijaona mpango wa kupeleka umeme eneo litakalojengwa Makao Makuu ya Wilaya ya Wanging'ombe pale Kijiji cha Igwachanya. Ni kweli Kijiji cha Igwachanya kina umeme wa kiwango cha Kijiji lakini eneo la Makao Makuu yanajengwa, ni takribani kilometra moja ambapo patahitaji kupelekewa umeme wa kiwango cha Makao Makuu ya Wilaya ambapo patajengwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Ofisi ya Halmashauri pamoja na Ofisi nyingine za Serikali na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wamegundua shaba maeneo ya Mtapa na wamejiunga kikundi, wamechimba shaba lakini hawajui soko waende wapi. Naomba Wizara hii itusaidie kutuelekeza soko, lakini pia watalaan wa madini wafike pale ili watoe utalaam namna ya kuendeleza uchimbaji huu wa shaba.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa umeme ni uchumi na uchumi ni maendeleo. Ni muhimu nchi ikaongeza upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima iangalie, pamoja na upatikanaji wa umeme, bei ya umeme ipungue. Hii tu ndio itaweza kushusha gharama za bidhaa na watu wengi waweze kuongeza thamani ya mazao na kulongzeza Taifa mapato.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya *Solar* vimikuwa vinatozwa kodi kubwa sana na kufanya wananchi wengi kushindwa kumudu manufaa ya upatikanaji umeme. Manufaa yake ni mengi sana hata kuonea tu (taa). Ni kwa nini basi Serikali isiangalie jinsi ya kupunguza bei ya vifaa vya *Solar* ili umeme huo wa *Solar* uweze kutumika majumbani kuonea, ili umeme wa vyanzo vingine utumike kwenye viwanda vikubwa na vidogo na na kuongeza uzalishaji? Suala hili nalisema kwa mara ya pili maana mwaka 2012 nilisema hili, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua suala la umeme, ni lazima liangaliwe kwa ujumla wake muda wa kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imezidiwa, ni vizuri sasa Serikali iangalie jinsi ya kuipunguzia majukumu *TANESCO*. Unalipa kutaka umeme, lakini inachukua muda mrefu kabla umeme haujaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wanaweza kuiongezea mapato Serikali iwapo Serikali

ingewapa mikopo ili waweze kuzalisha kwa faida na kuchangia kodi kwa Serikali. Siyo hii tu, lakini pia ingeweza kutoa ajira za moja kwa moja na hata zisizo ya moja kwa moja kwa kuongeza kipato cha wenyе ajira na kuweza kununua bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa msimamo wake wa kulinda maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla kwenye masuala ya upatikanaji na utumiaji wa gesi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana wanayofanya, na kuwapa Watanzania imani kubwa sana na Wizara hii.

Naunga mkono hoja.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya. Wizara ina changamoto nyingi, lakini lazima tuzishinde. Umeme ni maendeleo, ni chombo cha kuleta maendeleo. Hivyo kuwa na umeme majumbani ni haki na siyo anasa tena.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa usambazaji umeme nchini unaonekana kupendelea sehemu fulani za nchi, zaidi Mkoa wa Ruvuma, kwa mfano vijiji vyenye umeme havifiki vitano. Huu ni Mkoa unaotoa chakula kwa nchi. Kule Mbinga zao la Kahawa linachangia 1/3 ya kahawa ya arabika nchini. Lakini Wilaya ya Mbinga haina Kijiji chenye umeme mpaka sasa. Pamoja na kuishukuru sana Serikali kwa kuweka umeme katika sehemu ya Mji wa Mbinga, natumai umeme utapelekwa sehemu zote za Mji za Kihah, Mitarane, Lesaka na Lesonga.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia mpango wa kuweka umeme vijiji idadi ya 10 mwaka wa fedha 2012/2014, naomba kwa vile tunayo *record* //ya MCC Wilaya ya Mbinga ifikiriwe kuwekwa katika Mradi huu ili Kata zifuatazo ziwe na vijiji vyake

vipate umeme. Kata ya Ngima, Myangayanga, Luwaita, Mbuji, Langiro, Kipohilo, Ukate, Mpepai, Nyoni, Kitura, Kihangi, Mahuka, Namswee na Litumba Ndyosi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iweke nguvu na ushirikiano katika mradi wa Umeme Ngaka.

Mheshimiwa Spika, tatizo la fidia kwa wananchi – Serikali kupita *RC* iliweka ahadi ya kulipa wananchi ifikapo tarehe 15/6/2013. Naomba Serikali itimize ahadi yake, wananchi wamekuwa watulivu na tuiswabugudhi.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo ya *PPA* kati ya *TANCOAL* na *TANESCO* sasa yaishe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza wawekezaji kwa nia yao ya kujenga mtambo wa kufua umeme, lakini kama nchi hii, ina maslahi kwetu? Tunalo tatizo la umeme tunataka umeme leo, siyo kesho. Kwa nini tunaachia suala hili mikononi mwa wageni? Je, Serikali kupitia *TANESCO/NDC*, haiwezekani kupata fedha za ndani kujenga mtambo huo na kuachana na *capacity charges*? Naomba Serikali ifanya *review* ya wazo hili bila kuathiri upatikanaji wa umeme. *TANESCO*, wanatumia Shilingi bilioni 5.1 kwa siku. Je, hizi haziwezi kujenga mtambo huo?

Mheshimiwa Spika, ni kweli azma ni kufua umeme na kulisha *grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba fursa hii itumike kuleta umeme katika vijiji vya Wilaya ya Mbinga kwa kuanzia vijiji vya Ntuduwaro na Ruanda. Kwa fursa hii naiomba *REA* izungumze na *NDC/Tancoal* na kuona uwezekano wa kujenga mtambo mdogo wa MW 5 -10 ili umeme wake utumike kuwaka katika vijiji vya Mbinga na vijiji vyote vya Mkoa wa Ruvuma.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara na Viongozi wake, Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wote wawili, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa

Taasisi chini ya Wizara kwa kuonyesha dhamira ya dhati katika jitihada za kutaka kuondoa kwa kiasi kikubwa tatizo la nishati nchini baada ya muda siyo mrefu kuanzia sasa. Dhamira hii imejionyesha kwenye hotuba ya Wizara na vipeperushi vilivygawiwa. Pongezi sana na mwendeleze dhamira hii kwa uwezo wa Mungu pia.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazofanywa na *REA* ni nzuri sana na kama nchi, yaelekea tukichelewa tu kuunda mfuko huu, kwa sababu kwa muda mfupi tangu uanzishwe mafanikio yake yamekuwa ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, la msingi *REA* wapewe fedha za ruzuku za kutosha ili waweze kusambaza umeme katika vijiji vyote Tanzania ndani ya miaka michache ijayo. Zaidi nimefarijika kupata maelezo kuhusu ufufuaji wa Shirika la *STAMICO* hasa kwa dhamira mpya ya kuwa na hisa katika miradi watakayoitekeleza nchini. Naunga mkono maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusika na Wizara hii kuhusu *STAMICO* kukabidhiwa Mradi wa kufua Umeme wa Kiwira. Hivyo ni hatua nzuri kwa Serikali kumiliki rasilimali muhimu kuititia Mashirika yake.

Hata hivyo, suala la malipo kwa wafanyakazi waliokuwepo awali, malimbikizo ya mishahara na kadhalika. Lishughulikiwe kabla ya *STAMICO* kukabidhiwa ili Shirika lisianze kazi kwa matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni mara ya kwanza kuona Wizara yoyote ikitenga fedha za maendeleo nyangi kwa asilimia 90% kwa ajili ya miradi yake. Nashauri mfumo huu iwe ndiyo dira ya upangaji wa Bajeti katika Wizara zote ili kuleta mageuzi ya kiuchumi haraka badala bajeti zinapopangwa kwa matumizi *almost* ya anasa tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa bomba la gesi toka Mtwara, yaelekea baadhi ya wananchi wameamua kupinga tu utekelezaji wa mradi huu. Pamoja na elimu yote iliyotolewa na Wizara, yafaa vyombo husika vifanye uchunguzi wa kina ili kubaini sababu za upinzani

unaoendelea. Inasikitisha kusikia kwamba hata hii leo vurugu zimetokea wakati Wizara ikiwasilisha hotuba yake Bungeni. Yawezekana kuwa ni hujuma yenyé mizizi yake nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo machache, naunga mkono hoja na kuwatachia Wizara heri katika kutekeleza mikakati waliyojipangia.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya juu ya usambazaji wa umeme vijijiini.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Shirika la TANESCO kwa ujumla imefanya juhudhi kubwa kupeleka miundombinu ya umeme. Tatizo kubwa ni *speed* ndogo ya mkandarasi *SIMBION*, *Transforma* bado hazijawekwa kwa *line* ya Mlandizi hadi Mzenga. Kwa *line* inayotoka Kisarawe Mjini hadi Msanga, Mkandarasi *SIMBION* amefanya kwa *speed* ya kinyonga. Naiomba Serikali iweke mkazo kwa mkandarasi ili umeme uwafikie wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Madini naiomba Serikali iwasaidie wafanyakazi wanaofanya kazi katika Makampuni ya Madini. Kuna wafanyakazi wanasihamishwa kazi na kisha wanawekwa katika orodha ya *Black List*. Mfanyakazi huyo hawesi kupata kazi kokote kwenye Kampuni ya Madini yoyote. Naomba kauli ya Serikali: Je, ina mkakati gani wa kuzuia jambo hili ovu kwa wafanyakazi wa Tanzania? Pia kuna wafanyakazi wanaopatwa magonjwa wakiwa kazini katika Makampuni ya Madini wanawatelekeza bila huduma ya uhakika. Naomba kupata msimamo wa Serikali katika hili.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isiyumbe katika ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam.

Naunga mkono hoja.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Makamishna wote na Wakuu wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuja na mpango kabambe wa kuhakikisha Vituo vya Afya na Shule zote zinapata umeme. Ni jambo jema sana, kwani itasaidia sana kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma, lakini pia itaboresha maisha na kuleta tija.

Naomba sana kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria na Mahakama ya Tanzania, mtusaidie Mahakama zetu nchini, kuanzia katika Vijiji vyetu hadi Mikoni (Mjini). Ngazi zote nazo ziingizwe katika mpango huu muhimu, kwani huwezi kuamini, ziko Mahakama nyingi nchini hazina umeme, hata Dar es Salaam zipo pia. Hii inatukwamisha sana katika mipango mbalimbali tuliyonayo ya kutumia *TEHAMA* katika uendeshaji wa mashauri Mahakamani. Uchapaji wa nakala za hukumu kwa wahusika kwenye mashauri na washitakiwa wengi inafika wakati wanashindwa kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mahakama, kwani inabidi Mahakama za Wilaya nzima zikachapwe nakala za hukumu na miendo ya mashauri/kesi, katika Ofisi za Wilayani. Tunaomba sana mtusaidie katika azma hii itatusaidia sana na wananchi watanufaika sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara na Watendaji wote, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiwira *Coal Mine*, hali ikoje sasa? Kwa 2013/2014?

Mheshimiwa Spika, lleje ina vijiji 71. Kati ya hivyo, ni vinne tu vina umeme. Je, miradi ya vijijini itaanza lleje kwa kuwa wanakwenda kusaga mahindi nchini Malawi? Umeme

kutoka Ikuti Rungwe kwenda lleje inapitia vijiji kadhaa kabla ya kufika Itumba Makao Makuu kuititia Shikunga, Ibaba, kutokea Kijiji cha Powenda. Katikati ya Bwenda kuna Kata ya Ngulilo; naomba ijumuishwe katika mpango. Aidha, kati ya Sanga na Kalembo Kata ya Ngulugulu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mbele kidogo ya Ibaba, kuna Kata ya Itale na Nola. Naomba iongezwe.

MHE. ZABEIN M. MHITA: Mheshimiwa Spika, je, Serikali inaweza kututhibitishia kuwa fedha ya kutekeleza miradi iliyopo kwenye REA // ipo? Na kuwa, vijiji kutoka Babati ambako kuna umeme kuititia vijiji vya Bereko hadi Kolo mpaka Kondoa vitapatiwa umeme hasa ikizingatiwa kuwa umeme unapita juu ya vijiji hivyo?

Naunga mkono hoja.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni mionganini mwa Wizara ambayo ni tegemeo kubwa linalokuza uchumi na kuongeza pato la Taifa litokanalo na vyanzo husika kama vile machimbo yanayozalisha dhahabu, almasi, *tanzanite*, pamoja na mkaa wa mawe, lakini vilevile vyanzo maji ambavyo vinazalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Tanzania siyo masikini. Hata hivyo, imepelekea Watanzania walio wengi kuishi katika umasikini kutokana na kutotilia maanani maeneo ya uzalishaji ambayo yangaliwezesha kuwapatia njia Watanzania walio wengi. Ni wajibu wa Serikali sasa kuhakikisha kwamba maeneo yote ya uzalishaji wa madini nchini, wazawa wanapewa kipaumbele cha kuwapatiwa vibali juu ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uzalishaji wa umeme, Tanzania bado halijaweza kutosheleza mahitaji ya wananchi Mijini na Vijijini. Haya yote yanatokana na ubunifu mdogo ambaao ama wataalamu wetu wanao, au wamekosa uaminifu na uadilifu juu ya ukusanyaaji wa mapato

na njia mbadala ya namna ya kuwafikishia umeme wananchi Mijini na Vijiji. Hata hivyo, Wizara ina wajibu wa kuangalia uwezo wa viwango vya mapato ambayo kila Mtanzania anapata. Watanzania ni masikini, hivyo ni lazima tuangalie uwezo wao wa mapato.

Mheshimiwa Spika, umeme ni ukombozi, umeme ni uchumi, umeme ni maendeleo endelevu. Hivyo, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba Tanzania inazalisha umeme wa kutosha na unawafikia Watanzania popote walipo, Mijini na Vijiji. Endapo suala la umeme litachukuliwa kuwa ni suala la haki ya msingi na haki ya ukombozi wa mwanadamu na kinyume chake, ichukuliwe kuwa ni kinyume cha haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, suala zima la uchimbaji wa gesi ni suala ambalo litaweza kupunguza makali yatokanayo na upandaji holela wa bei za umeme nchini, hivyo Serikali ina wajibu wa kutanzua migogoro na mizozo iliyojitokeza ili kuhakikisha kwamba suala hili limepatiwa ufumbuzi wa kufaa ili uzalishaji wa gesi uweze kufanyika na hivyo kuwapatia Watanzania walio wengi ajira, lakini na kuwaondolea ukali wa maisha.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, kwanza, nitoe masikitiko yangu kwa yale yanayotokea Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa wote waliopatwa na majanga ya kuchomewa nyumba, magari na mali nyingine na hasa pole kwa familia za waliopotelewa na wapendwa wao katika vurugu za Mtwara kwa namna moja au nyingine, kwa ambao wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na kauli mbalimbali za Serikali kuwa Raslimali za nchi ni mali ya nchi na siyo mali ya mtu mmoja mmoja au kikundi au Chama chochote cha kisiasa au cha kidini. Lakini ijulikane wazi pia kwamba Serikali haipo Dar es Salaam peke yake, bali pia Vijiji na Mijini hasa kule ambapo Raslimali zinatoka.

Mheshimiwa Spika, leo ukienda China utajifunza mengi sana kutokana na mgawanyo wa maendeleo uliotapakaa maeneo yote, na siyo katika Miji Mikuu peke yake. Hicho ndiyo kilio kikubwa kwa Wana-Mtwara na ndiyo ujamaa aliojifunza Mwenyeekiti wa Kwanza wa CCM na aliyekuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mwalimu Julius K. Nyerere, alipanga kuyafanya hayo hapa kwetu ila waliopo sasa wamepuuza.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kutupia lawana baadhi ya watu walisababisha vurugu na hili ni jambo rahisi sana sana kutamkika mdomoni, lakini tukasahau Chama kinachounda Serikali, sasa hakiaminiki tena, kwa kuwafumbia macho wabadhirifu wa mali ya umma na kuacha wajimilikishe mali kinyume cha utaratibu na kuwachukulia hatua kali maskini, huku matajiri wakiwa huru mara wafanyapo uhalifu. Kumefanya Chama kinachotawala kuwa na mporomoko wa kasi wa kutoaminipa tena na wananchi. Ikumbukwe pia ahadi lukuki zilitolewa wakati wa kampeni za uchaguzi, imepelekea kabisa kutoaminika tena kwa kauli zitolewazo na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Chama kinachounda Serikali basi kiangalie upya namna nyingine kabisa ya kurudisha imani yake kwa umma ili kauli zake ziaminike.

Mheshimiwa Spika, leo tunachokishuhudia ni mwendelezo wa kauli zisizoaminika tena toka Serikalini ambazo zimepelekea kabisa uvunjifu wa amani huko Mtwara, kwani ahadi nyingi sana zilitolewa na sasa zimesahaulika na hiyo ndiyo imepelekea elimu na yote yatolewayo juu ya gesi ya Mtwara, sasa imeonekana haina ukweli wowote. Hiyo ndiyo sababu kubwa ya vurugu na siyo maamuzi ya Wizara au hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Serikali kufanya tathmini ya kina kwa ahadi na kauli zake na kuzitekeleza kwa wakati ili kauli zijazo ziweze kuaminiwa na utekelezaji wake uwe wa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo malalamiko ya muda mrefu sana kwa Watanzania kutosomewa mapato ya rasilimali na mchango wake katika kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa uwepo utaratibu mzuri wa kusoma kila mwaka mapato ya madini na rasilimali nyingine za nchi na kueleza Watanzania fedha hizo zimefanya nini na hiyo itaondoa kama siyo tu kupunguza tataruki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, najua kama Wizara inayo nia njema ya kusaidia amani na kufanya madini na gesi ikiwemo mafuta kuwa baraka badala ya laana, basi mawazo haya yatafanyiwa sana kazi na kupewa umuhimu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kama tutaamua kwa dhati kabisa kutoa punguzo kwenye uwekaji wa umeme kwenye mashule yetu Vijijini, basi vijana wetu wataweza sana kusoma Sayansi vizuri na kuongeza muda wa ziada wa kujisomea na kupata matoke mazuri ya kuwa na wanasayansi wazuri huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, linguine ni kuhusu umeme kwa njia ya mkopo. Nyumba ni kitu kisichohamishika na ni nyumba ndiyo iwekwayo umeme.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara iweke utaratibu wa kuwakopesha umeme (*installation*) na wao waweze kulipia polepole kila mwezi au kila wanapolipa kwenye manunuzi ya Luku.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki ya *NMB*ipo karibu Wilaya zote hapa Tanzania, basi ni vizuri sana Wizara ikaona ni vyema kuwatumia wataalamu wao na jinsi gani ya kuweka mikataba vyema ili *TANESCO* waweze kuwapa watu wengi zaidi kupata umeme na pia shirika liweze kujikusanya mapato zaidi na kuweza kuijendesha kwa faida, kwani watumiaji watakuwa wengi wanaolipa Ankara zao ambazo ndiyo tegemeo la mapato la Shirika la Umeme la *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu najua utanufaisha wengi na hasa wawekezaji wa viwanda vyta kati na vidogo ili tuweze kuwa na wawekezaji wengi ambao watavutiwa na aina hii ya uwekaji umeme na kuongeza ajira, pato la mtu mmoja mmoja na pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, itakuwa vigumu sana kuepuka fujo migodini kama hatutatenga maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo na ni vizuri sasa tukaweka sana utaratibu wa kuwatengea maeneo ili basi kuwanufaisha wananchi hasa katika maeneo yanayozunguka mgodi.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Spika, mimi nitaongelea kwanza Sekta ya Madini, wachimbaji wadogo wadogo kutolipa leseni zao za kila mwaka; kuficha mapato halisi ya dhahabu na madini mengine wanayopata ili kukwepa kodii; migogoro ya mipaka ya vitalu; utoaji wa leseni ndogo ndogo kwenye maeneo ya leseni kubwa kubwa ama leseni za utafiti; viongozi na watendaji wa Sekta ya Madini hasa Ofisi za Kanda Mtware kukiuka taratibu ambazo ziko kwenye Sheria ya Madini ya mwaka 2010; na viongozi wa ngazi ya vijiji kutoa vibali na kuruhusu wachimbaji wadogo wadogo kuchimba maeneo yenye leseni za *Plau PM*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo kutolipa lesseni zao za mwaka; wachimbaji wadogo wadogo kutolipa leseni zao kwa wakati, ni tatizo na kama Mheshimiwa Waziri alivyosema katika hotuba yake, wanalipunguzia Taifa mapato. Ushauri wangu ni kwamba uwekwe muda maalum kwamba wachimbaji hawa wadogo kama hawalipi lesseni zao kufikia muda fulani, leseni zao zifutwe kama ambavyo sasa Serikali imefanya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufuta leseni hizo, itasaidia sana kuleta *discipline* ya ulipiaji wa leseni zao kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo ni kweli hawatoi takwimu halisi na za kweli kwa Serikali kuhusu kiasi wanachopata kwa nia ya kukwepa kodii. Wilaya ya Liwale kuna machimbo mengi sana. Machimbo yaliyoko

katika Kijiji cha Kibutuka, wanayaita Kipelele Chini, yanakumbwa na hali hii. Wachimbaji wadogo wadogo wamevamia eneo hilo na Wilaya inashindwa kupata takwimu halisi ya mapato kutokana na wachimbaji hawa, walioko katika kijiji hiki.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ichukue hatua za kutembelea na kufanya ukaguzi katika machimbo haya ya Kubutuka kwa nia ya kufanya ukaguzi ili kuona: Je, wachimbaji hawa wadogo wadogo wana hati miliki za kuchimba maeneo hayo? Je, wamefuata taratibu zote za Sheria za Madini za mwaka 2010? Je, mapato wanayopata wanaripoti wapi na wanalipa kodi wapi? Nina uhakika wachimbaji hawa ambao wengi wao ni kutoka nje ya Wilaya ya Liwale, wanakiuka taratibu na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro ya mipaka ya vitalu na utoaji wa leseni kwa wachimbaji wadogo wadogo kwenye maeneo ambayo tayari yana leseni ya *PL* ama leseni za uchimbaji *PM*; kuna migogoro tayari eneo la Kibutuka Liwale ambapo wachimbaji wadogo wadogo wamevamia kwenye eneo hilo na kuendelea kuchimba. Nina mashaka kama wachimbaji hawa wadogo wana lesseni za kuchimba eneo hilo. Eneo hili tayari lina leseni kubwa za *PL*, lakini wachimbaji hawa wadogo wadogo wanadai wamepata leseni za kuchimba kutoka Ofisi za Madini kanda ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, hivi inakuwaje wachimbaji wadogo wadogo hawa wanaruhusiwa kufanya shughuli zao za uchimbaji kwenye maeneo ambayo tayari yana umiliki na mmliki anayalipia? Wachimbaji hawa sasa wanalipia maeneo hayohayo katika Ofisi zipi?

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wamevamia kwenye maeneo ambayo tayari yana leseni za *Pl*, na kuendelea na shughuli zao ndani ya maeneo hayo kwa kutumia Sheria ya Ardhi ya mwaka 2005. Viongozi wa Serikali za Vijiji pia wanawaruhusu wachimbaji wadogo wadogo, kuchimba na kuwaruhusu kulipia ardhi katika Serikali ya Kijiji

kwa kufuata Sheria ya Ardhi ya mwaka 2005. Viongozi wa Serikali za Vijiji wameshindwa kutofautisha kati ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Sheria ya Ardhi ya mwaka 2005, na hivyo wanasababisha vurugu na mitafaruku isiyo na tija kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini na hasa Ofisi za Madini Kanda ya Mtwara, ichukue hatua za haraka kufuatilia yanayoendelea katika eneo hili la Kibutuka ili katika siku zijazo tazito hili lisije likawa kubwa na kusababisha vurugu na migogoro isiyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa gesi kuletwa Wilaya ya Liwale; kwanza, nishukuru Wizara na hasa *TANESCO* kwa jitihada zilizofanywa za kuupatia mji wa Liwale umeme wa uhakika, sasa hivi tuna umeme wa uhakika na kila mtu mwenye kuhitaji umeme atapata.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umeme huu ambao unazalishwa kwa kutumia *generator*, bado ninaendelea kuomba sana Serikali, Liwale tupatiwe umeme na *gas*, kwa sababu umeme huu na *generator* ni ghali ukilinganisha na umeme wa *gas* kwa sababu *generator* hizi zinatumia kiasi kikubwa sana cha mafuta kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Lindi, ni Wilaya ya Liwale pekee ndiyo iliyobakia kuunganishwa ama kupata umeme wa *gas*. Wilaya zote Mkoa wa Lindi zina umeme unaotokana na *gas*.

Mheshimiwa Spika, katika takwimu na *data alizozitoa* Mheshimiwa Muhongo, ameiweka katika orodha yake Wilaya ya Liwale ya 43, na kwamba amesema Wilaya ya Liwale itaunganishwa katika umeme wa *gas* kutokea Ruangwa, na ni Sera ya Wizara ya Madini na Nishati kwamba kila kijiji ambacho umeme huo utapita, kitapata umeme. Wilaya ya Liwale tumewekwa kwenye *Budget* hii ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba, Wilaya ya Liwale itaunganishwa kwenye umeme huu wa *gas*

mwaka huu, na ikumbukwe pia kwamba imo kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Hata hivyo, umeme wa *gas* utapunguza sana gharama za mafuta ambayo nina uhakika kiwango kikubwa sana cha mafuta ya kuendeshea *generators* zilizopo kinatumika kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana katika ustawi wa Taifa letu. Naiomba Serikali itenje Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwezesha Wizara hii ili iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, gharama za umeme kupelekwa kwa wahitaji ni kubwa sana. Ni muhimu Serikali ikaangalia upya juu kupunguza gharama ambazo ni kubwa sana zainazomwathiri mwananchi wa kawaida mwenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu umeme wa vijijini (*REA*). Ili nchi iendelee, kunahitajika kupata umeme vijijini ambaao utasaidia sana wananchi wa vijijini kukuza uchumi wao. Nilikuwa naishauri Serikali ihakikishe inaongeza fedha za kutosha kuhakikisha Wakala wa Umeme Vijijini anakuwa na pesa za kutosha ili aweze kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliahidi kutoa huduma za umeme katika vijiji vya Kabungu, Mchakamchaka, Ifukutwa, Majalila (Mpanda ndogo).

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ihakikishe inapeleka umeme katika maeneo haya. Kama Serikali itapeleka umeme katika maeneo haya utatatua tatizo katika Taasisi za Shule za Sekondari zilizo katika Kata ya Kabungu na Kata ya Mpanda ndogo.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi ni lazima litolewe elimu ya kutosha kwa wananchi wa maeneo yanayotoa gesi hasa Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, gesi ni rasilimali ya nchi na siyo mali za watu wa eneo fulani. Ni vyema Serikali iwaelimishe wananchi kwa nguvu na kudhibiti wale wote wanaopotosha wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali. Nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, natoa hongera sana kwa Wizara hii kuongeza muda wa punguzo la kuunganishiwa umeme hadi Juni, 2014 kwa wananchi wa Mtwara na Lindi ila tuhakikishe pia vitendea kazi na nyaraka muhimu zinapatikana kirahisi ili isitokee tena kulazimika wananchi kuomba ongezeko la muda.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara ihakikishe miradi ya upelekaji umeme vijijini inatekelezwa kwa wakati. Kucheleweshwa kwa miradi kunakatisha tamaa na wakati mwininge kutoa mwanya kwa wachochezhi kupenyesha uongo na taarifa zisizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, tatu, napendekeza Serikali/Wizara hii kuwaelimisha Halmashauri zote nchini kuanza utaratibu wa kuweka Bajeti kila mwaka kwa ajili ya umeme angalau kijiji kimoja kila mwaka. Hii itasaidia sana kuongeza kiwango chetu cha umeme badala ya kungoja *TANESCO/REA* kutafuta fedha kwa ajili ya umeme pekee. Ziko Halmashauri zenyе mapato na uwezo wa kutosha kujunganishia umeme, zikihamasishwa na kueleweshwa.

Mheshimiwa Spika, nne wakati umefika sasa kwenda na kasi ya kuhakikisha *TANESCO* haifanyi kila kitu. Tuanzishe Taasisi za kusambaza umeme. *TANESCO* ızalishe tu ili kuleta urahisi wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, tano, iwe marufuku kijiji chochote

kurukwa au kutounganishwa na umeme inapotokea kuna *line* imetengenezwa, kwani kuchomwa kwa nguzo kunakotokea kwenye baadhi ya maeneo chanzo chake ni wivu wa kuona wenzao wameteremshiwa *Transforma* na hivyo wao hawana.

Mheshimiwa Spika, sita, ule mchango unaokwenda nje ya nchi pamoja na kuchakata madini kuangaliwe upya, kwani tunapoteza ajira nyngi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. SAIDI A. ARFI: Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ya kina juu ya mambo mawili.

Mheshimiwa Spika, mosi, ni lini *generators* ambazo tumekuwa tuklahidia ikiwa pamoja na Mheshimiwa Rais kusema jambo hilo. Je, ni lini sasa *generator* hizo zitapelekwa Mpanda? Aidha, nataka kujua mpango wa matengenezo ya *generator* zilizopo ambazo zinaharibika mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, wachimbaji wadogo wadogo ni wa muda mrefu, hauna ufumbuzi, matokeo yake mnapandisha ada ya viwanja na leseni ili Watanzania masikini washindwe na kuwapa wenye fedha na wageni. Eneo la mgogoro wa Mpanda ni eneo lao kuhodhiwa na matapeli na viongozi (waliokua) kumiliki eneo hilo ambalo wameshindwa kuliendeleza na kulimiliki tena kwa jina linguine, lakini ni watu wale wale.

Aidha, yapo madai na malalamiko juu ya Maafisa wenu wa madini Mpanda kushirikiana kuuza maeneo au kujimilikisha maeneo *potential*, na wachimbaji wadogo wadogo wapo tayari kuwataja na maeneo waliojimilikisha. Naitaka Wizara ishughulikie tatizo hili na kufuatilia.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mungu kwa neema ya uhai na afya njema nikiwa Bungeni. Nachukua fursa hii adhimu kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri kwa maslahi ya Taifa na watu wake.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake wote wawili kwa kusimamia vizuri Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kupandisha bei ya mafuta ya taa, ilingane na ile ya mafuta ya *diesel* kwa ajili ya kuondoa uchakachua ji wa mafuta ya *diesel*, imeathiri kwa kiasi kikubwa wananchi walio wengi hasa wale wa vijiji ni ambao ndio wahusika wakubwa wa nishati hii ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba wananchi wengi vijiji ni hawafaidiki na huduma muhimu ya umeme kwa sababu mbalimbali ikiwemo kutokufika umeme sehemu nydingi za nchi yetu, au uwezo wa wananchi kuwa mdogo kimapato na kushindwa kuutumia kutokana na gharama zake kuwa kubwa. Kwa hiyo, wote hawa ni watumaji wakubwa wa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, athari kubwa ya uchafuzi wa mazingira imekuwa kubwa sana kutokana na watu vijiji ni kutumia nishati mbadala ya kuni kwa bei kubwa ya mafuta ya taa ambayo hawaimudu. Mimi naionba Serikali, ile faida ya fedha ya mafuta ya taa ipelekwe *REA* kwa huduma ya umeme vijiji na kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadgo wa madini wamekuwa na kilio cha muda mrefu kwa kutotendewa haki katika sehemu mbalimbali za shughuli za kazi zao. Wanakosa elimu ya ufanisi kati shughuli za kazi zao, wanakosa fedha za kuwawezesha, wanakosa zana za kisasa katika uchimbaji, wanakosa soko endelevu la kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, naionba Serikali iangalie kwa makini sana wachimbaji wadogo wadogo, wawezeshwe kifedha, kielimu na nyanja zote muhimu katika shughuli zao wafanye kwa ufanisi.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza kazi nzuri inayofanywa na *REA*. Imeanza

kusambaza umeme katika Zahanati na Vituo vya Afya Jimbo la Kasulu Vijijini. Niombe mpango huo huo upelekwe katika Shule zote za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pili, nahitaji majibu sahihi ya kumaliza tatizo la wachimbaji wa chokaa Kijiji cha Makere ambaao walipewa leseni na Wizara, lakini watu wa Maliasili na Mazingira wanawazuia kuchimba madini ya chokaa. Mheshimia Naibu Waziri wa Madini analijua tatizo hilo vizuri na niombe alitolee maelezo ili vijana wenzake wapate maisha bora. Mbaya zaidi, chokaa imechimbwa tangu uongozi au utawala wa Mkoloni. Ni vyema wananchi wapewe elimu nzuri ili wanufaikie na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba wataalam wa utafiti wa madini waende Kijiji cha Nyenge Wilayani Kasulu Jimbo la Kasulu Vijijini illi kubaini madini yanayopatikana hapo kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii nami nichangie katika Wizara hii muhimu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia katika eneo la umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo ambalo litabadili maisha ya wananchi wetu wa vijijini, ni kuwapelekea nishati muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na changamoto ya muda mrefu kwamba wakulima wetu hawapati tija katika shughuli zao za kilimo, na hali hii inatokana na ukweli kwamba wanapata bei ndogo ya mazao yao kwa kuwa wanayauza yakiwa katika hali ghafi.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kuwawezesha wananchi wetu kuongeza thamani ya mazao yao ili wapate bei nzuri na faida nzuri ni kuwapelekea huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ambalo tunatakiwa tufanye ni kuimarisha Shirika la Maendeleo ya *Petrol (TPDC)*.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* ndiyo shirika ambalo linaiwakilisha Serikali kama mbia katika mikataba yote ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi ambayo inafanywa na Makampuni makubwa yenyе uwezo na maarifa ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuiwezeshe *TPDC* ili iweze kuwasimamia vizuri wawekezaji katika Sekta ya Gesi.

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika kitini cha mradi wa gesi asilia ya Songosongo ukurasa wa nne, *Equality Shareholders Preferred B TDFL \$ 4 million 8%: Je, FMO \$ 14.4 common share holding ni ngapi?* Nimejumlisha:-

<i>CDC</i>	54%	\$ 38.6M
<i>FMO</i>	?%	\$ 14.4M
<i>TDFL</i>	8%	\$ 4.0M
<i>TPDC</i>	29%	\$ 3.0M
<i>TANESCO</i>	<u>9%</u>	<u>\$ 1.0M</u>
JUMLA	<u>100%</u>	<u>\$ 61.0M</u>

Naomba ufanuzi *FMO share Equity \$ 14.4M*, lakini 0%?!

Mheshimiwa Spika, naomba mrahaba wa kokoto zinazochimbwa na *RAHCO* ya *TRL* tulipwe, kwani tangu reli ijengwe mwaka 1905 mpaka 2013, hakuna mrahaba Kijiji cha Tura. Wizara itusaidie tulipwe ili Tura ifanye miradi ya maendeleo. Mheshimiwa Simbachawene, Nailbu Waziri wa Nishari na Madini alifika Tura na kuwaahidi wananchi kwamba watalipwa. Walipwe sasa!

Mheshimiwa Spika, umeme Jimbo la Igulala, Mbuyuni, Kinamagi, Kigwa 'A' na 'B', Igulala, Imalakaseko, Goweko na Nsololo; Vijiji hivi viko kwenye mpango wa REA. Ahadi hii katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ni tangu mwaka 2000, 2005 na 2010. Naomba kabla ya mwaka 2015 umeme uje vijiji hivi na vingine vipewe kwa *solar*. Viko 50. Ahsante, Ni mradi namba 109 kwenye ramani.

Mheshimiwa Spika, *Panelya Peer Report (Cape Town Juzi)* ya Kofi Annan inasema mwaka 1998 – 2011 dhahabu iliyouzwa Tanzania ni *US\$ 11.3 billion*. Serikali inapata *U\$ 450m* hii inakuwaje? Mheshimiwa Waziri toa maelezo.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Loya, Tura, Kizengi na Malongwe pamoja na Karangasi kuna *Kimberlite pipes* za almasi kutoka ukanda wa Singida na mgodi mmoja ulifungwa wa Loya. Watafiti wako Mheshimiwa Waziri wafuatilie ili wana-Igulala wafaidike.

Mheshimiwa Spika, naomba mrejesho.

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia Wizara ya Nishati na Madini. Natoa pongezi kwa Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mrahaba wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime; naomba mgodi wa Bariadi *North Mara Wilayani Tarime* ulipe Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kiasi cha *US\$ 800,000* ambazo hazikulipwa toka mwaka 2002 – 2005. Tafadhalii nasisitiza hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, mradi wa wachimbaji wadogo wadogo ni muhimu ili kuepuka migongano isiyo ya lazima. Hivyo basi, naiomba Wizara iweke sera ya:-

(1) Kuwabaini wachimbaji wadogo wadogo hao ni akina nani?

(2) Mahitaji yao muhimu ni yapi?

(3) Ni wadogo kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikataba ya Elimu, Afya, Maji, Umeme na Barabara, nashauri wawekezaji watimize ahadi zao kama walivyowekeana na wanavijiji.

Mheshimiwa Spika, nashauri mgodi wa *Barrick North Mara* (Nyango) ulipe fidia halali kwa wananchi wa Tarime.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kukomesha mauaji ya raia yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahusiano mabaya ya mwekezaji/wananchi; nashauri elimu itolewe ili kuwaelimisha wananchi wanaozunguka migodi umuhimu wa uwekezaji. Pia wawekezaji watimize wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime ina vijiji vingi sana vipatavyo 130. Naishauri *REA* kupeleka umeme katika Kata za Bumera, Susuni, Nyandoto, Gorong'a, Nyarukoba, Bungurere, Kangariani, Getagasembe, Komaswa, Gibaso, Masanga, Kegonga na vijiji vingine vyote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii na kuileta Bungeni.

Mheshimiwa Spika, umeme ni chachu kubwa sana kwa maendeleo na kuinua uchumi wa Taifa na wananchi wote. Idadi ya wananchi wanaotumia umeme vijijini bado ni ndogo sana, inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, juhudhi bado zinahitajika kuhakikisha *programme* ya *REA* inawezesha ili umeme uwafikie wananchi wengi wanaoishi Vijijini. Pesa/fungu la *REA* lionezwe kwa kutafuta fedha pahali popote hata kwa mkopo ili miradi ya *REA* itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunayo makaa ya mawe huko Kiwira, Ngaka, Mchuchuma, na kadhalika. Ipo miradi ambayo imeanza uzalishaji wa makaa ya mawe, yanauzwa nchi za nje. Ni kwa nini makaa hayo hayatumiki kwenye viwanda vyetu hapa nchini? Ni kwa nini makaa haya hayatumiki kwa matumizi ya kupikia nyumbani?

Mheshimiwa Spika, vipo viwanda vinatumia kuni na magogo kama nishati. Watanzania zaidi ya 80% wanatumia mkaa na kuni. Nishati ya umeme ni ghali sana kupikia, mafuta ya taa hayashikiki, *gas bado* ni ghali, wengi wanashindwa kumudu.

Mheshimiwa Spika, mazingira yetu yapo hatarini, tutakuwa jangwa Taifa hili kama Serikali haitafuta nishati mbadala kwa matumzi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, gharama za malipo kwa mita za Luku ni kubwa sana ukilinganisha na gharama za mita za kawaida. Serikali itoe maelezo ni kwa nini gharama zimepanda zaidi ya mara nne?

Mheshimiwa Spika, Kata ya Usingi Wilaya ya Kaliya ina wakazi wengi sana na ni *centerya* biashara. Umeme wa eneo hili wanatumia *Alternator*. Umeme ni dhaifu sana, wakati mwingine mashine za nafaka hazifanyi kazi. Serikali ipeleke umeme wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *MCC* maeneo mengi nchini ulichelewa kutekelezwa. *TANESCO* waliendelea na kazi yao ya kusambaza umeme maeneo mbalimbali, cha ajabu wataalam wa *MCC* walipokuja wanapita kule kule ambapo tayari *TANESCO* wameshaweka umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni moja, ni muhimu kuwepo na *coordination* kwenye utekelezaji wa kazi zake. Kwa kuwa tayari *TANESCO* walishatumia rasilimali, nguvu na pesa nyingi kusambaza umeme maeneo hayo, ni kwanini Serikali ambayo tayari ina umeme mradi uhamie eneo la jirani ambalo halina umeme? Haya siyo matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi?

Mheshimiwa Spika, ni vigezo gani Serikali inatumia kupata uhakika wakati muafaka wa migodi ya madini kulipa kodi ya mapato (*corporate tax*)? Ni nani anatafiti kujua kwamba mgodi umeanza kupata faida? Haiwezekana mgodi kama Bulyankulu, Buzwagi, *North Mara*, Mwadui wanavuna madini kwa wingi kwa miaka yote hiyo! Hawalipi *Corporate Tax* eti hawajapata faida! Hapa tunaibiwa! Tunaomba maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema wameweka ukaguzi wa madini kwenye viwanja vyta ndege kabla ya kusafirishwa kwenda nje kwenye baadhi ya viwanja vyta ndege kwa mfano, *KIA*, *DIA*, na kadhalika na fedha nydingi imeokolewa.

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu gani unatumika kuangalia kiasi cha madini yanayosafirishwa moja kwa moja kutoka kwenye viwanja vyta ndege vilivyopo ndani ya migodi mbalimbali ya madini?

Mheshimiwa Spika, katika ziara ya Mheshimiwa Rais tarehe 09/01/2013 aliongea na wananchi wa Kata ya Usindi (W) Kaliua walipomsimamisha kwa vilio, wakaomba Kituo cha Afya cha Usindi kipatiwe umeme. Mheshimiwa Rais aliahidi na kuagiza pale pale kituo kile kipatiwe umeme ndani ya muda mfupi. Naomba Serikali leo iwjibuu wananchi ni lini ahadi ile itatekelezwa?

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapa pole wale wote waliokufa, kujeruhiwa na kukamatwa katika vurugu iliyotokea Mkoa wa Mtwara na natambua kuwa haki ina thamani kubwa kuliko amani kwa maana pasipokuwa na haki hakuna amani.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuishukuru Wizara ya Nishati na Madini kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha wafugaji wa Songosongo waliofiwa na mifugo yao kwa kuwalipa waathirika wote. Hongera kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naanza kunukuu: "Mwongozo wa

TANU 1971, Uchumi na maendeleo." "Maendeleo ya nchi huletw na watu "ukurasa wa 16." kwetu sisi maendeleo ya maana ni yale yanayotuondolea kuonewa, kunyonywa, kunyanyaswa na mawazo ya kufungwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kunukuu Mwongozo wa TANU 1971, napenda kuikumbusha Serikali kuwa sisi watu wa Mikoa ya Kusini tunahisi kuwa hatutendewi haki katika mambo mengi ya muhimu. Kwa lugha nyepesi tunaonewa.

Mheshimiwa Spika, mfano halisi, gesi ya Songo Songo imeanza kutumika mwaka 2004 na kuahidiwa kuwepo kiwanda cha mbolea, kuwekewa umeme vijiji vinavyopita bomba la gesi, lakini mpaka leo vijiji vya Marendego, Miteya, Matundu na Manzese Somanga hakuna umeme. Hata huo ushuru wa huduma 0.3 tumeanza kulipwa mwaka 2012. Miaka yote tulikuwa hatulipwi.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha zaidi, tangu mwaka 2004 hakuna mpango wowote wa kuvipatia umeme Viji vya Wilaya kama vile Mavuji, Kiwawa, Hoteltatu, Pande, Lilimalyao, Nanjirinji, Likawage, Mandawa, Miumba, Mtandi, Kirajeronje, na Mbwemkuru. Kwa kuwa mpaka leo hakuna mpango wowote wa kupatiwa umeme katika vijiji hivyo: Je, Serikali inasema nini kuhusu kupatiwa umeme katika vijiji hivyo. Katika majumuisho yako Mheshimiwa Waziri napenda unipatie jibu la upatikanaji umeme katika vijiji hivyo; pia lini tutapatiwa kiwanda cha mbolea *KILMCO Kilwa*?

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja mpaka njue ni lini vijiji nilivyoviorodhesha hapo juu vitapata umeme na lini kiwanda cha mbolea kitajengwa?

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuitaka Serikali ifike Mtwara kuongea na wananchi wa Mtwara. Kilichotokea Mtwara ni mambo waliyoyapata watu wa Kilwa. Watu wa Kilwa tumedanganywa na watu wa Mtwara wanajua kuwa Kilwa hatukutimiziwa yale tulioahidiwa.

Mheshimiwa Spika, ombi letu tulipwe mrahaba katika gesi, ushuru wa huduma uongezwe, napendekeza 1.5%.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia machache katika Wizara hii muhimu katika kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umeme wa gesi unaozalishwa Somanga Fungu unatumika katika Mikoa ya Lindi na Pwani hususan katika Wilaya ya Rufiji. Kumekuwepo na matatizo ya kukatika kwa umeme mara kwa mara. Je, ni kwanini umeme wa Somanga Fungu umekuwa ukikatika mara kwa mara na kusababisha usumbufu na hasara kubwa kwa wakazi wa Lindi na Rufiji wakati tunaelezwa kuwa gesi inayozalishwa ni nyangi kuliko inayotumika?

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa usambazaji wa umeme vijiji kupitia *REA* unasuasua sana, kwa mfano katika Wilaya ya Rufiji takribani robo tatu ya vijiji ambavyo vilitegemewa kupata umeme kupitia *REA* havijapatiwa umeme, mfano kijiji cha Mbunju, Mloka, na kadhalika. Je, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Je, ni lini Kijiji/Mji mdogo wa Jaribu mpakani (Rufiji) utapatiwa umeme?

Mheshimiwa Spika, Ahsante.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya Madini nashauri uchafuzi wa mazingira udhibitiwe na Jumuiya zinazoishi jirani na machimbo ya madini zilindwe, afya zao na wao pia wanufaike na madini yanayopatikana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba katika mikataba ya uzalishaji umeme haki itendeke. Mikataba itazamwe upya na irekebishwe ndani ya miezi sita. Mitambo isikodishwe tena. Katika programu ya "Big Results now" fedha za kutosha

zitengewe na Serikali ya Tanzania inunue mitambo yake na hii itumike.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TANESCO* igawanywe iwe Mamlaka ama Wakala tatu tofauti: (1) *Power Generation Agency*; (2) *Power Transmission Agency*; na (3) *Power Supply/ Provision Agency*.

(a) *Agency* namba 1, isimamie mabwawa na mitambo inayozalisha umeme ikiwemo Bomba la mitambo ya gesi;

(b) *Agency* namba 2, isimamie ujenzi wa *lines* za *high tension*, kwa mfano, usafirishaji wa umeme kutoka kwenye mabwawa hadi Mijini na Vijiji; na

(c) *Agency* namba 3, kazi yake iwe ni kuwafungia walaji umeme na kukusanya fedha za matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hii kutakuwepo na *check and balance*.

Mheshimiwa Spika, umeme wa *REA* Kiteto utekeleze ahadi ya kupeleka umeme katika kijiji cha Mbeli na Ndaleta.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwa kuwa nimetoa mchango wangu kwa kuzungumza, naomba kuongeza jambo moja au mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Serikali isiwanyamazie viongozi wa kisiasa hasa Waheshimiwa Wabunge ambao wanakubali kununuliwa na hivyo kuijingiza kwenye malumbano yasiyo na msingi na Serikali. Serikali na hasa Wizara kamwe isiwaonee haya Waheshimiwa Wabunge wa namna hii ambao baadhi pia wamekuwa licha ya kununuliwa tu, bali wamekuwa na maslahi binafsi na watu hao au wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu utekelezaji wa mradi

wa umeme wa Chalinze – Magindu – Lukenge. Mradi huu umeanza mwaka 2010: Je, utakamilika lini? Naiomba Serikali/Wizara hii iangalie mradi huu kwa jicho la karibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Naibu Waziri, Mheshimiwa Simbachawene atafuatiwa na Naibu Waziri Massele kila mmoja anapewa dakika 20, Mheshimiwa Waziri dakika 40.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uhai.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru sana wachangiaji wote. Kwa kweli yaliyosemwa kuhusiana na sekta ya nishati ni mengi na karibu wachangiaji wote waliozungumza na kuandika wamegusia suala la nishati. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naamini hawa waliopata bahati ya kusema na kuandika ni wachache, lakini wapo ambao hawakusema na hawakuandika lakini kwa hisia tu unaona namna ambavyo nishati inachukua sura ya pekee katika nchi yetu. Sisi tutakuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba tunafikia katika malengo ya sisi viongozi lakini pia malengo ya wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kauli iliyotolewa na Mheshimiwa William Ngeleja kwamba tusikatishwe tamaa na kauli za kupinga mipango ya Serikali na kubeza kila kinachofanywa na Serikali. Mheshimiwa Ngeleja, kauli hii ni kweli kwamba tunayo mipango mikubwa sana ya nishati vijijini na inafanywa na kutekeleza na Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliyopewa dhamana na wananchi wa Tanzania katika kuhakikisha kwamba inapanga programu na mikakati mbalimbali ili kuwalettea maendeleo wananchi wa Tanzania. Tutafanya hivyo na sisi hatutakatishwa tamaa na tutakuwa

begagwa bega na ye yote anayependa maendeleo katika kuhakikisha kwamba maendeleo yanafikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa ya kufanya ufunguzi wa miradi na Mheshimiwa Waziri ametuagiza mimi na Naibu Waziri mwenzangu kwamba kila mradi uliofanyika lazima tuuzindue kuhakikishia kwamba Serikali inafanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zimetolewa hoja nyngi, moja kati ya hoja zilizotolewa ni kuhusu ukamilishaji wa Sera na Sheria ya Gesi. Hili tunalitambua na ninawahakikishie wote waliozungumzia suala hili akiwemo Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Hamad A. Hamad, Mheshimiwa Fatuma Makidadi na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina na wengine wengi waliozungumzia hoja hii, sisi tumejipanga, Sera ipo tayari, Waheshimiwa Wabunge mmetoa mawazo yenu na nina hakika kwamba ndani ya mwaka huu Sera itakamilika na pengine kati ya mwaka huu na mwanzoni mwa mwaka unaokuja Sheria itakuwa tayari kwa sababu vitu hivi vilikuwa vinaandaliwa kwa pamoja. Kwa hiyo, msiwe na mashaka kwamba zitatumika Sheria au Sera gani wakati wa uuzaaji wa vitalu vinavyotarajia kuuzwa. Hapa tumefanya katika nia ya kutaka kuwahi kwa sababu tunashindana na wenzetu duniani, sisi hatuwezi tukalala hata tusizindue au tusiitangazie dunia kwamba na sisi tuna vitalu na tunatarajia kuviuza, ndiyo dhamira, lakini Sheria na Sera ndizo zitazotumika wakati huo mwakani mwezi Mei. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala kwamba kuzalisha umeme wa gesi, wapo Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa na Waheshimiwa Wabunge wengine wengi wamezungumzia suala la umuhimu wa kuzalisha umeme wa gesi ili tuweze kushusha gharama ya uzalishaji wa umeme. Nichukue nafasi hii kueleza Bunge lako Tukufu lakini niwaeleze Watanzania kwa ujumla. Leo umeme ambao tunauzalisha kwa kutumia *ma-generator* haya yanayotumia mafuta mazito na mepesi, *TANESCO* inaununua kati ya senti za kimarekani 40 - 55 lakini

endapo tutakuwa tunazalisha umeme wa kutumia gesi, tutaununua umeme huo kati ya senti 6 - 8 na kwa maana hiyo tutaokoa fedha nyingi sana. Kwa hiyo, niungane na wote waliosema kwamba gharama zishushwe, hatuna namna wala muujiza wowote Serikali wa kushusha gharama za umeme kama hatujaweza kusafirisha gesi ili tuweze kuzalisha umeme katika maeneo yote kuanzia Mtwara tutazalisha megawati 400 Mtwara na kuusambaza katika Mikoa ya Songea na Mkoa wa Lindi, lakini pia na Wilaya za jirani, lakini pia kuleta gesi hiyo ili kuweza kuzalisha umeme unaotumia gesi badala ya kutumia mafuta mazito na kuokoa hela inayotumika kwa kila siku iendayo kwa Mungu shilingi bilioni 5.5 kuzalisha umeme na badala yake tutatumia kiwango kidogo kuliko hicho. Kwa hiyo, hapa nadhani wala haihitaji uwe na *Masters* wala *PhD* kujua *economics* hizo namna zinavyokaa. Kwa hiyo, nikubaliane na wote walioitia moyo Serikali, tuendelea na suala la kuhakikisha kwamba gesi inakwenda kuzalisha umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini picha isiwe kwamba gesi kazi yake ni kuzalisha umeme tu, gesi ina mazao mengine mengi sana. Gesi yenyewe inatumika kwa kupikia majumbani, gesi yenyewe inatumika kama nishati viwandani, gesi inatumika katika kuzalisha mbolea ya ammonia na vitu vingine, ni vitu vingi sana vinavyoweza kutokana na gesi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hapa isizungumzwe gesi kama ni kwa ajili ya kuzalisha umeme tu. Hapa nipende kujibu hoja ya Mheshimiwa John Mnyika aliyesema kwamba gesi inayosambazwa Dar es Salaam ni ya kubeba kwenye mitungi. Sisi tunazungumzia gesi ya kusambazwa kwenye mabomba ili watu wafungue majumbani, wanapikia gesi, ndicho tunachokizungumza siyo kusambaza ile *LPG* inayosambazwa, hiyo ndiyo dhamira ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine lilirozungumzwa hapa ni suala la kwamba kujengewe mitambo ya kusafisha gesi kule kule Mtwara. Tumekuwa tukisema hili mara nyingi na tumesema sana, mitambo ya kusafisha gesi itajengwa hapo gesi ilipogundulika, huna muujiza, huwezi kuisafirisha gesi kabla hujaisafisha. Kwa hiyo, mitambo ya kusafisha gesi

inajengwa Madimba Mtwara na treni nne zenyе uwezo wa kubeba *cubic* milioni fiti za ujazo 70, 70 na pia Songosongo na kwenyewe hivyo hivyo kutajengwa mitambo ya kusafisha. Kwa hiyo, ni kauli tu za watu wasiopenda kuelewa jambo hili, sijui ni kwa makusudi au vipi ndiyo wanalirudia mara nyingi, lakini sisi tunasema mtambo wa kusafisha gesi unajengwa Mtwara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa hapa ni suala la elimu kuhusu manufaa ya gesi asilia kwa jamii. Ni kweli sisi Wizara tumejitahidi kufanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo lakini nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote, wanasiasa na viongozi wote wa kijamii, elimu hii haiwezi ikatolewa na Wizara tu. Kama wewe umeelewa kazi yako na wewe ni kwenda kumwelewesha ambaye hajaelewa. Inashangaza unapomkuta aliyeelewa na naye anasema watu hawaelewi, wewe uliyeelewa umefanya jitihada gani katika kutoa hiyo elimu kwa wasioelewa? Kwa hiyo, hili jukumu ikipewa Wizara tu kwamba Profesa Muhongo na Wizara yake ndiyo tufanye kazi hiyo, hatutaweza. Mimi niwaombe sana, ambao mmelewa walipo ndani ya Bunge na nje ya Bunge twende tukawaelimishe wenzetu ambao hawajaelewa ili tuweze kutunza amani ya nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la hapa la umeme katika Wilaya mpya 13. Niwahakikishie Wabunge wote wenye Wilaya mpya 13 ikiwemo ya Chemba na Wilaya zingine mpya zote, Buhigwe zote zilizotajwa, tupo katika mkakati na hii imewekwa katika miradi inayosimamiwa na TANESCO na REA na yote itagharamia karibu bajeti ya shilingi bilioni 71 na fedha ipo katika hii iliyopo katika vitabu, itaanza kutekelezwa kwenye Wilaya hizo mpya ili na wenzetu twende sambamba tunapozungumzia usambazaji wa umeme vijijini. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wote wanaotoka katika Wilaya mpya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini limezungumzwa suala la maeneo mengine Mheshimiwa Mturura amelisema kwamba je, tuna mipango gani ya kuboresha umeme kwenye maeneo

ambayo hayako-connected na gridi. Jamani, ni mpaka pale tutakapokuwa na uwezo wa kuzalisha umeme na umeme ambao kwa sasa ni wa haraka ndani ya miezi 18 ni wa gesi. Tukiwa na uwezo tukatia ndani ya gridi usambazaji huu ni kazi nyepesi. Niseme tu kwamba kutokana na mradi utakaojengwa wa megawati 400 Mtwara, *lineile* itatoka pale kupitia Wilaya hizo kwenda mpaka Songea, hatutaruka, kila tunapopitisha huo umeme na *hapo tunashusha* na kwa hiyo mnaachana na *ma-generator*, huo ndiyo mpango wa Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia limezungumziwa suala zima la ucheleweshwaji wa kuwaunganisha wateja na hili limesemwa na Wabunge wengi ambalo linafanywa na *TANESCO*. Nichukue nafasi hii kuwaomba sana, ni kweli kwamba tuliposhusha bei ya kuunganisha umeme kwenye majumba, tuliposhusha toka mwezi Januari, 2013 mpaka leo hii mwezi Mei, 2013, wateja karibu 90,000 wameomba kuunganishiwa umeme na tumewaunganishia umeme wateja zaidi ya 50,000, kuna wateja karibu 26,000 ambao hawajaunganishiwa umeme. Changamoto hii tumeambana nayo, sasa hivi vifaa vimeshuka na vifaa vitaanza kusambazwa katika Mikoa yote na Wilaya zote, na tuna hakika kwamba tutawasambazia umeme. Natoa mwezi mmoja tu kwa Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa kuhakikisha kwamba wakipokea vifaa hivyo kila mtu mwenye *backlog* ya wateja ambao wameomba ndani ya mwezi Juni na Julai wawe wamekwisha wote kuunganishiwa umeme. Kwa sababu vifaa viro na vimeingia, tunazo nguzo karibu 65,000 ni nyngi sana na vifaa vingine vyote viro msiwe na wasiwasi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa James Lembeli amezungumzia kuhusu umeme wa Kahama na kwamba *option* ile ya kuunganisha na Buzwagi tunakubali na Serikali imechukua hatua kali sana. Tumezungumza na Buzwagi, tumekubaliana kituo kile tunashirikiana sasa kiwe kikubwa sana na sasa badala ya kutoka Ibadakuli sasa tutachukulia pale ili tusambaze umeme katika maeneo yale. Hiyo pia haitasaidia kitu kama haitaenda sambamba na ubadilishaji

wa nguzo na vifaa vyote kutoka Shinyanga hadi Kahama. Lazima tubadilishe na hiyo ipo kwenye mpango na itatekelezwa katika mwaka 2014. Kwa hiyo, Mheshimiwa James Lembeli na Mheshimiwa rafiki yangu Ezekiel Maige msiwe na wasiwasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Iakini nizungumzie suala la ucheleweshaji wa miradi ya *REA* na miradi ya *MCC*. Hilo limesemwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Lucy Mayenga, Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijiini na Waheshimiwa Wabunge na wengine wengi wamesema kwamba ucheleweshaji huu tumekubaliana na Wakandarasi hawa kwamba mwisho ni mwezi Septemba, kama mwezi Septemba, watakuwa hawajamaliza bora tuvunje hiyo mikataba. Tumefanya hivyo kwa sababu ya *complication* ya utekelezaji wa miradi, inaweza ukute fidia ililipwa kwa njia hili, Iakini unakuta mradi unatakiwa upite hapa, mnaanza *negotiation* upya. Kwa hiyo, ucheleweshaji nao una sababu nyingi tu. Kwa hiyo, niwaombe sana hadi mwezi Septemba, hakuna mradi wa *MCC* au *REA Phase 1* utakaokuwa haujatekelezwa na itakuwa imekamilika na kukabidhiwa. Tumekubaliana kwa maandishi na Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyine ni kwamba Serikali ianzishe miradi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Tumezungumza miradi kwa maana ya viwanda, tumezungumza miradi kwa maana ya kuweka centre kwa ajili ya biashara mbalimbali zinazotokana na mazao yatokanayo na gesi na kwamba pale Mtwara na Lindi mpaka sasa viro viwanda. Pale Lindi kuna kiwanda cha sementi tayari na sementi inapatikana pale na bei yake ni tofauti kabisa na bei ya sementi huku kwingine. Pale Mtwara kuna kiwanda cha Dangote, nimesikitika wakati huyu anayejenga kiwanda hiki anashusha vifaa pale Mtwara wananchi hao wanaosema kwamba lazima viwanda vijengwe, makontena karibu zaidi ya 15 yanashushwa pale, Waziri wa Viwanda na Biashara anayapokea, wananchi wanazomea. Sasa tunajiliza wanajua wanataka nini? Wamesema wanataka viwanda, jitihada ya Serikali ya kujenga viwanda inafanyika, watu wana-mobilize kuleta vifaa *site*, wananchi badala ya

kufurahia wanazomea. Mimi ninasema hii elimu tujitahidi wote, isije ikawa wengine tunatoa elimu na wengine wanaharibu elimu inayotolewa. Sasa hapo lazima tuwe makini kuona ni nini hasa ambacho kipo kwa sababu viwanda viro. Tumetenga eneo la *industrial pack*, tumekwenda mara chungu nzima. Mimi nimetumwa na Waziri wangu wangu, Mheshimiwa Mwakyembe, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Kigoda tumefanya pale hadharani, tumezungumza na vyombo vya habari, wananchi wanaona, tunaongea na *local media* wananchi wanaona. Kwa nini jamani elimu tunayotoa wananchi wanaona kwa macho, ujenzi wa viwanda Dangote, maeneo yaliyotengewa ya *LNG* bado inasemekana elimu haifiki. Tujitahidi sote kutoa elimu. Mimi nakubali lakini tujitahidi sote kutoa hiyo elimu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kushirikishwa katika uamuzi wa masuala ya huduma za jamii (*cooperate social responsibility*), hili tunalifanya, Mheshimiwa Anne Kilango alilizungumzia, Mheshimiwa Khalfa Sulemain Khalifa amelizungumzia, ndiyo maana tumeiweka katika sera. Kwa mfano, kwenye Sera ya Gesi tunesema *cooperate social responsibility* iwekwe katika sera maana yake itasemwa pia katika sheria, kwa hiyo, hili lisiwape mashaka. Katika sekta ya gesi mikataba iliyopo ni mizuri na ni ya *production sharing agreement*, Serikali ikiwakilishwa na *TPDC* inaanza kupata kutoka siku ya kwanza uzalishaji unapoanza, siyo kama mikataba inayotumia *formular ya concession*. Hii ya *production share agreement* ni mikataba mizuri na mara nydingi sana tumekuwa tukijaribu kwa kweli kupambana sana katika kuitetea kwa sababu mabeberu wasingependa iwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, *REA* itengewe fedha za kutosha ili iweze kutekeleza miradi yake, hili limesemwa na watu wengi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Shaffin Sumar, rafiki yangu Mheshimiwa Gosbert Blandes, akiwemo Mheshimiwa Charles Mwijage, sisi tunakubali. Sisi tunasema na Mheshimiwa Waziri wangu atalisema hapa, katika shilingi bilioni 881 tunazozihitaji katika kutekeleza miradi hii, tuanze

hata kwa kupata shilingi bilioni 450, kazi itaanza na tutaweza kutekeleza miradi kadri ambavyo tutaweza kwenda kwa sababu miradi hii yote haiwezi ikatekelezwa siku moja ikaisha siku moja. Kwa hiyo, msiwe na mashaka, Serikali imekubali kilio chenu na wamesema na Kamati ile ya Bajeti imefanya kazi nzuri, naipongeza sana Kamati yako imetuweka vizuri na tunakwenda vizuri, tutakubaliana na naamini Kamati ile ni nzuri na itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lilirozungumzwa hapa ni kuhusiana na suala zima la umeme vijiji kwa maana ya vijiji ambavyo vimeachwa, watu wengine hawajaridhi, havijakaa sawa, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ukiwepo na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika vile vijiji vyako unavyovitaja, nimekaa nimeongea na wataalam wamenihakikishia kwamba hakuna jambo gumu. Kwa sababu fedha zile zikiwepo, tukaanza kutekeleza mradi, *adjustments* zinawezekana kwa kushauriana na wadau na Mbunge ndio mdau namba moja, leteni mawazo yenu, tutayazingatia na tutatekeleza mnavyotaka hata kwa kuangalia vipaumbele mnavyovitaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Mwijage amezungumzia umeme kwenye Kata zake, hii itakuwa *very specific*, lakini Mheshimiwa Mwijage nikuhakikishie mambo yako ni mazuri, unatusaidia sana Kamati kufanya kazi na sisi tunakubaliana kabisa kwamba tutafanya kazi hiyo vizuri kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini amezungumzia Kampuni ya Mafuta ya Taifa kama ndio mwarobaini na kwamba lazima Serikali ya kisasa iwe inafanya biashara na ndio Serikali za wajanja wote duniani zinafanya biashara, sisi tuiseme tu Serikali isifanye biashara. Tunakubaliana, tunachukua wazo hilo na tunalfanya kazi na jitihada zipo na tuna hatua tulizozifikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* umeme wa ghali. *TANESCO* umeme ghali ni kwa sababu ya gharama za uzalishaji, ikiingia gesi unashuka na umeme utakuwa bei rahisi,

hatuna njia yoyote ya haraka zaidi ya gesi ikiingia kuzalisha umeme tutaona gharama ya umeme inashuka na hivyo hakuna tena tatizo katika hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi kuleta neema kwa wananchi, hili nimeshalizungumzia. Serikali ianze uwekezaji wa viwanda mbalimbali Mtwara, hili nimelizungumzia. Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Serikali ihakikishe kuwa bomba la gesi ya kutoka Mtwara/Dar es Salaam linajengwa tumesema lazima ijengwe. Kwa hiyo, nasema wenzetu watuelewe tu kwamba dhamira ni nzuri na watakuja kujuta baadaye kwamba kwa nini walikuwa wanachelewesha maana manufaa ni ya watu wote bila kubagua anatoka sehemu gani.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme vijiji hili limezungumzwa na watu wengi na hili nimelizungumzia, upungufu wa bei tayari Mheshimiwa Madabida alisema na wengine walisema. Lini mradi wa Kiwira utafunguliwa, hili jambo linaendelea vizuri *STAMICO* tumewaweka pale Mheshimiwa Godfrey Zambi na tumeshalipa fidia zote. Kwa hiyo, sasa hivi mgodi wa Kiwira unamilikiwa na Serikali, kwa hiyo, kwanza tulirejesha sasa ndio tuanze na shughuli hizo zingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hassan Ngwilizi alizungumzia kuhusu bei ya nguzo, nimesema katika suala hili kwamba *TANESCO* hawaazi nguzo, *TANESCO* wanaweka umeme kulingana na umbali wa mahali ambapo umeme unatakiwa kupelekwa. Kwa hiyo, niwaombe wenzangu wa *TANESCO* hebu neno nguzo, nguzo liondoke kwenye misamiati ya *TANESCO*, tuzungumzie umbali kama ni mita 60 gharama yake ni hii, kama ni mita 120 gharama yake ni hii. Kwa sababu mita ndizo zinazosema waya kiasi gani, vikombe kiasi gani, sasa ukianza kusema nguzo, mbona husemi vikombe, mbona husemi waya tuondoke kwenye huo msamiati tuzungumzie umbali uliopo kati ya anayehitaji kuwekewa umeme na umeme unapotoka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Arfi, alizungumzia

bei ya umeme iwe Sh.99,000/= maeneo yote, tutaendelea kulifiria lakini tulishusha bei hapa na imeweza kuleta matokeo makubwa ambapo tumepata walioomba wengi kuliko tulivyotarajia mpaka wengine tunashindwa kuwahudumia, ingawa tunakubaliana tutawahudumia tu ndani ya miezi miwili tutahakikisha wote wamekwisha nchi nzima, watu wawe wanaenda pale analipia siku hiyo hiyo kesho yake anawekewa umeme, ndicho tunachotaka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, amezungumzia pia habari ya jenereta za Mpanda, Biharamulo, Ngara, ni kweli, siku nilipokuwa najibu hapa swali, niombe radhi kwamba ulimi ultereza, jenereta ilikuwa inashushwa Ngara maeneo ya Rulenge, sasa nilipojua ni Rulenge nika-*generalise* lakini ukweli ni kwamba mradi huu utatekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha na tunahakikisha kwamba jenereta hizo zinafungwa katika Wilaya za Mpanda, Biharamulo na Ngara. Suala la kwamba zilikuwa mbili sasa ni moja, ni moja kwa sababu uwezo wake sasa ni mkubwa kuliko hizo mbili za awali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo limezungumzwa ni mpango wa kuweka umeme wa *solar* katika shule za sekondari na vituo vya afya. Hili tunalisema na nirudie kusema dhamira ya mradi wa *REA* ni kuboresha maisha ya watu wa vijijini. Huwezi ukasema umeboresha maisha kama hujapeleka umeme kwenye zahanati, shule za msingi au sekondari na hujapeleka umeme kwenye kisima cha maji. Kwa hiyo, *priorities* za *REA* na mimi nataka niliseme hili, ni kwamba mnapoingiza umeme kwenye kijiji hakikisheni kwanza umefika sehemu hizo ndio watu wengine wafuate. Haina maana kama tunafikisha umeme kwenye vijiwe watu wanacheza pale karata na *pool*, tunataka uende kwenye huduma za jamii, kwa hiyo, hayo ndiyo malengo ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Naibu Waziri, Mheshimiwa Maselle kwa dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE): Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi nichukue muda mfupi sana kukushukuru wewe binafsi, napenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini kwa maandishi na kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia niwashukuru Wakuu wa Nchi, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Gharib Bilal, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa miongozo mbalimbali ambayo wamekuwa wakitupatia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuishukuru Kamati ya Nishati na Madini kwa ushauri na michango waliyoitoa na napenda pia kuishukuru Kambi Rasmi ya Upinzani kwa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge nikijielekeza zaidi kwenye hoja ya *service levy* ambayo imezungumzwa kwa uchungu sana na Waheshimiwa Wabunge. Kwa haraka tu, kwa kuwataja majina Mheshimiwa Ezekiel Maige amezungumzia hili, Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Cecilia Paresto kule Karatu, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na Waheshimiwa wengine wote. Waheshimiwa Wabunge wote wanafahamu kwamba Bunge lako mwaka 1982 lilitunga Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ikizipa mamlaka Serikali za Mitaa kuanzia kwenye Mamlaka za Miji, Halmashauri za Miji mpaka vijiji kuweza kujikusanya mapato ambayo yatatumika kwa shughuli mbalimbali za maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, jukumu hili kimsingi ni la Serikali za Mitaa lakini kwa kuwa baadhi ya wadau wanaohusika na kudaiwa kodi hizi ni makampuni ya madini, ni wazi

kwamba Waheshimiwa Wabunge wana kila namna na haki ya kuuliza Wizara ya Madini inawasaidiaje kuhakikisha kwamba wanapata fedha hizi. Mwaka jana tulianza kufuatilia kwa karibu sana eneo hili la madini na kuangalia namna gani makampuni ya migodi yamekiuka, nitumie lugha ya kukwepa lakini hayakulipa *service levy* kwa mujibu wa sheria hii niliyoitaja kwenye Halmashauri mbalimbali nchini. Tulifanya hivyo kwa ushirikiano wa karibu sana na Wabunge wa Nzega wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na Mheshimiwa Selemani Zedi na Halmashauri nzima ya Nzega na tuliweza kufaulu kupata mapato haya zaidi ya shilingi bilioni 2.3 ambazo ziko kwenye Halmashauri ya Nzega.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna madai mengine ambayo Halmashauri ya Nzega wanayo, mimi wito wangu ni kwamba wafuate tu taratibu zilezile kwa sababu ni wajibu wao kudai. Sisi Wizara ya Nishati na Madini tutatoa ushirikiano wote wa taarifa sahihi ambazo watazihitaji na tutatoa *forum* hiyo ili waweze kupata haki yao wanayostahili.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa James Lembeli kwa kazi kubwa ambayo wameifanya pia kwa kufuata njia ileile ya Halmashauri ya Nzega tumeweza kwenye kikao ambacho tumekifanya tarehe 22 baina ya Halmashauri ya Kahama ikiongozwa na Waheshimiwa Wabunge hawa pamoja na Mkurugenzi, mgodi wa Barrick umekiri kwamba kuna *service levy* haikulipwa kuanzia mwaka 2001 mpaka 2005 kiasi cha jumla ya dola za Marekani milioni moja, wamekiri watazilipa hizi kwenye Halmashauri ya Kahama dola milioni moja lakini hivyo hivyo kwenye Halmashauri ya Tarime watalipa kiasi cha dola laki sita ambazo ni za tangu mwaka 2001 mpaka 2005. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Iakini kuna madai mengine ambayo Halmashauri ya Kahama imeyaleta na Mheshimiwa Mbunge ameyazungumza. Tulichofanya tumechukua

takwimu zile ambazo kimsingi wamezitoa kwenye ofisi yangu na tumezi peleka rasmi kwenye migodi hii na wao waka-*verify* baada ya hapo nitasimamia kikao hicho kuhakikisha kwamba Halmashauri zote zinazodai *service levy* zinapata mapato yao kwa mujibu wa sheria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *service levy* si tu kwa migodi, naomba nitoe wito kwa Halmashauri zote kwa sababu Waheshimiwa Wabunge pia ni Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani wahakikishe kwamba shughuli zinazofanyika kule kwenye sheria inasema kabisa "*any corporate entities*" ziko *corporate entities* nyingi zinafanya shughuli kwenye Halmashauri zetu na zenyewe zina wajibu wa kulipa *service levy* kwa mujibu wa sheria ambayo ni 0.3% ya *turnover*.

Mheshimiwa Spika, sasa yako makubaliano baadhi ya maeneo ambayo ndiyo yalikuwa msingi mkubwa wa malalamiko ya Mheshimiwa Maige kwamba mikataba iliyofungwa ilisema italipa dola laki mbili, lakini kwa hoja za msingi na mazingira na mahitaji ya Halmashauri zetu na kasi ya ukuaji wa miji yetu, tunashawishi migodi hii iweze kuridhia kulipa kwa mujibu wa sheria na waweze kuwalipa Halmashauri ya Kahama. Naomba niliweke wazi, Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla hatuwezi kuvumilia ukwepaji wowote wa kulipa kodi zinazostahili kwenye Halmashauri na ndio maana tumesimamia kwa karibu na kwa nguvu zote kuhakikisha Halmashauri zetu zinapata mapato.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine napenda nilzungumzie katika eneo hili ambalo Halmashauri zetu zimenufaika, Halmashauri ya Geita mwaka jana ilipata 1.4 *million dollar*, fedha hizi wako kwenye mazungumzo ya kukubaliana wajenge miradi ya kusambazia maji katika mji wa Geita. Mradi mkubwa ambao unajengwa na mgodi wa *GGM* wa kuyatoa maji Ziwa Victoria na kujenga *reservoir* ambayo sasa hatua ya pili itakuwa ni kuyasambaza maji katika mji wa Geita. Kazi hiyo inaendelea na ni matumaini yetu mwisho wa mwaka huu kazi hiyo itakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa James Lembeli amezungumza hapa *ABG* kwa mara ya kwanza inaanza sasa kutekeleza miradi ya kujenga barabara. Itajenga kilomita tano katika Mji wa Kahama na hizi zote ni juhudini za Waheshimiwa Wabunge hao kwa kushirikiana na Wizara kuhakikisha kwamba migodi hii inatambua sasa mchango wao katika jamii ambazo wanafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo katika Wilaya ya Tarime wameweza kujenga shule mbili ambazo zilikuwa zikilalamikiwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wa Tarime, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine pamoja na Mheshimiwa Esther Matiko, shule hizo nina hakika sasa hivi zitakuwa zimekamilika ama ziko kwenye hatua za mwisho za ukamilishaji. Wamejenga kituo cha afya na wamekarabati shule za msingi katika Wilaya ya Tarime na kuweka madawati mapya. Nzega pia wamepata shilingi 2.3 billioni wanazifanya nini, ni matumaini yetu kuwa fedha hizo walizopata watazitumia vizuri kwa manufaa ya wananchi wote wa Nzega.

Mheshimiwa Spika, watu wengi wamezungumzia mgawanyo wa rasilimali za nchi. Wote tunafahamu, kodi mbalimbali zinazolipwa kutoka kwenye sekta ya madini labda tu kwa uchache nizitaje, watu wengi wanaangalia mrabaha kama ndio kodi pekee lakini naomba nizitaje kwamba Serikali inapata kodi nyingi ikiwemo *corporate tax*. Kuanzia mwaka 2005 mpaka sasa jumla ya shilingi bilioni 444 zimelipwa Serikalini kama *corporate tax, PAYE* kuanzia mwaka 1999 jumla ya shilingi bilioni 415 zimelipwa Serikalini, *withholding tax* zimelipwa shilingi bilioni 146, *Skills Development Levy* jumla ya shilingi bilioni 90, *VAT* na kodi zingine shilingi bilioni 117, *sub total* ya yote hii ni zaidi ya shilingi trillioni 1.2 lakini *total* ya jumla yote ni shilingi trillioni 1.6 zimelipwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, mrabaha ni sehemu pia ya mapato ambayo Serikali inayapokea kutoka kwenye

uwezekaji huu wa madini. Mtakumbuka kwamba na hapa nijibu tu hoja ya Mheshimiwa Mnyaa kwamba kuna 2.5 bilioni kwenye ripoti ya CAG imeonesha kwamba hazikulipwa Serikalini. Mtakumbuka Sheria ya Madini ilifanyiwa marekebisho mwaka 2010 ikaanza kazi Novemba, 2010. Baada ya kuanza kazi kipindi hicho toka Novemba 2010 mpaka 2011, ndio kipindi ambacho Mheshimiwa anakizungumzia lakini migodi hii iliweza ku-*migrate* kutoka kwenye 3% ambayo walikuwa wakilipa *royalty* kwenda kwenye 4% ilipofika Mei 2012. Sasa kipindi cha mwaka 2010 mpaka 2012, huu mwaka mmoja wa 2011, Serikali wakiwepo watangulizi wetu waliokuwepo ofisini Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Malima walianzisha kazi hii na Katibu Mkuu Bwana Maswi ya kujadiliana na migodi ku-*migrate* kutoka kwenye 3% kwenda kwenye 4%. Sisi tulipofika pale tukaweka mkazo kukamilisha kazi ile na kuanzia Mei Kampuni zikaanza kulipa 4% ya *royalty* na si tu kwamba wamelipa wanalipa *under protest*. Kwa hiyo, hata sasa wanaendelea kulipa 4% na sisi kusema kweli tuliamua kufanya kwa makusudi kwamba mapendekezo ya sheria ile yatekelezwe. Kwa hiyo, kwa kuwa mikataba waliyofunga MDAs zile ziliwu zinatamka 3% na mabadiliko ya mkataba hayo ndio tunaendelea kuyajadili.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wanajiuliza mikataba hii tunai-*review* vipi? Katika hatua za ku-*review* mikataba hiyo na ndio hapo tulipofika kwenye ku-*review* eneo hili la *royalty* na kuwaambia kwa sheria zetu za sasa mnapaswa mlipe asilimia nne ya mapato yote mnayopata. Kwa hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako kwamba migodi hii kuanzia Mei 2012 imekuwa ikilipa 4% ya *royalty* na kiwango hiki tofauti ya asilimia tatu iliyokuwa ikilipwa kwa mwaka jana tumeweza kukusanya shilingi bilioni 30 kama nyongeza baada yaku-*migrate* kwenda kwenye 4%.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumzia *incentives*, mtakumbuka kwamba pamoja na kuwa Wizara ya Nishati na Madini inasimamia sera pamoja na Sheria ya Madini, lakini inapokuja masuala ya majadiliano haya, maeneo ya kodi haya yaliwekwa makusudi na yanasisimamiwa

kikamilifu na Wizara ya Fedha na *incentives* hizi zilikuwa ni sehemu ya *package* katika Sera yetu ya Uwekezaji kuangalia namna gani Serikali itashawishi wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu. Sasa kwa kuwa wawekezaji wanakuja na Tanzania imejulikana kwamba ni kitovu na kituo cha uwekezaji, Serikali itazingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuangalia katika *incentives* hizi kuzipunguza ili tuweze kunufaika zaidi na mapato yanayotokana na madini. Kwa kufanya hivyo, wale ambao tunaendelea kufanya kazi mkataba wa MKUJU mnaweza kuona Serikali imekuwa inachelewesha mkataba huu kwa sababu tunataka maeneo ya kodi lazima Taifa linufaike zaidi na eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia akiwepo Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Serikali imeamua kwa makusudi kabisa kuwatambua wachimbaji wadogo lakini naomba nikiri, ukiangalia taarifa mbalimbali zilizoko Wizarani, maeneo ya nchi yetu mengi yalikuwa yameshikiliwa na leseni mbalimbali. Ukiangalia ramani karibu maeneo yote yamekuwa *covered* na leseni. Sasa wachimbaji wadogo wanataka leseni Serikali inaitoa wapi eneo la kuwapa. Mheshimiwa Arfi amezungumza hapa kwamba wameenda kutengewa maeneo mapya, ndiyo maana Wizara ikafikiria kwamba tufanyeje ili tuweze ku-*unlock* nchi iwe wazi kwa baadhi ya maeneo ili tuweze kuyatoa kwa wachimbaji wadogo na ndio msingi wa kuongeza pia hizi ada za leseni.

Mheshimiwa Spika, unakuta mtu mmoja anamiliki leseni zaidi ya 200 peke yake, sasa mtu yule ameshikilia Wilaya nzima, Wilaya hiyo ina wachimbaji wadogo na Serikali inapaswa itoe leseni kwa wachimbaji wadogo, unatoa wapi eneo hilo. Mfahamu kabisa leseni ni *document* ya kisheria, mwenye leseni ana haki zote za kisheria, ukimnyang'anya kwa nguvu atakushtaki. Kazi ambayo tunafanya ni kutafuta *mechanism* ambayo hao wanaoshikilia maeneo makubwa washindwe kuyamudu wayaachie na tumefanya hivyo na

matokeo yake ndio tumeppata baadhi ya maeneo kwa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, napenda hilo lieleweke kwa nini tulikuwa tunafanya hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa maeneo ya Kahama ambayo kwa historia ni muda mrefu yamekuwa yakiaminika kuwa na madini pamoja na Kilindi, taarifa za madini ziko katika ofisi zetu za *GST*. Watu wengi wana *access* na taarifa hizo. Kwa hiyo, wanakwenda kwenye maeneo ambayo ni *hot spot* kwenda kukamata maeneo yale na bahati mbaya sana wachimbaji wetu hawakufahamu hizi sheria kwamba anayewahi kupewa leseni ile ya utafiti ndio ana haki tayari ya madini, ile *minerals rights*. Sasa wewe ambaye ulikuwa unachimba kwa sababu ni shamba la babu, shamba la bibi, maana yake huna *mineral rights* na hii iko wazi kabisa, mwenye *kiosk* hawezি kufanya biashara ya *kiosk* kama hana leseni. Kwa hiyo, hata mwenye madini ni lazima akachukue leseni ili aweze kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara tumeimarisha Chama cha Wachimbaji Wadogo kote nchini, wana uongozi kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa mpaka Taifa tunayajadili haya kwa kina na tunatafuta ufumbuzi wa matatizo yao kwa namna ya kudumu. *STAMICO* ndio itakuwa inashughulika na wachimbaji wadogo na tunaendelea kuangalia *model* mbalimbali ni namna gani tutakuwa na *model* ambayo itaiwezesha *STAMICO* kuweza kuwa na *agent* wa kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo na *agent* yule aweze kulipa kodi na *royalty* na kodi zote kwa mujibu wa sheria ili aweze kuwa mkusanyaji wa mapato ya Serikali. Kwa hiyo, tunaendelea kutafuta mbinu mbalimbali kuweza kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo nao wanachangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mambo ya mikopo, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia uwepo wa *TIB* Dar es Salaam. Naomba niseme kwamba hakuna aliyetangaza *TIB*, tulitangaza zabuni ili tuweze kupata benki ambayo itaweza kusimamia fedha hizi kwa wachimbaji wadogo. Mambo ya mikopo ni taaluma na taaluma hii inasimamiwa na mabenki. Kwa hiyo, Serikali iliamua kwa makusudi kupeleka fedha hizi

kwenye benki ili ziweze kusimamiwa kama ilivyo *funds* zingike kama Mfuko wa JK. Kwa hiyo, niseme tu kwamba mchakato wa zabuni ile unaendelea na unafanyika kwa uhuru na sisi Wizara tunaendelea kusubiri matokeo ya zabuni hiyo atakayeshinda ndiye atakayekuwa na fedha hizo na kuweza kuwashudumia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Mayenga amezungumzia utoroshwaji wa madini na nimwambie Mheshimiwa Wenje amenkuu taarifa kutoka sijui kwenye taasisi gani. Niseme kwamba sisi Tanzania kwa mujibu wa Sheria, 2009 Serikali iliunda hiki chombo cha *TMAA*. Baada ya kuunda *TMAA* imefanya kazi nzuri sana, haya madeni yote ya nyuma tunayozungumza, *TMAA* ndiyo iliyoyaibua.

Mheshimiwa Mnyaa amezungumzia *TEITI*, *TEITI* iko kidunia kama *EITI* lakini Tanzania na sisi ni wanachama na inafanya kazi nzuri ya kukagua na kuhakikisha kwamba kasoro zote zilizopo kwenye madini tunaweza kuzibaini na kuzitafutia suluhu hapohapo. Niseme tu kwamba bila kujua kasoro, huwezi kupata tiba ya tatizo. Serikali kuitia *TMAA* na Wizara ya Nishati na Madini tumeweka mitego mbalimbali kwenye *airport* zetu na sehemu mbalimbali za mipaka. Nataka niwahikikishe Waheshimiwa Wabunge hata Wabunge wengine humu wamekamatwa na mitego yetu na wamenipigia simu kuniomba, Mheshimiwa vijana wako wamenishika hapa na madini, mimi nimenunua ya kuvaan mwenyewe, naomba unisaidie nipite. Sasa ukiangalia kweli unakuta Mheshimiwa kanunua cheni zake za *Tanzanite* pale Arusha anataka kuja Dar es Salaam. Nawaambia mwachenii Mheshimiwa haendi kufanya biashara wala hafanyi biashara ya madini. Kwa hiyo, nataka kuwaonyesha tu kwamba Serikali iko makini na mitego ipo na kama unabisha ukitoka hapa nenda *airport* chukua madini ficha, utashikwa. Hao wote ambaao wamekuwa wakikamatwa tangu tumeweka mitego hii tumeweza kuokoa shilingi bilioni 13/- ambazo zilikuwa zinotorosha. Kwa hiyo, kuna jitihada kubwa sana inafanyika kuhakikisha kwamba sekta hii inaendelea kuimarika na Serikali inapata mapato yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, viwanja hivi nya ndege, hata mimi zamani nilikuwa nikifikiri kwamba Wazungu wale wanaruka tu kule wanaondoka kwenda nje. Kuna *regulations* nyingi sana ili ndege itoke nje ya nchi. Hakuna ndege inatoka tu kwa kuwa imeruka inaweza kwenda popote. Ndege lazima iongozwe kutokea chini. Kwa hiyo, ni fikra tu kwamba ndege ikitua uwanjani inaondoka. Ndugu zangu, viwanja vile vimewekwa kwa ajili ya *security*. Una *gold* kilo kumi unaishisha na gari kutoka Kahama kwenda Dar es Salaam? Haufiki. Kwa hiyo, viwanja vile vimewekwa kwa ajili ya *security* ya kuondoa mali ile kutoka sehemu ambayo imehusika na vituo vile vyote vina *TRA*, kuna vyombo vyetu nya ulinzi na usalama pamoja na Wakaguzi wetu wa *TMAA*, wote wako pale kuhakikisha kila kinachozalishwa kinakuwa *recorded* na kodi inalipwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ntukamazina na Mheshimiwa Blandes wamezungumzia mradi wa Kabanga Nickel na Mheshimiwa Wenje alizungumza utafiti tangu miaka ya 1970. Hii ni kazi ya kisayansi, huwezi kukopa fedha za kuendesha mradi wa mgodi wa zaidi ya dola bilioni laki tano, hauwezi ukapewa fedha kama huwezi kuonyesha mashapo ya kile ambacho unaenda kukifanya. Kwa hiyo, kazi hii imekuwa ikifanyika kwa muda mrefu kwa sababu ina gharama kubwa na makampuni haya mengine yamekuwa yanaafilisika yanaachia njiani, mwingine ananunua anaendelea lakini kwa taarifa tulizonazo sasa hatua ziko mwishoni, wana-*finalize* hizo *feasibility study* na mradi ule utaanza. Kuna changamoto zaidi upande wa Serikali. *Nickel* ni madini mazito, yanahitaji reli kuyasafirisha, yanahitaji umeme sio chini ya *megawatt* 40kuendesha mgodi ule. Kwa hiyo, kuna changamoto za kimiundombinu ambazo na zenyewe zimekuwa kama *setback* kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Niwahakikishie kwamba timu yetu ya majadiliano ya Serikali tayari imeshaanza kazi ya majadiliano na *Kabanga Nickel* kwa ajili ya mkataba na tutazingatia maslahi ya Taifa ili mradi huu uweze kuanza kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nizungumzie *CSR*.

Tunafanya jitihada kubwa kama Serikali kuhakikisha kwamba makampuni ya migodi yote, suala la *CSR* sio la hiari. Tunayashawishi kuwa na mfuko maalum ambaao kila mwaka migodi hii itaweka *fund* kule kwa ajili ya huduma za jamii. Wote mtakumbuka kwamba uwepo wa mgodi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE): Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo kidogo hapa. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba baada ya kuahirisha kikao hiki watakuwa na kikao chao chumba namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho tarehe 26 kuanzia saa nne asubuhi kutakuwa na semina kwa Wabunge wote itakayohusu Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo. Semina hii itafanya katika ukumbi wa Pius Msekwa. Wabunge mna tabia ya kuchelewa kufika, kwa hiyo mnakuta watu wako *half way* halafu mnakosa mwanzo.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azzan, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo hii jioni kutakuwa na mechi ya kirafikiri ya mpira wa pete kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge na timu ya vijana ya Dodoma. Mechi hizo zitachezwa katika uwanja wa Jamhuri Dodoma kuanzia saa kumi kamili jioni.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kwenda kuishangilia timu yenu.

Mheshimiwa mtoa hoja!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, niwashukuru Wabunge mawazo yenu ni mwanana, tumeyachukua na sisi tunachukua mawazo ya pande zote mbili ya Wapinzani na ya CCM kama ni mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kama nilivyofanya mwaka uliopita, safari hii nimeleta wataalam wangu wa TANESCO wa kila Kanda Tanzania. Hawa watakaa hapa mpaka Jumatano, saa mbili mpaka saa kumi na mbili kwenye ofisi yetu ya Madini ambayo iko nyuma ya *Dodoma Hotel*. Kwa kuwa muda ni mfupi, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, dukuduku nydingi hatutazijibu hapo lakini nendeni pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nimeleta Maafisa wa Kanda wa Madini wa Tanzania nzima, wako hapa na niliwaambia waje na orodha ya wachimbaji wadogo kwenye Kanda zao zote na narudia kusisitiza, wachimbaji wadogo hawalipi kodi. Sasa kama mtu nauli ya kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ni Sh.20/- na ye ye hajawahi kusafiri kwenda Morogoro, ukiongeza ukaweka Sh.30/- ana haki gani ya kujadili nauli hiyo, hata kusafiri hajawahi kusafiri. Hao wote wanaotetea hizi kodi, mtagundua kuna baadhi yetu Watanzania wana maeneo karibu Wilaya nzima. Hakuna mtu anayeongelea wachimbaji wadogo hapa, wengine ni biashara zao tu. Hiyo mkitaka tutaweza kuthibitisha kwa kutaja makampuni na mtu na maeneo walijonayo. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Wataje!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Haitoshi hapa, kule wako wataalam wangu, nendeni kule.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sipendi kuongelea hili la Mererani lakini kwa sababu Mheshimiwa Rais ametajwa inabidi nitoe ufanuzi. Mheshimiwa Ole-Sendeka wapigakura wako Simanjiro wamekusikia lakini uliyosema yote si kweli. Tulikaa mimi na wewe Arusha ukarudia hili la Mheshimiwa Rais kutoa ahadi na bahati nzuri Mkuu wa Mkoa wa Simanjiro alikuwepo, nikamuuliza Mkuu wa Mkoa wa Simanjiro akaangalia kwenye daftari la ahadi...

SPIKA: Mkoa gani?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Samahani Manyara, hakukuta ahadi ya Mheshimiwa Rais. Sasa ndugu zangu Watanzania Mheshimiwa Ole-Sendeka anataka tumsikilize, tukune kichwa hapa wakati Mkuu wa Mkoa wa Manyara hana hiyo ahadi. Isitoshe kwa kuwa nilikuwa naenda kwenye hicho kikao mimi mwenyewe nikampigia Mheshimiwa Rais simu, nikaongea naye, Mheshimiwa Rais akanambia wasiniwekee maneno mdomoni mwangu, Rais hakutoa hiyo ahadi. Sasa mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ole-Sendeka unayoyasema mimi msimamo wangu na wa Wizara ni huohuo Rais hakutoa hiyo ahadi.

Mheshimiwa Spika, isitoshe basi ukaja kwangu una wazo Halmashauri ipewe hisa. Mimi nikasema sehemu ambapo migodi ipo tukianza kila Halmashauri kuchukua hisa ndio kuigawa nchi. Je, Halmashauri zisizokuwa na madini? Nilikataa hilo wazo na Watanzania mnaonisikiliza hapa mna imani na Halmashauri zenu kwa matumizi ya fedha?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Sendeka akanijia na kikundi cha watu wanaanzisha ushirika. Mimi nikamwambia hivi mnaweza kuanzisha ushirika kwa ajili tu ya *Tanzanite* hii? Kwa hiyo, ndugu zangu niachie hapohapo. (*Kicheko/Makofii*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Kuhusu Utaratibu!

SPIKA: Tuko kwenye majumuisho utaratibu hauruhusiwi.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Sasa ni uongo.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hili la Buhemba, ninaomba Mwenyekiti wa wachimbaji Mkao wa Mara na Mwenyekiti wa wachimbaji wa Buhemba ambapo juzi nilikuwa naongea nao najaribu kuwatafutia eneo. Ukweli wa sheria unasema, huwezi ukatoa leseni juu ya leseni, hivyo ndiyo sheria inavyosema ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, hili eneo wamepewa *STAMICO* kisheria, wana leseni, sasa nitatoaji leseni juu ya leseni? Badala yake nimejaribu kuwatafutia eneo na nimetuma watu na nikasema natuma na ma-*geologist* wa *Geological Survey* kabla hilo eneo hawajapewa wale wachimbaji wahakikishiwe kwamba kuna chochote kama alivyosema Mheshimiwa Mama Shellukindo nilimwomba *CEO* wa *Geological Survey* na kweli tutampelekea ma-*geologist* kule. Haya mambo tunayoyangea hapa ndugu zangu hata kama humpendi mtu au hupendi ukweli si maneno ya porojo ni ya uhakika. Kwa hiyo, hili la Buhemba nimewatuma kule wawatafutie na nikawauliza watu wa Buhemba kwani nyie lazima mchimbe hapohapo au mko tayari kwenda Mkao mwingine? Wakasema hayo maeneo mliyotenga tuko tayari kwenda. Vilevile nimemwomba Mwenyekiti wa wachimbaji wa Mkao wa Mara, namwomba na nadhani ananisikia na Mwenyekiti wa wachimbaji wa Butiama waje kwangu ofisini niwaonyeshe kampuni ambazo zimekosa hilo eneo na sasa linataka kutuvuruga, watasoma wataniachia *document*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa hotuba ya

Kambi ya Upinzani. Wametumia muda mwingu sana kuongelea juu ya Mwalimu Nyerere. Ndugu zangu Watanzania mnaonisikia na wengine ambao sisi ni wanafunzi wazuri tulimwelewa, Mwalimu maandiko yake yalikuwa ya sehemu tatu. Kwanza, ilikuwa ubinadamu na utu, ndiyo maana lilitokea Azimio la Arusha. Mkienda Butiama nendeni kwenye Library yake mtaona Mwalimu alivyokuwa anasoma. Sehemu ya pili ilikuwa ni ujenzi wa Taifa. Ilikuwa ni utaifa na uzalendo na sehemu ya tatu ilikuwa ni kusahihisha uongozi, haya amekuja kuandika baadaye sana. Sasa kama wewe unataka kumwelewa Mwalimu vizuri, huwezi ukashika theluthi moja tu ya mwisho ya kusahihisha uongozi. Kwa hiyo, kama ni maksi kwa sababu ana sehemu tatu na wewe umejibu theluthi moja, una 33.3, wewe ni *fail*. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, vitu viwili muhimu kabisa kwa Mwalimu na kwa umri wangu ambao tulikwenda sekondari ulikuwa unakuta kwenye madarasa, kwenye mabweni yetu, Mwalimu anasisitiza kwa wale wenye bahati ya kupata hii elimu, *those who have the privilege to receive education*, hawa ni watu sawasawa na watu wanaopewa chakula kilichoko kwenye kijiji chenye njaa ili wale wapate nguvu watembee, waendee mbali wakaleta chakula kwa wanakijiji wasiokuwa na chakula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania wote niwakumbushe, mtu aliyekula kile chakula akaenda hakurudi Mwalimu alisema ni Mhaini, *Traitor*. Kwa hiyo, yote yanayotokea sasa, kama wewe ulipata elimu, unaenda unawadanganya wanavijiji wewe ni Mhaini. Kama wewe ulipata elimu, unazunguka kwenye makampuni unakusanya fedha, wewe ni Mhaini. Kama wewe ulipata elimu, makampuni yako yakikosa kazi unaanza vurugu wewe ni Mhaini. Hiyo ndiyo *statementya kwanza ya Mwalimu*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini shule niliyosoma mimi, Mara Secondari ilikuwa inaitwa *Musoma College* ilikuwa ya Wamarekani, *Neil Armstrong Apollo Mission 11* ilivyotua

mwezini ilikuwa ni tarehe 21/7/1969, mimi nilikuwa *form one* na nilikuwa shule ya Wamarekani na walituletea *film* inamwonyesha Armstrong anatua mwezini na *statement* ambayo Armstrong aliitoa ni hii hapa, " *That's one small step for man; one giant leap for mankind.*" Hatua ndogo lakini maendeleo kwa mwanadamu. Mwalimu alikuwa mjanja sana na sijui kama wengi wanasoma, mwaka huohuo alitueleza akasema, wengine wakienda mwezini sisi twende vijijini. Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote mimi nimeleta bajeti ya kwenda vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mambo ya rasilimali kwamba Mwalimu alisema zisitumike, ni uongo na makosa. Mwaka 1969 ndijo alianzisha Shirika la Mafuta la Petroli (*TPDC*). Kama Mwalimu alitaka rasilimali zisitumike, kwa nini alianzisha shirika hilli? Mwaka 1972 alianzisha Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*). Kwa hiyo, ndugu zangu ninaomba tuwe wanafunzi wazuri wa Mwalimu na tujaribu kusoma vitabu vyake kwa undani zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hapohapo kwa kuwa tunaenda vijijini ni suala la *REA*. Ndugu zangu bila umeme vijijini hakuna maendeleo. Dira yetu ya Maendeleo ya mwaka 2025 itafanikiwa ikiwa wanavijiji watatumia umeme. Mambo ya fedha tumeyasikia, sio ya kwangu peke yangu, ni ya Serikali nzima, hili jambo tutakwenda kulitafakari na ushauri wenu tumeuchukua tunashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye huohuo umeme nataka niwaombe na nyie Waheshimiwa Wabunge mtusaidie. Sisi tuko hatua nyngi mbele sana, hatulali pale Wizarani. Tumevida mahesabu ya kuweka umeme shule zote za Tanzania na zahanati na vituo vyaya afya vyote, tukafikia hesabu ya kupata shilingi bilioni 2.2 *USD*. Kwa hiyo, sasa tusingoje tu Serikali, nawaomba nyie Wabunge kwa kuwa na nyie ni Madiwani, muanze kwenye Halmashauri msikae tu kungoja Serikali, itatuchukua muda, kama tulivyofanya kwenye shule.

Mheshimiwa Spika, *REA* wamepiga hesabu, kuweka umeme kwenye shule yenye madarasa nane inahitaji milioni 3.9, karibu milioni nne, kwa nini Halmashauri zetu zisijé kuomba *REA* zina milioni nne mkononi, vijana wakawekewa umeme na *dispensary* zetu zikawekewa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile tumepeiga hesabu kuweka umeme kwenye Zahanati na vituo vya Afya ni karibu milioni 13. *REA* iko tayari kwa sababu ni ya Serikali, tafuteni hizo hela njoo ni Wizarani au nendeni moja kwa moja *REA*, kama wakikataa kuwawekea umeme msiwape posho kwa sababu watakuwa wana posho ya Serikali, basi mtakuja kuniambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo hapo tuna miradi mingi ambayo itakuja, kwa mfano, *MCC* ndugu zangu tusijidharau *program* yetu ya umeme ni katika *programs* ambazo zinaheshimika sasa hivi na ndiyo maana tumeshinda miradi ya Marekani *MCC one* na *MCC two* na ndiyo maana *European Union* wamekuja hapa kufanya mazungumzo na sisi tuwe nao pamoja kwenye mambo ya umeme. Serikali ya Marekani *focus* yao/ushirikiano wao na sisi ni juu ya umeme. Kwa hiyo, ndugu zangu tutatumia njia zote, kuhakikisha umeme unawafikia wanavijiji (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, nije kwenye kutengeneza bajeti, ndugu yangu upande wa Kambi ya Upinzani bajeti za karne hii na karne inayokuja zina *formular* moja ndogo, lakini nzito. *Economic prosperity in the 21 Century and beyond, equation* hiyo inasema ni sayansi ukijumlisha teknolojia, ukijumlisha ubunifu, unajumlisha mtaji, unajumlisha na rasilimali watu, *the Economic prosperity of the 21 Century equals; Science plus Technology plus innovation, plus financial capital, plus Human Capital.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuanzia hapa nawaomba Watanzania wanaonisikiliza, itakuwa ngumu mengine mtasahau, nawaombeni mlipo mchukue kalamu na karatasi.

WABUNGE FULANI: Ahaa!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Watanzania walioko huko nje, nyie Wabunge kama hampendi acheni, lakini Watanzania kwa sababu haya ndiyo yatatoa mengi.

Ndugu zangu CHADEMA, nasema kwamba, mapato yangu yote kwenye bajeti yangu, fedha za ndani zinazokwenda kwenye miradi ni 98%. Wewe ukija hapa kama unatengeneza bajeti nzuri, ni lazima uje na tarakimu inayopingana na hii au inayokubaliana na hii siyo ya maneno. Nasema kuwa miradi ya maendeleo kwenye bajeti yote itachukua 90% na mengineyo 10%.

Mheshimiwa Spika, ukiwakilisha bajeti ya kileo *contemporary budgets* ni lazima uje na tarakimu inayopingana na hiyo siyo maneno. Kwa maneno mengine, bajeti iliyowasilishwa hapa ya upande wa pili, wao wanasema kuwa *Economic Prosperity* kwa karne ya 21, nisikilize vizuri, ni sawasawa na porojo, unaongeza kesi zisizokwisha, unajumlisha matusi, unajumlisha upotoshaji, halafu unajumlisha uchovu wa kitaaluma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu nawaomba CHADEMA mkajifunze, hata wafadhili wenu wakawafundishe kutengeneza bajeti, nenda ukafuatilie Mabunge yote, nenda Bunge la Marekani, Bunge la Uingereza, bajeti wanakwenda na tarakimu zinazokinzana, siyo mwingine analeta tarakimu wewe unaleta porojo, haiwezekani! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije uchumi wa Tanzania, hapo ndipo nilisema kuwa kuweni na kalamu ndugu zangu, ni lazima dira yetu ya maendeleo ya mwaka 2025 itufanye tuwe na uchumi shindani. Sasa nataka kuthibitisha kwa nini lazima tuwe na uchumi shindani na kwa nini sisi tulileta hii bajeti.

Mheshimiwa Spika, nachukua pato la mtu mmoja mmoja kwa baadhi ya nchi. Kwa mwaka jana, GDP *per capital* Tanzania sasa hivi ndio dola za Marekani 599 karibu

600, Kenya ni 977, Uganda ni 589 na kwa kuwa wao mafuta yakianza wataruka na kutuzidi sasa sisi tulishiriki katika harakati za kulkomboa Afrika, sikiliza nchi ambazo tulizisaidia.

Mheshimiwa Spika, Zimbabwe *GDP per capital* ni 756, mbali ya vita yote wanatuzidi, Msumbiji *GDP per capital* ni 650 wanatuzidi, South Afrika wamekuwa *trained* sehemu nyingi, wao ndiyo wakubwa, ni dola 7507, Shelisteli wakati nilipokuwa Seychelles, Mheshimiwa Ngwilizi unaheshimika sana pale, mwagine alinitambulisha kuwa wewe ni *President* wa Seychelles, wenyewe wana dola 11,226, Djibouti, Kisiwa kidogo ni dola 1,523, wanatuzidi sisi. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Vyama vyote nchi hii muda wa porojo na siasa umekwisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaongelea uchumi na maendeleo na ndiyo maana ukinitajia hapa mlolongo wa kesi ukategemea, nikafukue yale mafaili Wizarani, nadhani kuwa kwanza ni Mbunge wa kuteuliwa, nikapewa Uwaziri, nadhani hawakunituma pale kupekua mafaili. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu mtu una ushahidi na vyombo vya dola viro, nenda mbele kama alivyosema Mheshimiwa Mwijage kuwa vitu tuvimalize. Haliwezi kuwa Taifa, wewe unapata mtoto wako leo hii mpaka anamaliza shule ya msingi unaongelea kitu hicho hicho, anaingia mpaka ana-graduate unaongea kitu hicho hicho, hiyo ni *stagnation* ya ajabu sana, *stagnation of minds*.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna *energy mix*; umeme wetu utatokana na gesi, makaa ya mawe, *hydro* (maji), juu, upepo, joto ardhi pamoja na *bio energies* kama mabaki ya miwa.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kugusia mambo ya bomba, ndiyo maana nilisema muwe na kalamu vizuri. Umeme ambaao tunanunua sasa hivi na hii siyo siri, siyo kwamba Serikali inaficha, mtu mwagine atasimama hapa atasema wamechukua hela wamepeleka *TANESCO*, sasa ultaka tubaki gizani?

Mheshimiwa Spika, *Economy* gani inakufanya wewe unazuia *TANESCO* isipewe fedha, hiyo ni *primitive economy*. Ni uchumi upi unafanya *TANESCO* isipewe fedha kuzalisha umeme. Ni vitu vya ajabu sana na sisi hatufichi, tunawapatia na ni fedha za walipa kodi na mnasikia kuwa Mheshimiwa mmoja alisema umeme ukiwepo *inflation* inashuka. Sasa mwininge anasema tukae gizani. Sasa hawa ni baadhi ya wale ambao labda wana biashara za majenereta au biashara za mafuta, ni hawahawa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna kampuni saba ambazo zinatuuzia umeme. Tuli- *sign* mkataba wa kujenga bomba mwaka jana China, Septemba 2011. Tumepiga hesabu toka tuweke sahihi ya kujengewa bomba, Septemba 2011mpaka tarehe 22 ambapo hapa wengine wanasema muwasikilize, mpaka tarehe 22 juzi tulivyoahirisha Bunge, mafuta yaliyotumika ni pesa za Marekani millioni 596.49.

Mheshimiwa Spika, toka tuweke mkataba mwaka jana Septemba mpaka juzi hapa ndugu zetu wanafanya matatizo tarehe 22, katika mafuta tumetumia pesa za Marekani milioni 596.49, ni sawasawa kwa fedha za kwetu Triliioni 940.66,

WABUNGE FULANI: Ni bilioni.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: *No, no* hizi ni milioni 500 dola za Marekani, sasa Tanzania zinaingia kwenye matrilioni.

SPIKA: Haya sawa ni kiasi kikubwa.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, mtatafuta *exchange rate*, hii ndiyo *figure* nilipiga *anyway*, lakini bado itakuwa ni zaidi ya hiyo, labda niongee kwa dola, hii *conversion* ina matatizo.

Mheshimiwa Spika, tumepiga kuanzia sasa hivi kuanzia mwezi ujao, Juni bomba letu tunesema litakamilika Desemba mwakani. Angalia mafuta tutakayotumia, ni fedha za

Kimarekani Triliuni 1.44. Sasa ndugu zangu, Mwanasiasa mtu wa uchumi anayepinga bomba, unashangaa ye ye amesoma uchumi upi na ameusomea wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa niwaambie vile vile umeme wa maji ndiyo wa bei nafuu sana, lakini unahitaji fedha zaidi, umeme *unit* moja ni senti kati ya tatu mpaka tano, lakini wenyewe ni *capital intensive*; umeme wa gesi ni kati ya senti sita mpaka senti nane, umeme wa makaa ya mawe ni kati ya tano mpaka sita. Umeme wa mafuta Naibu Waziri alisema kuwa, ni senti 31 mpaka 55. Je, watu wako tayari kuachana na senti 55 warudi sita?

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo ndugu zangu njia pekee ya kukuza uchumi ni kuwa na hili bomba na hesabu zinaonesha hapa, hata ukila porojo bado hesabu zinakusuta hizi kwamba, tutakuwa na vitu vizito sana.

Mheshimiwa Spika, wengine nadhani Kambi ya Upinzani ilisema mikataba ije hapa gharama hizo siyo za kweli. Tumekwenda vile vile ku- *search* bomba letu ni kilomita 542, ujenzi wa kilomita ni milioni 1.31.

WABUNGE FULANI: Ni shilingi au dola?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Ni dola nimeona shilingi zina matatizo maana zinabadilika *conversion* zinabadilika. Halafu hii ni *International Business we have to quote in Dollars. (Makofî)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bomba kwa kilomita, halafu kwa kipenyo kwa milimita *USD per millimeterya* kwetu ni 1,426 ambalo wanasema la bei mbaya. Tukaenda Mabara mengine, hivi kweli tumedanganywa? Hawa wapiga maneno wanasema sijui tumeibiwa, sijui Wanasheria hawakuwepo.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda bomba moja, Marekani wanayo mengi, la *Texas* tumechukua la umbali wa kilomita 172.8. Wakati ujenzi wa kilomita moja sisi ni 1.31 milioni

wao ni 1.61 milioni. Halafu ule ujenzi wa dola kwa kilomita kuendana na kipenyo, wao ni 1,759, sisi ni 1,426. Tulivyotoka Marekani tukaenda Bara la Ulaya, tukachukua bomba lililojengwa na *Ope/ya Ujeruman*i, kilomita 470.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kilomita moja ni Dola za Marekani milioni 2.98, la kwetu msisahau ndiyo maana nilisema Watanzania wanaonisikiliza wachukue kalamu, la kwetu ni milioni 1.31, ukichukua kwa kipenyo hili la Ujeruman i la kwetu ni Dola 1,426, wao ni Dola 2,124. Tukaingia Bara la Asia; kuna bomba linajengwa katika Iran na Pakstani litakwisha mwakani na kwa kuwa bado linajengwa kwa hiyo, hawajakamilisha mahesabu.

Mheshimiwa Spika, wao kwa kilomita moja ni katika ya *USD in millions* 1.35 mpaka 1.91. Halafu kwa kipenyo ni 1,427 mpaka 1,784. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanaonisikiliza, hawa wanaopiga kelele kuwa tumedanganywa, tumefanya nini, ni walewale ambao walitumwa miradi yao haikushinda, sasa wanatuchafua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mitambo ya kusafisha gesi tulisema inabaki kule kule Lindi na Mtwara, hesabu za kujenga mtambo wa kusafisha gesi Songo Songo - Lindi itachukua milioni 151.74 Dola, nimesema niko kwenye *International currencies*, *USD* milioni 151.74 na kule Mnazi Bay tutajenga huko huko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtu anayetia propaganda kuwa gesi itasafirishwa na nini, ni vitu ambavyo tumevieleza mara nyingi. Ya Mtwara itakuwa ni Dola za Kimarekani milioni 197.87. Kwa hiyo, ndugu zangu, huu ni ujenzi ambao unahitaji fedha. Je, ni sisi wenye hapa duniani tumeanza kuwa na haya mabomba?

Mheshimiwa Spika, nimechukua mabomba matatu marefu duniani kote; bomba la kwanza liko China na linaitwa *North East Pipeline*, linatokana Jiangjin mpaka Shanghai. Kwa nini wamejenga bomba kutoka huko wakaleta kwenye

Center ya uchumi Shanghai, si ndiyo center ya uchumi ya China? Hii ni kilomita 8,656 kwa hiyo zetu za 542 ni kama mchezo, kilomita 8,656. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, bomba linalojengwa kati ya Bolivia na Brazil bado ukiangalia uchumi wa Brazil na Bolivia, Barazil iko katika nane bora kiuchumi duniani sasa hivi, ni katika nchi iliyoingia kwenye matrillioni ya *GDP*. Kwa hiyo, bomba la kutoka Bolivia kwenda Brazil, kilomita 4,960, bado hapa wametumia akili wanatoa bomba huku, wanapeleka kwenye uchumi mkubwa na sisi hapa Tanzania kwa sasa hivi Dar es Salaam ndiyo inatumia nusu ya umeme wote tunaozalisha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la tatu ni lile la Ulaya ambalo ni la kilomita 4,172.8. Kwa hiyo, ndugu zangu uchumi wote duniani wa gesi unakwenda na mabomba hakuna mahali kwenye gesi hakuna bomba, msidanganywe haipo duniani hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Afrika labda sisi Tanzania tunakosea, sehemu zingine Afrika wako makini. Mabomba mawili yanayojengwa Afrika; moja linaitwa *Trans-Saharan* linatoka Nigeria mpaka Algeria na kule unajua Algeria, Tunisia na Egypt wamejenga mabomba yanapita *Mediteranian Sea* yanapeleka gesi Ulaya. Hayo yapo ni ya siku nyingi mengine yana miaka 20, 30 siyo mapya.

Mheshimiwa Spika, lakini hili *Trans-Saharan* inayotoka Nigeria mpaka Algeria ni ya kilomita 4,128, wenzetu Waafrika wanajenga hilo. Mnigeria anajenga anataka kuuza gesi yake, lakini Mtanzania hutaki gesi yako uitumie kwenye uchumi.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni *West African Gas pipeline*, linatoka Nigeria linakwenda Benin linaingia Togo na mwisho wake ni Ghana, kilomita 678. Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge na Watanzania, niseme kwamba, bomba hili ndiyo litakuja kutoa umaskini nchini. Yeyote ukimsikia anapinga hili bomba, huyo siyo mwenzetu. Huyo atakuwa anawatumikia

watu wengine au anatumikia makampuni mengine. Ndiyo maana nimewapatia hizi fedha za mafuta, mjue ni fedha kiasi gani kama Taifa tutaingia hasara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Taifa letu sasa hivi unakua kati ya asilimia sita mpaka asilimia saba, lakini tumeweka dira yetu ya maendeleo ambayo inasema kwamba, ifikapo mwaka 2025, tunataka kuwa nchi ya kipato cha kati (*Middle income country*). Sasa pale kuna *layerstatu*, kuna wale wa juu, wale pato lao la Taifa kwa mtu kwa siku ni zaidi ya dola elfu kumi na mbili, wanakuja wa kati na wa chini. Chini kabisa ni kati ya dola 1250 mpaka 4800.

Mheshimiwa Spika, tuchukulie sisi tunakuwa wa chini kabisa hapo. Tuchukulie tunataka kwenda dola 3,000 na sasa hivi pato letu ni dola 6,000, inabidi lazima tuzidishwe mara tano. Inamaanisha uzalishaji wetu ni lazima uzidishwe mara tano. Inamaanisha umeme tunaoutumia sasa hivi ni lazima uzidishwe mara tano, ndiyo maana ya uchumi huo.

Mheshimiwa Spika, kama tukifika mwaka 2025, sisi ni nchi ya kipato cha kati, hesabu zinaonesha ni lazima tuwe na umeme siyo chini ya megawati 10,000, ndiyo maana niliwaambia tunatengeneza bajeti ya kwenda karne ya 22. Tunaanza sasa hivi kujitayarisha kutengeneza megawati 10,000, lazima hizo megawati 10000 uanze sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, huko tunakokwenda tukipata vyanzo vingine, kama vile katika makaa ya mawe tukapata umeme, hata umeme wa maji hatujasema kwamba hatutaki, ila hali ya sasa ya *climate change* inaonesha kwamba tusivuke nyuzi mbili, lakini huku Indian Ocean tayari tupo kwenye *one degree Celsius* na kuna sehemu zingine ndani ya Tanzania wameshavuka nyuzi mbili. Kwa hiyo, hatusemi kwamba maji hatuyataki, lakini tunasema kwanza tutulie, tuendeleze vyanzo vingine, ili tutakopofika huko tuwe na umeme ambaa unaweza ukatufanya tukafika huko.

Mheshimiwa Spika, lakini kufika huko, nimesema uchumi wetu sasa hivi unakua kwa asilimia sita mpaka saba,

tunapigana ili ifikapo mwaka 2015 uwe umeshafika asilimia nane na huwezi ukafika huko bila umeme wa uhakika. Anayepinga tusiwe na umeme wa uhakika, siyo mwenzetu huyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda kwenye nchi za kipato cha kati, sasa hivi *GDP* yetu ilikuwa 25, yaani pato la mwaka dola, naona shilingi zitakuwa nyangi kutamka, dola ni rahisi kidogo. Kwa kuwa, pato letu sasa hivi limetoka dola za Kimarekani bilioni 23 kwenda mpaka bilioni 28, lakini tutakapofika mwaka 2025 kama kweli tunataka kufuta umaskini na kama kweli sisi ni nchi ya kipato cha kati, ni lazima pato letu la Taifa livuke dola bilioni mia moja. Kwa hiyo, namaanisha uchumi tulionao sasa hivi inabidi tuzidishe mara nne, ndiyo dira yetu ya maendeleo iwe na maana kama tulivyokuwa tumekusudia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, ndiyo maana sisi Wizara na Serikali tumeamua kulisuka upya Shirika la Umeme la Taifa. Hata kama una rafiki yako pale alikuwa anakupatia fedha siyo mambo ya ubinafsi haya ni mambo ya Taifa. Kuisuka *TANESCO* haimaanishi tunamchukia mtu. *TANESCO*imeundwa mwaka 1964, lakini wazazi wa *TANESCO* wamekuwepo toka ukoloni mwaka 1931.

Ikiwa toka mwaka 1931, mwaka 1964 mpaka sasa hivi, ni asilimia 21 tu ya Watanzania wana umeme, tena ambao hautabiriki, umeme ambao tunagombana, umeme ambao kila mwaka mnafukuza Mawaziri, nadhani kama Taifa itakuwa ni vitu vya ajabu eti Taifa huo ndiyo mtindo wetu wa kuendesha Serikali wa kila mwaka tunagombana, tunafukuza, nadhani ndiyo maana tumedhamiria kulisuka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, safari tumeianza tarehe 30 mwezi huu, Menejimenti na Bodi nimewaambia, hivi ninyi wenyewe, mkitaka *TANESCO* ibadilishwe mnataka iwe na sura ipi? Watnipatia ripoti yao na watalaam wangu Wizarani wameshanipa ninayo.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri tumetafuta hela *Africa Development Bank* na tumetia wenyewe *terms of reference*, tutapata *document* tatu. Lakini hatuwezi kulibadilisha Shirika ambalo lina madeni mengi, tumetafuta fedha *World Bank*, watatupatia jumla ya dola milioni mia tatu, (milioni mia mia mara tatu). (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tumekwenda *African Development Bank*, tumpata milioni mia mbili, zote hizo ni dola. Kwa hiyo, Wabunge na Watanzania, hapa tunapoongea ndiyo maana nasema siongei vitu vya maneno, ni vya vitendo, ninazo dola milioni mia tano kuibadilisha *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* tunawaachia vitalu kule chini, mwininge anasema mmeacha kwa sababu ya Wachina, nadhani ilikuwa kwenye *speech*, sasa na wewe tuseme umetumwa na nani na Mwingereza? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hatuwezi kupata faida kama *TPDC* haiwezi kufanya biashara ya kuchimba na ya mafuta haiwezekani! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaeleza Wabunge kwamba, safari imeanza, tarehe 30 Mwezi huu watanipatia ripoti, Menejimenti na Bodi, Wizarani wameshanipa, tumpata *grant* za *African Development Bank*, siyo mkopo ni *grant* ya ku-transform *TANESCO* na *TPDC*.

Mheshimiwa Spika, nimefika mwisho niseme tu watu walioandika riwaya nyingi za mambo ya vifo walisema kwamba binadamu hafi na wengine wanaulizwa ukifa utaenda wapi? Anasema nikifa sitakwenda mbali, nitakuwa nimepumzika chumba jirani, lakini nawaangalia mnayoyafanya. Ndugu zangu Watanzania, Mwalimu anatuangalia, Karume anatuangalia, Kawawa anatuangalia na Sokoine anatuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sokoine alitoa msemo mmoja, alisema: "Kwenye nchi hii kuna watu hawajafanya kosa lolote, hawajatufanya bayo lolote, lakini nao hawajawahi kufanya zuri lolote, akasema watu hao hawafai". Sasa kila Mtanzania anayenisikiliza ajipime mwenyewe. (*Makof/ Kicheko*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:
Mheshimiwa Spika, Naafiki. (*Makof*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA: Mwongozo wa Spika.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management...* ... Sh. 8,505,134,000/=

MWENYEKITI: Ndiyo mshahara wa Waziri, mkiwa *brief and nice* mtapata nafasi wengi, Mheshimiwa Chenge!

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Katika hatua hii tunapitia mafungu ya Wizara hii, nimesimama kujaribu kuiomba Kamati yako ione umuhimu wa kusikiliza kauli na maombi ya Wabunge wengi waliochangia katika hoja hii hasa kwenye eneo la umeme vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mtoa hoja mwenyewe na kama tunavyofahamu sote kwamba umeme ni uchumi, umeme ni kichocheo cha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kushawishi Kamati yako kwamba, nilipochangia nilisema mahitaji ya REA kwa

mwaka ujao wa fedha ni bilioni mia nne na hamsini. Tunafahamu uwezo wa bajeti yetu ndiyo huo, lakini nilibahatika kuwa Mwenyekiti wa Kamati yako ya kutafuta vyanzo vipyta vya mapato, nashukuru pamoja na Wajumbe wengine tulifanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, tunaamini yale mapendekezo yakichukuliwa na Serikali katika maeneo mawili, upande wa simu za mikononi ile miito tu kupiga simu. Tuiachie Serikali kuhusu viwango, hiyo ndiyo kazi ya Serikali, watakapoleta sisi ndiyo tunaweza kusema hapa jamani muongeze au mpunguze. Lakini ule msingi wa maeneo ambayo tunafikiria tunaweza tukapata pesa, tukapaleka kwenye *REA*, lakini tusisahau pia tupeleke kwenye Mfuko wa Mawasiliano Vijijini. Msingi kwenye eneo la simu, lakini pia katika miamala ya kutuma na kupokea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini pale tutapata pesa nyingi, tumevida mahesabu tunajua. Kwa hiyo, nashauri Serikali waliangalie eneo hilo, kwa mahesabu tunaweza tukapata very *easily* pesa ya kutosha kupeleka kwa Wakala wa Umeme Vijijini lakini pia kwa Mfuko wa Mawasiliano Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunaliona na hapa napenda niwe muwazi kabisa kwamba, Serikali imewekeza sana kuitia Bunge hili katika ujenzi wa barabara. Mwaka 2007 nilipobahatika kuwa Waziri wa Miundombinu, tuliongeza tozo ya mafuta kwa shilingi mia mbili. Hii imetufikisha hapa tulipo, lakini tunaamini kwamba tunaweza pia tukaongeza tozo kwenye mafuta kwa kiwango ambacho kimesemwa, tuiachie Serikali. Naamini tukienda mpaka 100 au 113 tupo sawa, kwa *inflation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukichukua siyo yote iende kwenye barabara, sehemu moja iende kwenye barabara na sehemu nyininge iende kwenye *REA*, tutafika vizuri tu. Ahsante sana.(*Makof*)

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Wakati nikichangia

nilizungumzia kuhusu kero kubwa inayowapata wananchi wa Kahama na hususan wananchi wa Kahama Mjini kuhusu kukatikatika kwa umeme kwa sababu ambazo zimekuwa haziridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kama hayatatolewa maelezo mazuri ya kuwafanya wananchi wa Kahama waelewe kwamba, Serikali ipo, sikuwa tayari kuunga mkono hoja. Lakini kwa moyo wa dhati kabisa, majibu yaliyotolewa na Waziri na Serikali yanakidhi, kwa hiyo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.(*Makof*)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru. Mambo mengi sana yamezungumzwa juu ya faida nyingi na kubwa tunazotazamia kuzipata kutohana na utajiri mkubwa wa Gesi Asilia iliyopatikana katika nchi yetu. Hii inanikumbusha ahadi lukuki zilizotolewa wakati Sheria ya Madini ya mwaka 1998 inapitishwa kwenye Bunge hili. Ahadi zilikuwa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala hili na nipate majibu kutoka kwa Waziri Profesa Muhongo. Katika rasimu ya sera ya gesi asilia ambayo Wabunge mmegawiwa kwenye ukurasa wa tisa, Serikali inasema kwamba, Sera hii ya Gesi Asilia inahusu shughuli za katikati na shughuli za chini katika mchakato mzima wa biashara ya gesi. Kwa maana kwamba, ni shughuli za usambazaji na uchuuzi wa gesi. Sera hii inasema kwamba, shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi zitaongozwa na sera nyingine itakayoandaliwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Ni kwamba, kuna mikataba zaidi ya 27 nafikiri ya utafutaji, uendelezaji na uchimbaji wa gesi ambayo Serikali imeingia na makampuni mbalimbali ya kigeni. Haya hayatakuwa chini ya hii sera ya gesi asilia, haya yapo chini ya utaratibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 1980, pamoja na mikataba ambayo Serikali imeingia ile inaitwa *Production Sharing Agreements*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la Mikataba ya aina hii Waheshimiwa Wabunge ni kwamba gharama zote za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji ambazo makampuni haya yanaingia zinaingizwa katika kitu kinaitwa kwenye mafuta kinaitwa *costal oil* kwenye *gas* kitakuwa *cost gas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, wawekezaji hawa itabidi warudishe gharama zao zote hizo za utafutaji, uzalishaji uendelezaji na uzalishaji kabla hawajaanza kutupatia sisi fedha. Sasa, kimsingi nataka Mheshimiwa Waziri atuambie, hii mikataba ambayo tayari Serikali imeshaingia na watafutaji *gas*, iletwe Bungeni, tujue tumesaini kitu gani ambacho hakitafungwa na Sera hii ambayo Sera hii inasema hii mikataba haihusiki na hii *gas*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa mujibu wa mikataba hiyo *TPDC*, Shirika la Mafuta linatakiwa lifanye ukaguzi, lifanye *audit*ya gharama zote za utafuta, uendelezaji na uzalishaji wa gesi. Itakuwa vizuri Bunge lako Tukufu lileteewe taarifa za ukaguzi za *TPDC* ambazo zimeshafanywa kwa makampuni ambayo tayari yamepewa mikataba hii ili Wabunge waelewe, tayari hizo gharama ambazo inabidi zije ziondolewe katika mali yote itayopatikana ndiyo tuanze kuchangia kwenye kupata faida za huu utajiri mkubwa ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipofanyika hiyo, hatutakuwa tofauti na yaliyotokea kwenye Sekta ya Madini ambayo kwa takwimu za Waziri mwenyewe katika dola bilioni 11 ambazo zimepatikana...

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaondoa shilingi niseme wazi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Mawaziri naomba muwe mnaandika. Nimwite Mheshimiwa Mangungu atafuatiwa na Mheshimiwa Bungara. Mheshimiwa Mangungu!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kumshukuru

sana Waziri wa Nishati na Madini na Katibu Mkuuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa na ushirikiano waliotupa kuhakikisha pesa zetu Wilaya ya Kilwa kutokana na uchimbaaji ule wa *gas* zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliyotaka kufahamu ni kwamba, Serikali inatamka nini na inachukua hatua gani kuweza kuwafahamisha wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, ni jinsi gani ambavyo wananaufaika au watakuja kunufaika katika Sekta hii ya *Gas*na sekta nyingine mtambuka kama vile Kilimo, Ufugaji pamoja na Uvubi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana kwa kutokufanyika hili, ndio kunaleta matatizo na wananchi wanajichukulia sheria mkono kwa sababu wana wasiwasi kwamba uwekezaji huu utawanufaishaje. Hii inatupa wasiwasi maana tunaweza tukakosa mwana na maji ya moto. Naomba ufanuzi wa Serikali.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia habari ya Kiwanda cha Mbolea kilichoahidiwa na Serikali kuhusu *gasya Songo Songo*. Hii inamaanisha kwamba, Watanzania sasa hivi wanapoahidiwa jambo inabidi Serikali itekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mliahidi Wilaya ya Kilwa, wananchi wangu wanaauliza ni lini Kiwanda cha Mbolea kitajengwa Kilwa kutokana na *gasya Songo Songo*? Tukiamini kwamba watu wa Songo Songo au watu wa Kilwa, tumeruhusu *gas* kuja Dar es Salaam. Tuliishtaki Serikali na Serikali mkatuambia tuondoe kesi Mahakamani ili *gas* ije Dar es Salaam, kesi tukaondoa na mkatuahidi kwamba, mtajenga kiwanda cha mbolea na mpaka leo kiwanda hicho hakijajengwa.

Je, Serikali inasema nini kuhusu jambo hili, kiwanda cha mbolea kitajengwa lini? Haya ndiyo matatizo ambayo yanawapa wasiwasi watu wa Mtwara huko, kwamba

mnapoahidi sivyo mnavyotenda. Je, Kilwa itapata lini kiwanda cha mbolea kutokana na *gas*? Ahsante sana. (Makofi)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasimama kuunga mkono kabisa dhana ya Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamezungumza kwamba, pale palipo na rasilimali watu wa pale wafanane fanane na hilo. Hili nalisema kwa sababu nilipokuwa nafanya ile biashara ya jumla ya Urais ndicho nilichosema 1995. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ili watu wafanane fanane na dhahabu, kwa hiyo nakubali. Lakini kwa rafiki zangu, ndugu zangu, watani zangu wa Mtwara, kama kuna watu ambao ndiyo wangechangamkia kabisa bomba ni wao. Kwa sababu wangechangamkia ile *gas* ichenjuliwe Mtwara na Waziri amesema hakuna njia yoyote, lazima ichenjuliwe Mtwara. Ukishaichenjua imekuwa mali na mahali sasa pa kuombea ni hapa, una kitu cha kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hajachenjuliwa huna kitu cha kuuza na mahali pa kuuza hata ukiweka Kiwanda cha Mbolea, wao wanunuua iliyochenjuliwa, kiwanda cha kufufua umeme wanunuua *gas* iliyochenjuliwa. Soko liko Dar es Salaam, wapelekee haraka watu wa Dar es Salaam wanunue upate pesa, ukipata pesa ndiyo unasema sasa nimegee basi kidogo na mimi nifanane fanane kidogo na *gas* ambayo unayo. Naona kuwa lile ndiyo tungepigania, mambo mengine tunadanganywa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri *figure* moja kubwa ameizungumza ni ya umeme, *one point five trillion in a year*. *The trillion* moja kwa mwaka. Nimeangalia vitabu vyake vyote hapa, hii trilioni 1.5 iko wapi kwenye kitabu chake na vitabu vingine sioni. Ndiyo kusema kila anapochukua pesa kupeleka *TANESCO* unakata *REA*, unakata na wengine, ndiyo unapeleka kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshukuru Mheshimiwa Waziri angesema hiyo *1.5 trillion* jamani, hii ndiyo gharama na iko hapa. Kama hajawekewa kwenye kasma yake, basi atuambie *fortunately* name niko kwenye Kamati ya Bajeti, atuambie na ni lazima hii ionekane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia hata kwenye *Appendix I*, hakuna *transfer to TANESCO*. Sasa hizo zinatoka wapi? Kwa hiyo, ningependa hilo aliseme wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, hela yote ambayo tutakasimia kwa ajili ya *REA*, naomba iwe *ring fenced* isitumike mahali pengine. (*Makof*)

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi nzuri, kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ni kutaka kumwunga mkono Mheshimiwa Chenge aliloulizia kuhusu tufanye nini sisi Wabunge katika kusambaza umeme vijiji. Naomba tufanye maamuzi magumu, maamuzi ambayo yanaweza yakatupatia fedha za kusambaza umeme vijiji. Nafikiria *Yarabi*, hii kazi baadaye tutailaumu Waziri, tutailaumu Wizara, tutasema haifanyi kazi. Miezi mitatu tu iliopita kule Vunjo, *transformer* nne ziliungua na nyingine zikaibiwa na wezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumehangaika sana na Kaimu Mkurugenzi wa *TANESCO* namna ya kupata hizo *transformer* ilikuwa ni kazi ngumu sana hazipo, hazipatikani, ina maana hakukuwa na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna vijiji kule Vunjo kama 10 ambavyo tayari tumechimba mashimo, nguzo za umeme ziko chini, nyaya hakuna na hizo nguzo zimekaa zaidi ya miaka 10. Leo tukisema wasambaze umeme zile nguzo wanakwenda kufanya nazo nini kama hatutafuti fedha za kutosha za kuwapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Vunjo na Rombo sisi mara nyingi umeme unakatika katika. Unakatika kwa sababu zile njia ambazo zinasafirisha umeme kwanza ni za zamani. Kwa hiyo, ina maana kwamba mvua zikinyesha nyingi, matawi yakianguka kwenye nyaya zile umeme unakatika, umeme unakuwa mdogo. Sasa tunafanyaje kusafirisha umeme huo wa Vunjo mpaka kwenda kule Rombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, kama tunataka kuinua maendeleo ya wananchi vijiji hasa vijiji vyangu karibu vyote vya Vunjo kutokana na maendeleo mliyokwishawaonyesha wale wananchi wa Vunjo mambo ya barabara nzuri, mambo masoko, watu sasa wanataka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, naomba tufanye maamuzi kwenye umeme, tuweke hela na kwenye mambo mengine tupate hela za kwenda vijiji. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mzee. Suala la kutafuta fedha katika maendeleo ambayo tumependekeza, nadhani mlifanyie kazi Serikali na Kamati ya Bajeti kwa sababu bado tuna nafasi ya kuangalia.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake alisema kwamba, tumfikirie Mwalimu Nyerere na mimi niungane naye kumfikiria Mwalimu Nyerere kwamba alisema ili nchi yetu iendelee inahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo hiyo ya Mwalimu, mwaka jana, kwenye hatua hii ya Kamati, niliomba ufanuzi kwa Waziri kuhusu utekelezaji wa maamuzi ya Bunge. Maamuzi ambayo kama yangetekelezwa tusingefikia hatua tuliofikia. Mheshimiwa Waziri akijibu kuhusu hoja hiyo ya kuhoji kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, akasema

kwamba, yeye hafanyi kazi na vyombo nya habari wala magazeti. Nilikuwa nahoji kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka mmoja umepita na naamini Mheshimiwa Waziri alipata nafasi ya kufikiria haya. Sasa ningependa kupata ufanuzi kutoka kwake. Kwa sababu watu wengi na hili ndiyo ametumia sana Mheshimiwa Waziri. Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge anachukulia kama ni kufukua mambo ya zamani, anachukua ni kama ya magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mambo haya yana uhusiano. Maazimio ya *Richmond* yalisema kwamba kuanzia baada ya *Richmond*, Tanzania Bunge liwe linashirikishwa kwenye maandalizi ya mikataba. Leo nchi inaingia kwenye migogoro ya mikataba ya *gas*, mikataba ya madini na mikataba mengine. Azimio hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maazimio ya *Richmond* yaliagizwa toka mwaka 2008 kufanyike uzalishaji mkubwa wa umeme na *megawatt 300* za Mtwara zikatajwa. Maazimio haya hayajatekelezwa. Yakapitishwa maazimio mengine ya *gasasili*, yakataka ushirikishwajii wa wananchi. Maazimio yote haya hayajatekelezwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukapitisha maazimio mengi ya Bunge ambayo kama yangetekelezwa, tungepata ufumbuzi na tukapitisha vile vile mwaka jana Bajeti, pesa tumetenga za *REA*. Mwaka mzima umekwisha, pesa zilizokwenda kwenye REA ni asilimia 13 tu za umeme vijijini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi. Maana yake ametumia maneno mengi sana ambayo mimi nayaona ni siasa chafu tu siyo siasa safi ya kutumia asilimia, kuzipotosha na kila kitu.

Kama tunatekeleza umeme vijijiini kwa maana kupeleka pesa kwa asilimia 13 tu, hivi kwa takwimu ya kawaida ni nani aliyeshindwa. Kwa asilimia 13 tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri, atupe ufanuzi, ni kwa nini maazimio ya Bunge mpaka leo hayajatekelezwa kwenye maeneo yote haya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, tunaendelea. Maana yake leo wote mnahutubia. Haya Mheshimiwa nilisema nani, Mheshimiwa Kayombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Mwaka 2006 wakati nikichangia, nilisema kwamba, kwa wakati mrefu ujao nchi hii uchumi wake utachangiwa zaidi na Mikoa ya Kusini na mimi natoka Mkoa wa Ruvuma, niko katika Mtwara *Corridor*. Nasimama kwa ufahari kabisa kwamba Mungu ametujalia na rasilimali hizi ili kuchangia uchumi wa Taifa letu na ni wakati wa ndugu wa Mikoa ya Kusini kuchangia Taifa hili. Hii ni fahari kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu ni kwa Serikali yetu tu, kuona kwamba, wakati wananchi wako tayari kuchangia rasilimali hii kwa Taifa wanapewa haki zao za msingi. Katika *budget speech* ya Mheshimiwa Waziri ameelezea mikakati ya umeme na umeme ambao ni *mixed* kwa maana ya kwamba kutakuwa sasa na makaa ya mawe ambao unatokana na ule mradi wa Ngaka. Ule mkaa wa mawe kule una mambo mengi sana. Yale majadiliano ya TANESCO yanavyochelewa, fidia za wananchi na umeme vijijiini katika vile vijiji. Lakini hapa nataka tu kujielekeza katika hili la fidia kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 30, ule mgodi Mkuu wa Mikoa alifunga kwa sababu ya *pressure* ya wananchi ya kudai tu fidia zao. Mgodi unaendelea, wale wananchi wanadai nyongeza ya fidia na wengine hajawalipwa kabisa. Hakuna juhudzi zinaonekana kwamba wale wananchi

watalipwa leo au kesho. Mpaka baada ya kufungwa mgodi, mpaka baada ya vurugu zile ndiyo Serikali inakuja na *fix date* ya tarehe 15 mwezi Juni, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu huu mradi unachangia *megawatt* karibu 400 kwenye gridi ya Taifa, nataka tu Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wale kwamba, huu mradi kweli utakuwepo. Maana yake bila kulipa hii fidia tarehe 15 utafungwa tena. Sasa sitaki tufike hapo na ikaonekana kwamba Mbunge anafanya vurugu na wananchi wakati Serikali ndiyo inakuwa chanzo. Je, fidia kwa wananchi kama ambavyo Sera inavyosema miradi hii isiendo mpaka pale ambapo fidia kamili kwa wananchi imetolewa, itafanyika katika mradi huu wa Ngaka ili tuweze kupata umeme na nina hakika utaweza kulisha Taifa letu, lakini pia nina hakika wale wananchi watapata umeme? Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Katika mchango wangu wa maandishi nilichangia suala la wachimbaji wadogo, kwamba, Serikali iangalie sasa na ifuate namna ambavyo wachimbaji wadogo wamekuwa wakiomba maeneo yao kwa shughuli zao za uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mkoa wa Katavi nilipendekeza kwamba, pamoja na kwamba pana eneo jipya la Mihama limetolewa kule kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Nilipendekeza wachimbaji wadogo na walishaandika barua kwa Wizara kwa namna ambavyo walipenda kupewa maeneo ya Ibindi, maeneo ya Magamba, maeneo ya Singililwa, maeneo ya Kasese Kampuni na Kasinde. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nillongelea suala la kampuni ya *GBA* ambayo ipo Mpanda kule maeneo ya Kampuni na Kakesi kwamba, kuna eneo leseni yao inawaruhusu kufanya kazi katika eneo fulani, lakini wana eneo lingine la ziada ambalo hawalitumii. Nilipendekeza wapewe wachimbaji wadogo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka tu kuulizia je, Serikali ina mpango gani wa kununua mitambo yake yenye ya kufulia umeme kuititia *gas* badala ya kusubiri kutumia mitambo ambayo imekuwa ikiikodisha na hivyo kuwa na gharama kubwa zaidi kutokana na ile *capacity charges?* Napendekeza wangenunua mitambo yao wenyewe ya kufulia umeme, kwa sababu wanapokodisha inakuwa na gharama kubwa zaidi ya kiuendeshaji. (*Makofii*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Napenda tu kupata ufanuzi kutoka kwa Serikali. Tumejaliwa neema Tanzania kuwa na makaa ya mawe katika maeneo mengi na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa tumeona kwamba, kuna mgodi wa makaa ya mawe Kiwira na kuna mgodi wa makaa ya mawe Ngaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kupata ufanuzi kwamba, kwenye mgodi wa makaa ya mawe wa Ngaka kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba tumeshaanza ku-*export*, tunauza nje na baadhi tani kama 121,685 zinauzwa ndani ya nchi. Ningependa kujua ni kwa nini mpaka sasa hivi Watanzania wengi hawatumii makaa ya mawe kama nishati ya kupikia nyumbani chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia viwanda ndani ya nchi yetu ambao wanatumia kuni, wanatumia magogo, wakati tayari tunayo makaa ndani na mpaka tuna-*export* nje. Sasa ningependa kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, tunatumia makaa ya mawe ambayo tayari tunayo na tumeshaanza kuuza nje.

Kwanza, viwanda vyetu vitumie makaa ya mawe, lakini pia Watanzania zaidi ya asilimia 80 ambao wanatumia mkaa waweze kutumia kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ili kuepusha matumizi makubwa na uharibifu wa misitu ambao unaendelea ndani ya nchi yetu. Ahsante.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Muhongo, kwa kutupa shule na hasa kwa kumwelimisha Mheshimiwa John Mnyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa na nitasema maneno kwa uchungu sana na naomba Mwenyezi Mungu, aniongoze. Ninayasema maneno haya kwa niaba ya wananchi wa Nzega, ambao miaka 15 iliyopita walinyang'anywa ardhi yao kupisha uwekezaji kwenye mgodi wa uchimbaji wa dhahabu wa *Resolute*, pale Nzega na mpaka leo hii hawajalipwa fidia wala kifuta jasho, mbali na Sera za nchi yetu zinayoyelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nasimama kuyasema hayo kwa niaba ya wananchi wa Nzega, ambao kwa miaka 15 wamekuwa wakiathirika na uwepo wa mgodi wa uchimbaji dhahabu pale Nzega. Nayasema hayo kwa uchungu mkubwa nikitazamia kuona mgodi ukifungwa miezi michache ijayo wakati kukiwa hakuna *rehabilitation bond* ambayo inapaswa kuwekwa, ili kutunza mazingira baada ya mgodi ule kuondoka. Lakini pia nayasema hayo, tukiwa tunadai bilioni nne na zaidi za ushuru wa huduma ambazo hazijatolewa Kisheria, kwa mujibu wa *Local Government Finances Act* ya mwaka 1982.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema hayo *niki-take stock* ya mazungumzo ambayo tuliyafanya mwaka jana baina ya Serikali, Wawekezaji na sisi Wabunge na Madiwani wawakilishi kutoka Nzega, ambapo tulikubaliana hayo yote yatatekelezwa kabla mgodi haujafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, wananchi wa Nzega wamenituma. Kama Serikali, isipoingilia kati kama ilivyokuwa ahadi yake kwa kuwanyima kibali cha kusafirisha dhahabu wachimbaji wa *Resolute*, ili waweze kutulipa na kutekeleza hayo yote, wananchi wa Nzega wamenituma niseme kwamba, hawatakuwa tayari mgodi ule kuondoka bila sisi kulipwa fidia wala kulipwa ushuru wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili hayo yasitokee, Mheshimiwa Waziri, ananiambia nini kuhusu kutekeleza makubaliano yale ndani ya mwezi huu mmoja ama miwili ijayo, ili vurugu zisitokee Nzega? Naomba ufanuzi na natoa nia ya kutoa Hoja ya Kuondoa Shilingi kwenye Mshahara wa Waziri.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie mchango huu.

MWENYEKITI: Ni hoja moja, sio mchango tena, ni jambo moja.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu ya msingi kimaandishi nilisema, tatizo la Buhemba limekuwa sugu kwa zaidi ya miaka 13, wakati wananchi wangu wa Buhemba, wanaambiwa kuna Kampuni ya Serikali ya MEREMETA inameremeta, inakuja pale itawapa maji, itawapa barabara nzuri, nilisimama hapa nikasema hawa ni wahuni, watatuibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye, muda ulivyokwenda, hawa Makaburu walichimba dhahabu pale Buhemba, wakachukua kila kitu wakaondokanacho, wakakimbia. Eneo la Buhemba, walikuwa wanalimiliki pale, wao wa MEREMETA. MEREMETA ilipoondoka haikuaga, iliacha ma-*cynide*, madawa yale mabaya, yamemwagika hovyo na watu wangu wote wa Buhemba na mifugo inakunywa hiyo dawa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma iliyopita, aliyekuwa Waziri Mkuu, nilimwomba akaone hali halisi ya Buhemba; alipeleka Mawaziri watatu akiwemo Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Maji, pia Waziri Wassira, alikuwa pale. Wakaenda wakaona pale ndani ya mgodi kuna dawa, kuna *chemicals* zinaitwa *cynide* yamemwagika hovyo; wakahoji je, ni *safe* kwa wananchi ama hapana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakaambiwa na hawa Makaburu kwamba, mambo yako sawa. Mambo hayakuwa sawa; mwaka hadi mwaka mifugo ikawa inakufa na binadamu pia wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuwa napiga kelele Bungeni hapa, tutafanyaje? Mpaka nikaomba tafadhalisana mtusaidie jinsi gani ya kuepuka, kuepusha tatizo kubwa ambalo ni janga la Kitaifa hapa nchini, kuhusu Buhemba. Baadaye, wananchi wenye hasira wakaanza kugombana na hawa wa MEREMETA, MEREMETA wakatimka, wakaondoka bila kuaga, madawa bado yanazagaa pale, wananchi wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palepale Buhemba, kuna wachimbaji wadogo wadogo walikuwepo enzi hizo, tangu wakati wa Mkoloni mpaka leo. Walipoondoka, je, hawa watu wa STAMICO, ambao niliomba waje pale, walirithi *assets* na *liabilities* za MEREMETA ama hapana? Kama walirithi, je, watafanya hiyo...

MWENYEKITI: Muda umekwisha, dakika tano tayari zimekwisha. Mheshimiwa Ole-Sendeka?

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Nilipokuwa nachangia na baada ya majibu ya kaka yangu Mheshimiwa Waziri, nilinukuu ahadi ya Mheshimiwa Rais, katika eneo la machimbo ya *tanzanite*, Mererani. Waziri, akasema Mkuu wa Mkoa alimwambia ahadi hiyo hakuiona na ndio maana labda pengine Wizara yake imefika mahali pa kuamua kutoa leseni hiyo na kuwaacha Wachimbaji Wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme siwezi kutumia jina la Rais vibaya. Naijua Kanuni ya 64 (1) (d), hairuhusu; nalisema jambo hili na kurudia kusema Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 25 Oktoba, 2010, Orkesmet aliahidi. Mwaka 2005 alipoombwa na wananchi wa Mererani, pale Mererani, alisema nipe ni kwanza kura, tutahangaika na haya kwa mujibu wa Sheria, wakati huo Sheria hairuhusu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2010 aliahidi na nitatoa ushahidi kwako na kwa Waziri Mkuu na kwa Kamati yoyote ya Bunge kwamba, Rais, aliahidi kwamba, eneo hilo leseni ya *Tanzanite One* itakapokwisha, ataligawa baada ya kwamba, Sera tumebadilisha, sasa uchimbaji wa madini ya vito ni kwa ajili ya Watanzania; hilo nitathibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilimwambia Waziri, aepuke kuuziwa mbuzi kwenye gunia. Sheria ya Madini inasema bayana, wazi kabisa kwamba, kuna aina sita za leseni na mionganoni mwa leseni hizo ni pamoja na leseni ya kuchimba *Germstone*, ni pamoja na leseni ya kuchimba *Industrial Materials* na leseni zingine. Huwezi kutoa leseni ya aina ya madini yanayoangukia kwenye leseni ya *Germstone*, leseni hiyo ukatoa idhini ya kuchimbwa kwa *Marble* na *Grafite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ili kuthibitisha hili, hata Mwanasheria wa Wizara ya Mheshimiwa Waziri, katika dokezo lilioandikwa tarehe 12 Aprili, samahani nilipenya kwenye Ofisi yake mpaka nikahakikisha kwamba, ninazo nyaraka. Madokezo yote ya Wataalam yanakataa kwamba, huwezi ukatoa leseni kuruhusu leseni hiyo hiyo moja ichimbe madini yasiyoangukia kwenye leseni hiyo, Wizara yake imefanya. Sasa nataka niombe hili, lakini sio hivyo tu, ukubwa wa eneo la kuchimba madini ya vito kwa mujibu wa Sheria ni kilometra moja ya mraba. *Offer illyotolewa, Notification of Grant*, imetolewa ya kilometry na Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie tu Waziri kwamba, nataka maelezo juu ya eneo hili na kwa kweli, nakusudia kuondoa shilingi, ili kuhakikisha kwamba, maelezo sahihi yanapatikana katika kuhakikisha kwamba, madini ya vito yanachimbwa na Watanzania, bila kigugumizi. Nimhakikishie Naibu Waziri wake, ndiye alikuja tukashirikiana wote, tukaazimia kuunda ushirika katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nataka maelezo, vinginevyo nitatoa shilingi.

MWENYEKITI: Haya. Waheshimiwa Wabunge, dakika zetu zinakuwa 25, nimeongeza mpaka zimefika karibu 35; sasa naomba muanze kujibu. Mnapojobu, mna-refer yule aliyetoa hoja na isitoshe ninazo shilingi-shilingi nydingi hapo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, muulizaji wa kwanza, alikuwa ni Mheshimiwa Chenge, ambaye alitoa ushauri tu kwa Serikali, kuona namna ya kuweza kuongeza mapato na sisi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sisi tunalipokea Serikalini. Tutaona namna ya kuweza kufanya kwa ushirikiano na Kamati yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mchangiaji mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Lembeli, ambaye ye ye kasema ameunga mkono baada ya kupata maelezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine alikuwa ni Mheshimiwa Tundu Lissu, ambaye amesema katika Rasimu ya Sera, shughuli zinazozungumzwa ni zile za *Mid Stream* na *Down Stream*, lakini *Up Stream* haisemwi na inaelezwa kwamba, tutakuwa na Sera Maalum kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa hapa ni kwa sababu ya *Industry* hii ya gesi. *Industry* ya gesi na mafuta ni kitu cha kitaalam sana na pengine kama majibu ya utaalami huu ambao watu wanafanya mpaka *Ph.D.* yanatakiwa kutolewa hapa, tutapata kazi kubwa kweli. Kwa sababu, najaribu kutafuta, wakati mwingine nikiulizwa, kwa sababu ingawa si mtaalam wa sekta hiyo, lakini kwa kuwa ndiyo sekta ninayoismamia, najifunza kweli kweli, usiku na mchana na naona tofauti iliyopo katika uelewa wa Sekta hii. Naona kuna kazi kubwa, tutachukua muda mpaka tufikie wakati mzuri wa kuelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Up Stream* inazungumzia uwekezaji mkubwa sana. Huwezi ukaiunganisha na *Mid Stream* na *Down Stream* kwa sababu, haya mambo ni tofauti na ukichanganya hutapata vizuri zile hesabu zake. Sasa yeze anasema kwamba, dhamira ya hii ni kwa sababu ya Mikataba hii kwamba, inataka kuwa-favour wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni hapana. Naomba Mheshimiwa Tundu Lissu, tutachukua muda kidogo kuelewana katika hili na pengine Ukumbi huu kwa muda huu hautoshi kueleweshana, maana inahitaji karibu saa nzima tukae tunajadiliana, ili tuweze kuelewana kwa nini, tunakwenda katika msimamo huu wa kusema tutenganishe hizi Sera mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uwekezaji wake ni tofauti. Anayefanya *exploration* ni mtu tofauti na anayekuja kufanya hizi biashara ni mtu mwingine kabisa. Uwekezaji wake ni tofauti na aina ya *business* yake ni tofauti kwa hiyo, ndio sababu, tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa juu ya kwamba, hii aina ya *Regime* au *Modal* ya Mikataba tunayoingia ya *PSA* (*Production Sharing Agreement*), akiwa anafanya *comparison* na aina nyngine inayoitwa *Concession*. *Concession* ndio tunayotumia kwenye madini. Tofauti ya *Concession* na *Production Sharing Agreement* ni kwamba, kwenye *Concession* mnatakiwa, kwa maana ya Serikali na Mwekezaji, kuchangia katika mtaji kabla hamjaanza kupata faida; sasa unajuliza sisi tunayo mitaji ya kuweza kuchangia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana sehemu kubwa ya michango hatukutoa na ndio maana *share* zetu zikawa zinaondoka. Pale tunazungumzia habari ya mgawanyo wa *share*. Lakini kwenye *Production Sharing Agreement* ni kwamba, mnagawana mapato ya uzalishaji na mnagawana kutoka siku ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mikataba yetu, Mikataba ya Tanzania, Mikataba yetu toka siku ya kwanza

watakopoanza. Mheshimiwa Tundu Lissu, anasema itabidi warudishe kile walichowekeza, halafu ndio sisi tuanze kupata; si kweli. Utaratibu ni kwamba, *from day one* sisi tunakuwa tuna asillimia za *sharesna* wao wana za kwao. Sasa wakianza kuzalisha wanacheza na ile *margin* yao na sisi tunaendelea kuingiza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu ni kwamba, sisi katika Mikataba yetu yote ya uchimbaji wa gesi, hakuna ambapo tunashuka chini ya 30% kutoka siku ya kwanza. Mikataba hii wala isiwe kwamba, ni kitu cha kutisha, wala watu wakasema kuna ujisadi. Ilisialetwa kwa Katibu wa Bunge, mkitaka tulete tena tutaleta, anayetaka kusoma afuate tu utaratibu wa Kibunge, Mikataba iko hapa hapa kwa Katibu wa Bunge; hakuna siri katika jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilliona nichukue muda mwingi kulielezea hilli, lakini Mheshimiwa Mangungu, amezungumzia suala la Lindi na Mtwara, ni jinsi gani watanufaika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa ya gesi hayaji bila kuanza na miundombinu. Ni mpaka uanze na miundombinu ndio uyaone manufaa. Vinginevyo tutabakia tunataka manufaa, tunasema hatuyaoni. Nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Mangungu, kama utulivu utatokea katika maeneo haya, wawekezaji wengi watakuja kuwekeza na manufaa yataanza kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa hayo ni pamoja na ajira na biashara, kwa sababu, kama *Industry* hii itaendelea vizuri katika Mikoa hiyo, ni dhahiri kwamba, biashara kubwa itakuwepo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kubwa hapa ni mgawanyo wa mapato. Katika Sheria yetu ya Fedha kwa Serikali za Mitaa, inasema kabisa kuna mgawanyo wa 0.3 wa mapato, tena ni *Gross*. Sasa kama 0.3 unazungumzia gesi tunayoizungumzia mabilioni ya fedha yatagawiwa kwa mujibu wa Sheria ile, ni fedha nyingi. Pengine, ndio nasema,

ukiisoma Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa vizuri, kuna Kifungu kinachosema Waziri ana uwezo akagawanya yale mapato kadiri anavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna ugomvi mnaweza mkagawana hata katika Mkoa, mkagawana katika Wilaya; maana kuna mivutano mingine inasema sisi hatupati, wa Mtwara Mjini hatupati, wa Mtwara Vijini, si kweli. Sheria nimeisoma vizuri ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, inasema Waziri anaweza akaamua atakavyoona inafaa, mwenye dhamana na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, manufaa yapo na ni makubwa. Ukiacha manufaa mengine ya viwanda na ajira ambayo yapo wazi na kila mtu anajua kwa hiyo, kukitokea utulivu, wananchi wataona manufaa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bungara, anasema ahadi ya Kiwanda cha Mbolea Kilwa. Wakati mwengine mambo haya unasikitika kidogo. Mheshimiwa Bungara, ye ye ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Eneo walilokuwa wametenga la Kilamko, ye ye akiwa humo kwenye Halmashauri hiyo, wameligawa viwanja, ambalondilo lilikuwa eneo la kujenga Kiwanda cha Mbolea. Sasa tena anakuja hapa anasema, basi tutajitahidi tutafute eneo lingine, lakini wako wawekezaji ambao wana nia na wameonesha dhamira ya kweli ya kutaka kuwekeza, tutawatafutia, lakini na ninyi mtusaidie kupata eneo, msigawe tena kama lile mliloligawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cheyo, anasema palipo na rasilimali, wananchi wa pale ni lazima wafanane. Ni kweli, nakubaliana, lazima wafanane na ndio maana kuna migawo hii. Kuna *Corporate Social Responsibilities*, ambazo zinayataka haya makampuni yafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii katika Sera ya Gesi, tumesema *Corporate Social Responsibility*, ni wajibu kwa

makampuni hayo, tumeweka kwenye Sera na tunatakiwa ikitoka kwenye Sera, lazima iwekwe kwenye Sheria kwamba, wafanye kiasi gani. Kama ni kwa *percent*, basi hiyo *Corporate Social Responsibility*, lazima tuione, iwe *visible*, kwa hiyo, sio kama ile iliyokuwa kama hiyari hiyari hivi, tunataka ione kane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wataanza kunukia katika hali hiyo. Uki jumlisha na ile *Service Levy*, ukiweka na mambo ya ajira, utaona wanankia tena watakuwa wanankia kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo amelisema ni *distribution*, kwamba *1.5 trillion* inayoonekana inatumika kwa mwaka kwa ajili ya kuendesha mitambo hii ambayo, kwa hakika mwaka jana ndio iliyofanya tukaenda kuzalisha umeme badala ya kuendeleza kama wengi walivosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kwa wote kwamba, kwa kweli jamani, busara ya wakati huo ilitutaka kwa hakika, huwezi ukaenda kusambaza umeme vijiji ni wakati huo umeme wenye haupo. Huwezi kwenda kupeleka ukatekeleze mradi Kijiji ni kupeleka umeme, wakati nchi inaingia gizani, viwanda vinakufa, uchumi unaanguka, wewe unasema tusizalisho umeme, twende tupeleke umeme vijiji ni; kwa kweli, busara yetu ilikuwa hivyo, lakini tulifuata Kanuni na Taratibu za Fedha za Serikali na kubadilisha matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu huu ni utaratibu wa Kiserikali. Kwa hivyo, pale tunapotaka kufanya mambo ambayo tunajua yana tija kwa maslahi ya Watanzania, lazima Serikali, iachiwe ifanye mambo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikubaliane kwamba, umesema huioni katika bajeti; ipo kwenye miradi ya maendeleo, tutakapofika kwenye Kitabu cha Maendeleo, utaona kiwango kile cha kuanzia, ambayo kwa kweli, fedha ile tumeitenga maalum kabisa kama mradi. Wakati ule hatukuwa na mradi wa namna hiyo, lakini sasa tuna mradi

kwamba, mafuta sasa yatakayotakiwa kuendesha hayo *generator* yanaonekana kwenye bajeti ya kwenye Kitabu cha Bajeti yetu cha Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mrema, amezungumzia kwamba, kuna nguzo zipo kule kwenye Jimbo lake la Vunjo na Rombo na umeme sio wa uhakika. Kuhusu nguzo hizo Mheshimiwa Mrema, nimewahi kujibu siku moja hapa, uliuliza swali la nyongeza; nikuhakikishie kwamba, tutajaribu kuona kama bado zina uimara na bado tunaweza tukatekeleza mradi. Vinginevyo Mheshimiwa Mrema, tuna mpango mkubwa wa umeme vijiji na wewe hujaachwa, nikuhakikishie kwamba, tutashirikiana na tutaifanya hiyo kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini jambo lingine ni kwamba, umeme katika maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro na maeneo ya baadhi ya Tanga na maeneo mengine Same na wapi, si wa uhakika sana kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu. Tuna mradi mkubwa wa *TEDAP* ambao unatoka, pia upo katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utakapotekelezwa, kwa hakika utatusadia sana, kwa hiyo, huu mradi utakapotekelezwa na unaanza kutekelezwa kuanzia mwaka huu mwishoni, utaanza kutekelezwa na mwakani utakuwa umekwisha. Tatizo la umeme katika maeneo hayo halitakuwepo tena na umeme utakuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyika amezungumzia utekelezaji wa maazimio ya Bunge na mikataba ya gesi. Nirudie kusema tu mikataba yote ya gesi ipo kwa Katibu wa Bunge Mheshimiwa Mnyika, unaweza ukaiona na kama una ushauri wako unaweza ukautoa, fursa unayo ni kufuata taratibu za kawaida na kwa hiyo hili la mikataba linakuwa limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini suala la maazimio, suala la maazimio ni suala la Serikali na Bunge. Ukitaka hapa tuseme kwa namna gani tumetekeleza maazimo ya Bunge,

taarifa hii inahitaji muda wa kutosha na inahitaji muda maalum. Nafikiri Spika anaweza akatenga muda maalum tukafanya hivyo, lakini kwa maana ya hapa, ukitaka kukamata shilingi Mheshimiwa Mnyika hutaki tu nikupelekee umeme kwenye maeneo yako ya Jimbo lako la Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kayombo amezungumzia, hili atalijibu mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kikwembe amesema kwa nini Serikali au *TANESCO* haijengi miundombinu ya kuzalisha. Mheshimiwa ukiangalia kwenye miradi yetu ya maendeleo, kwenye kitabu chetu cha maendeleo tutakapofika, utaona tuna *megawatt*, Kinyerezi *One megawatt* 150 na Kinyerezi *Two megawatt* 240.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni miradi ambayo ni ya *TANESCO* na fedha zake zimetengwa na miradi hii itatekelezwa, lakini tutaenda kwa awamu. Tukimaliza hii tunakuja *megawatt* 300, kwa hiyo utaona tunalifanya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunao uzalishaji wa mradi wa umeme ambao lazima tushirikiane pia na sekta binafsi kwa mfano, kule Mtwara kama tulivyosema tuna *megawatt* 400 ambazo zitazalishwa pia pale, lakini pia tutaunganisha Mtwara na Somangafungu na Mtwara na Songea. Hiyo yote inakaa kwenye mradi mmoja ambao tumeshaingia makubaliano na *Symbion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie kabisa pengine huwezi kujua mradi huu unaweza ukakamilika mapema sana kwa sababu ya mikakati na mahusiano mazuri tuliyonayo na baadhi ya nchi marafiki wakiwepo Marekani kuititia *MCC* au vyovyyote vile. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba, mradi utatekelezwa na wala msiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale ambayo yalikuwa yananihusu nimeyatolea ufanuzi. Ahsante sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN

J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba name nijibu hoja zilizoelekezwa hapa. Nianze na hoja ya Mheshimiwa Sendeka kuhusu Mererani. Labda niseme masuala ya madini yana uhusiano wa karibu sana na sheria. Hakuna maamuzi yanafanyika kwenye madini bila kufuata Sheria ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Bunge liliazimia madini ya vito yachimbwe na Watanzania kwenye Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Lakini Sheria hiyo hiyo ya madini ya 2010, kifungu namba 116, kinasema kwamba, kinaipa mamlaka Serikali kuhuisha leseni ya nyuma. Kwa mfano, leseni ambazo zilitolewa wakati wa Sheria ya mwaka 1998, zinaweza kuhuishwa kupitia kifungu hicho namba 116 kama mwekezaji yule tayari alikuwa akiendelea kufanya shughuli zake wakati hiyo Sheria mpya imetungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika Sheria hiyo hiyo ya Madini ya 2010 kwenye eneo la vito, kifungu namba 8(3), kinasema kwamba: "Madini ya vito yatachimbwa na Watanzania", nakubaliana lakini kifungu namba 8(4) kinampa mamlaka Waziri wa Nishati na Madini, pale anapoona inafaa na kwa maombi maalum pale mradi ambaao Mtanzania anadhani kwamba anahitaji msaada wa mwekezaji wa kigeni kuweza kuchimba kwa teknolojia ambayo anadhani kwamba anahitaji msaada wa mwekezaji wa kigeni, Sheria inampa Mheshimiwa Waziri mamlaka hayo kupitia kifungu cha 8(4) kuweza kuwapa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vifungu hivyo vyote ndivyo vilivyotumika kujadili mkataba wa *Tanzanite One*. *Tanzanite One* walikuwepo kabla ya Sheria ya 2010 waliwekeza na walikuwa wakifanya kazi. Sheria imekuja kutungwa, huwezi ukawafukuza ukawanyang'anya maana ile itakuwa ni *nationalization, otherwise* kama tunakubaliana kwa Bunge hili tutaifishe migodi ile kinyume na Sheria hii jinsi iliyowekwa, basi nitaomba nijifunze kwa wataalam wa Sheria. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Buhemba Mheshimiwa Waziri amelieleza vizuri sana kwenye maelezo yake. Ni kweli palikuwa na historia ndefu sana nisingependa kuirudia. Kilichopo mbele yetu sasa *STAMICO* inamiliki leseni ya Buhemba na imeshapata mwekezaji kwa maana ya Mbia ambao watafanya kazi pamoja kwa taratibu ambazo zilifuata taratibu zote za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kuna hoja za wananchi, kuna madai ya wananchi, yatahudumiwa pale *STAMICO* itapoanza *operation* katika eneo la Buhemba kwa taratibu kama tulizoziongea kwa wawekezaji wengine wa uzalishaji. Pia Mheshimiwa Waziri amesema wale wananchi wa Buhemba anawatafutia eneo lao na amewaita kupitia viongozi wao na ameshaagiza *GST* na taasisi zetu kuwatafutia maeneo ambayo yatafaa na hili tunalifanya kwa nguvu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla amezungumzia fidia kwa wananchi wa Nzega. Katika *Land Act* ambayo Mheshimiwa mama Anna Tibajuka ndiyo anasimamia Sera na Sheria za Ardhi inaeleza wazi kwamba, kama kuna uwekezaji sehemu na kuna wananchi ambao wanamiliki eneo lile kisheria, wana haki zote za kupata fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la Nzega limepelekwa Mahakamani, kesi imekaa zaidi ya miaka saba na Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa Mwanasheria wa wale wananchi waliokuwa pale, anazo taarifa vizuri ni kwa nini ile kesi walishindwa Mahakamani. Kwa misingi hiyo, kuna hukumu zimeshatolewa na Mahakama kwamba wananchi wale hawakustahili kupata fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichojaribu kukifanya mwaka jana tukishirikiana na Mheshimiwa Kigwangalla ni kushawishi mgodi kwa njia zingine kwamba wananchi hawa wameathirika kwa namna fulani baada ya uwekezaji huu kuja, whether ni negative au positive.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na wao katika *rehabilitation* lazima wafikiriwe kwamba ni sehemu ya jamii ambayo imeathirika. Kwa hiyo, wanapotenga *rehabilitation fund* wa-make sure kwamba, wanafanya *consideration* kwa wananchi hawa, lakini kwa utaratibu tu ule wa fidia kisheria kesi hii ilikwenda Mahakamani na ilidumu miaka saba ama nane na wananchi walishindwa kupitia kwa wanasheria wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika majadiliano hayo hayo ambayo nampongeza tena Mheshimiwa Kigwangala, alifanya kazi kubwa na tumesaidiana, wamepata fedha 2.3 *bilion* kutockana na madeni ambayo mgodi ule ulikiuka huko nyuma. Sasa kweli tulitumia vitisho mbalimbali ikiwemo kuwatishia, kuwanyima *export permits* ambayo kimsingi ni haki yao kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa misingi hiyo mgodi huu umeshafungwa hauzalishi, kama hauzalishi ina maana kama tulikuwa tunatumia gia au silaha ya *export permit* kuwanyima, sasa ile silaha haipo ina maana tunatakiwa tutafute njia nyingine ya kuangalia hizi haki ambazo Halmashauri ya Nzega inazidai watazipata kwa njia ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni jukumu la msingi la Halmashauri kuptitia Mbunge wao kuendelea kudai haki zao kutoka kwenye uwekezaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sakaya, amezungumzia maka ya mawe ya Ngaka. Makaa ya mawe ya Ngaka yanatumika kwenye viwanda vyetu vya ndani. Kiwanda cha Mbeya *Cement* kinatumia maka ya mawe haya, Twiga *Cement* kule Wazo wanatumia, Tanga Cement wanatumia. Lakini kwa sababu *location* ya mgodi ule ipo karibu kabisa na mpaka wa Malawi, kampuni ile pia ina mikataba ya kuuza katika kampuni za Malawi kule na wanafanya hivyo kwa taratibu zote za kisheria. Kwa hiyo hatu-*export* tu na sisi tunatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niunganishe hapo hapo na Mheshimiwa Kikwembe aliuliza, nafikiri ni yeye

mwenyewe Sakaya kwamba kwa nini tusiyatumie kupikia. Makaa ya mawe huwezi ukayapikia moja kwa moja labda uzalishé kwanza nishati, halafu ndiyo utumie nishati kupika. Kwa jinsi yalivyo na moto wake hizo sufuria mama, itakuwa ni ngumu sana kupikia moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Mheshimiwa Kikwembe amezungumzia wachimbaji wadogo. Suala ni lile lile maeneo yale yanamilikiwa kisheria maana wameshapewa leseni wale watu na Wizara ama Serikali haiwezi kutoa leseni juu ya leseni. Kwa hiyo, njia pekee iliyopo ni kwamba *either* mwenye leseni ile aridhi kuachia baadhi ya maeneo yake. Kimsingi kisheria kama ni leseni ya utafiti zile kubwa, anapomaliza muda wake wa kwanza miaka minne anatakiwa aachie eneo nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yale wanapoyaachia tunawapa wachimbaji wadogo, lakini kama ule muda haujafika huwezi kutumia mabavu kumnyang'anya mtu leseni yake, tuna kesi nyngi Mahakamani, tunadaiwa pesa nyngi na tunalipa pesa nyngi. Tusingependa kuingia kwenye kesi zingine ambazo tunajua mwisho wake tunakwenda kushindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya sasa, maeneo yale ya Mpanda kweli yameshikiliwa na baadhi ya watu na tuna wa-*engage* kuwaomba ili waweze kuangalia kwamba kuna Watanzania wengine wanahitaji kuchimba madini katika maeneo hayo. Kwa hiyo, watakaporidhia, basi tutamega yale maeneo, tutatoa leseni kwenye vikundi vya wachimbaji wadogo kwenye maeneo ya Kata ya madini na maeneo mengine aliyyoyazungumza kwenye ya maganda na kadhalika. Eneo lile la ziada tulilowapatia ni kwa sababu lilikuwa liko wazi, halikuwa na leseni ndiyo maana tumeyatenga kwa ajili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kayombo amezungumzia rasilimali za Taifa. Waheshimiwa Wabunge, huu wimbo wa rasilimali za Taifa kama *revenue shared plan* ni wimbo ambao kila mtu angependa kuuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo fedha zote zinazotolewa kwenye Bodi ya Mikopo, fedha zote tunazogawana hapa kupitia Hazina ndiyo zinatokana na makusanyo mbalimbali ambayo Serikali inakusanya kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwemo madini ya Usukumani. Kwa hiyo, madini ya Usukumani kodi zote ziliwa zinakwenda Mfuko Mkuu wa Hazina na ndiyo tulikuwa tunagawana wote wa Pwani, wa Mtwara, wa Shinyanga na kadhalika tunagawana fedha hizo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo kama leo tunataka sasa tuangalie namna gani kila mmoja aanze kuchukua mapato yake kuna njia mbili; njia ya kwanza Mbunge aandae *Private Members Bill* ailette Bungeni, Bunge liridhie tubadilishe Sheria zetu ili tuangalie kama Mrabaha ama tozo ama Sheria, ama kodi zibaki kule, lakini kwa jinsi zilivyo sasa hivi haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafuata mfumo ulivyo kwa mujibu wa Sheria za Kodi na Sheria za Fedha. Kwa misingi hiyo sasa Serikali imesikia, inaweza kupitia Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali ilete hoja hiyo Bungeni, sheria ibadilishwe, itungwe kama Wabunge wote na Watanzania watadhani kwamba, hoja hiyo itakuwa na maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vinginevyo ni mjadala ambao unahitaji kabisa maamuzi mapana na si tu Waziri wa Nishati na Madini kuamua kuanzia leo *loyalty*ibaki Shinyanga, gesi nayo ibaki kule. Sisi hapa tunasimamia tu Sera na Sheria ya Madini, mambo ya kodi yanasmamiwa na Wizara ya Fedha kupitia *TRA* na taratibu ziko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya wananchi kule Ngaka, Serikali imeingilia katika kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata haki yao. Nitoe wito tu kwa viongozi wenzetu Mikoani, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Halmashauri tusichukue maamuzi ya kufunga migodi hii bila kufanya *consultations* na Wizara kwa sababu kuna madhara makubwa ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi ile imefunga mikataba ya ku-supply, nimetaja viwanda hapa, viwanda vile vikipungukiwa *supply* ya makaa ya mawe maana yake uzalishaji unapungua, uzalishaji ukipungua maana yake kutakuwa na *shortage*ya simenti kwenye viwanda vyetu. Kwa hiyo, kuna madhara makubwa sana ambayo yanaweza kujitokeza ya kisheria kama mtu ataamua tu kufunga mgodi bila kufuata taratibu ambazo zinatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe viongozi wenzetu kule tunatambua mchango wenu, tunatambua kazi yenu, lakini tuwaombe sana, tuwasiliane kama kuna tatizo lolote la kiusalama, ama la madai ili tuweze kushauriana vizuri namna bora ya kufanya kabla ya kuchukua maamuzi. Ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 104 zimebakia dakika kumi tunaingia kwenye *guillotine*.

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> ...	Sh. 1,909,224,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> ...	Sh. 1,715,299,000/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> ...	Sh. 948,080,000/=
Kif. 1005 – <i>Legal Service</i> ...	Sh. 1,952,138,000/=
Kif. 1006 – <i>Government Communication Unit</i> ...	Sh. 1,404,320,000/=
Kif. 1007 – <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh. 1,099,591,000/=
Kif. 1008 – <i>Environment Management Unit</i> ...	Sh. 578,227,000/=
Kif. 1009 – <i>Management Information System</i> ...	Sh. 1,987,018,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – Minerals Sh. 33,046,292,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 2004 – *Tanzania Diamond Sorting Agency (TANSORT)* Sh. 1,941,404,000/=

Kif. 2005 – *Eastern Zone* Sh. 1,765,080,000/=

Kif. 2006 – *Western Zone* Sh. 960,016,000/=

Kif. 2007 – *Lake Zone* Sh. 1,610,893,000/=

Kif. 2008 – *Northern Zone* Sh. 1,470,385,000/=

Kif. 2009 – *Southern Zone* Sh. 999,771,000/=

Kif. 2010 – *Central Western Zone* Sh. 1,344,468,000/=

Kif. 2011 – *Central Zone* Sh. 965,131,000/=

Kif. 2012 – *Southern Western Zone* Sh. 1,134,744,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 3001 – *Energy and Petroleum*... ... Sh. 44,879,169,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini

Kif. 1003 – *Policy and Planning*... Sh. 0/=

Kif. 1008 – *Environment Management Unit*... Sh. 0/=

Kif. 2001 – *Minerals*... Sh. 45,240,000,000/=

Kif. 2002 – *Madini Institute*... Sh. 1,220,000,000/=

Kif. 2003 – *Research and Laboratory*

Services... Sh. 1,000,000,000/=

Kif. 3001 – *Energy and Petroleum*... ... Sh. 944,752,745,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge ilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2013/2014 na kuyapitisha pamoja na mabadiliko yake. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)
(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yenu kuwapongeza Waziri na Manaibu wake na Wataalam wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri mnayoendelea kufanya na mwendelee kufanya na kama mnavyoona suala la umeme, naamini ni suala ambalo linamgusa kila mtu katika kipindi hiki cha dunia. Kwa hiyo, nawatakieni heri, huu ni mwaka mmoja toka mmechukua kazi hiyo, sasa mwendelee kufanya vizuri zaidi katika miaka ijayo.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mheshimiwa nikisimama mimi naomba wewe usisimame, ndiyo Kanuni inavyosema. Mimi nikisimama wewe huwezi kusimama na muda umekwisha, hakuna namna.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe taarifa ifuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyokumbuka, tarehe 31, Januari, 2013 kulitokea vurugu Mkoani Mtwara kutokana na mpango wa Serikali wa kujenga bomba kubwa la kupeleka gesi Dar es Salaam kutoka Mtwara, ili kusaidia kupunguza tatizo kubwa la ukosefu wa umeme nchini.

Matumizi ya umeme wa maji yamekuwa tatizo kutokana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, umeme wa mafuta ni ghali sana na ni mzigo kwa Taifa ikilinganishwa na gesi asilia ambayo Mwenyezi Mungu ameipatia nchi yetu.

Pamoja na kwamba Waziri Mkuu alikwenda Mtwara kuwasikiliza wananchi na wadau mbalimbali wakati ule na tukaamini kuwa mambo sasa yameeleweka. Bahati mbaya sana tarehe 22 Mei, 2013 hali ya usalama ikawa mbaya katika Mkoa wa Mtwara baada tu ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuwasilisha hotuba yake hali ambayo ilifanya Bunge kuahirisha shughuli zake ili Serikali itoe taarifa ya hali halisi ya usalama katika Mkoa wa Mtwara inavyoendelea.

Baada ya taarifa hiyo ya Serikali, Kamati ya Uongozi ya Bunge ilikutana na kujadili hatua ambazo Bunge litachukua. Kamati ya Uongozi ya Bunge iliamua kuwa iundwe Kamati Maalum ili iende Mtwara na kuwasikiliza wananchi kuhusu wasiwasi wao wa azma ya Serikali ya kujenga bomba la gesi kwenda Dar es Salaam. Kamati ya Uongozi, iliagiza kuwa katika mazingira ya utulivu na amani Kamati ikutane na wananchi mbalimbali na kuwasikiliza hoja zao.

Nawasihi wananchi wa Mtwara, Kamati itakapokuja wawe watulivu, wawazi na huru kutoa mawazo yao bila wasiwasi wowote ule au mashaka. Kamati itapata nafasi ya kutosha ya kukutana na wananchi, vikundi, taasisi hata na watu binafsi. Kubwa tunaloomba sote ni amani, utulivu, upendo na maendeleo ya kila mmoja na jamii zetu na nchi yetu bila kubagua mtu, kabilia, eneo, rangi wala Mkoa.

Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya tano ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013, naunda Kamati Maalum ambayo itakuwa na hadidu za rejea zifuatazo:-

Katika kutekeleza kazi hiyo naipa Kamati hiyo hadidu za rejea zifuatazo:-

- (i) Kuchunguza chimbuko la mgogoro;
- (ii) Kufuatilia hatua zilizochukuliwa na Serikali kutatua mgogoro huo;
- (iii) Kukutana na wadau mbalimbali ili kupata maoni yao kuhusu miradi ya gesi asilia; na
- (iv) Kuangalia mambo mengine yoyote yenye uhusiano na mgogoro huu.

Sasa Wajumbe ambao nimewateua ni hawa wafuatazo:-

Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Dokta Dalali Peter Kafumu, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa *Engineer* Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

Mwenyekiti wao atakuwa Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage. Hiyo ndiyo Kamati niliyounda, wataanza kazi kwanza kwa kuelewa mazingira yaliyo huku, mpaka tutakapokuwa tunajua hali imetulia kule, ndiyo watakwenda, lakini wataanza kupata taarifa kwa vyombo ambavyo vilihusika kwanza. Kwa hiyo, hii ndiyo Kamati tuliyonayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nina tangazo moja tu, kesho nimesema kuna semina ya

kuhusu Sera ya Elimu, makabrasha mnayo kwenye *pigeon holes*. Kwa hiyo, msije mkategemea mtapewa kule, yako kwenye *pigeon holes* waliwagawieni muda mrefu myachukue na myasome.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naomba niwashukuru sana kwa kukubali kufanya kazi ya ziada mpaka leo saa tisa hii, ikiwa ni *weekend* na tumeweza kurudia kwenye ratiba yetu. Siku ya Jumatatu ni Wizara ya Ardhi. Kwa hiyo, wanaohusika wote wajiandae.

Baada ya kusema hivyo, naahirisha kikao cha Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(*Saa 9.00 Alasiri Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Mei, 2013 Saa tatu Asubuhi*)